

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 17 Aprili, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA - MAKAMU MWENYEKITI  
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIBU K.n.y MWENYEKITI  
KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI-KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa, swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum. Mheshimiwa Silafu.

Na. 87

**Kutokamilika kwa Ujenzi wa Barabara ya Namanyere  
Ninde**

**MHE. SILAFU J. MAUFI** aliuliza:-

Serikali ilitoa shilingi milioni 300 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya kutoka Namanyere Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi hadi Ninde yenye urefu wa kilometa 40 lakini hadi sasa ujenzi wa barabara hiyo bado haujakamilika kwa muda mrefu sasa.

(a) Je, ni lini Serikali itachukua hatua kwa kufuatilia na kuchunguza matumizi ya fedha zilizotolewa na kuchukua hatua ili ujenzi wa barabara hiyo uweze kukamilika?

(b) Je, ni lini wananchi wa Ninde wataondokana na changamoto ya barabara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Namanyere - Ninde yenye urefu wa kilomita 60 katika mwaka wa fedha 2014/2015 ilitengewa shilingi milioni 350 za kufanya matengenezo kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa daraja moja lenye urefu wa mita 20 kwenye Mto Lwafi kwa shilingi milioni 73.69;

(ii) Ujenzi wa daraja moja lenye urefu wa mita 50 kwenye Mto Ninde kwa shilingi milioni 33.922 ;

(iii) Ujenzi wa madaraja mawili yenye urefu wa mita tano kila moja kwenye msitu wa Lwafi kwa shilingi milioni 26.65; na

(iv) Kuifungua sehemu iliyokuwa imebakia ya barabara ya urefu wa kilometa 25 kwa kufanya matengenezo kwa kiwango cha udongo na kujenga makalvati mistari 15 kwa shilingi milioni 154.735 pamoja na gharama za usimamizi jumla ya shilingi milioni 61.003.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kupambana na changamoto ya barabara kwa wananchi wa Ninde kwa kuitengea fedha za matengenezo barabara hiyo. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 shilingi milioni 44.58 zilitengwa

kwa ajili ya kufanyia matengenezo ya muda maalum kwa urefu wa kilometa mbili. Aidha, mwaka wa fedha 2016/2017 shilingi milioni 20 zilitengwa na kutumika kuimarisha sehemu korofi zenye urefu wa mita 500.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufanyia matengenezo barabara hiyo kulingana na upatikanaji wa fedha ili iweze kupitika na kuondoa tatizo la usafiri kwa wananchi wa Ninde na maeneo jirani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi swali la nyongeza.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu suala hili, bahati nzuri mwenyewe anayezungumza ni ametoka Mkoa wa Rukwa, kwa hiyo, barabara hii anaifahamu vilivyo. Akina mama wengi na watoto wanapata shida kwenye barabara hii wanapokuja kupata huduma ya afya Namanyere.

Napenda kuiuliza Serikali, je, ina mpango gani kwa hivi sasa kwa sababu tupo katika kipindi cha bajeti kuweza kutenga fedha za kutosha kuikamilisha hii barabara badala ya kuendelea kutengeneza maeneo korofi kila mwaka hadi mwaka na kuonekana kana kwamba ni mradi wa Serikali?  
(Makofi)

Swali la pili, ninapenda kuiomba Serikali ijaribu kuona hizi barabara zetu za Bonde la *Lake Tanganyika* na Bonde la *Lake Rukwa*, barabara hizi ni tata, zinahitaji matengenezo yaliyokamili kama vile Kitonga na inavyoelekea kutumika katika kipindi chote cha mwaka mzima.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Josephat Kandege, Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa

Spika, ni ukweli usiopingika kwamba barabara hii ina changamoto kubwa maana kuna maeneo ambayo kuna milima mikubwa sana na azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wa Ninde wanapata barabara inayoweza kupitika kwa vipindi vyote.

Mheshimiwa Spika, kabla ya hapo ilikuwa hakuna barabara kabisa na ndiyo maana Serikali kwa kulitambua hilo ikaanza kutenga kiasi cha shilingi milioni 350 na maeneo yaliyokuwa korofi zaidi ilikuwa ni maeneo ya madaraja. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ilimradi madaraja yameshajengwa ambayo ndiyo yalikuwa ni changamoto kubwa sana, nia na azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba maeneo yaliyobaki yataweza kutengenezwa kwa kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu.

Katika swali lake la pili, ameongelea Ukanda wa Ziwa Rukwa. Sifa ya Ukanda wa Ziwa Rukwa na hii barabara aliyoitaja ya kwenda Ninde hazina tofauti sana na Mbunge, Mheshimiwa Malocha amekuwa akiipigia kelele sana na kwa mara ya kwanza Serikali imesikia kilio chake na barabara hii inaweza kuimarishwa ili iweze kupitika katika kipindi chote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige nilikuona.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mwaka huu tumebarikiwa mvua lakini mvua hizi zimeleta madhara sehemu mbalimbali na kuharibu miundombinu ya barabara.

Ningependa kujua, je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na majanga haya ya barabara hususani zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Vijijini (*TARURA*)? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kuna msaada nyuma yako, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali tumejipanga na kama ilivyo kawaida kila mwaka tunatenga fedha kwa ajili ya kutibu dharura kwa maana ya *emergency*, kwa sasa hivi maeneo mengi ambayo barabara hazipitiki tumewaagiza Meneja wa *TANROADS* washirikiane na *TARURA* ili kuweza kuokoa sehemu hizi ambazo hazipitiki na Wizara tunaendelea kuratibu na kufuatilia ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma wanapita kwenda kwenye shughuli zao za maendeleo. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kwandikwa. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 88

### **Upimaji wa Vitunguu kwa Kutumia Debe-Tarafa ya Eyasi**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Wananchi wengi wa Tarafa ya Eyasi katika Wilaya ya Karatu wanajishughulisha na kilimo cha vitunguu maji, hata hivyo mavuno yanayotokana na kilimo hicho hupimwa kwa debe yanapouzwa badala ya kilo.

Je, ni kwa nini Serikali isihakikishe na kusimamia uuzwaji wa mazao haya kwa kutumia kilo badala ya vipimo vya debe?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Namba 340 ya mwaka 2002 na mapitio yake ya mwaka 2016, vipimo sahihi ni kutumia mizani iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo na siyo vinginevyo ambapo kipimo chake ni kilo kwa bidhaa za aina hii yaani vitunguu vikiwa ni mojawapo vinavyostahili kupimwa kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Vipimo inaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya vipimo kwa njia ya radio, luninga, makala za magazeti na kwa kushiriki katika maonesho mbalimbali. Vilevile Wakala wa Vipimo wametoa elimu kwa wadau wa biashara hiyo ya vitunguu huko Mang'ola Tarafa ya Eyasi wakiwemo wakulima, viongozi wa vijiji, kata, tarafa, halmashauri ya wilaya kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu matumizi sahihi ya vipimo vinavyoruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria ya Vipimo ilipitiwa na Bunge lako Tukufu mwezi Novemba, 2016 ili kuruhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa na Sheria Ndogo (*by-laws*) za kuwawezesha kuanzisha vituo vya ununuzi wa mazao na bidhaa katika eneo la mamlaka husika vitakavyokuwa na mizani iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo. Hali kadhalika, Serikali inaendelea kuhamasisha ujenzi wa vituo maalum vya ununuzi wa mazao (*buying centres*) vyenye nafasi ya maghala ya kuhifadhia mazao, ambapo kwa Tarafa ya Eyasi, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kwa kushirikina na wadau wa maendeleo tayari imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa kituo katika kijiji cha Mang'ola chenye maghala matatu kwa ajili ya kuhifadhi vitunguu. Kituo hiki kinatarajia kuanza kutumika katika msimu wa mwaka huu wa ununuzi wa vitunguu. Vituo vya aina hii vitasaidia wakulima kuwa na nguvu ya pamoja kujadiliana na wanunuzi na kutumia vipimo sahihi ili kupata bei yenye ushindani na haki katika soko.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu ninapenda kuwatahadharisha wakulima na wafanyabiashara wote wanaojihusisha na biashara ya vitunguu na mazao mengine yote kuhakikisha kuwa

wanatumia vipimo sahihi. Aidha, Serikali itaendelea kufuatilia kuchukua hatua za kisheria pale inapobidi kufanya hivyo kwa wanaokiuka sheria hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, vifungashio vya mazao haya ya vitunguu katika Tarafa ya Eyasi hufanyika kwa aina mbili. Kuna kifungashio cha Mkenya maarufu wanaita *net* ambapo *net* hii ikijazwa *net* tatu inakuwa sawa na debe kumi; na kuna kifungashio kingine kinaitwa kifungashio cha Mganda ambapo kifungashio hiki cha Mganda kinachukua kati ya debe nane mpaka tisa jambo ambalo kwa kweli linawaumiza wakulima.

Je, ni kwanini Serikali isihakikishe kunakuwa kuna *standard* ya vifungashio kwa wakulima hawa ili tusiweze kuwaumiza?

Swali la pili, tatizo la ujazo kupita kiasi maarufu kama lumbesa bado ni changamoto kwa wakulima hawa katika maeneo mbalimbali na zao hili linapofika sokoni wanunuzi wanachukua yale ambayo yamejazwa kwa maana ya lumbesa kuliko yale ambayo yana ujazo wa kawaida. Mfano, labda ujazo huu unatokea Singida, unatokea Kilimanjaro, unatokea Mang'ola wale ambao wana ujazo zaidi ndiyo itanunuliwa zaidi na wale ambao wana ujazo wa kawaida ambao ni *standard* inakuwa hainunuliwi.

Je, ni kwa nini sasa Serikali isiendeele kutia msisitizo ili jambo hili lisimamiwe katika maeneo yote kwa ukamilifu wake ili kuwepo na ujazo ambao unafanana?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, *Engineer* Stella Manyanya, tafadhali.



**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwanza, nisisitize tu kama ambavyo swali limejibiwa kwamba kipimo sahihi cha uzito wa aina ya bidhaa kama vitunguu ni *kilogram*, kwa hiyo tunachosema ni kwamba *whether* hicho kifurishi kitawekwa kwenye *net*, kitawekwa kwenye debe, kitawekwa kwenye kitu chochote kile ilimradi baada ya kuwekwa humo basi kipimwe kwenye uzito sahihi ambao ni *kilogram* ndivyo inavyostahili.

Pili, ulivyouliza kuhusu suala la lumbesa ni hivyo hivyo kwamba kwa mfano, unavyofungasha kwenye gunia likaitwa hili ni gunia la kilo 50 wakati ndani yake kumbe kuna kilogramu zaidi ya 50 inasababisha kwamba kwanza mkulima mwenyewe ananyonywa, lakini vilevile hata Halmashauri inaweza ikakosa mapato kutokana na kuwa na uzito ambao haustahili kutokana na kwenye kile kitu ambacho kimefungashiwa. Ijulikane kwamba siyo kwamba bidhaa zote zinakuwa na ujazo unaofanana. Kwa mfano, ujazo wa pamba kwenye kiroba ni tofauti na ujazo huo huo ukiwa ni wa viazi na ndiyo maana tunasisitiza kilogramu ambayo ndiyo kipimo sahihi ambacho kinastahili katika kupimia.

Mheshimiwa Spika, hivyo ninawaomba sana wananchi wote pamoja na wafanyabiashara kuhakikisha kwamba tunakuwa na mizani katika maeneo yetu ya kibiashara na hilo ndiyo linalosisitizwa sasa kuwa na masoko ya pamoja ili kuweza kuwafanya hawa wananchi wanaolima mazao kama hayo, kuweza kuwa na ushirikiano katika kudhibiti hali kama hiyo ya kuwa na vipimo ambavyo haviruhusiwi kisheria.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Nape Nnauye swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ka kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa msimu uliopita soko

la mbaazi lilisababisha kuanguka kwa bei ya mbaazi kutoka shilingi 2,000 kwenda mpaka shilingi 150, Serikali ilihaidi hapa Bungeni kwamba itahakikisha inahangaika kupata soko la kuaminika la zao hili. Sasa ni msimu wa kilimo hicho, Serikali imefikia wapi kupata soko hili na kama hali bado haileweki tuwashauri wananchi wetu waachane na mbaazi badala yake wajikite kwenye mazao mengine ambayo yana soko la uhakika?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Stella Manyanya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni kweli kabisa katika msimu huu ulioisha kulikuwa na hali isiyopendeza katika soko la mbaazi, hiyo ni kutokana na kwamba wadau ambao tulikuwa tunawategemea sana katika biashara hiyo ilikuwa ni wenzetu kutoka India. Niseme tu kwamba mbaazi ni chakula kizuri, mbaazi ni chakula ambacho kina protini na hata sisi wenyewe tunaweza tukala siyo kuwategemea tu watu wa maeneo mengine. Kama tunaavyosema kwamba biashara ni ushindani na kila watu wanajitahidi kuhakikisha kwamba wanakidhi soko lao la ndani, upande wa Tanzania tunaendelea kutafuta soko wakati huo tunaendelea kusisitiza kwamba hata wenyewe tupende kutumia mbaazi.

Mheshimiwa Spika, nimepita hapa katika masoko yetu kwa mfano soko la hapa Dodoma, nilipofuatilia nilikuta kwamba mbaazi zinazwa mpaka shilingi 1,800 kwa kilo. Soko la pale Dar es Salaam kwenye *supermarket* mbaazi inazwa mpaka shilingi 2,400 kwa kilo. Kwa hiyo, tusitegemee tu soko kutoka nje hata ndani ya nchi bado kuna watu ambao wananweza kula mbaazi na mimi mwenyewe ni mtumiaji wa mbaazi, vilevile tunategemea kwamba hata kupitia shule zetu tutaweza pia kuhamasisha na kuweza kupeleka chakula cha aina hiyo wakati masoko mengine ya nje yakiendelea kutafutwa.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali linalofuata la Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

linaulizwa na Mheshimiwa Hassan Seleman Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini.

Na. 89

**Ujenzi wa Barabara ya Ngongo - Ng'apa - Milola  
kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. HASSAN E. MASALA (K.n.y. MHE. HASSAN S. KAUNJE)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Ngongo - Ng'apa - Milola ambayo ipo chini ya *TANROADS*?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Kaunje, Mbunge wa Jimbo la Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ngongo - Ng'apa - Milola yenye urefu wa kilometa 42 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Lindi. Barabara hii ni sehemu ya barabara ya Ngongo - Ruangwa na Nanganga yenye urefu wa kilometa 162.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii imeendelea kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali ili iendelee kupitika kiurahisi ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya shilingi bilioni 1.149 zimetengwa naa jumla ya kilometa 30 zimefanyiwa matengenezo ya muda maalum.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya barabara ya Ngongo - Ng'apa - Milola kilometa 42 kwa sasa kipaumbele ni kukamilisha kwanza barabara za kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa pamoja

na nchi jirani ndipo barabara za kuunganisha Wilaya zitafuata. Hivyo, barabara hii itaendelea kufanyiwa matengenezo ya aina mbambali kwa kiwango cha changarawe ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka wakati Serikali ikitafuta fedha za kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kama sehemu ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pamoja na hayo naomba nitumie nafasi hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni muda mrefu sasa toka fedha hii shilingi bilioni moja itengwe na barabara ambayo imetajwa imefanyiwa sehemu tu ya matengenezo naomba kupata kauli ya Serikali, hizi kilometa 12 zilizobaki ni wakati gani zitamaliziwa kwa fedha ambayo imetengwa?

Swali la pili, naomba kuuliza Serikali imekuwa na kipaumbele cha kuunganisha barabara za Mikoa kama ambavyo jibu la msingi linavyojieleza. Nini mpango wa Serikali wa kukamilisha au kuanza ujenzi wa barabara ya lami kutoka Masasi kwenda Nachingwea, Nachingwea kwenda Nanganga ikiwa ni ahadi ambayo imetolewa kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna kiasi cha fedha kilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii na ilikuwa ni mkakati wa Serikali kulipa madeni. Katika kipindi hiki hadi Desemba Serikali ime-*clear* madeni kwa makandarasi zaidi ya shilingi trillioni 1.385 kwa maana hiyo hii ni fursa inatosha sasa kuanza kuendelea kutoa sasa mikataba kwa ajili ya ujenzi wa

barabara. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge hizi kilometa 12 zitatangazwa na kuanza kutengenezwa wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, pia niseme tu ni mpango wa Serikali kuunganisha Mikoa kama nilivyojibu katika jibu la msingi na Mheshimiwa Mwalimu Masala unakumbuka kwamba katika mpango ambao unaendelea kwa ajili ya ujenzi wa barabara kile kipande cha Nachingwea kwenda Nanganga kilometa 46 kitatangazwa wakati wowote, kipo kipande kingine cha Nachingwea - Ruangwa kilometa 45, lakini kuna kipande cha Ruangwa - Nanganga kilometa 58. Pia unatambua kwamba kuna ujenzi wa daraja kule kwenye Mto Lukuledi hii ni dhamira ya Serikali kuweza kuunganisha maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya eneo hili kuwa limekamilihwa itakuwa ni sehemu ya kuunganisha Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Ruvuma kwa maana kuwa unatambua kwamba ukitokea Nachingwea kwenda Kilimarondo utakuwa unaelekea kule Mindu upande wa Tunduru tutakuwa tunaunganika na wenzetu wa upande wa Ruvuma. Upande wa Morogoro pia kilometa 129 ukitokea Nachingwea kuelekea Liwale naona Mheshimiwa Kuchauka ananitazama hapa ni kwamba barabara hii sasa tutakapokuja kuanza kutengeneza itakuwa ni sehemu ya barabara ya kuunganisha upande wa Lindi kuelekea Mahenge kule Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge nikuombe tu uvute subira ni mpango mzuri wa Serikali kuhakikisha kwamba tunaweza kutengeneza barabara hizi kuunganisha Mikoa na hii itatupa fursa sasa ya kuunganisha barabara ambazo zinakwenda kwenye Wilaya. Kwa hiyo tuvute subira na wananchi wajue Serikali inafanya kazi kubwa kulipa madeni na kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama kuomba nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza)*

**SPIKA:** Hee! Mheshimiwa Naibu Waziri Uchukuzi, Ujenzi hebu angalia tu jinsi barabara zilivyoharibika na mvua ya mwaka huu. Wabunge wamesimama wima kweli, nimekuona Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Igunga kwenda Mwanzugi hadi Itumba ilikuwa na mkandarasi wa *TARURA* aliyewekwa na *TARURA* anajenga, lakini uharibifu ulikuwa mdogo sana. Sasa hivi kutokana na mvua kama ulivyosema barabara hiyo imeharibika sana, naiomba Serikali itakuwa tayari kweli kuongezea bajeti kwa ajili ya kujenga hiyo barabara ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa Igunga? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Elias John Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwa ujumla ni kweli hali ya mvua zimekuwa *excessive* kwa maana ya kwamba kuna maeneo mengi yameharibika. Tunazo taarifa kule Koga hapapitiki, lakini tunazo taarifa kule Solwa hapapitiki na maeneo mbalimbali. Kama nilivyosema wakati nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine kwamba tumejipanga kuhakikisha kwamba maeneo yanapitika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dalaly Kafumu sana muda mwingi tumezungumza juu ya barabara hii na kwa kweli swali lako nazungumza juu ya kuongeza bajeti. Tumejipanga kuitazama hii barabara, najua pia una hamu ya kwenda kuunganika na wenzetu kule upande wa Nyahua. Kwa hiyo, tunaitazama kwa umakini na tutakapopata fursa tutaendelea kuongeza bajeti ili hatimaye hii barabara iweze kutengenezwa vizuri na ipitike muda wote na pia ni huduma

kwa wananchi wetu wa Igunga na maeneo ambayo yanazunguka Igunga. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la mwisho la nyongeza Mheshimiwa Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu.

**MHE. DANIEL N. NSWANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri barabara ya Kidawe - Kasulu kilometa 63 tumezungumza na wewe na nikakujulisha kwamba mkandarasi hafanyi kazi sasa, anafanya kazi ndogon dogo tu kwa sababu hajalipwa fedha zake, barabara hiyo sasa ni miaka 12 inajengwa, ni kwa nini mkandarasi hapewi fedha zake akamaliza barabara hii?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge najua tumeongea mara nyingi sana kuhusu barabara za Kigoma, lakini niseme tu kwa wananchi wa Kigoma na Watanzania kwa ujumla, Serikali imejipanga vizuri sana kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara kwa sababu kipaumbele chetu ni kuunganisha Mikoa yetu ya jirani na nchi za jirani. Kwa hiyo Mheshimiwa Nsanzugwanko unafahamu Kidahwe kwenda Kasulu kilometa 63 yuko mkandarasi pale, lakini kwa sasa kutokana na hali ya hewa kuna kazi ambazo zinafanyika wakati wa kipindi cha mvua, pamoja na kuwa tuna deni na mkandarasi yule upande wa Wizara tunafanya kila juhudi tuweze kuhakikisha kwamba tutapeleka fedha ili mvua zitakapopungua *speed* iwe kubwa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa barabara zote ukianzia Nyakanazi kuja Kakonko; kutoka Kankonko kuja Kibondo na kuja kuunganika Kigoma kuna juhudi nzuri na hatua nzuri tumefikia kwa ajili ya kutengeneza mikataba kwa

ajili ya ujenzi wa barabara hii ili pamoja na viungo vyake kutoka Kasulu kwenda Manyovu pale *border* ziko kilometa 58 hivi lakini zipo tena kutoka Kakonko kwenda Mabamba na wewe unafahamu.

Kwa mkoa huu ambao ulikuwa umechelewa kufanya matengenezo ya barabara kiwango cha lami kwamba sasa ziko fedha ambazo harakati zinaendelea, kwa hiyo, Kigoma itafunguka na itaungana na mikoa mingine. Mheshimiwa Nswanzugwanko na wananchi wa Kigoma naomba wavute subira na tutaendelea kukupa *feedback* kujua hatua nzuri zinazoendelea kule Kigoma. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 90

### **Mkakati wa Kusimamia Maadili kwa Vijana Nchini**

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI (K.n.y. MHE. NURU A. BAFADHILI)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kuhakikisha vijana wetu wanakuwa na maadili pamoja na silka na desturi za Kitanzania kama walivyo wazazi wao?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuisitiza kuwa wazazi na familia kwa ujumla ndiyo walezi wa kwanza wenye jukumu la makuzi ya mtoto kuanzia hatua za awali. Wazazi



hufuatiwa na vyombo vya elimu kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari hadi elimu ya juu. Jukumu la kusimamia malezi na makuzi ya watoto na vijana ni pamoja na kuelimisha kwa maneno na vitendo kuhusu utambuzi wa mambo mema na mambo mabaya, mambo yanayofaha na mambo yasiyofaha yanayostahili na yasiyostahili yakiwemo masuala ya mavazi, kauli, staha, mwenendo pamoja na muonekano kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, hatua ya awali ya malezi ya makuzi ikishapita ndipo wajibu mkubwa wa Serikali unajitokeza katika ukuaji wa vijana kupitia sera, kanuni, sheria, taratibu pamoja na miongozo na kwa kutumia majukwaa mbalimbali ya elimu na nasaha kama vile semina, warsha, makongamano, mikutano, maonesho pamoja na matamasha.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayolikabili Taifa letu leo ni athari ya utamaduni wa nje kwa maadili, mila na desturi zetu kupitia muingiliano mkubwa wa watu wa dunia kwa njia ya utalii, biashara na kadhalika, vilevile kupitia maendeleo ya kasi ya TEHAMA. Pamoja na juhudi za Serikali kudhibiti wimbi la utamadunisho hasi nchini kwa kutumia sheria, kanuni na vilevile kuboresha mitaala yetu toka shule ya msingi hadi elimu ya juu ili izingatie elimu ya uraia, utaifa, uzalendo, mchango wa wazazi na wananchi kwa ujumla katika kufanikisha jitihada za Serikali hauna mbadala. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kahigi swali la nyongeza.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nina majibu mawili ya nyongeza...

**SPIKA:** Maswali.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwa kuwa luninga zinapoteza watoto wetu katika kupotosha watoto wetu katika maadili, je, Serikali ina mkakati gani wa kutusaidia katika suala hili?

Swali la pili, kuna changamoto katika wasanii wa muziki hasa katika nyimbo zao zina matusi, je, Serikali itatusaidiaje kwa sababu wanawake wanavaaa mavazi ambayo hayana staha Serikali itatusaidiaje kusudi waweze kuacha mambo hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa; majibu ya maswali hayo Naibu Waziri Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Juliana Shonza, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi kuweza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri sana, tumefaidika sana kama Wizara tunapopata maswali kama haya ningeweza pia kuweza kumshauri Mheshimiwa Waziri kama kuna uwezekano Mheshimiwa Nuru Awadhi aweze kuwa Balozi wa Maadili katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ameelezea kwamba luninga zinasaidia sana katika kupotosha mmomonyoko wa maadili katika Taifa letu na mimi niseme kwa namna moja ama nyingine nakubaliana na mawazo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema, lakini hilo huwa linatokea tu pale ambapo kunakuwa hakuna chombo maalum cha kuweza kusimamia maudhui mbalimbali ambayo yanarusha na vyombo vyetu vya luninga. Kwa kutambua hilo na ndiyo maana Serikali imeunda vyombo viwili ambavyo ni *TCRA* pamoja na Bodi ya Filamu ambavyo vyote hivi vina lengo kubwa la kuhakikisha kwamba vinasimamia maudhui yanayorushwa katika vyombo vyetu vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba pamoja na changamoto hizo, Wizara tumeendelea kuhamasisha jamii kwa ujumla kuhakikisha kwamba suala la maadili ni suala

ambalo lazima jamiii kwa ujumla wetu kuendelea kulifanyia kazi siyo suala tu la Serikali kama ambavyo nimejibu kwenye jibu la msingi kwamba ni suala ambalo la Serikali, lakini vilevile pamoja na jamii nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, habari njema ni kwamba Wizara kwa sasa hivi imeandaa kanuni mbili ambazo tunaamini kabisa kwamba kanuni hizo ambazo ni kanuni zinazosimamia maudhui katika redio, maudhui katika mitandao ya kijamii na tunaamini kabisa kwamba kwa kupitia kanuni hizi itakuwa ni muarobaini wa kuhakikisha kwamba mmomonyoko wa maadili katika Taifa letu unadhibitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kuchukua nafasi kuweza kuomba vyombo vyote vya habari viweze kuzingatia kanuni hizo ili kuhakikisha kwamba tunatunza maadili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili ametaka pia kuweza kujua kwamba kumekuwa na tatizo la nyimbo ambazo haziendani na maadili ya Taifa letu hususani wanawake ambao wanavaa mavazi ambayo siyo ya staha.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme kwamba sisi kama Serikali tunatambua kwamba tuna changamoto hiyo na kitu ambacho tumekifanya kwa sababu tuna vyombo vyetu viwili ambavyo ni vyombo vinasimamia maudhui kwa wasanii kwa maana ya BASATA pamoja na Bodi ya Filamu. Hivi vyombo viwili vimekuwa vikisitiza mara kwa mara kuhakikisha kwamba wasanii kabla hawajatoa nyimbo zao wanapeleka nyimbo zao BASATA, wanapeleka video zao Bodi ya Filamu ili ziweze kuhaririwa na ziweze kupewa madaraja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba...

**SPIKA:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mimi nikushukuru lakini niseme kwamba tumekuwa tuna changamoto kubwa sana k wasanii wetu hawapeleki nyimbo zao kwenda kuhaliliwa BASATA naomba kuchukue nafasi hii kuweza kuwaambia kwamba wasanii wote wahakikishe kwamba wanapeleka nyimbo zao BASATA ili ziweze kuhaririwa kabla hawajaanza kuchukuliwa hatua. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Goodluck Mlinga nilikuona swali la nyongeza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana ushoga usagaji na kutukuna matusi mithili ya bomu la nyuklia siyo maadili yetu na desturi ya Mtanzania, lakini vitendo hivyo vimekithiri kartika mitandao yetu ya kijamii. Kwa mfano, wapo mashoga maarufu wanajitangaza katika mitandao yetu ya kijamii na siyo utamaduni wa Kitanzania; kwa mfano kuna mtu mmoja maarufu anaitwa James Delicious.

Mheshimiwa Spika, kuna vikundi vya matusi kabisa katika mitandao ya kijamii. Mfano kuna *team Wema, team Zari, team Diamond, team Shilole*, hawa wamekuwa wakitukana matusi katika mitandao ya kijamii.

Je, nini kauli ya Serikali kutokana na hili kwa sababu linachangia kwa kiwango kikubwa sana kuharibu maadili na utamaduni wa Kitanzania? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Mwakyembe majibu tafadhali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Tullitunga Sheria ya *EPOCA* mwaka 2010 lakini tulikosa Kanuni za kuweza kubana hasa maudhui upande wa mitandao. Tumeshatunga hizo Kanuni na sasa hivi hizo Kanuni zimeanza kufanya kazi. Naomba nitoe taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna baadhi ya wasanii wetu ambao walianza kufanya uhuni

uhuni ndani ya mitandao, jana tumeweza kumkamata mwanamuziki nyota Tanzania, Diamond tumemfikisha polisi na anahojiwa kutokana na picha alizozirusha. Vilevile imebidi hata Binti Nandy naye apelekwe polisi kuhojiwa. Tunaangalia namna ya kuwapeleka mahakamani.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito kwa vijana wote nchini, mitandao siyo kokoro la kupeleka uchafu wote ambao umezuwa na sheria zingine. Hii nchi ina utamaduni wake. Tunahitaji kulinda kizazi cha leo, kesho na kesho kutwa cha Taifa hili. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Rombo nilikuona.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza mmomonyoko wa maadili kwa vijana mara nyingi tunazungumza habari ya vijana wasanii, wanaocheza filamu, wanamuziki na kadhalika. Lakini mmomonyoko pia mkubwa sana upo kwa vijana wa mitaani na hawa mara nyingi ni kwa sababu ya kukata tamaa.

Sasa naomba niulize Serikali, pamoja na mifuko mbalimbali ya kuwaendeleza vijana, ni mkakati gani ambao Serikali inao ili kuwasaidia kisaikolojia na namna vilevile ya kuweza kuona matumaini katika maisha yao vijana waache kuingia kwenye tabia ambazo kwa kweli zinasababisha mmomonyoko mkubwa sana wa maadili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Jamani, jambo hili siyo la Serikali peke yake ni la jamii yote. Mheshimiwa Waziri, nimekuona tafadhali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na ninakushukuru kwa kujibu sehemu ya hilo swali kwamba huu ni wajibu wa jamii nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imekuja

kwa nguvu sana na kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu ili Watanzania wathamini kazi. Kazi ndiyo ufunguo wa kila kitu ningeomba Watanzania wote tushirikiane kuhakikisha kwamba kila mtu Tanzania anafanya kazi, mambo ya njia za mpito kuweza kuishi hayana nafasi tena ndiyo yanayozua matatizo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili wazazi tuna nafasi kubwa sana kuweza kubadilisha hii hali kwa upande wa watoto wetu tukiweka mbele suala la kazi kama tulivyokuwa tunafanya wakati wa uhuru ambapo tulikuwa tunasema uhuru ni kazi na leo ni hapa kazi tu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, swali linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi. Kabla ya Mheshimiwa Chuachua, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kwanza niungane na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kwa kukubaliana naye kwamba suala la kubadilisha utaratibu wa mfumo wa maisha kwa vijana pamoja na kwamba ni suala la jamii kwa ujumla, lakini napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba pia kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tumeandaa programu mbalimbali ambazo tunashirikiana na Halmashauri za Wilaya kuhakikisha Halmashauri zetu Idara za Vijana zinajipanga kutoa elimu ya kubadilisha mawazo na mtazamo kwa vijana ili kuwasaidia kujenga mtazamo mpya wa kujiajiri na kuondoka katika tabia za kupoteza muda kwenye vijiwe na kuingia kwenye shughuli ndogondogo za kuweza kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kwa pamoja na Halmashauri zetu, hasa wale vijana ambao wamekuwa wakipoteza muda mwingi kwenye vijiwe. Wageuze vijiwe vyao kuwa ni shughuli za kiuchumi badala ya kutumia vijiwe kuwa ni maeneo ya kupoteza muda. Mifuko ya kuwawezesha hao vijana kupitia

Idara ya Vijana kwenye Halmashauri zetu ipo na Serikali tumeshajiandaa na Wabunge ambao wapo tayari tutafanya nao kazi hiyo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu hayo tunashukuru sana. Mheshimiwa Waziri wa Michezo kuna huu mchezo wa *pool*, yaani unachukua muda wa vijana vijijini hadi kwenye vitongoji *pool*/iko, kutwa nzima wako kwenye *pool*/tu! Mchezo huu nao uje uangaliwe vizuri huu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi.

Na. 91

**Dhuluma na Ukandamizaji Wanaofanyiwa  
Wakulima wa Korosho**

**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaondoa kabisa malalamiko yanayotokana na makato, rushwa, uwazi na matatizo mengine yaliyopo katika mfumo mzima wa ununuzi wa zao la korosho?

(b) Je, ni lini Serikali itaondoa utaratibu wa wakulima kulipwa mara mbili na badala yake walipwe pesa zao mara moja na wasubiri *bonus* baadae?

(c) Ni lini Serikali itadhibiti usambazaji wa pembejeo kwa watu ambao siyo wakulima wa korosho?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Mohamed Chuachua Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makato yanayotokana na biashara ya zao la korosho yapo kwa mujibu wa sheria na mjengeko wa bei ambayo huamuliwa na wadau wa zao la korosho. Aidha, makato mengine ni kwa ajili ya maendeleo ya Mikoa na Halmashauri za Wilaya zao la korosho linakozalishwa.

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilifuta tozo tano na katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Serikali imefuta tozo mbili zilizokuwa zinatozwa kwenye biashara ya zao la korosho. Vilevile Serikali inaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria Namba. 6 ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013 pamoja na sheria nyingine za nchi ikiwemo kuwavua madaraka na kuwachukulia hatua za kisheria viongozi na watendaji wa vyama vya ushirika wanaotuhumiwa kushiriki katika vitendo vya ubadhirifu, rushwa na ukiukwaji mwingine wa sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa malipo kwa wakulima wa zao la korosho kwa sasa hivi hufanyika mara moja tu. Aidha, malipo kwa wakulima waliouza korosho hulipwa kwenye akaunti za vyama vikuu vya ushirika kutoka kwa makampuni yanayonunua korosho kupitia minada. Baadae fedha hutumwa kwenye akaunti za benki za vyama vya ushirika vya msingi na hatimae kulipwa kwa mkulima mmoja mmoja kupitia akaunti yake ya benki.

Mheshimiwa Spika, Serikali inadhibiti usambazaji wa pembejo za zao la korosho kwa watu ambao sio wakulima wa korosho kwa kutumia sensa ya wakulima wa zao la korosho (wanachama na wasio wanachama wa vyama vya ushirika). Sensa hii inawezesha kujua mahitaji halisi ya pembejeo kwa wakulima wa korosho.

Aidha, pembejeo inayoonekana kwa watu ambao sio wakulima wa korosho, inatokana na wakulima wa zao la korosho ambao siyo waaminifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chuachua, swali la nyongeza tafadhali.



**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza nikupongeze kwa sababu ulipopata tu Unaibu Waziri ulikuja Masasi na ukatembelea wakulima wa korosho. Kwa hiyo, changamoto za wakulima wa korosho unazifahamu. Nina maswali mawili yanyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa hadi sasa wakulima wa korosho waliouza korosho zao katika msimu uliopita wanadai fedha zao takribani zaidi ya shilingi milioni 90 katika Jimbo langu tu la Masasi kwa hiyo fedha hizo ni zaidi ya shilingi milioni 90. Je, ni lini Serikali itahakikisha wakulima hawa wamelipwa fedha zao?

Swali la pili, lini Serikali sasa itaingiza *sulphur* ambayo itauzwa kwa wakulima kwa sababu tunafahamu wakulima wananunua *sulphur* kwa mwaka huu. Sasa lini Serikali itaingiza *sulphur* hiyo na kuisambaza kwa bei nafuu kwa wakulima wetu, kwa sababu kwa sasa begi moja ya *sulphur* imefika shilingi 70,000 mpaka shilingi 80,000? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo kwa kifupi sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu ya muda tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa umahiri wake wa jinsi anavyofuatilia wakulima wa zao la korosho katika Mkoa wa Lindi na Mtwara hususan katika Jimbo lake la Masasi na ninaomba kwa maana hiyo nijibu maswali yake yenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikianza na lile la (a) ni kweli wakulima wa zao la korosho wanadai Serikali na naomba niseme tu kwamba Mkoa mzima wa Lindi na Mtwara ikiwemo Masasi wakulima wanadai zaidi ya shilingi bilioni 5.770 Serikali naomba niseme tu kwamba katika Mkoa wa Lindi wataanza kulipwa mwezi huu mwishoni na vilevile katika Mkoa wa Mtwara watalipwa mwezi ujao mwishoni.

Mheshimiwa Spika, nikija katika swali lake la (b) kuhusu suala zima la pembejeo, ni kweli kabisa tunaielewa kwamba kumekuwa na changamoto kubwa sana ya pembejeo katika zao zima la korosho na ninaomba nilitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa upande wa *sulphur* habari njema ni kwamba Serikali tumeagiza tani 35,000 na lita 520 za viwatilifu na tunategemea mwezi huu Aprili awamu ya kwanza itafika na awamu ya pili itafika mwezi ujao mwishoni.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba pembejeo hizi kuanzia sasa zitanunuliwa kwa bei ambayo kwa upande wa *sulphur* haijazidi shilingi 40,000; vilevile kwa upande wa vile viwatilifu haitazidi shilingi 30,000; kwa maana hiyo ni habari njema haitakuwa shilingi 70,000 au 80,000 kama Mheshimia Dkt. Chuachua alivyosema bali itakuwa shilingi 40,000. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tuwiane radhi bado tuko Wizara hiyo hiyo, swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 92

**Serikali Kuwasaidia Wakulima Wadogo wa  
Vitunguu na Alizeti**

**MHE. ALLAN J. KIULA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua za makusudi kutenga mitaji kwa wakulima wadogo wadogo wa mazao ya vitunguu na alizeti katika Wilaya mpya ya Mkalama kupitia benki za mikopo au ruzuku toka Serikalini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mikopo na mitaji kwa wakulima ni mhimili muhimu katika maendeleo ya kilimo. Hata hivyo upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wakulima unakabiliwa na changamoto kutokana na sekta ya kilimo kukabiliwa na majanga mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabianchi na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea. Aidha, kumekuwepo na changamoto ya kukosekana kwa hatimiliki zinazoweza kutumika kama dhamana (*collateral*) pamoja na riba kubwa isiyoendana na msimu wa uzalishaji mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali ilianzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo inayotoa mikopo ya riba nafuu kati ya asilimia 7-15 ambapo kwa Benki za Biashara riba ni kati ya asilimia 18 - 24. Aidha, masharti mengine kwa waombaji mkopo katika vikundi ni kutumia mashamba yao kama dhamana ya mikopo ambapo muda wa kuanza urejeshaji mikopo (*grace period*) hufika hadi miezi sita na kipindi cha kurejesha mkopo kufikia hadi miaka 15 kulingana na aina ya mkopo. Aidha, benki hiyo, hadi kufikia mwezi Machi 2018, imeidhinisha mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 38.79 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kilimo nchini, ambapo kwa Mkoa wa Singida peke yake, benki inatarajia kutoa mikopo kulingana na maombi yatakawasilishwa na wakulima kwa kuzingatia vigezo na masharti.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaendelea kutoa mikopo kupitia Mfuko wa Pembejeo (*Agriculture Input Trust Fund – AGITF*) ambao unalenga kukopesha wakulima pembejeo na zana za kilimo kwa gharama nafuu, ambapo riba ya mikopo ya *AGITF* ni kati ya asilimia sita hadi nane ambapo waombaji wa mikopo katika vikundi vilivyosajiliwa hawahitajiki kuwa na dhamana ya hati au mali isiyohamishika.

Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 hadi 2017/2018 Mfuko wa Pembejeo umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 789,650,000 kwa wakulima wa Mikoa ya Singida na Dodoma ambapo mikopo hiyo ilijumuisha matrekta, pembejeo za kilimo, nyenzo za umwagiliaji na usindikaji.

Aidha, kwa kutambua umuhimu wa mitaji kwa wakulima, Serikali imekuwa ikiimarisha Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) kuhamasiasha benki za biashara na wadau mbalimbali ikiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali kutoka mikopo kwa wakulima nchini.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Serikali kwamba mikakati hiyo itasaidia katika upatikanaji wa mikopo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kwa riba na masharti nafuu ili kuwawezesha wakulima wadogo kuendesha kilomo chenye tija. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiula, swali fupi sana la nyongeza tafadhali.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza mafupi sana.

Kwa kuwa Serikali imetoa takwimu za mikopo inavyotolewa, lakini uhalisia wenyewe mikopo imekuwa haiwafikii wananchi wa vijijini ikiwemo Mkalama na Wilaya ya Dodoma ambako wanalima sana alizeti.

Je, Serikali iko tayari kuzielekeza benki hizo kwenda kwenye maeneo hayo mahsusi ili kununua zao la alizeti na vitunguu.

Swali la pili, swali la pili, je, Waziri yuko tayari kufuatana na mimi kwenda kuona wakulima wa vitunguu ambao sasa wanavuna ili aweze kutoa maelekezo ya upatikanaji wa mbegu bora na pembejeo kwa haraka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nikianza na lile swali lake la nyongeza la (b) kwanza niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda katika Jimbo lake la Iramba Mashariki ili kujionea hilo.

Vilevile ni kwamba Serikali sasa hivi tunaimarisha tafiti zetu kuhakikisha kwamba tunapata mbegu ambazo zitakuwa bora na za uhakika na za bei nafuu tukishirikiana na wakala wetu wa mbolea.

Mheshimiwa Spika, pia tuko katika awamu ya mwisho ya kufanya tafiti ya mbegu tatu za alizeti na zenyewe hizo tafiti hatua ya mwisho tunategemea mwakani tutaanza kutumia.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye swali lake la (a) ni kwamba lengo la Benki ya Kilimo ni kuhakikisha kabisa kwamba Wilaya zote za Tanzania wanapata mikopo kupitia Benki hii ya Kilimo na kama nilivyosema kwa kujibu katika swali langu la msingi Benki ya Kilimo riba yake ni asilimia nane mpaka 14 kitu ambacho ni masharti nafuu. Vilevile unalipa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, pia Benki ya Kilimo tumeigawa au imegawa kwa Kanda Nane na Mkalama iko katika Mkoa wa Singida na Mkoa wa Singida uko katika Kanda ya Kati kwa maana hiyo na yenyewe iko katika huo mpangilio.

Mheshimiwa Spika na vile vile Benki ya Kilimo ni kwamba inawafuata wakulima kule waliko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaenda Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki swali la Mheshimiwa saada Mkuya Salum, Mbunge wa Welezo. Kwa niaba yake Mheshimiwa Khadija Nassir.

Na. 93

**Kuunganisha *Diaspora* na Shughuli za  
Maendeleo ya Kijamii**

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI (K.n.y MHE. SAADA MKUYA  
SALUM)** aliuliza:-

Serikali nyingi duniani zinaunganisha *diaspora* katika mikakati yao ya kukuza uchumi na huduma za kijamii.

(a) Je, Serikali imefanya mikakati gani ya kuunganisha *diaspora* katika shughuli za kukuza uchumi na huduma za kijamii?

(b) Je, ni kwa kiasi gani *diaspora* imechangia uchumi wa nchi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
(K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA  
AFRIKA MASHARIKI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mbunge wa Welezo, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inatambua umuhimu wa *diaspora* katika kuleta maendeleo hapa nchini kupitia utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021. Kuelekea uchumi wa kati *diaspora* ni moja wa wadau. Ili kutekeleza jukumu hili Serikali imeweka mikakati ifuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa katika kila eneo lenye uwakilishi wetu Ubalozzi unawatambua Watanzania wanaoishi katika maeneo hayo pamoja na Watanzania hao kuunda Jumuiya zao.

(ii) Kupitia ziara za viongozi pindi wanapokuwa nchi za nje Serikali imehakikisha kuwa, kunakuwa na utaratibu wa viongozi kukutana na *diaspora* wa Tanzania ili kuwaeleza masuala yanayotokea nyumbani, hasa fursa za kiuchumi na uwekezaji.

(iii) Serikali imekuwa ikiratibu zoezi la kuwakutanisha *diaspora* na wadau wa hapa nchini na nje kupitia makongamano, ambapo kumekuwa na jitihada, mijadala yenye tija katika maeneo ya uchumi na maendeleo kwa ujumla.

(iv) Wizara imeunda timu ya kufanikisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya *diaspora* itakayoainisha mikakati na kutoa miongozo kuhusu ushiriki wa *diaspora* katika kuchangia maendeleo nchini.

(v) Wizara imeelekeza Balozi zetu kusajili Watanzania waliopo katika maeneo yote ya uwakilishi na kuainisha shughuli wanazozifanya, taaluma na ujuzi walionao, ili kusaidia kuwa na takwimu sahihi na kuhusu *diaspora* wetu na kuweka mazingira wezeshi ya kuchangia maendeleo nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, *diaspora* wetu wamekuwa wakichangia uchumi wa nchi yetu kupitia uwekezaji katika sekta mbalimbali kama biashara, afya na elimu, kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, yaani 2013 hadi 2017, *diaspora* kwa ujumla wao walituma nchini kiasi kisichopungua dola za Kimarekani milioni 2282 ikiwa ni wastani wa dola milioni 455 kwa mwaka.

(ii) Jumla ya nyumba 108 za Shirika la Nyumba la Taifa zilinunuliwa na *diaspora* wetu.

(iii) Mnamo mwezi Julai, 2017 tulipokea Madaktari wa Kitanzania waliopo Marekani, Dakota ambao walikuja kutoa huduma bila malipo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja iliyopo Zanzibar.

(iv) Katika kipindi cha mwaka 2015/2017 timu ya Madaktari wa Kitanzania waishio Marekani, kupitia Taasisi ya Afya ya Elimu na Maendeleo – *Head Incorporated*, walitoa huduma za afya na matibabu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar na kukabidhi dawa na vifaatiba vyenye thamani ya dola 459,075; msaada wa mashine ya kupimia saratani ya matiti katika Hospitali ya Lugalo Dar es Salaam yenye thamani ya dola 200,000; huduma za matibabu ya ushauri na ushauri katika Hospitali ya Mwananyamala Dar es Salaam na Hospitali ya Mnazi Mmoja iliyopo Zanzibar, kukabidhi msaada wa vifaatiba vyenye thamani ya dola 300,000.

(v) Jumuiya ya Watanzania nchini Marekani Dakota iliandaa jukwa la afya lililofanyika nchini humo mwezi Novemba, 2017 ambapo walialika taasisi mbalimbali zinazohusika na masuala ya afya kutoka hapa nchini ili kupeana ujuzi na uzoefu walioupata Marekani katika kipindi wanachoishi na kufanya kazi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika masuala hayo.

(vi) *Diaspora* wa Kitanzania waliopo Bujumbura walitafuta soko la bidhaa za wajasiriamali wa Kitanzania walioshiriki katika maonesho ya Juakali yaliyofanyika mwezi Disemba, 2017. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Nassir swali fupi la nyongeza.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, *diaspora* kwa umoja wao wamekuwa wakipigania kurudi nyumbani kufanya kazi. Tangu Awamu ya Tano ianze ni *diaspora* wangapi wameajiriwa katika sekta ya umma ili kutumia ujuzi wao katika kuisaidia Serikali?



Swali langu namba mbili, ni jinsi gani Serikali inawapa fursa *diaspora* katika uchumi wa viwanda? Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yanayohitaji takwimu za papo kwa papo huwa tunaya-*discourage* kidogo kwa sababu Waziri hawezi kutembea na takwimu.

Mheshimiwa endelea kujibu hilo swali la pili.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosikia swali ni kama moja hasa kwamba ni namna gani Serikali imejipanga kutoa fursa kwa ajili ya *diaspora* wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya makongamano ya mara kwa mara na *diaspora* ili kuweza kuwaonesha fursa zilizopo waweze kuwekeza nchini kwa sababu tunatambua *potential* kubwa iliyopo kwa *diaspora* kama ilivyo katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa kutambua umuhimu na *potential* ya *diaspora* wetu Serikali sasa iko mbioni kuja na sera mahsusi ya *diaspora* ili kuweza kuweka mazingira mazuri ya namna ambayo wanaweza kushiriki katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari kuna mipango inaendelea na *diaspora* tayari wameshaanza kuwekeza katika maeneo mbalimbali. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. swali la mwisho kwa siku ya leo la Katiba na Sheria linaulizwa na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo.

Na. 94

### Hukumu za Kutozwa Faini

**MHE. JOSEPH R. SELASINI** aliuliza:-

Wapo wananchi wengi waliotuhumiwa na kushtakiwa katika Mahakama tofauti na kutozwa faini na baada ya kulipa faini hizo wakakata rufaa Mahakama za juu kulalamikia hukumu hizo na Mahakama za juu zikawaona hawana hatia.

(a) Je, Serikali inayo kumbukumbu ya taarifa za wananchi wa namna hiyo?

(b) Na kama Serikali inazo taarifa hizo, je, ni lini wananchi hao watarejeshewa fedha zao?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inazo kumbukumbu zote na taarifa za wananchi wanaolipa faini na baadae kushinda rufaa za kesi zao na hivyo kustahili kurejeshewa faini walizotoa kwani mashauri yote na hukumu zinazotolewa kumbukumbu zake zinatunzwa na Mahakama. Urejeshaji wa fedha hutegemea upatikanaji wa nyaraka zinazothibitisha malipo ya faini kupokeleawa na uwepo wa nakala ya hukumu kwani mara nyingi rufaa inaweza kuwa imetolewa baada ya muda mrefu tangu hukumu ya kwanza kutolewa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumiwa na Mahakama ni kuwasilisha hazina nyaraka husika kwa ajili ya uhakiki na uidhinishwaji wa malipo kabla ya fedha zao kurejeshwa tena Mahakamani ili mwananchi husika aweze kulipwa. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya shilingi 60,152,487.65 zililipwa na

Mahakama kama fidia kwa mashauri 16 yaliyohakikiwa na kuthibitishwa na Mahakama baada ya kupokea fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, madai 24 yenye jumla ya shilingi 87,046,649.38 yameshachambuliwa na kuwasilishwa Hazina na tayari yanasubiri malipo na wakati huo huo jumla ya madai 12 yenye thamani ya shilingi 6,920,000 miongoni mwao yakiwemo madai mapya yamewasilishwa Hazina. Mara uhakiki utakapotengamaa na Mahakama kupokea fedha kutoka Hazina malipo hayo yatafanyika bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, kama kuna mtu yeyote ambaye amecheleweshewa malipo yake nashauri awasiliane na Wizara au Mahakama ili kutatua tatizo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini nilikuona.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri haya ya kaka yangu Profesa Kabudi, nina maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi sana wanakosa haki zao, kwanza kwa kutojua kwamba wanapaswa kudai fedha zao walizolipa kama faini baada ya kushinda kesi na pili kwa sababu nakala za hukumu *custodian* wake ni Mahakama yenyewe.

Je, Serikali haioni kwamba kwa kutotoa maelezo kwa hawa warufani wakati rufani zao zikiwa zinasomwa kwamba wanatakiwa wafuatilie zile faini walizolipa baada ya kushinda, Serikali haioni kwamba inawadhulumu na au inaendelea kuwaadhibu kutokana na kutowarejeshea fedha zao?

Swali la pili, kwa kuwa Mahakama huwa inatoa muda maalum wa kukata rufaa na mtuhumiwa yule anapokata rufaa Mahakama inakuwa inajua. Je, ni kwa nini Mahakama inapokea fedha zile isiziingize kwenye akaunti ya akiba kwa ajili ya kusubiri rufani itakapoamuliwa na badala yake

inaingiza kwenye akaunti ya mapato na hivyo kusababisha fedha zile zinatumika, zinapohitajika inakuwa shida kupatikana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Profesa Palamagamba Kabudi tafadhali.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, moja ni kweli inawezekana wananchi wengi hawafahamu kwamba mara baada ya kuwa wameshinda rufaa zao wana haki ya kurejeshewa faini ambayo walikuwa wamelipa. Kwa hiyo, Wizara pamoja na Mahakama tutafanya jitihada kutoa elimu na maelezo kwa wananchi kwamba mara wanapokuwa wameshinda rufaa zao za mwisho basi waweze kufuatilia malipo ya rufaa zao kwa sababu ni haki yao. *(Makofi)*

Kuhusu swali la pili, kwa kuwa utaratibu wa Serikali ni kwamba, faini zinachukuliwa kama maduhuli na zinakatiwa risiti ya Hazina, basi jambo hilo tutakaa na Hazina ili tuweze kuona utaratibu unaoweza kutumika ili kuhakikisha kwamba malipo ya faini yanarejeshwa kwa haraka iwezekanavyo ili wananchi ambao wamelipa fedha hizo waweze kuzipata hela zao kwa wakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umeisha na maswali ya leo pia yameisha.

Waheshimiwa Wabunge, tunapoendelea na shughuli zetu hapa ndani mnaongea sana, hata ninyi wenyewe mkisikilizana mtaona tu. Ni vizuri kupunguza sauti ili shughuli nyingine nazo ziweze kuendelea. Mwenzako mwingine anataka kusikiliza kinachoendelea wewe unongea, inakuwa haipendezi kila wakati kuwaambia jamani tusikilizane, jamani tusikilizane. Kwa hiyo, naomba tupunguze sana sauti tunapokuwa tunawasiliana sisi kwa sisi.

Jambo la pili, maswali yawe mafupi na maswali ya nyongeza yawe mafupi, pia majibu ya upande wa Mawaziri yawe mafupi kwa sababu tuna saa moja tu kwa maswali

kumi ambayo ni wastani wa dakika tano, sita kwa muuliza swali kusimama, kwa Serikali kujibu, kwa swali la msingi na kwa swali la nyongeza. Sasa ukizitazama hapo maana yake ni wastani wa dakika mbili kwa kila kimojawapo. Kwa hiyo, ukisoma majibu kurasa mbili, kurasa tatu kwa kweli, tunaumia. Wakati wa maswali tuna utaratibu ambao yanatangazwa *live*, kwa hiyo, tuna makubaliano ya muda halisi wa nini cha kufanya kwa wakati huo. Nawaombeni Waheshimiwa Mawaziri mzingatie hilo kwenda kwenye jibu moja kwa moja bila kurembaremba na wauliza maswali na sisi tujitahidi kuuliza swali moja kwa moja. Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, nina wageni katika *gallery* ya Spika ambao ni Balozi wa Iran nchini Tanzania, Ndugu Mussa Farhan, lakini pia amefuatana na Waheshimiwa Wabunge watano kutoka Bunge la Iran. Karibuni sana Mheshimiwa Balozi na Wabunge wa kutika Iran. Iran ni nchi rafiki sana kwa Tanzania na mimi kwa niaba yenu nimeshafika katika Bunge la Iran na wakatupokea kwa upendo mkubwa sana. (*Makofi*)

Walipotualika wao wana utaratibu ambao nadhani Waziri wa Katiba na Sheria ni vizuri ukauangalia, Rais wao wa nchi akishachaguliwa anaapishwa ndani ya Ukumbi wa Bunge, kwa hiyo, nilialikwa kushuhudia hilo. Kwa hiyo, nasi badala ya kwenda Uwanja wa Taifa ni vizuri ikawa ndani ya nyumba. Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni tulionao leo waliopo Jukwaa la Spika pia ambao ni wageni wa Mheshimiwa January Makamba - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ni Mhandisi Joseph Malongo - Katibu Mkuu, karibu sana Katibu Mkuu; Ndugu Butamo Philip - Naibu Katibu Mkuu, karibu; Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *NEMC* - Dkt. Vedasto Makota, karibu sana; Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira - Ndugu Ali Mafuruki, karibu kama upo; wameongozana na wageni wawili kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambao ni Mkurugenzi Uratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar - Ndugu Khalid Bakari Amran

na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili Zanzibar - Ndugu Abdallah Hassan Mitawi. Pia wameambatana na Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais. (Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni mgeni wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaye ni ndugu yake kutoka Mkoani Dodoma, Ndugu Suraiya Nyamkunga, karibu. Pia kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni viongozi wa Chama cha Wafanyabiashara wa Pikipiki na Bajaj kutoka mkoani Dar es Salaam, karibuni. Wageni watatu wa Mheshimiwa Nuru Bafadhili ambao ni familia yake kutoka Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjari, wako kule, karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mussa Ntimizi ambao ni wakulima wa kutoka Igalula, Mkoa wa Tabora, karibuni sana Wanyamwezi ninyi. Kuna wageni tisa wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambao ni wawekezaji katika viwanda vya dawa za binadamu pamoja na hospitali kutoka Afrika Kusini kwa kushirikiana na wawekezaji wa ndani wa Hospitali ya Uhuru, Mwanza. Wageni wetu kutoka *South Africa* karibuni popote pale mlipo. (Makofi)

Wageni 36 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, ambao ni Wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Gonda, Wanamaombi wako pale, karibuni sana, mtuombee ndugu zangu. Pia kuna wageni 27 wa Mheshimiwa Felister Bura ambao ni Wanakwaya ya Waadventista Wasabato kutoka Dodoma wakiongozwa na Mchungaji David Mbagha, karibuni sana wanakwaya. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Sebastian Kapufi ambao ni wafanyakazi wa mradi wa *Advance Family Planning* ya Jijini Dar es Salaam na *Partners in Population and Development* ya Mjini Kampala, Uganda, karibuni sana wako pale. Wapo wageni 31 wa Mheshimiwa Juma Nkamia ambao ni Jumuiya ya Wanafunzi kutoka Kondo na Chemba wanaosoma Chuo Kikuu cha

Dodoma wakiongozwa na Ndugu Lucas Masiru, karibuni sana na hongereni sana. (*Makofi*)

Pia, mgeni wa Mheshimiwa Aeshi Hillary ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Vijana wa CCM Taifa anayewakilisha Mkoa wa Rukwa, Ndugu Nyansio Dismas Gregory, karibu. Pia tuna wanafunzi 22 kutoka Taasisi ya Ustawi wa Maendeleo ya Jamii iliyoko Ihumwa, Mkoani Dodoma wakiongozwa na Ndugu Emilian Mathew, karibuni sana. (*Makofi*)

Tangazo la jumla kwa Waheshimiwa Wabunge wote tunawatangazieni kuhudhuria Ibada katika Ukumbi wa *Pius Msekwa Chapel*, orofa ya pili, leo siku ya Jumanne Tarehe 17 Aprili mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge, saa saba Mchana mchana. Katika ibada hiyo kutakuwa na Mtumishi wa Mungu, Mchungaji David Mbaga wa Kanisa la Wasabato. Waheshimiwa Wabunge, baada ya saa saba hapa wale wa imani ya Kikristo karibuni pale *Pius Msekwa Chapel* kutakuwa na ibada maalum. Tuna mgeni Mchungaji David Mbaga wa Kanisa la Waadventista Wasabato atakuwa anatoa huduma ya neno pale. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba, Tarehe 12 Aprili, Mheshimiwa Mwita Waitara aliomba mwongozo wa Spika akilalamikia kitendo cha Bunge kuwaondoa Watumishi waliokuwa wamepangwa kuhudumia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na akaeleza kwamba, watumishi hao walikuwa ni wa mkataba na kuwa baada ya mikataba yao kuisha hawajaruhusiwa kuendelea na huduma katika Kambi hiyo na ilidaiwa na Mheshimiwa Mwita kwamba jambo hilo limesababishia Kambi hiyo usumbufu mkubwa na imekuwa kikwazo kwa Kambi hiyo kuwasilisha hotuba za bajeti mbadala za upinzani na nyaraka nyingine muhimu zinazoandaliwa na kambi hiyo kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni.

Nilikuwa nauliza kama leo kwenye hii Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kama kuna Hotuba ya Upinzani nimeambiwa hata leo haipo pia. Kwa hiyo, ni hotuba ya

tatu mfululizo haipo na sababu yake inavyoelekea ni hiyo ya kwamba hakuna watumishi wa kuandika hotuba hizo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo akauliza kwa nini Ofisi ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina watumishi hao, lakini pia akauliza je, itahudumiwaje? Tatu, Spika aseme je, Kambi Rasmi ya Upinzani imefutwa Bungeni na nne, kwa nini Kiongozi wa Upinzani Bungeni hana gari?

Nianze na hili rahisi zaidi la gari ni kwamba gari analo na lipo hapa kwenye *compound* ya Bunge. Pana jambo tu la kiofisi la ndani ya kwamba dereva aliyekuwa anaendesha gari hilo ni mstaafu, kwa hiyo alitakiwa abadilishwe, sasa pamekuwa kidogo na sintofahamu ya nani aendesha gari hilo ni mambo ya ndani. Mambo mengine Mheshimiwa Mwita Waitara siyo vizuri sana kila kitu tukijadili hapa, vitu vingine ni vya kuulizana tu kwenye *corridor* huko tunafafanua.

Dereva huyu ni dereva ambaye alistaafu wakati Mzee Sitta akiwa Spika, akapewa mkataba, nadhani wa mwaka mmoja na ameendelea kupewa mikataba miaka mitano ya Mama Makinda na miaka miwili ya mimi nikiwa hapa, unaweza ukahesabu karibu miaka nane au zaidi, baada ya miaka 60. Kwa hiyo, kwa kweli tumevumilia vya kutosha sasa ni wajibu kwamba apumzike. Kwa hiyo, sioni kama kuna haja tena ya malumbano ya kwamba endelea, aendelea.

Ni mtu mzima sasa, ni vizuri kama akafanya kazi kwa mkataba binafsi kwa mtu huko, hilo ni suala lingine, lakini kiserikali haiwezekani tena. Kwa hiyo lazima apatikane dereva mwingine, na madereva wapo. Kwa hiyo, sidhani vitu kama hivyo Mheshimiwa Mwita vinahitaji sana kuvileta kwenye uwanja hapa. Kwa hiyo, gari lipo saa yoyote na madereva wapo kwa hiyo sidhani kama tunahitaji sisi kama Bunge kwa kweli kuzungumzia hilo la gari.

Kuhusu watumishi, hili tunaliangalia upya, ni kwamba tuna kambi mbili, tuna kambi ya Chama Tawala na tuna Kambi Rasmi ya Upinzani. Chama Tawala wamekuwa na watumishi watano wanaowaleta wao wenyewe kwenye ofisi



ya CCM ya kwao hapa bungeni, na tumekuwa tukiwapa mikataba ya muda mfupi, walipata miaka miwili na nusu na sasa ilitakiwa utaratibu huo kama utaendelea au hautaendelea wapate mkataba wa miaka miwili na nusu, na Kambi ya Upinzani ni hivyo hivyo pia, wao walikuwa na watumishi wanne ambao vilevile nao ni kwa mkataba wa muda sasa mkataba ule umeisha uliishia Disemba, 2017.

Tunaangalia kama kuna haja ya kuendelea na utaratibu huo, inatupa ugumu kidogo kufanya mambo haya kwa sababu nyingi tu, baadhi za kiusalama kutokana na majengo yetu haya na hali halisi inavyoendelea duniani hivi sasa, lakini pia kuangalia kama vyama vya siasa vinaweza kuleta watu wao wakaajiriwa na Bunge hata kama ni kwa mkataba iwe Kambi Rasmi au ya upande wa Chama Tawala au ya Upinzani, halafu vyama vingine kama kina Mheshimiwa Zitto yuko peke yake yeye haleti mtu yeyote na yeye anahitaji vilevile msaada, misaada hiyo hiyo ya kufanyiwa utafiti, watu wa kuwatumia kufanya hiki na kile, kwa hiyo inaleta *inbalance* fulani ambayo haijakaa sawasawa.

Kwa hiyo jambo hili tunaliangalia, tunadhani kwa sasa mawazo yetu ni kwamba ni vizuri watumishi wa aina hiyo wasiwepo. Kwa hiyo, hata watumishi wa CCM nao wameshafungasha virago, hawapo na watumishi wapinzani hawapo. Kwa hiyo, kuendelea kugoma kuleta hotuba kwa kisingizio cha kwamba hatuna wa kutuandikia, maoni yangu ni kwamba tunajishusha kidogo Wabunge sisi, naamini kabisa tunaweza kuandika hotuba zetu, kwa hiyo tuandike hotuba zetu. (*Makofi*)

Kama kuna hoja za msingi sana na kwamba lazima tuandikiwe basi tuna vikao vyetu vingine tunaweza tukavizungumza huko ndani. Nia yangu tusianzishe mjadala mwingine waadaka huko kwamba tuna aina ya Wabunge ambao hawawezi hata kuandika hotuba zao wenyewe.

Basi huo ndio mwisho wa maelezo yangu kuhusu swali la Mheshimiwa Mwita Waitara. Kama hakuna Mwongozo tuendeleo.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Haya Katibu nisomee majina, nitajie.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Paresso, Mheshimiwa Mwambe na Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mimi Gekul siyo Paresso.

**KNDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** *Oh! Sorry* Mheshimiwa Gekul.

### MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Anza Gekul. Dakika chache chache sana kwa sababu muda hatuna Waheshimiwa, *straight* unataka kusema nini.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, mimi naomba mwongozo wako kwa kanuni ile ile ya 68, naomba nisiisome, lakini naomba mwongozo wako juu ya kanuni ambazo zinaendesha Bunge letu; nazo ni kanuni ya 103 na 104. Naomba tu nisome, kwamba; kanuni ya 103(1) na (2) halafu nitasoma kanuni ya 104 (2). Zinasema; “Kwa kuzingatia utaratibu wa majadiliano uliowekwa na kanuni hizi Mbunge yeyote anaweza kuomba ufafanuzi au maelezo zaidi katika kifungu chochote cha fungu linalohusika wakati kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi. Vilevile Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja ya kuondoa shilingi moja katika kifungu chochote cha fungu hilo.”

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 104 (2) inasema hivi; “Iwapo zimesalia dakika 10 kabla ya kumaliza muda ulioongezwa chini ya fasili ya moja na Kamati bado haijamaliza kupitisha mafungu yote Mwenyekiti atafunga mazungumzo yanayoendelea na papo hapo atawahoji Wajumbe kuhusu mafungu yaliyosalia kama yapo.”

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Mwongozo wako, naamini kwamba wakati Bunge tunapokaa kama Kamati ya Matumizi tunazingatia kanuni hizi, lakini kwa bahati mbaya sana sijui ni tunakosea Wabunge wakati wa kupanga ratiba yetu hatutengi muda wa kutosha kwa ajili ya kuhoji mafungu. Hili limekuwa likijitokeza kila mwaka kwa kila bajeti. Bajeti muhimu kama Wizara ya TAMISEMI, kama jana tulikuwa tunahitimisha Waheshimiwa Wabunge wengi hatukupata nafasi, lakini imekuwa ikitafsiriwa kwamba mtu anaweza akatoa tu shilingi kwenye mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwenye vifungu vingine mtu hawezi akatoa shilingi na akapata ufafanuzi wa hoja yake kwa madai ya kwamba muda umekuwa mdogo, lakini pia haizingatiwi sana. Hata hivyo, kubwa ambalo nilihitaji kupata ufafanuzi kutoka kwako ni suala ambalo limetokea jana wakati tuko kwenye Kamati ya Matumizi. Aliyekuwa anaongoza kikao hicho Mheshimiwa Naibu Spika kidogo alileta kitu ambacho ni kipya kwangu, sijui kwa wengine, kwamba hatukutakiwa kuhoji mafungu mengine yaliyoendelea baada ya mshahara wa Waziri kukamilika na hususani kwenye mikoa yetu.

Mheshimiwa Spika, kimsingi kanuni ilikuwa inaruhusu na hata kama muda ulikuwa umeenda nilitegemea kwa mujibu wa kanuni hii ya 104(2) alitakiwa aende kwenye *guillotine*, ahoji kwa ujumla tumalize biashara pale na si kwenda mkoa kwa mkoa, kifungu kwa kifungu mpaka *development* lakini haturuhusiwi kuhoji.

Mimi nikuombe kuna kanuni zingine tofauti na hizi au ni hizi? Kama ni hizi tunazozitumia naomba mwongozo wako kwa haya ambayo yametokea jana; tumeshindwa kuhoji masuala muhimu ambayo tunahitaji kupata ufafanuzi. Mimi nilibomoka (niliuliza) hapa maswali ya *standya* Babati nilitaka kuhoji lakini hatukupewa nafasi.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimwa Gekul kwa sababu ya muda tumeshakuelewa hilo tutalitolea ufafanuzi kwa wakati muafaka kadri tunavyoendelea. Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi nilikuwa naomba Mwongozo kupitia hiyo hiyo kanuni ya 68(7) juu ya jambo ambalo umelitolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, ninaheshimu sana maamuzi yoyote yale ambayo unayatoa ndani ya Bunge lako tukufu, lakini nilitaka nitoe ufafanuzi ambao ndio utautolea mwongozo baadae; kwamba sisi kama Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunashindwa kuandika hotuba kwa sababu hotuba zinazoandikwa na Serikali zinaandikwa na wataalam kwa kipindi kisichopungua miezi sita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wao wanakaa miezi sita wanawaandikia, hotuba zile haziandikwi na Mawaziri, hakuna Waziri anakaa kwenye *computer* kuchapa. Sisi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wale watumishi wanne wako kikanuni. Ukisoma Kanuni za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambazo zimekasimiwa na Kanuni za Bunge zima zinaruhusu Kambi kuwa na watumishi ambao watafanya kazi kwa niaba ya kambi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watumishi wanne wale si watumishi wa CHADEMA wala si wa *CUF* wala si wa *ACT* wala *NCCR Mageuzi*, ni wa kambi, kama *caucus* yetu. Ingekuwa ni wa CHADEMA *I would agree* na ndiyo maana sisi tukawa tunajuliza hawa watumishi wanaoenda kwenye kambi ya CCM kwenye *majority* wanafanya kazi gani? Kwa sababu kazi yote inaandikwa na watumishi wa Serikali. Waziri anakuja hapa kuwakilisha. (*Makofi*)

Sasa changamoto tunayoipata hebu *imagine* mbunge ambaye anakaa hapa kuanzia saa tatu asubuhi mpaka saa mbili usiku, halafu arudi kesho ana hotuba akachape hotuba usiku kucha halafu aje ai-*present* hapa; hebu tuoneeni huruma kwenye hili jambo. Kwa sababu *request* yetu ni hao watu wanne watakaotusaidia kuchapa na kuandika hotuba na kufanya tafiti kwa ajili ya Kambi nzima, na wale siku zote ndio tumekuwa tukiwatumia sisi kama Kambi. Kwa hiyo, ukiwaondoa kwa kigezo tunawaondoa watu wa CCM kwa hiyo tuwaondoe na watu

wa Upinzani hapo mnakuwa hamjatutendea haki kama Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na sisi tungependa kuwawakilisha watu wachache kupitia Bunge lako tukufu kwa maoni yetu ya sisi ambao tuko kwenye Kambi Rasmi. Kwa hiyo ningepomba kwa hekima zako suala la Kambi Rasmi ungeliangalia kwa namna nyingine kama ambavyo kanuni zetu zinatungoza. Usiliangalie kama ambavyo, na sisi ni watu wa mfumo wa Mabunge ya *Commonwealth* ninajua wewe una busara sana na hekima kwenye hili tunaomba utusaidie na kwa kufuata kanuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba Mwingozo wako.

**SPIKA:** Hili nianze nalo nianze nalo sasa hivi. Kama nilivyosema bado ni eneo ambalo tunalitazama vizuri na tutalitazama vizuri zaidi katika vikao vyetu vya Kamati. Hata hivyo hoja za kuchapa na nini tunakuwa na masekretari wa Bunge ambao wapo *full time including* kwenye ofisi hiyo ya upinzani wapo kabisa na vifaa vipo. Tukumbuke pia kwamba Waheshimiwa kazi zetu kimsingi zinafanywa ndani ya Kamati mbalimbali, ambapo ndani ya Kamati hizo wamo Chama Tawala na Upinzani. Halafu kutokana na kazi zile kwenye kamati Serikali inapoleta jambo kamati inaandika maoni yake. Kamati inapoandika maoni yake inakuwa na Wabunge wa Chama Tawala na Wabunge wa Upinzani kwa pamoja.

Hata hivyo katika demokrasia hii upinzani bado wana nafasi nyingine ya kuandika hotuba yao mbadala kuhusu mambo yaleyale yaliyozungumzwa kwenye Kamati na wanakuja kuyasoma hapa. Hawa wanaoandika maoni haya, hawa vijana wala hawahudhuri kwenye kazi za Kamati. Kwa hiyo wakati mwingine hata hotuba inakuja kusomwa hapa inakuwa yaani iko *out of context* kwa sababu ya..., lakini niseme ni jambo ambalo tutalizungumza katika vikao mbalimbali linahitaji uchambuzi mpana zaidi na kuweza kuliangalia kwa undani zaidi. (*Makofi*)

Mimi ningewashauri muendelee tu kusoma hotuba wakati tukiendelea kulitazama jambo hili kwa sababu haisaidii sana kwa kweli kuendelea kugoma kwa ajili ya jambo hili, tutaendelea kulizungumza Mheshimiwa Silinde. Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nimesimama kwa Kanuni ya 68 (7) pamoja na 46 nikiomba Mwongozo wako kutokana na suala lililotokea leo mapema hapa ndani.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo akijibu swali namba 91 aligusia kidogo masuala ya korosho ambayo kimsingi wakati Serikali inatoa kauli yake mwaka jana na mwaka juzi pia wakati wa kikao cha wadau wa korosho ambacho ni muhimu sana kwenye sekta nzima ya korosho kinachofanya maamuzi kuhusiana na mambo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na masuala ya uagizaji wa pembejeo, magunia na vitu vingine. Lakini leo wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu amesema kwamba wakulima watalipwa pesa zao mwisho wa mwezi huu, wale ambao hawakulipwa kutokea mwezi wa 11. Wakati wa kile kikao Serikali yenyewe ilitoa ahadi kwa wakulima hao ikiwaambia kwamba ndani ya siku saba watakuwa wamelipwa pesa zao zote baada ya kufanyika mnada uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba Mwongozo wako ili tupate kauli ya Serikali, wamebadilisha ule utaratibu au kwamba kuna makosa yaliyotokea kiasi kwamba wale wote ambao wamesababisha haya wachukuliwe hatua ili hawa wakulima waweze kuendelea kuandaa mashamba yao badala ya kutuambia watalipa mwisho wa mwezi huu ikiwa Serikali yenyewe iliahidi italipa ndani ya siku saba.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako ili watu waweze kuelewa hii sintofahamu inayotokea, na inaleta shida sana kwa wakulima kwa sababu hawafahamu stahiki zao, na madeni ya wakulima hawa yamekuwa mengi kwa muda mrefu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe lazima nikiri kabisa yaani sijakuelewa kabisa, kwa sababu kama Serikali iliahidi kwamba italipa baada ya siku saba, lakini sasa wamesema mwezi huu wanalipa sasa ugomvi wa nini? Yaani swali lako liko wapi.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nilichokuwa najaribu kukisema ni kwamba kutokana na utaratibu ambao Serikali yenyewe ilijiwekea na kua hidi wakulima kwamba kila baada ya mnada mmoja watakuwa wanawalipa wakulima pesa zao ndani ya siku saba kutoka siku ya mnada uliopita. Kwa mfano kama mnada utafanyika Ijumaa tunategemea mpaka mnada unaofuata Ijumaa inayofuatia maana yake wakulima wale watakuwa wamelipwa pesa zao. Jambo hili lingekuwa lifanyike mwezi wa 11 au 12 mwaka jana, lakini leo Serikali inasimama tena na kusema watawalipa mwisho wa mwezi huu, waliosababisha hili tatizo wamechukuliwa hatua gani? Ndilo suala letu sisi la msingi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kama kuna ufafanuzi kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba tu nitoe ufafanuzi kwamba kwanza Serikali haidaiwi na wakulima, yaani ni picha isiyo sahihi kabisa kusema kwamba Serikali inadaiwa na wakulima. Serikali haidaiwi na wakulima. Serikali inachokifanya ni kusimamia fedha ya wakulima ipatikane kutoka kwa wale walioidokoa. Kwa hiyo, sisi tunachokifanya ni kuchukua hatua kwa vyama vikuu vilivyohusika na ku-*transact* zile pesa, tunawasukuma vyama vya msingi (*AMCOS*) ambao wao wali-*miss manage* hizo pesa ili hii pesa ipatikane wakulima wanaostahili kupata hizo pesa wapate.

Mheshimiwa Spika, mwanzo mwaka jana walikuwako vyama kadhaa na wakulima kadhaa ambao fedha yao ilikuwa haionekani, imekuwa *miss-managed* katika taratibu za malipo. Kwa hiyo, wale ndio walikuwa wameahidi kwamba utaratibu unafanyika wa kuzi-*collect* ili

zipatikane, na sisi tukatoa kauli kwamba ahadi tuliyopewa na hawa wahusika ni tarehe fulani tukasema hivyo. Sasa hili jambo msimu huu tena limeendelea kujitokeza tu. Katika ushirika kule watu wasio waaminifu wanachukua hizi pesa wanafanya matumizi mengine au wanapeleka kwa mtu mwingine halafu aliyestahili hapati. Mkianza kuzi-*trace* ndipo mnakutana na hizi ahadi kwamba hizi fedha tutakuwa tumesha-*reconcile*, zitapatikana *say* mwanzoni mwa mwezi Aprili, na sisi tunapeleka hiyo habari kwa wakulima *accordingly*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba tu kwanza tuelewane vizuri kwamba Serikali haidaiwi, wakulima wenyewe ndio wanafanyiana mambo ya kijanja kijanja kule *through* uongozi wao wanaibiana hizo pesa. Sisi wahusika kwanza tumewapeleka mahakamani, wengine wamefilisiwa mali zao lakini ahadi zilizopatikana ni hivyo kama tulivyozisema.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana. Mheshimiwa Mbarouk kifupi sana.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa hii nafasi na mimi nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, umejibu wakati akizungumza Mheshimiwa Silinde hapa lakini mimi Mwongozo wangu unafanana katika suala hilo hilo. Labda Watanzania wamezoea kuona zinaposomwa hotuba za Bajeti ya Serikali ni kawaida tangu vimeanza vyama vingi kunasomwa hotuba za Bajeti za Upinzani.

Sasa leo hapa kwa maneno ambayo umeyasema kwamba kuna watumishi ambao walikuwa wanaingia kwa mkataba, sasa na wale walioletwa na CCM wameondolewa na wa Upinzani nao waondoke. Kutokana na uzoefu wako je, katika mabunge ya nchi ambazo zina vyama vingi wewe umeyatembelea utaratibu kama huu unafanyika au ni sisi Tanzania tunaanzisha jambo jipya? Naomba Mwongozo wako.



**SPIKA:** Hili jambo nishalimaliza mnanirudisha rudisha nyuma lakini, tena si utaratibu Mheshimiwa Mbarouk, nikishamaliza jambo hulifukui fukui, yaani sipendi sana kufunguka funguka kila wakati, ndiyo maana nikasema hebu kwenye vikao vingine vya ndani tukae tuzungumze tufunguke kidogo. Kuna watu wengine wanasema hata wale watumishi wa CCM hawakuwa na kazi, hapana walikuwa na kazi kubwa sana. Kwa sababu kazi yao mojawapo ya watumishi wale ni kufanya utafiti kwa ajili ya Wabunge ambao si mawaziri wala kitu kingine, na ni wengi kweli hao. Kuhudumiwa na watumishi watano kama ninyi mna watumishi wanne maana yake ni kwamba maana yake hapa tulivyo ni robo kwa robo tatu.

Kama ninyi mna watumishi wanne ilitakiwa huku wawe mara tatu ya wale wanne, kumi na mbili lakini bado walikuwa ni wachache. Kwa ujumla ni kwamba kwa sasa hawapo, tutakaa tutazungumza ikionekana kuna umuhimu huo itakuwa imeonekana hivyo, lakini kwa sasa hawapo, pande zote hawapo. Kwa hiyo, kama tunaendelea kutokusoma kama ndiyo uamuzi wa busara haya! Mheshimiwa Lubeleje mwisho kabisa, kifupi sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje mwisho kabisa na kwa kifupi sana.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dodoma na Singida tunalima sana mazao ya mchanganyiko alizeti, ufuta na karanga na iliundwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko, lakini Bodi ile inalegalega. Sasa naomba kauli ya Mheshimiwa Waziri ile bodi ipo ili kutusaidia Mikoa ya Dodoma na Singida kupata hiyo biashara yetu mazao yaweze kununuliwa na wafanyabiashara kuliko ilivyo sasa tu kila mmoja ananunua anavyotaka.

**SPIKA:** Ahsante sana, Bodi ya Mazao Mchanganyiko, kwa kifupi sana Mheshimiwa Waziri

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nitoe taarifa rasmi tu kwamba hii Bodi ya Nafaka na Mazao

Mchanganyiko ipo na inafanya kazi. Mheshimiwa Lubeleje namuomba avute tu subira tutakapokuwa tunawasilisha bajeti ya Wizara ataona ni kiasi gani cha fedha hii bodi imetengewa mwaka huu kwa ajili ya kuendesha shughuli zake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, tumemaliza masuala yote hayo. Sasa kabla hatujaendelea na shughuli zinazofuata, nimkaribishe Mheshimiwa Najma Giga ili aje aendelee na shughuli.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu!

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukukuru kwa kunipa heshima na fursa ya kuwasilisha Bungeni hapa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha unaokwisha na malengo ya Ofisi ya mwaka wa fedha unaokuja, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa kuendelea kuniamini kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira. Namshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kazi nzuri wanaoiofanya na kwa maelekezo mbalimbali wanayotupa katika kutekeleza majukumu yetu. Tunawapongeza kwa kazi nzuri ambayo imefanya mafanikio makubwa sana yapatikane katika uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano katika kipindi hiki cha miaka miwili na nusu. *(Makofi)*

Namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoitoa ambayo imetoa tathmini ya utekelezaji wa jumla wa masuala ya mipango, uchumi na utumishi Serikalini na malengo ya Serikali kwa ujumla kwa mwaka wa fedha unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge ukiwemo wewe kwa kazi nzuri mmnayoifanya kuliongoza Bunge letu. Napenda niwapongeze Wabunge wapya waliochaguliwa katika chaguzi zilizopita na kujumuika na sisi hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ndugu yangu Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, pamoja na Waheshimiwa wajumbe wa Kamati zote hizo kwa kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kutoa maelezo ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 na malengo ya mwaka wa fedha 2018/2019. Pia naomba kwamba hotuba tuliyoiweka mezani leo na iliyopo kwenye vitabu ndiyo

iingizwe kama rekodi ya Bunge (*Hansard*) na haya maneno ninayosoma ni muhtasari tu wa uwasilishaji wa hotuba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dira ya Taifa ya Maendeleo, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015 – 2020), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Malengo ya Maendeleo Endelevu, Sera ya Taifa ya Mazingira, Sheria ya Mazingira na maelekezo na miongozo mbalimbali inayotolewa na viongozi wakuu wa nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuzungumzia masuala ya Muungano; Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa kikatiba na kisheria ya kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano baina ya Serikali zetu mbili na pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokwisha, kazi zifuatazo zilitekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano, kuratibu vikao vya sekta vya masuala ya Muungano, kufuatilia utekelezaji wa masuala ya Muungano ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Pia tumeshughulikia kuratibu masuala yasiyo ya Muungano ili kuimarisha ushirikiano kati ya pande mbili, lakini vilevile tumetoa elimu kwa umma kuhusu masuala yanayohusu Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokwisha, Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ imeendelea kuzitafutia ufumbuzi hoja zilizobakia chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Makamu wa Rais. Mnamo tarehe 27 Novemba 2017, Ofisi ya Makamu wa Rais ilizikutanisha sekta za fedha, uchukuzi na biashara ili kuendelea kutafuta ufumbuzi wa hoja za sekta hizo. Katika sekta za fedha hoja kadhaa zilijadiliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao hicho hoja mbalimbali za sekta ya biashara zilijadiliwa ikiwemo upatikanaji wa fursa za masoko kwa bidhaa za Zanzibar kwa Tanzania Bara, miradi inayohusu maendeleo ya wajasiriamali, masuala ya viwango vya bidhaa hususan ushirikiano kati ya ZBS na TBS, usali wa viwango vya bidhaa vya Afrika Mashariki na fursa za miradi inayohusu maendeleo ya viwango vya ubora wa bidhaa. Pia kikao hicho kilizungumzia kuondoa vikwazo vya biashara kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, ushirikiano baina ya Mamlaka ya ZFDA na TFDA, lakini pia tulizungumzia kwa ujumla masuala yanayohusu leseni za viwanda na masuala yanayohusu hatimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililojadiliwa katika kikao hicho ni ushirikiano katika uhibitaji wa vyombo vya moto. Suala hili si jambo la Muungano, hivyo kila upande una sheria inayosimamia usajili wa vyombo vya moto. Lakini vilevile ilikubalika kwamba kila upande ufanye marekebisho madogo ya sheria zinazohusu usajili wa vyombo vya moto. Tayari maagizo haya yameanza kufanyiwa kazi na pande zote mbili za Muungano. Pamoja na kikao hicho, Ofisi pia iliratibu vikao vya kisekta vya kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Kamati ya Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kufuatia meli mbili zilizokuwa zikipeperusha bendera ya Tanzania kukamatwa na kukutwa na makosa zikiwa nje ya nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais iliratibu vikao mbalimbali vya pande zote mbili ili kulishughulikia jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa unaokuja, Ofisi yetu ya Makamu wa Rais itaendelea na uratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja pamoja na ufuatiliaji wa maelekezo mbalimbali yanayotolewa katika vikao hivyo, lakini pia yanayotolewa na viongozi wetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kufuatilia miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika pande

zote za mbili za Muungano kama tunavyotakiwa kufanya. Miradi hiyo inahusu sekta za elimu, afya, masoko, maji, miundombinu, mazingira, usafiri na usafirishaji. Tumeorodhesha miradi hiyo katika kitabu chetu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo kwa kiasi kikubwa imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato kwa wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea na jukumu lake la kufuatilia utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo zinazotekelezwa pande zote mbili za Muungano na kuhakikisha kwamba gawio la Zanzibar linapelekwa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mwaka wa fedha unaokwisha sekta za pande mbili za Muungano zimefanya vikao mbalimbali, sekta zisizo za Muungano. Sekta za viwanda na biashara walikaa tarehe 23 Agosti 2017 na tarehe 23 Machi, 2018. Sekta ya maliasili na utalii pia ilikaa, sekta ya ujenzi, uchukuzi na usafirishaji ilifanya vikao mbalimbali na sekta za kilimo kwa pande zote mbili pia zilifanya vikao. Vikao hivi ni mwendelezo wa jitihada zinazofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuhamasisha sekta zisizo za Muungano kukutana na kujadili masuala yanayohusu sekta zao, kubadilishana uzoefu na wataalam ili kupunguza changamoto, kuleta ufanisi na uwiano wa maendeleo kwa pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaopita, viongozi mbalimbali pamoja na wataalam walifanya ziara za kikazi kwa upande wa Zanzibar kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali zetu mbili. Vilevile Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa Kamati kadhaa na wenyewe walifanya ziara katika taasisi 11 na kampuni za simu kwa upande wa Tanzania Bara. Vilevile ziara za viongozi wengine wa kiserikali na kisiasa kwa pande zote mbili zilifanyika. Ziara hizo zilisaidia kubadilishana uzoefu, kupata

taarifa za utekelezaji wa changamoto za Muungano pamoja na kujifunza masuala mbalimbali ya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar tutapitia na kukamilisha mwongozo wa vikao vya ushirikiano vya kisekta kwa lengo la kuongeza ufanisi. Aidha, Ofisi yetu imejizatiti kuongeza idadi ya ziara za kikazi kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kuhusu Muungano ni moja ya changamoto kubwa hasa kwa vijana wa kizazi cha sasa. Ofisi yetu imeendelea kuelimisha umma kuhusu faida zinazotokana na Muungano kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Vilevile makongamano kadhaa yamefanyika yaliyohusisha vijana katika jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuelekea maadhimisho ya miaka 54 ya Muungano, Ofisi imefanya mahojiano na viongozi wakuu wastaafu, wananchi pamoja na kuandaa makongamano ya wanafunzi na warsha mbalimbali za wanafunzi hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka unaokuja, ofisi itaendelea kutoa elimu ya Muungano kwa makundi tofauti ya kijamii likiwemo kundi la vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkazo utatolewa katika kuandaa warsha na makongamano katika pande zote mbili za Muungano ili kuamsha ari kwa makundi haya juu ya umuhimu wa kuenzi, kuulinda, kuuimarisha, kuudumisha na kuuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu hifadhi ya mazingira. Sote tunajua kwamba sekta zote za uzalishaji mali zinategemea hifadhi ya mazingira. Hivyo rasilimali zitokanazo na mazingira zina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, shughuli zisizo endelevu za uzalishaji mali zimechangia kwa kiasi kikubwa sana katika uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ushahidi wa wazi kabisa unaodhihirisha kwamba mazingira yetu si salama. Ushahidi huo ni pamoja na kuongezeka kwa jangwa na ukame, mafuriko, kuongezeka kwa magonjwa ya kuambukiza na mabadiliko ya hali ya hewa. Maendeleo endelevu hayawezi kupatikana bila kutunza mazingira. Ingawa jitihada kubwa zimefanyika kuhusu utunzaji wa mazingira, hali ya mazingira nchini bado si ya kuridhisha na inatishia mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hizi mbalimbali, ofisi yetu imeendelea kuchukua hatua za kukabiliana nazo ikiwa ni pamoja na kuteua wakaguzi wa mazingira kutoka taasisi nyingine, kutoa elimu ya umma kuhusu mazingira kwa makundi tofauti, kufanya tafiti mbalimbali ili kupata taarifa na takwimu zinazohitajika, kuhamasisha Halmashauri kutenga maeneo na kujenga miundombinu ya kutupa taka, kuhamasisha ubunifu katika teknolojia ya nishati mbadala pamoja na mambo mengine ambayo yatasaidia hifadhi ya mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Mazingira ambayo imetungwa mwaka 1997 imetumika sasa kwa zaidi ya miaka 20. Sera hii imekuwa na mafanikio makubwa sana katika utekelezaji wake. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa sera hiyo, changamoto mbalimbali zilijitokeza ambazo ni pamoja na kukosekana kwa matamko mahususi ya kiseru, na vilevile kujitokeza kwa changamoto mpya za mazingira ambazo zimeongeza kasi kubwa ya uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kutokana na changamoto hizi, Ofisi sasa imeamua kurekebisha sera hiyo ili kuimarisha juhudi za uhifadhi na usimamizi wa mazingira na tumeanza mchakato wa jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja, ofisi yetu sasa inatarajiwa kukamilisha marekebisho ya sera hiyo ya mazingira na mkakati wa utekelezaji wake ili sera hiyo mpya ianze kutumika.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inaelekeza kuandaliwa ripoti ya hali ya mazingira nchini kila baada ya miaka miwili na ripoti hiyo kuwasilishwa Bungeni. Tangu kuanza kutekelezwa kwa sheria hii, ripoti mbili za hali ya mazingira nchini zimeandaliwa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea na maandalizi ya ripoti ya tatu ya hali ya mazingira nchini kwa kukusanya taarifa mbalimbali kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kuandaa taarifa hiyo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokuja, ofisi yetu itakamilisha ripoti ya tatu ya mazingira na kuiwasilisha hapa Bungeni ili ijadiliwe, lakini pia kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Dhamana wa Taifa wa Mazingira ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira na ilibainika kwamba utakuwa chanzo muhimu cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kuhifadhi mazingira nchini. Baada ya bodi ya mfuko huo kuundwa, changamoto iliyojitokeza ni mfuko kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu kutokana na mapungufu ya kisheria. Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha Ofisi yetu ilipendekeza marekebisho ya sheria ili mfuko uweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali Ofisi imeendelea kubaini vyanzo vipya vya mapato ambavyo havitozwi na taasisi nyingine ili kuuwezesha mfuko kufanya kazi zake kwa ufanisi kwa kupata rasilimali. Katika mwaka wa fedha unaokuja marekebisho ya mapungufu ya kisheria tunaamini yatakamilika na mfuko utasajiliwa na kuanza kazi yake kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila tarehe 5 Juni dunia huadhimisha Siku ya Mazingira Duniani ili kutoa hamasa kwa watu kutunza mazingira. Kitaifa mwaka jana Siku ya Mazingira Duniani ilifanyika Butiama, Mkoani Mara alipozaliwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Lengo lilikuwa ni kumuenzi Baba wa Taifa kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuhifadhi mazingira nchini ikiwemo kuanzisha msitu wake yeye mwenyewe na kuutunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya maadhimisho ya mazingira duniani kwa mwaka huu yatafanyika kidunia India, na hapa nchini tutayafanya Mkoani Dar es Salaam na kaulimbiu ya kidunia ya siku hiyo ya mazingira mwaka huu inahusu udhibiti wa mazingira unaotokana na *plastic*. Na kaulimbiu ya kitaifa kwa sisi mwaka huu inahusu kudhibiti matumizi ya mkaa kwa kutumia nishati mbadala. Kauli mbiu hii inalenga kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala wa kuni na mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkaa unaotokana na miti umeendelea kuwa chanzo kikubwa cha nishati hasa za kupikia hivyo kuendelea kuchangia ukataji holela wa miti. Katika mwaka wa fedha unaokwisha, Serikali imeendelea na jitihada za kupunguza mkaa unaotokana na miti. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mashindano ya ubunifu wa teknolojia mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu kutakuwa na maonesho makubwa ya teknolojia ya nishati mbadala. Ofisi itatangaza washindi wa ubunifu wa teknolojia hiyo wakati wa kilele cha maadhimisho tarehe 5 Juni mwaka 2018 Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha ujao, ofisi yetu itaendelea kuzihamasisha taasisi zote za Umma kusitisha matumizi ya mkaa na kuni na kuanza kutumia nishati mbadala, ikiwemo gesi ya kwenye mitungi pamoja na nishati jadidifu ili kuhifadhi mazingira yetu. Hili tumeanza kwa Chuo Kikuu cha Dodoma, tumetoa waraka, pale pana wanafunzi 30,000 ambao wanakula mara tatu kwa siku na chakula chao kinapikwa kwa kuni. Kwa hiyo taasisi ile itakuwa ya kwanza kuhama kwenye kuni na baadaye taasisi nyingine za umma, ikiwemo shule, magereza, kambi za jeshi, zote zitaachana na matumizi ya kuni na kutumia nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati kupitia Mradi wa Nishati Endelevu kwa

Wote itaboresha na kukamilisha Rasimu ya Mkakati wa Tungamotaka (*National Biomass Energy Strategy*) na kuusambaza kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya mifuko ya plastiki. Dhamira ya Serikali ya kupiga marufuku uzalishaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya mifuko ya plastiki tuliyoitangaza mwaka 2016 bado iko pale pale. Dhamira hiyo ni kwa lengo la kupunguza madhara ya kiafya, kimazingira na kwenye miundombinu yanayosababishwa na mifuko ya plastiki. Wazalishaji na wenye viwanda vya mifuko ya plastiki walipewa muda wa kutosha kujiandaa na kubadilisha teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita, ofisi yetu ilifanya kazi mbalimbali katika kujiandaa na kusitisha matumizi ya mifuko ya plastiki. Kwanza, tulikutana na wadau wanaozalisha na kufanya biashara ya mifuko ya plastiki kwa lengo la kupata maoni yao pamoja na kutoa elimu kwa Umma kuhusu madhara ya mifuko ya plastiki. Katika mwaka wa fedha unaokuja Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuhamasisha utengenezaji, upatikanaji na matumizi endelevu ya mifuko mbadala ya plastiki; na uhibitaji wa uingizwaji wa mifuko hiyo kutoka nje ya nchi kwa sababu majirani zetu karibu wote wamezuia uzalishaji wa mifuko ya plastiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mazingira, inaelekeza kuundwa kwa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Mazingira (*National Environmental Advisory Committee*) ambayo wajumbe wake watakuwa wanatoka katika taasisi mbalimbali za umma, binafsi, taasisi za elimu ya juu na asasi za kiraia. Katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita Ofisi imezindua rasmi Kamati hiyo na ilifanya kikao cha kwanza hapa Dodoma mwezi Desemba, 2017. Katika mwaka wa fedha unaokuja Kamati itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba Bonde la Mto Ruaha Mkuu lina umuhimu mkubwa katika

uchumi wa taifa hili. Inakadiriwa kuwa asilimia 26 ya maji yatakayotumika kufua umeme katika mradi mkubwa wa *Stiegler's Gorge* yatatoka katika Mto Ruaha Mkuu. Kwa kutambua umuhimu wa bonde hili na changamoto za mazingira zilizojitokeza, mwezi Aprili, 2017 Ofisi ya Makamu wa Rais iliunda Kikosi Kazi cha Kitaifa ili kuokoa ikolojia ya Mto huu wa Ruaha Mkuu. Taarifa ya kikosi kazi iliwasilishwa kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais na ilikuwa na mapendekezo mbalimbali, na Makamu wa Rais alitoa maelekezo mahsusi ili kutekeleza mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita, ofisi yetu iliendelea kuaratibu utekelezaji wa maagizo ya Makamu wa Rais kuhusu kuokoa Bonde la Mto Ruaha Mkuu pamoja na utekelezaji wa mapendekezo ya kikosi kazi ili tuunusuru mto huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa maelekezo ya Makamu wa Rais pamoja na mapendekezo ya kikosi kazi imeonesha kuwa hali ya Bonde la Mto Ruaha imeanza kuimarika baada ya hatua ambazo ofisi yetu iliziratibu na kuchukua kuhusu uharibifu wa mazingira katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja, ofisi yetu itaendelea kuratibu utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Makamu wa Rais na mapendekezo mbalimbali ya kikosi kazi ili kuhakikisha kwamba hali ya mfumo-ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu inaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokwisha, ofisi yetu ilianza utaratibu wa kuyatangaza baadhi ya maeneo nchini ambayo yana umuhimu wa kimazingira na kiikolojia nchini mwetu kuwa Maeneo ya Mazingira Lindwa (*Environmentally Sensitive Areas*) na Maeneo ya Mazingira Tengefu (*Environmentally Protected Areas*) kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira, lakini bila kuathiri matumizi endelevu ya binadamu kwa maeneo haya. Hadi sasa ofisi yetu imeyatambua maeneo 20 yaliyopendekezwa kuwa maeneo lindwa/tengefu, na kwa mwaka wa fedha

unaokuja ofisi itanza mchakato wa kuwashirikisha wadau ikiwa ni pamoja na Halmashauri za maeneo husika ili kuwezesha maeneo haya kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwamba yamelindwa ili yasiendelee kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie, tumebaini maeneo 20 ambayo ni nyeti kwa mazingira ya nchi yetu ikiwemo vyanzo vikubwa vya maji na mito na maziwa makubwa yanayosaidia watu wetu. Maeneo haya hayalindwi na sheria yoyote. Kwa sababu hiyo tumeamua yalindwe na Sheria ya Mazingira, na katika mwaka ujao wa fedha tutazungukia maeneo hayo na kuzungumza na wadau ili tuyatangaze katika Gazeti la Serikali kwamba ni maeneo ambayo yamelindwa na matumizi yake kwa shughuli za kibinadamu yatadhibitiwa kwa Sheria ya Mazingira, lakini bila kuathiri, bila kuondoa watu, bila kuathiri watumizi endelevu ya binadamu na hapa Bungeni tutawaletea orodha ya maeneo hayo kwa sababu maeneo mengi yapo katika majimbo yenu vilevile ili mfahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha unaopita, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu shughuli za Kikosi Kazi cha Kuhifadhi Mazingira ya Bahari kwa kupambana na uvuvi haramu wa milipuko. Tathmini ya utekelezaji inaonesha kuwa kuna mafanikio makubwa katika kudhibiti uvuvi haramu wa kutumia milipuko, kwani matukio ya milipuko baharini yamepungua kwa kiasi kikubwa. Aidha, Ofisi imeandaa rasimu ya Mpango wa Elimu kwa Umma Kuhusu Kudhibiti Uvuvi Haramu wa Milipuko, na kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ofisi itakamilisha mpango huo na kuimarisha kikosi hicho ili kiendelee kudhibiti uharibifu wa mazingira katika bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu kwamba moja ya changamoto kubwa nchini mwetu ni hiyo ya uvuvi haramu wa vilipuzi na Ofisi ya Makamu wa Rais iliratibu mkutano wa wizara saba ikiwemo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambapo mikakati mikubwa kabisa iliwekwa na Serikali tulifanya kazi kwa pamoja na kwa kweli tunayo fahari kubwa

sana kama Ofisi ya Makamu wa Rais kusema kwamba matishio ya mazingira yanayotokana na ulipuaji yamepungua kwa kiasi kikubwa. Lakini jambo hili pia linahusu usalama kwa sababu unapokuwa na vijana wengi wanaokuwa na uwezo wa kutengeneza mabomu basi hatari ile haitakuwa ya mazingira peke yake bali pia itakuwa hatari ya usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na vilevile ofisi yetu inazungumza na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili kuhakikisha kwamba baruti haipatikani kwa urahisi na baruti sasa inafanywa kuwa silaha ili upatikanaji wake upitie mchakato wa kujua ni nani anapata na anaenda kuitumia vipi ili kupunguza hatari ya kusambaa baruti hovyoy. Kwa hiyo, katika mambo makubwa ambayo tumefanikiwa ni hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha, ofisi yetu imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti. Katika kampeni hii kila Halmashauri imeelekezwa kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka. Hata hivyo, katika kutekeleza kampeni hii, ofisi imekabiliwa na changamoto mbalimbali za ufuatiliaji na tathmini ili kujua idadi ya miti iliyopandwa na kukua. Katika kukabiliana na changamoto hii ofisi itaimarisha kampeni kwa kutoa motisha na kuratibu ujumuishaji wa utekelezaji wa kampeni hii katika mikakati na mipango ya kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba kampeni hii inafanikiwa na kuwa endelevu, kamati ya kitaifa ya utekelezaji wa kampeni hii imeundwa. Kamati hii inajumuisha wajumbe kutoka sekta ya umma, sekta binafsi na kampuni binafsi zikiwemo zenye mashamba makubwa ya miti. Tunaendelea kusisitiza kwamba kampeni hii izingatie kupanda na kutunza aina sahihi ya miti na kwa wakati sahihi na katika eneo sahihi. Aidha, tunashauri kwamba nguvu kubwa pia ielekezwe katika kutunza na kuhifadhi miti ya asili. Siri kubwa ya kulinda uoto wa miti si kupanda miti bali ni kudhibiti miti ya asili kukatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza kampeni hiyo, Mheshimiwa Makamu wa Rais alizindua rasmi Kampeni au Programu ya Kuifanya Dodoma kuwa ya Kijani mwezi Desemba, 2017 kule eneo la Mzakwe, Dodoma. Ofisi yetu katika kuendeleza kampeni hiyo mwezi huu wa kwanza ikishirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma na Jeshi la Kujenga Taifa, tulipanda miti 30,000 katika eneo la Ng'ong'ona, Manispaa ya Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja, ofisi yetu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia taasisi zilizo chini yake ili kuwajengea uwezo wadau kushiriki katika kampeni hii. Aidha, ofisi itaendelea kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa programu ya upandaji miti katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto za kimazingira zinazoikabili nchi yetu ni suala la taka ngumu. Sheria ya Mazingira inaelekeza majukumu ya Halmashari katika kudhibiti suala la taka. Pamoja na jitihada zilizofanyika bado kumekuwa na changamoto kubwa katika eneo hili. Hivyo, Ofisi yetu ya Makamu wa Rais imechukua mtazamo mpya na kutaka kuzifanya takataka sasa kuwa rasilimali kwa kuzichakata na kuzirejeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita, Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa Mwongozo wa Uwekezaji katika taka ngumu ili kuwawezesha wawekezaji ambao wanataka kubadilisha taka kuzalisha umeme na kufanya shughuli nyinginezo, kupata taarifa muhimu wanazozihitaji ili waweze kuwekeza katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo huu umeainisha fursa za uwekezaji katika taka ngumu likiwemo suala la ukusanyaji wa taka, usafirishaji na urejelezaji. Kutumia taka kama malighafi ya kutengenezea mbolea ya mboji, kuzalisha nishati ya umeme na madampo ya kisasa; kutibu majitaka na uteketezaji wa taka hatarishi. Katika mwaka wa fedha unaokuja, ofisi yetu inakusudia kusambaza mwongozo huu kwa wadau na kufuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taka zenye madhara; taka hatarishi zinazalishwa viwandani, kwenye migodini na mahospitali na baadhi ya maeneo ya biashara. Ofisi yetu imeendelea kudhibiti uzalishaji na utupaji wa taka zenye madhara kwa mujibu wa Kanuni za Udhibiti wa Taka zenye Madhara za mwaka 2009. Aidha, Ofisi yetu imeendelea kutoa vibali vya kukusanya, kusafirisha na kurejeleza taka kwa kampuni zilizokidhi vigezo hivyo. Hadi mwezi Machi, 2018 vibali 60 kati ya maombi 70 vimetolewa. Katika mwaka wa fedha unaokuja, Ofisi yetu itaendelea kuimarisha usimamizi wa taka hatarishi kwa kuwahimiza wadau kupunguza uzalishaji wa taka hizo na kudhibiti uteketzaji na utupaji wa taka hizo hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yetu imeendelea na uratibu wa shughuli za Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*Global Enviroment Facility*) hapa nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita, ofisi imeratibu maandalizi ya miradi mbalimbali ya Mzunguko wa Saba wa Ufadhili (*GEF – 7*). Aidha, ufuatiliaji wa fedha za utekelezaji wa miradi iliyoidhinishwa na *GEF* umefanyika. Ofisi ilibuni miradi mbalimbali ambayo kwa sasa imeanza kutekelezwa. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Kuzuia Uharibifu wa Ardhi na Mradi wa Kuongeza Usalama wa Chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie; baadhi ya miradi hiyo ni Mradi wa Kuhifadhi Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa na Mradi wa Kuzuia Uharibifu wa Ardhi na Kuongeza Usalama wa Chakula. Miradi hiyo tunaitekeleza katika mikoa mingi na katika Halmashauri kadhaa. Leo jioni tutawasambazia Waheshimiwa Wabunge maeneo ambayo miradi hii inatekelezwa ikiwemo majimboni mwao ili waweze kutusaidia kufuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokuja, Ofisi itaendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mazingira wa Dunia hapa nchini. Aidha, Ofisi itashirikiana na wadau wengine kuendelea kuandaa miradi mbalimbali na kufuatilia utekelezaji wa miradi iliyopatiwa fedha.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uratibu na utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na ya kikanda; kama unavyofahamu, Ofisi yetu ndiyo inayoratibu miradi mbalimbali ya kimataifa na kikanda inayohusu mazingira. Katika mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na wadau mbalimbali tumeendelea kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kifupi nipitie mikataba ambayo tunaitekeleza na miradi iliyoko chini yake:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na Itifaki ya Kyoto. Ninapenda kutumia fursa hii kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kwamba Bunge lako Tukufu limeridhia Makubaliano ya Paris hapa Bungeni tarehe 3 Aprili, mwaka huu. Makubaliano haya yatasaidia kuimarisha utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita, Ofisi yetu iliendelea kuratibu utekelezaji wa miradi mikubwa miwili ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi iliyo chini ya mkataba huu. Miradi hiyo ni Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii za Pwani Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi na Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Jiji la Dar es Salaam. Chini ya miradi hii mikubwa miradi kadhaa midogo midogo inatekelezwa ikiwemo ya kujenga ukuta wa kuzuia mawimbi ya bahari kule Dar es Salaam, ikiwemo Mradi wa Mifereji kule Bungoni Ilala, Mradi wa Kuta Pangani na miradi mingineyo mingi inayotekelezwa Zanzibar, Rufiji, Bagamoyo na maeneo mbalimbali ya Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja, Ofisi inatarajia kuendelea kutekeleza miradi mingine chini ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Maeneo ya Vijijini kupitia Mfumo Ikolojia (*Ecosystem-Based Adaptation for Rural Resilience*). Mradi huu utatekelezwa

katika maeneo ya Kishapu, Mpwapwa, Mvomero, Simanjiro na Kaskazini A Unguja.

(ii) Mradi mwingine ni Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi katika Kuhisha Taarifa za Mabadiliko ya Tabianchi kwenye Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo (*Institutional Support for Climate and Seasonal Weather Information for Adaptation Planning in Northern Tanzania*) na tutatoa maeneo ambayo mradi huu unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita, Ofisi iliendelea na mchakato wa kuwezesha sekta za umma na binafsi hapa nchini kupata ithibati (*accreditation*) katika Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund*).

Katika mwaka wa fedha unaokwisha, Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira lilisajiliwa na Bodi ya Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (*Adaptation Fund Board*) kuwa msimamizi wa kitaifa wa shughuli za Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (*National Implementing Entity for Adaptation Fund*). Hili ni jambo kubwa sana kwa NEMC, kwa maana hiyo itakuwa na uwezo wa kupata rasilimali moja kwa moja kutoka kwenye *Adaptation Fund* na hivyo kujenga uwezo wake wa kutusaidia kusimamia Sheria ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Ofisi ilizijengea uwezo taasisi katika sekta za umma na binafsi kuhusu fursa za kupata fedha za kutekeleza miradi ya mazingira katika mifuko mbalimbali duniani. Tumewasaidia TAMISEMI na wamefika pazuri ili na wenyewe waweze kupata ithibati ya kuweza kupewa fedha moja kwa moja kwenye mifuko mikubwa duniani ili kutekeleza miradi ya hifadhi ya mazingira kwenye Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunatarajia kuisaidia Wizara ya Fedha nayo ipate ithibati ili iweze kupata fedha moja kwa moja katika mifuko hii ya mazingira duniani ili iweze kupelekwa katika maeneo yetu na kutekeleza miradi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja, Ofisi itaendelea kuratibu uchambuzi wa miradi chini ya ufadhili wa Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi ili kuhamasisha sekta binafsi, taasisi za umma na mashirika ya umma kuandaa miradi ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Ofisi yetu; kama unavyofahamu nchi yetu inakabiliwa na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame na hivyo tunashiriki katika Mkataba wa Kimataifa wa Kupambana na Jangwa. Katika mwaka wa fedha unaopita ofisi iliratibu maandalizi ya programu ya Taifa yenye madhumuni ya kufanya tathmini ya maeneo yaliyoathirika ili kuzuia malengo ya uharibifu wa mazingira. Katika mwaka wa fedha unaokuja ofisi itakamilisha maandalizi ya mradi wa kuongoa/kuainisha maeneo yaliyoharibika kwa ajili ya kupatiwa fedha za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina utajiri wa viumbe hai wa aina tofauti. Ili kulinda na kutunza baioanuai hiyo, Tanzania inashiriki katika Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Baioanuai. Katika mwaka wa fedha unaopita, kwa mamlaka yangu kama Waziri mwenye dhamana ya mazingira, nimeteua wakaguzi sita wa kusimamia matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa. Aidha, ofisi imeendelea kukusanya taarifa za utekelezaji wa Mkakati wa Mpango Kazi wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai (*National Biodiversity Strategy and Action Plan*). Taarifa hizi zitatumika katika maandalizi ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kuhifadhi Mazingira 2019 – 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumemetoa kibali cha kufanya utafiti wa mahindi yanayovumilia ukame na wadudu waharibifu katika Kituo cha Utafiti hapa Makutupora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha unaokuja tutaendelea kukuza uelewa wa jamii na kujenga uwezo wa wataalam kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa nchini. Vile vile Ofisi itaendelea kuratibu ukaguzi katika maduka ya vyakula na maeneo mengine ili kuhakikisha kwamba bidhaa zenye viambata vya mazao yanayotokana na Uhandisi Jeni (*Genetic Engineering*)

zinadhibitiwa nchini. Nchi yetu haijaruhusu matuzmizi ya bidhaa zilizofanyiwa uhandisi jeni (*Genetically Modified Organisms*). Kwa hiyo, kama taifa na ofisi yetu ndiyo ina wajibu huo wa kushirikiana na wadau wengine kudhibiti uingizwaji wa vyakula ambavyo vina hivyo vimelea. Kwa hiyo, tunafanya ukaguzi katika *supermarkets* na maeneo mbalimbali kuhakikisha kwamba bidhaa zinazouzwa hazina vitu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokuja 2018/2019 Ofisi yetu itaratibu maandalizi ya miradi ya utekelezaji wa Mpango wa Mkataba wa Nairobi kuhusu wa Uhifadhi wa Mazingira ya Bahari ya Hindi Kutokana na Vyanzo na Shughuli Zinazofanyika Nchi Kavu inayolenga kupunguza uchafuzi wa bahari na ukanda wa pwani na Programu ya Kuwianisha Sera na Kuimarisha Taasisi Zinazosimamia Hifadhi Mazingira ya Bahari. Sisi ni wanachama wa Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi Bahari ya Hindi na tunafanya kazi mbalimbali kusimamia mkataba huu na tutaendelea na kutekeleza miradi itakayoweza usalama wa bahari yetu ya hindi.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kipindi cha mwaka 2017/2018 Ofisi yetu imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mkataba wa Basel kuhusu Udhibiti wa Usafirisahaji wa Utupaji wa Taka za Sumu kati ya nchi na nchi. Katika mwaka wa fedha unaokuja, Ofisi itaendelea kuratibu Mkataba huu kuhakikisha kwamba mkataba huu kuhakikisha kwamba nchini kwetu hakuingizwi taka zozote zenye sumu au taka nyingine zozote kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha 2017/2018 Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm unaohusu Udhibiti wa Kemikali zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu. Katika jitihada za kuzuia madhara ya kemikali zinazodumu kwa muda mrefu, Ofisi yetu imefanya miradi mbalimbali ikiwemo kushirikiana na *TANESCO* kuhusu yale mafuta yale wanayotumia kupikia chipsi ya trasfoma,

kuhakikisha kwamba hayatupwi na hayasambai hovyoy ili kuharibu mazingira yetu kwa kitaalam yanaitwa *Polychlorinated Biphenyls-PCBs* ambazo zinatumiika kwenye kwenye transfoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yetu imenunua maalum na imeshirikiana na *TANESCO* kwa sababu tunasambaza umeme vijijini tunajenga trasfoma nyingi kwa hakika mafuta haya yatakuwa mengi na yale mafuta yanadumu katika mazingira na yaliharibu mazingira. Kwa hiyo, moja ya mambo ambayo ofisi yetu imefanya ni pamoja na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokuja, ofisi iliratibu ukusanyaji wa takwimu za uingizaji na matumizi ya kemikali mbadala wa zinazoharibu tabaka la ozoni. Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokuja ofisi yetu itaendelea kuratibu utekelezaji wa mkataba huu ili kuzuia matumizi ya kikemikali zinazoharibu tabaka la ozoni na kuepusha madhara ya uharibu wa tabaka la hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya zebaki katika shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini yameongezeka na yamehatarisha afya za binadamu na viumbe hai pale inapotumika bila taratibu. Katika mwaka wa fedha uliokwisha Ofisi yetu imekamilisha ukusanyaji wa takwimu kwa ajili ya kuandaa mpango kazi wa kitaifa kuhusu kupunguza matumizi ya zebaki. Kwa mwaka wa fedha unaokuja ofisi yetu itakamilisha mpango wa kitaifa wa kazi wa kupunguza matumizi ya zebaki na kutoa elimu kwa wadau kuhusu utekelezaji wake. Aidha, Kanuni za Usimamizi wa Matumizi ya Zebaki au *mercury* na viambata vyake zitaandaliwa na Ofisi yetu na mimi nitazisaini kuhakikisha kwamba zinatumiika na kudhibiti matumizi ya *mercury* ambayo inaharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa umma kuhusu mazingira changamoto kubwa. Tumejitahidi katika mwaka wa fedha unaokwisha kuhakikisha kwamba tunaelimisha watu wetu kuhusu hifadhi ya mazingira na kazi hiyo

tutaendelea nayo katika mwaka wa fedha unaokuja. Tutashirikiana na Kamati yetu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na vile vile tumelekeza kwamba katika mwaka wa fedha unaokuja ofisi iandae mkakati wa mawasiliano ya elimu ya umma kuhusu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Ofisi itaanzisha Mfumo Mkuu wa Taarifa Kuhusu Mazingira (*Central Environmental Information System*) utakaoendana na mfumo wa teknolojia ya simu za mkononi ili kuwawezesha wananchi kokote walipo kwa kutumia simu zao za mkononi waweze kuripoti uharibifu wa mazingira na waharibifu wa mazingira. Hivi tunavyoongea tunaongea na washirika wa maendeleo ili kutengeneza mfumo huo na tutautangaza kwa wananchi ili tuwashirikishe wananchi kwa mapana katika hifadhi ya mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Hifadhi ya Mazingira ni msimamizi mkuu wa sheria na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Katika mwaka wa fedha unaokwisha *NEMC* imeendelea kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi 627 katika mikoa mbalimbali. Miradi iliyokiuka sheria ilichukuliwa hatua stahiki kama sheria inavyotaka. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Baraza litandelea kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi ya uwekezaji na kuchukua hatua zinazostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mwaka wa fedha ulipita tulipokea malalamiko mbalimbali kuhusu uchafuzi wa mazingira na kufuatilia malalamiko hayo na katika mwaka wa fedha tutaendelea kuimarisha mfumo wa kupata malalamiko ya wananchi kuhusu uchafuzi wa mazingira na kuyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha Baraza lilishirikiana na taasisi mbalimbali kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo wa madini kuhusu hifadhi ya mazingira na matumizi ya sumu kwa wale wanaochenjua dhahabu. Katika mwaka wa fedha unaokuja

tutaendelea na jitihada hizo kwa nguvu kubwa zaidi. Vilevile katika uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira nimeteua wakaguzi wa mazingira nimeteua wakaguzi 452 kutoka katika taasisi mbalimbali na hadi sasa wote ambao nimewateua wamefika 512, tumewapa mafunzo na wengine wataendelea kupewa mafunzo mwaka ujao. Tunaamini kwamba uteuzi wa wakaguzi hao wakati Serikali ya Awamu ya Tano inaingia tulikuta wakaguzi wasiozidi 70 sasa hivi tuna wakaguzi wa mazingira 512, tunaamini wataongeza jitihada zetu za kusimamia hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tathimini kwa ya athari kwa mazingira yaani *EIA* ni jambo ambalo limekuwa linazungumzwa kwa muda mrefu. Baraza limeendelea kusajili miradi na kuifanyia mchakato na upatikaji wa vyeti vya mazingira. Lakini vilevie tunafahamu kwamba kuna malamiko mbalimbali ya wawekezaji kuhusu kuchelewa kwa kupata vyeti vya mazingira hivyo Serikali imelielekeza Baraza la Mazingira kuchukua hatua zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekitiki, kwanza kutengeneza orodha ya mambo muhimu ya kuzingatia yaani *checklist* ya miradi ya majengo chini ya ghorofa tatu, na viwanda na umeme jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tumeamua kwa miradi ile ambayo tumeona kwamba haina madhara makubwa kwa mazingira baada ya kufanya *checklist*, but tunatoa *provional of permit* yaani vibali vya muda ili waanze hii miradi ya uwekezaji ili isichelewe wakati tathimini ya athari kwa mazingira inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunaangalia Kupunguza gharama za kufanya *EIA* ambazo nyingi pia zina fanya wawekezaji wachelewe kuwekeza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika pamoja na kufanya yote haya katika mambo ambayo hatu *compromise* ni uharibifu wa mazingira. Tunaamini kwamba uwekezaji unaweza kufanyika ndani ya hifadhi ya mazingira kwa

uharaka wa upatikaji wa vyeti vya mazingira haitakuwa sababu ya kufanya shughuli zinazoharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita Baraza la *NEMC* limeendelea kutekeleza ajenda ya taifa ya utafiti wa mazingira *National Enviromental Research Agenda* na kwa kufanya tafiti na tathmini ya mazingira katika maeneo mablimbali nchini. Hili eneo la utafiti ni muhimu sana na katika mwaka wa fedha unaokuja tutaendela kulipa uzito wake unaostahili ikiwemo kukusanya takwimu na kuandaa taarifa ya hali ya mazingira ya milima hapa nchini. Tumelekeza kwamba hapa nchini kuna vilima na milima mingi ambayo ni vyanzo vya shughuli za utalii, vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, lakini hatuna tathmini halisi ya uharibifu wa mazingira kwenye vilima na milima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mwaka ujao unaokuja tutawaletea ripoti kubwa kabisa hapa nchini ya hali ya milima na vilima hapa nchini. Vilevile tutakuwa na taarifa ya mazingira ya Pwani (*State of Coast Environment*) kwa mwaka unaokuja lakini tutafanya utafiti wa mifumo ya ikolojia ya hali mabonde ya mito mikubwa na maeneo ya malisho ya mifugo na wanyamapori ili kuhakisha kwamba shughuli za ufugaji na shughuli za utalii nchi zinaendelea kwa tija kwa kujua kiwango cha uharibifu wa mazingira katika malisho hapa nchini kwetu. Vile vile Baraza litaendelea kuratibu miradi mbalimbali ambayo inaendelea sasahivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita tunayo furaha kuwaeleza kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais iliamia hapa Dodoma ikiongozwa na Makamu wa Rais mwenyewe na watumishi 127 wa Ofisi hii. Kwa hiyo, shughuli za Makamu wa Ofisi ya Makamu wa Rais sasa zinafanyika kutokea Dodoma. Ofisi itakamilisha taratibu za kuhamisha watumishi wachache walibaki Dar es Salam kwa mwaka ujao wa fedha.

Vilevile tutaendelea kuimarisha utendaji wa *NEMC* ambao wote tunafahamu kuna changamoto za uongozi pale na vilevile katika mwaka wa fedha unaokuja



tutaendelea kulijengea uwezo Baraza hili kwa kutoa mafunzo na ajira mpya na kuboresha mazingira kazi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimalize kwa hitimisho na shukrani. Kama tunavyoelewa nchi yetu ni ya Muungano tunaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nchi yetu ni Muungano wa Tanzania Jamhuri limekuja baadae tumeunda Muungano tukautengenezea Jamhuri na Muungano wetu una umuhimu wa pekee kwa Taifa letu na umekuwa ndio utambulisho na ndicho kielelezo cha cha umoja wetu katika kudumisha amani na usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwneyekiti, nadhani Mheshimiwa atapata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwneyekiti, ninatoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kuuthamini, kuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano wetu kwa sababu ndiyo unaotutambulisha. Tunaamini kabisa kwamba ndani ya Muungano fursa za ustawi wa wananchi wa pande zote mbili fursa za ustawi na maendeleo kwa pande zote mbili zitapatikana zaidi ndani ya umoja wa Taifa letu nasio kwenye utengano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chini ya uongozi wa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Makamu wake, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Muungano wetu unaendelea kuimarika na unaendelea kushamiri. Naomba niseme kwamba chini ya uongozi wao na kwa ujumla hakuna changamoto yoyote ya Muungano inayoweza kutufarakanisha wala kututenganisha wala kuturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za Muungano ambazo zilikuwepo tangu siku ya kwanza, zipo leo, na sisi zote hata tukifa humu kila mtua atafika wakati wake, changamoto hizi zitaendelea kuwepo na waliopo

wataendela kulishughulikia kuwepo kwa changamoto siyo ubaya wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipengependa tu kutahadharisha kuhusu lugha mbalimbali ambazo zinatimia changamoto za Muungano kuupa jina baya Muungano. Sisi Ofisi yetu tunayo faraja kubwa kwamba kwa nchi yetu ilivyo sasa, kwa bahati nzuri kwa watu wa itikadi zote na kutoka pande zote mbili za Muungano, mjadala si uhalali wa Muungano; mjadala sasa ni mbinu za kuuimarisha na mbinu za kutatua changamoto zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naamini kwamba tukijadiliana na tukielekeza mjadala wetu huko basi tutaweza kujenga nchi yetu katika umoja ambao wote tunajivunia. Ofisi yetu ya Makamu wa Rais na Serikali kwa ujumla tutaendelea kuyafanyia kazi maoni na mawazo ya watu mbalimbali wenye nia ya kuuona Muungano wetu unashamiri. Na sisi tunafurahi kwamba Wabunge karibu wote humu wote wana nia ya kuona Muungano wetu unaimarika na kushamiri. Nadhani tunatofautiana kwenye lugha tu na mbinu za namna ya kuimarisha. Sisi tuko tayari kusikiliza maoni na ushauri bora zaidi na wa ziada ili kuweza kuimarisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu pia kwamba mazingira yana umuhimu mkubwa katika mustakabali wetu na katika maendeleo ya uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kuwa mazingira na maliasili za nchi yetu zinalindwa na kuhifadhiwa. Ofisi yetu ina dhamira ya kuendelea na utaratibu wa kumshirikisha kila Mtanzania katika hifadhi ya mazingira. Napenda kutoa wito kwa wananchi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kuwa dhamira ya Serikali ya kulinda na kuhifadhi mazingira inazingatiwa na kupewa kipaumbele kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha unaokuja Ofisi yetu itaendelea kushika hatamu kwa uthabiti kabisa katika wajibu wake wa usimamizi wa uratibu wa

mazingira nchini. Tutaendelea kutoka miongozo ya hifadhi ya mazingira katika sekta na nyanja mbalimbali. Pia lengo letu katika Ofisi yetu ni kuongoza Hifadhi ya Mazingira kwa namna pana zaidi kwa kuangalia mifumo ya ikolojia, mifumo ya uzalishaji, mifumo ya uchumi na mifumo ya rasilimali asili. Ninaomba nitumie fursa hii kutoa shukrani kwa wote walionisaidia kufanikisha utekelezaji wa kazi za Ofisi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa kwanza ni Rais wetu ambaye kwa uongozi wake na dira mwelekeo wapi tulipopitia kwenye majukumu yetu; lakini pili Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye ndiye hasa ndiye mwenye Ofisi yake kwa miongozo mbalimbali ambayo amekuwa anaitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola ambaye wote mnamfahamu na wote mnajua kazi nzuri anayoifanyakatika ofisi yetu. Pia napenda kuwashukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais Mhandisi Joseph Kizito Malongo na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Butamo Kasuka Phillip ambaye juzi ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu, tunampongeza. Tumepata pigo lakini mwenzetu anaenda kutumikia nchi kwa namna nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza ndugu Ndugu Ali Mufuruki, Mwenyekiti wa Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Mazingira, Ndugu Makota Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa NEMC pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo mbalimbali na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kuanzia wahudumu, madereva masekretari na wengineo kwa kazi nzuri na ushirikiano nzuri tulionanao katika Ofisi yetu na kwa kweli kila mmoja katika Ofisi ya Makamu wa Rais ametoa mchango katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kuwashukuru wahisani wetu wa maendeleo kwa kazi nzuri ambayo wanafanya na misaada mbalimbali ambayo wametupatia katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee zaidi ni Kamati zetu mbili za Bunge, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Murad (Mheshimiwa Suleiman Saddiq) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Innocent Bashungwa, kwa kweli mmekuwa ni wenzetu na mmesaidia kuboresha hoja ninayowasilisha. Vilevile Kamati ya Katiba na Sheria chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mchengerwa na Makamu Mwenyekiti ambaye umekalia kiti hapo Mheshimiwa Najma Giga mmetusaidia kuiboresha hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niombe pesa; naomba Bunge lako tukufu liidhinishhe makadilio ya Matumizi ya shilingi 600,308,631,000 fedha za matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kiasi hiki kinajumuisha fedha za mishahara ya watumishi shilingi 1,053,666,000 na fedha za matumizi mengineyo shilingi 5,254,965,000, hilo ni Fungu la 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu la 31, naomba Bunge lako tukufu liidhinishhe makadirio ya matumizi ya shilingi 14,784,456,560 kwa fungu hili. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi 9,721,116,560 fedha za matumizi ya kawaida inajumuisha na shilingi 5,063,340,000 fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha shilingi 5,942,065,000 fedha za mishahara na shilingi 3,779,051,560 fedha za matumizi mengineyo. Fedha za mishahara zinajumuisha shilling 3,017,072,000 ruzuku ya mishahara ya watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha fedha za ndani shilingi bilioni tatu na fedha za nje shilingi bilioni 2,063,340,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
WAKATI WA KUWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 –  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Mhe. January Y. Makamba (Mb.), Waziri wa Nchi,  
Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira*

**A: UTANGULIZI**

1. *Mheshimiwa Spika*, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2017/18; na malengo ya Ofisi ya mwaka wa fedha 2018/19, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2018/19.

2. *Mheshimiwa Spika*, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira. Aidha, ninapenda kutoa pongezi kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake wa Awamu ya Tano. Mafanikio haya ni matokeo ya uongozi makini na thabiti katika masuala ya kiuchumi na kijamii. Katika awamu hii ya tano ya uongozi tumeshuhudia maendeleo makubwa katika sekta za afya, elimu, viwanda, nishati, madini na miundombinu. Aidha, katika kipindi cha uongozi wake Serikali imeweza kutimiza azma ya muasisi wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Dodoma. Vilevile, baadhi ya miradi mikubwa ya maendeleo inatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani. Miradi hii ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa ya kiwango cha kimataifa SGR, Ufufuaji wa Shirika la Ndege, Ujenzi wa vyanzo vipya vya umeme kama vile *Stiegler's Gorge*, Utoaji wa Elimu ya msingi bure na Ongezeko la bajeti ya Sekta ya afya. Haya ni mafanikio makubwa sana.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati ninapenda kuwashukuru: Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo anayotupa katika kusimamia masuala ya Muungano na kuhifadhi Mazingira; na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Uongozi wao thabiti unadhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri inayofanywa ya kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu.

4. **Mheshimiwa Spika**, ninawashukuru na kuwapongeza pia Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waheshimiwa Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni, ambazo zimetoa tathmini ya utekelezaji wa jumla katika masuala ya mipango na uchumi; utumishi na utendaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/18 na malengo na mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/19. Aidha, ninawashukuru waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu ya Muungano na Mazingira.

5. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutoa shukrani na pongezi za dhati kwa Bunge lako tukufu kwa kazi nzuri ambayo limeifanya kwa kipindi cha uongozi wako na pia ninakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza Bunge letu kwa hekima na busara kubwa. Ninampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu. Aidha, ninatoa pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kujiunga na Bunge lako tukufu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, ambao ni Mheshimiwa Janeth Masaburi (Mb.) Mbunge wa kuteuliwa, Dkt. Damas Ndumbaro (Mb.) Mbunge wa Songea Mjini, Mheshimiwa Justine Monko (Mb.) Mbunge wa Singida Kaskazini, Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa (Mb.) Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel (Mb.) Mbunge wa Siha na Mheshimiwa Maulid Mtulia (Mb.) Mbunge wa Kinondoni.

Ninawatakia heri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya.

6. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq (Mb.) na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mb.) pamoja na Waheshimiwa wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2018/19. Vilevile, ninatoa shukrani kwa wasemaji wakuu wa kambi ya upinzani kwa ushirikiano na michango yao katika kuboresha hoja hii.

7. **Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, marafiki na wananchi wa Jimbo la Songea Mjini, kwa kifo cha Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini kilichotokea mwezi Novemba 2017. Aidha, ninatoa pole za dhati kwa wananchi kwa ujumla kwa kuwapoteza ndugu zao na mali kutokana na ajali na maafa yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Ninaomba Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

8. **Mheshimiwa Spika**, sasa ninaomba kutoa maelezo ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 na malengo ya mwaka wa fedha 2018/19.

## **B: UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2018/19**

9. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake, Ofisi imeendelea kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015 - 2020); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi - CCM ya mwaka 2015 - 2020; Malengo ya

Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals – SDG*); Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; na maelekezo na miongozo mbalimbali inayotolewa na viongozi wakuu wa nchi.

## I. MASUALA YA MUUNGANO

10. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa kikatiba na kisheria ya kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Katika mwaka wa fedha 2017/18, kazi zifuatazo zilitekelezwa:- Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano; Kuratibu vikao vya kisekta vya masuala ya Muungano; Kufuatilia utekelezaji wa masuala ya Muungano ya kiuchumi, kijamii na kisiasa; Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano ili kuimarisha ushirikiano kati ya SMT na SMZ; na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano.

### **Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano**

11. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ imeendelea kuzitafutia ufumbuzi hoja zilizobakia chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tarehe 27 Novemba 2017, Ofisi ilizikutanisha sekta za Fedha, Uchukuzi na Biashara ili kuendelea kutafuta ufumbuzi wa hoja za sekta hizo. Katika sekta za fedha hoja zilizojadiliwa zilikuwa ni pamoja na: Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki; Taarifa ya Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha; na Mgawanyo wa mapato yatokanayo na faida ya Benki Kuu.

12. **Mheshimiwa Spika**, katika kikao hicho hoja za sekta ya Biashara zilizojadiliwa zilikuwa ni:- Upatikanaji wa fursa za masoko Tanzania Bara; Miradi inayohusu maendeleo ya wajasiriamali; Masuala ya viwango vya bidhaa hususan



ushirikiano wa Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS); Uasili wa viwango vya bidhaa vya Afrika Mashariki na fursa za miradi inayohusisha maendeleo ya viwango na ubora wa bidhaa; Kuondoa vikwazo vya biashara kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar; ushirikiano baina ya Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) na Mamlaka ya Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA); na Leseni za viwanda na masuala yahasuyo hati miliki.

13. **Mheshimiwa Spika**, suala lingine lililojadiliwa katika kikao hicho ni ushirikiano katika udhibiti wa vyombo vya moto. Suala hili si jambo la Muungano, hivyo, kila upande una sheria inayosimamia usajili wa vyombo vya moto. Ilikubaliwa kuwa kila upande ufanye marekebisho madogo ya Sheria zinazohusu usajili wa vyombo vya moto. Tayari maagizo haya yameanza kufanyiwa kazi na pande zote mbili za Muungano. Pamoja na kikao hicho, Ofisi iliratibu vikao vya kisekta vya kufuatilia utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa katika vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ.

14. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia meli mbili zilizokuwa zikipeperusha bendera ya Tanzania kukamatwa na kukutwa na makosa zikiwa nje ya nchi, Ofisi iliratibu vikao vya wataalamu kutoka SMZ na SMT ili kujadili changamoto za usajili wa meli katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kikao hicho ilikubaliwa kuwa Serikali itafanya uhakiki wa taarifa za meli zote zilizosajiliwa nchini ili kuondokana na changamoto hiyo. Aidha, Serikali imeazimia kupitia Sheria za ndani za usajili na kufanya uchunguzi wa kina wa meli zitakazoomba usajili ili kuepusha nchi kuingizwa tena katika fedheha.

15. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Ofisi itaendelea na uratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano pamoja na ufuatiliaji wa maelekezo na maagizo yanayotolewa katika vikao hivyo.

## Uratibu wa Masuala ya Kiuchumi, Kijamii na Kiasia

### Ufuatiliaji wa Miradi ya Pamoja ya Maendeleo

16. **Mheshimiwa Spika, katika** kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imeendelea kufuatilia miradi ya maendeleo inayotekelezwa pande zote za Muungano. Miradi hiyo inahusu sekta za elimu, afya, masoko, maji, miundombinu, mazingira, usafiri na usafirishaji. Miradi hiyo ni:- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund – TASAF III*); Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (*Market Infrastructure, Value Addition and Rural Finance - MIVARF*); Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Maeneo ya Pwani; na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA). Miradi hiyo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato.

17. **Mheshimiwa Spika, katika** mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaendelea na jukumu lake la kufuatilia utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo zinazotekelezwa pande zote za Muungano na kuhakikisha kuwa gawio la 4.5% linapelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

### Uratibu wa Masuala Yasiyo ya Muungano Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano

18. **Mheshimiwa Spika, katika** mwaka wa fedha 2017/18, sekta za pande mbili za Muungano zimefanya vikao vya ushirikiano, sekta hizo ni:- Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji tarehe 23 Agosti 2017 na tarehe 23 Machi 2018; Maliasili na Utalii tarehe 7 Februari 2018; Ujenzi, Uchukuzi na Usafirishaji tarehe 23 Agosti 2017, tarehe 25 Januari 2018, tarehe 28 Februari 2018 na tarehe 1 Machi 2018; na Sekta ya Kilimo ilikutana tarehe 22 - 23 Machi 2018. Vikao hivi ni mwendelezo wa jitihada zinazofanywa na Ofisi katika kuhamasisha sekta zisizo za Muungano kukutana na kujadili masuala yanayohusu sekta zao, kubadilishana uzoefu na wataalamu ili kupunguza changamoto, kuleta ufanisi na uwiano wa maendeleo kwa pande zote mbili za Muungano.

## Ziara za Kikazi

19. *Mheshimiwa Spika*, kwa kutambua umuhimu wa tunu tuliyoachiwa na waasisi wetu yaani Muungano, katika mwaka wa fedha 2017/18, Viongozi pamoja na wataalam walifanya ziara ya kikazi Zanzibar kwa lengo la kuimarisha ushirikiano baina ya SMT na SMZ. Aidha, Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar ilifanya ziara katika Taasisi 11 na kampuni mbili za Simu za Tanzania Bara. Ziara hizo zimesaidia kubadilishana uzoefu, kupata taarifa za utekelezaji wa changamoto za Muungano pamoja na kujifunza masuala mbalimbali ya kisekta.

20. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar tutapitia na kukamilisha mwongozo wa vikao vya ushirikiano vya kisekta kwa lengo la kuongeza ufanisi. Aidha, Ofisi imejizatiti kuongeza idadi ya ziara za kikazi.

## Elimu ya Muungano kwa Umma

21. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imeendelea kuelimisha umma kuhusu faida zinazotokana na Muungano kupitia radio, televisheni na magazeti. Aidha, kongamano la vijana kuhusu fursa zilizopo katika Muungano liliandaliwa na kufanyika Zanzibar tarehe 22 Oktoba 2017. Tathmini ya kongamano hilo ilionyesha uhitaji mkubwa wa elimu ya Muungano hususan kwa vijana. Vile vile, kuelekea maadhimisho ya miaka 54 ya Muungano, Ofisi imefanya mahojiano na viongozi wakuu wastaafu, wananchi pamoja na kuandaa kongamano la wanafunzi wa vyuo vya Elimu ya Juu vya Dodoma na warsha kwa wanafunzi wa shule za Msingi za Dodoma.

22. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaendelea kutoa elimu ya Muungano kwa makundi tofauti ya kijamii likiwemo kundi la vijana. Aidha, mkazo pia utatolewa katika kuandaa warsha na makongamano ili kuendelea kuamsha ari kwa makundi hayo juu ya umuhimu wa kuenzi, kuulinda na kuuimarisha Muungano wetu.

## II. HIFADHI ENDELEU YA MAZINGIRA

23. *Mheshimiwa Spika*, Sekta zote za uzalishaji mali zinategemea mazingira. Hivyo, rasilimali zitokanazo na mazingira zina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Hata hivyo, shughuli zisizo endelevu za uzalishaji mali zimechangia kwa kiasi kikubwa katika Uharibifu wa ardhi; Ukosefu wa maji safi na salama kwa wananchi wa mijini na vijijini; Uchafuzi wa mazingira; Upotevu wa bioanuai na makazi; Uharibifu wa mifumo ikolojia ya majini; Uharibifu wa misitu; na Mabadiliko ya tabianchi; Baadhi ya shughuli hizo ni: - ukataji holela wa miti, kilimo na ufugaji usio endelevu, uvuvi haramu, uzalishaji na utupaji holela wa taka, utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi.

24. *Mheshimiwa Spika*, kuna ushahidi wa wazi unaodhihirisha mazingira yetu si salama. Ushahidi huo ni pamoja na kuongezeka kwa hali ya jangwa na ukame, mafuriko, kuongezeka kwa magonjwa ya kuambukiza na mabadiliko ya hali ya hewa. Maendeleo endelevu hayawezi kupatikana bila kutunza mazingira. Ingawa jitihada kubwa za utunzaji wa mazingira zimefanyika hali ya mazingira nchini bado si ya kuridhisha na imekuwa tishio kwa mustakabali wa Taifa letu.

25. *Mheshimiwa Spika*, shughuli ya uhifadhi wa mazingira inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo: Teknolojia ya uhandisi jeni; Viumbe wageni vamizi; Biofueli; na Taka za kielektroniki Aidha, changamoto nyingine ni wataalam wa kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 katika ngazi zote; uelewa wa jamii kuhusu umuhimu na wajibu wa kuhifadhi mazingira; upatikanaji wa takwimu sahihi za mazingira kwa wakati; maeneo maalum ya kutupa taka; na utegemezi wa nishati ya kuni na mkaa.

26. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na changamoto hizi, Ofisi imeendelea kuchukua hatua za kukabiliana nazo ikiwa ni pamoja na kuteua Wakaguzi wa Mazingira kutoka taasisi na sekta nyingine, kutoa elimu kuhusu Mazingira kwa makundi tofauti, kufanya tafiti ili kupata taarifa na takwimu

zinazohitajika, kuhamasisha Halmashauri kutenga maeneo na kujenga miundombinu ya kutupa taka na kuhamasisha ubunifu katika teknolojia ya nishati mbadala.

### **Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 na Mkakati wa Utekelezaji**

27. *Mheshimiwa Spika*, Sera ya Taifa ya Mazingira (1997) imetumika kwa Miaka 20 tangu kutungwa kwake. Sera hii imekuwa na mafanikio katika utekelezaji wake ikiwa ni pamoja na: kutungwa na kutekelezwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake ambazo ziliweka mfumo wa kitaasisi na kisheria katika kusimamia masuala ya mazingira nchini. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Sera hiyo, changamoto mbalimbali zilijitokeza ambazo ni pamoja na kukosekana kwa matamko mahususi ya Kisera na kujitokeza kwa changamoto mpya za kimazingira ambazo zimeongeza kasi ya uharibifu wa Mazingira. Hivyo kutokana na changamoto hizi Ofisi inaendelea na mchakato wa kurekebisha Sera hiyo ili kuimarisha juhudi za uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

28. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imeboresha rasimu yamarekebisho ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na Mkakati wa utekelezaji kulingana na maoni ya wadau. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi inatarajia kukamilisha marekebisho ya Sera na Mkakati wa utekelezaji na kuanza kutumika.

### **Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira**

29. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imekuwa ikiratibu na kusimamia utoaji wa Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti iliyokuwa ikitolewa kwa washindi kila baada ya miaka miwili. Lengo la kutoa Tuzo hii ni kutoa motisha kwa watu binafsi, kampuni, Taasisi au vikundi vinavyojihusisha na hifadhi ya mazingira. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imeendelea kuboresha Tuzo hiyo na kuwa yenye mawanda mapana zaidi ya mazingira. Mwaka

wa fedha 2018/19, Ofisi itaendelea kuandaa utaratibu wa kushiriki pamoja na vigezo vya tuzo hii ili kutoa motisha kwa wadau wanaohifadhi mazingira na pia kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika utunzaji wa mazingira.

### **Ripoti ya Tatu ya Hali ya Mazingira Nchini**

30. *Mheshimiwa Spika*, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 inaelekeza kuandaliwa Ripoti ya Hali ya Mazingira nchini kila baada ya miaka miwili na kuwasilishwa Bungeni. Tangu kuanza kutekelezwa kwa Sheria hii, ripoti mbili zimeandaliwa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imeendelea na maandalizi ya Ripoti ya Tatu ya Hali ya Mazingira Nchini kwa kukusanya taarifa kutoka Wizara za kisekta, Mikoa, Halmashauri, Asasi za Kiraia na wadau wengine kwa ajili ya kuandaa rasimu ya ripoti hiyo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itakamilisha ripoti ya tatu ya hali ya mazingiranchini na kusambaza kwa wadau.

### **Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira**

31. *Mheshimiwa Spika*, Mfuko huu umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sur 191 na utakuwa chanzo muhimu cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kuhifadhi mazingira nchini. Baada ya Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira kuundwa, changamoto iliyojitokeza ni Mfuko ushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu kutokana na mapungufu ya Kisheria. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imependekeza marekebisho ya Sheria ili mfuko uweze kutekeleza majukumu yake. Aidha kwa kushirikiana na wadau imeendelea kubaini vyanzo vipya vya mapato ambavyo havitozwi na taasisi nyingine ili kuuwezesha Mfuko kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa kipindi cha 2018/19, marekebisho ya mapungufu ya kisheria yatakamilika, Mfuko utasajiliwa na kuanza kufanya kazi.

## Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani

32. **Mheshimiwa Spika**, kila mwaka tarehe 5 mwezi Juni, Dunia huadhimisha Siku ya Mazingira ili kutoa hamasa kwa watu kutunza mazingira. Kitaifa, maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka 2017 yalifanyika Butiama, Mkoani Mara, mahali alipozaliwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Lengo lilikuwa kumuenzi Baba wa Taifa kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuhifadhi mazingira ikiwemo kuanzisha msitu wake. Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani kwa mwaka huu yatafanyika nchini India na Kitaifa yatafanyika mkoani Dar es Salaam. Kaulimbiu ya Kimataifa ni **Beat Plastic Pollution** yaani dhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na plastiki. Kaulimbiu ya Kitaifa ni **Mkaa gharama, Tumia Nishati Mbadala**. Kaulimbiu hii inalenga zaidi kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala wa kuni na mkaa.

## Kupunguza Matumizi ya Mkaa Unaotokana na Miti

33. **Mheshimiwa Spika**, mkaa unaotokana na miti umeendelea kuwa chanzo kikubwa cha nishati hasa kwa kupikia, hivyo kuendelea kuchangia ukataji holela wa miti. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Serikali imeendelea na jitihada za kupunguza matumizi ya mkaa unaotokana na miti. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Ofisi kwa kushirikiana na wadau imeandaa mashindano ya ubunifu wa teknolojia ya nishati mbadala. Katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, mwaka huu kutakuwa na maonesho makubwa ya teknolojia za nishati mbadala. Ofisi itatangaza washindi wa ubunifu wa teknolojia hizo wakati wa kilele cha Maadhimisho hayo tarehe 05 Juni 2018, Jijini Dar es salaam.

34. **Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha 2018/19, Ofisi itaendelea kuzihamasisha Taasisi zote za Umma kusitisha matumizi ya mkaa na kuni na kuanza kutumia nishati mbadala, hususan gesi ya kwenye mitungi (*Liquified Petroleum Gas – LPG*), *Biogas* na nishati jadidifu ili kuhifadhi mazingira yetu. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati kupitia mradi wa Nishati Endelevu kwa Wote itaboresha na

kukamilisha rasimu ya Mkakati wa Tungamotaka (*National Biomass Energy Strategy*) na kuusambaza kwa wadau.

### **Matumizi ya Mifuko ya Plastiki**

35. *Mheshimiwa Spika*, dhamira ya Serikali ya kupiga marufuku uzalishaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya mifuko ya plastiki iliyotangazwa mwaka 2016, bado ipo kwa kuwa inalenga kupunguza madhara ya kiafya, mazingira na kwenye miundombinu yanayosababishwa na mifuko hiyo. Wazalishaji walipewa muda wa kutosha wa kuwawezesha kujiandaa na kubadili teknolojia. Katika mwaka wa fedha 2017/18, kazi zifuatazo zilifanyika: Ofisi ilikutana na wadau wanaozalisha na kufanya biashara ya mifuko ya plastiki nchini kwa lengo la kupata maoni yao pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya mifuko ya plastiki. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaendelea kuhamasisha utengenezaji, upatikanaji na matumizi endelevu ya mifuko mbadala na udhibiti wa uingizwaji wa mifuko ya plastiki kutoka nje ya nchi.

### **Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Mazingira**

36. *Mheshimiwa Spika*, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 inaelekeza kuundwa kwa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Mazingira (*National Environmental Advisory Committee – NEAC*) ambayo wajumbe watatoka katika sekta za Umma, Binafsi, Taasisi za Elimu ya Juu na Asasi za Kiraia. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imezindua rasmi Kamati hiyo na ilifanya kikao cha kwanza tarehe 19 Desemba 2017. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Kamati itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

### **Kuokoa Ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu**

37. *Mheshimiwa Spika*, Bonde la mto Ruaha Mkuu lina umuhimu mkubwa katika uchumi wa taifa hili. Inakadiriwa kuwa asilimia 26 ya maji yatakayotumika kufua umeme katika Mradi wa *Stiegler's Gorge* yatatoka katika mto Ruaha Mkuu. Kwa kutambua umuhimu wa Bonde hili na changamoto za



mazingira zilizojitokeza, mwezi Aprili 2017, Ofisi iliunda Kikosi Kazi cha Kitaifa ili kuokoa ikolojia ya bonde la mto huo. Taarifa ya Kikosi kazi iliwasilishwa kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na alitoa maelekeza ili kutekeleza mapendekezo hayo. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, na mapendekezo ya kikosi kazi ili kuokoa ikolojia ya bonde la mto huu.

38. **Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mapendekezo ya Kikosi Kazi imeonesha kuwa hali ya Bonde imeanza kuimarika baada ya hatua mbalimbali za udhibiti wa uharibifu kuchukuliwa ambapo jumla ya vyanzo vya maji 6,457 katika mikoa saba vilitambuliwa na kuwekewa mipaka na taratibu za kuvilinda kwa mujibu wa Sheria. Aidha, kaya 112 zilizovamia maeneo ya hifadhi ziliondolewa pamoja na mifugo 1,685. Vilevile, vibali 20 vya watumiaji wa maji visivyo halali vilifutwa na zoezi la kuhakiki vibali linaendelea; Uvunaji holela wa mazao ya misitu umedhibitiwa; Vijiji 82 vya Mikoa ya Iringa, Mbeya, Morogoro na Njombe vilivyomo ndani ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu vimewezeshwa kuandaa, kutekeleza na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi. Aidha, kazi ya kusafisha mifereji ya skimu za umwagiliaji imefanyika na inaendelea kufanyika ili kupunguza upotevu wa maji katika Bonde hili.

39. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mapendekezo ya kikosi kazi ili kuhakikisha hali ya mfumo-ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu inaendelea kuimarika.

### **Kutangaza Maeneo ya Mazingira-Lindwa na Tengefu**

40. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Ofisi ilianza taratibu za kuyatangaza baadhi ya maeneo nyeti na muhimu kwa mazingira na ikolojia nchini mwetu (*Environmentally Sensitive Areas*) na maeneo ya Mazingira

Tengefu (*Environmental Protected Areas*), kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 bila kuathiri matumizi endelevu ya maeneo haya. Hadi sasa, Ofisi imetambua maeneo 20 yaliyopendekezwa kuwa maeneo lindwa/tengefu. Kwa mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaanza mchakato wa kuwashirikisha wadau ikiwa ni pamoja na Halmashauri husika ili kuwezesha maeneo haya kutangazwa kuwa lindwa/tengefu.

### **Mkakati wa Kupambana na Uvuvi Haramu wa Kutumia Milipuko**

41. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha 2017/18, Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Kikosi Kazi cha Kuhifadhi Mazingira ya Bahari kwa kupambana na uvuvi haramu wa kutumia milipuko. Tathmini ya utekelezaji inaonesha kuwa kuna mafanikio katika kudhibiti uvuvi haramu wa kutumia milipuko, kwani matukio ya milipuko baharini yamepungua. Aidha, Ofisi imeandaa rasimu ya Mpango wa Elimu kwa Umma kuhusu Kudhibiti Uvuvi Haramu wa Milipuko. Kwa mwaka w fedha 2018/19, Ofisi itakamilisha Mpango wa Elimu kwa Umma kuhusu Kudhibiti Uvuvi Haramu wa Milipuko na kuimarisha kikosi kazi hicho ili kielelee kudhibiti uharibifu wa mazingira ya bahari.

### **Kampeni ya Upandaji miti**

42. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti. Katika kampeni hii kila Halmashauri ya Wilaya imeelekezwa kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka. Hata hivyo, katika kutekeleza kampeni hii, Ofisi imekabiliwa na changamoto ya ufuatiliaji na tathmini ili kujua idadi ya miti iliyopandwa na kukua. Katika kukabiliana na changamoto hii ofisi itaimarisha kampeni kwa kutoa motisha, na kuratibu ujumuishaji wa utekelezaji wa kampeni hii katika Mikakati na Mipango ya Halmashauri.

43. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha kwamba kampeni hii inafanikiwa na kuwa endelevu, Kamati ya Kitaifa

ya utekelezaji wa kampeni imeundwa. Kamati inajumuisha wajumbe kutoka Sekta ya umma, sekta binafsi na kampuni binafsi zikiwemo zinazopanda miti. Ninasisitiza kwamba kampeni hii izingatie kupanda na kutunza aina sahihi ya miti kulingana na eneo husika. Aidha, ninashauri tuongeze nguvu katika kutunza na kuhifadhi miti ya asili.

44. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza Kampeni hiyo, Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alizindua rasmi Programu ya kuifanya Dodoma kuwa ya Kijani tarehe 21 Desemba 2017, eneo la Mzakwe, Dodoma. Ofisi katika kuendeleza Kampeni hiyo tarehe 26 Januari 2018 ikishirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma na Jeshi la Kujenga Taifa ilipanda miti 30,000 katika kata ya Ng'ong'ona, Manispaa ya Dodoma. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaendelea kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia taasisi zilizo chini yake kuwajengea uwezo wadau kushiriki katika Kampeni ya Upandaji miti. Aidha, Ofisi itaendelea kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa programu ya upandaji miti katika mikoa yote ili hatimaye tuwe na Tanzania ya kijani. Kila Halmashauri inahimizwa kuendelea kupanda na kutunza angalau miti milioni 1.5 kila mwaka.

#### **Udhibiti wa Taka Ngumu Nchini**

45. **Mheshimiwa Spika**, moja ya changamoto ya kimazingira tunayokabiliana nayo ni udhibiti wa taka ngumu. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 (kifungu 114 – 119) inaelekeza majukumu ya Halmashari katika kudhibiti taka ngumu. Pamoja na jitihada zilizofanyika bado kumekuwa na changamoto kubwa katika eneo hili. Hivyo, Ofisi imechukua mtazamo mpya wa kuzifanya taka kuwa rasilimali kwa kuchakata na kurejeleza taka ngumu. Katika mwaka 2017/18, Ofisi imeandaa Mwongozo wa Uwekezaji katika Taka Ngumu ili kuwawezesha wawekezaji kupata taarifa muhimu watakapohitaji kuwekeza. Mwongozo umeainisha fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta hii ikiwemo ukusanyaji; usafirishaji na urejelezaji wa taka ngumu; kutumia taka kama mali ghafi ya kutengenezea

mbolea aina ya mboji; uzalishaji wa nishati ya umeme; madampo ya kisasa; kutibu majitaka na uteketezaji wa taka hatarishi. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi inakusudia kusambaza mwongozo huu kwa wadau na kufuatilia utekelezaji wake.

### **Usimamizi wa Taka Zenye Madhara**

46. *Mheshimiwa Spika*, taka hatarishi zinazalishwa viwandani, migodini, hospitalini na baadhi ya maeneoya biashara. Ofisi imeendelea kudhibiti uzalishaji na utupaji wa taka zenye madhara kwa mujibu wa Kanuni za Udhibiti wa Taka zenye Madhara za mwaka 2009. Aidha, Ofisi imeendelea kutoa vibali vya kukusanya, kusafirisha na kurejeleza taka kwa kampuni zilizokidhi vigezo, ambapo hadi mwezi Machi 2018, vibali 60 kati ya maombi 70 vimetolewa. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaendelea kuimarisha usimamizi wa taka hatarishi kwa kuwahimiza wadau kupunguza uzalishaji wa taka hizo na kudhibiti uteketezaji na utupaji wake.

### **Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK)**

47. *Mheshimiwa Spika*, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 inaelekeza kufanya TMK ya Rasimu za Sera, Miswada ya Sheria, Mikakati na Programu, zinazoweza kuwa na athari katika Mazingira. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imeendelea kutoa vibali vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK) kwa mujibu wa sheria. Katika kipindi hicho, Ofisi imetoa jumla ya vibali 12 vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati. Aidha, Ofisi iliandaa orodha ya maeneo yanayopaswa kufanyiwa TMK na kuwajulisha wadau kuhusu haja ya kufanya TMK. Maeneo hayo ni pamoja na Ujenzi wa Reli; Miundombinu ya umwagiliaji; Hifadhi za wanyamapori; Makambi ya wakimbizi; Utafiti wa mafuta na gesi na maeneo ya uchimbaji wa madini. Mipango miji; rasimu za Sera, miswada ya Sheria na Kanuni.

48. *Mheshimiwa Spika*, ninapenda kuwakumbusha mamlaka zote kuwa suala la TMK liko kisheria na linapaswa kutekelezwa. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaendelea kufuatilia utekelezaji wa suala hili.

## **Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*Global Enviroment Facility - GEF*)**

49. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi imeendelea na uratibu wa shughuli za Mfuko wa Mazingira wa Dunia hapa nchini. Katika kipindi cha 2017/18, Ofisi imeratibu maandalizi ya miradi kwa ajili ya Mzunguko wa Saba wa Ufadhili (GEF - 7, 2018 – 2022). Aidha, ufuatiliaji wa fedha za utekelezaji wa miradi iliyoidhinishwa na GEF umefanyika. Ofisi ilibuni miradi ambayo kwa sasa imeanza kutekelezwa, miradi hiyo ni mradi wa Kuhifadhi Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa na Mradi wa Kuzuia Uharibifu wa Ardhi na Kuongeza Usalama wa Chakula. Katika kipindi hiki, Ofisi imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi hii.

50. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19 Ofisi itaendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mazingira wa Dunia hapa nchini. Aidha, Ofisi itashirikiana na wadau wengine kuendelea kuandaa miradi mbalimbali na kufuatilia utekelezaji wa miradi iliyopatiwa fedha.

## **Uratibu na Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda ya Mazingira**

51. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na Wadau wa Maendeleo, imeendelea kuratibu na kutekeleza Mikataba ya Mazingira ya Kimataifa na Kikanda ifuatayo: -

## **Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na Itifaki ya Kyoto**

52. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutumia fursa hii kuwajulisha watazania kuwa Bunge lako tukufu limeridhia Makubaliano ya Paris tarehe 3 Aprili, 2018(*The Paris Agreement under the UN Framework Convention on Climate Change*). Makubaliano haya yatasaidia kuimarisha utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi.

53. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa

fedha 2017/18, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa miradi miwili ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi iliyo chini ya Mkataba huu. Miradi hiyo ni: Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii za Pwani Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi; na Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Jiji la Dar es Salaam.

54. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imeendelea kutekeleza mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Jiji la Dar es Salaam. Kupitia mradi huu ukuta wa fukwe wa bahari wenye urefu wa mita 920 katika Barabara ya Obama na ukuta wa bahari wenye urefu wa mita 500 katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere umejengwa. Aidha, huduma muhimu kama vile vyoo, taa za usalama na sehemu za kupumzikia zimewekwa katika eneo la mradi.

55. **Mheshimiwa Spika**, kupitia mradi huu, mitaro/ mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 475 katika maeneo ya Bungoni, Manispaa ya Ilala na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 550 katika Manispaa ya Temeke imejengwa. Mirefeji hiyo pia imewekwa vivuko vya waenda kwa miguu.

56. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii za Pwani Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi. Kupitia mradi huu ukuta wa mita 600 katika ufukwe wa Pangani Tanga na ukuta wa mita 50 katika ufukwe wa Kisiwa Panza, Pemba umejengwa. Aidha, makinga mawimbi (*Groynes*) yamejengwa katika eneo la Kilimani-Unguja. Vilevile, mikoko imepandwa katika wilaya ya Rufiji (hekta 792), wilaya ya Pangani (hekta 10) na Zanzibar (hekta 235). Kazi nyingine zinazoendelea kufanyika ni uchimbaji wa visima 10 pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua katika shule za Sekondari Kingani na Matipwiri, Bagamoyo.

57. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Ofisi inatarajia kuendelea kutekeleza miradi mingine chini ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi kama ifuatavyo: -

i. Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Vijijini kupitia Mfumo Ikolojia (*Ecosystem-Based Adaptation for Rural Resilience in Tanzania*). Mradi utatekelezwa katika maeneo ya Kishapu, Mpwapwa, Mvomero, Simanjiro na Kaskazini A Unguja ; na

ii. Mradi wa kujenga uwezo wa kitaasisi katika kuhuisha taarifa za mabadiliko ya tabianchi kwenye usimamizi wa mipango ya maendeleo (*Institutional support for climate and seasonal weather information for adaptation planning in Northern Tanzania*).

58. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi iliendelea na mchakato wa kuwezesha sekta za umma na binafsi hapa nchini kupata ithibati (*accreditation*) katika Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi, *Green Climate Fund – GCF*. Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Baraza lilisajiliwa na Bodi ya Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (*Adaptation FundBoard*) kuwa msimamizi wa kitaifa wa shughuli za Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (*National Implementing Entity for Adaptation Fund*). Vilevile, Ofisi ilizijengea uwezo taasisi katika sekta za umma na binafsi kuhusu fursa za kupata fedha za kutekeleza miradi ya mazingira kutoka mifuko mbalimbali ya mazingira duniani.

59. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaendelea kuratibu uchambuzi wa miradi chini ya ufadhili wa Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi na kuhamasisha sekta binafsi, taasisi za umma na mashirika ya kitaifa kuandaa miradi ya mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Ofisi itaendelea kuhamasisha wizara, taasisi, sekta binafsi na benki kuomba ithibati (*accreditation*) ili kuiwezesha Tanzania kupata fedha chini ya mfuko huu bila kupitia taasisi za kimataifa (*International Accredited Entities*) na hivyo kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi. Katika utekelezaji wa mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, hadi sasa Tanzania imenufaika kwa kutekeleza miradi yenye thamani ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 300.

## Mkataba wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame

60. *Mheshimiwa Spika*, nchi yetu inakabiliwa na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame hivyo tunashiriki katika mkataba wa kimataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame. Katika kipindi cha 2017/18, Ofisi imeratibu maandalizi ya Programu ya Kitaifa yenye madhumuni ya kufanya tathmini ya maeneo yaliyoathirika ili kuweka malengo ya kuzuia uharibifu wa ardhi (*Land Degradation Neutrality Target setting*) ifikapo mwaka 2030. Kwa mwaka 2018/19, Ofisi itakamilisha maandalizi ya mradi wa kuongoa maeneo yaliyoharibika kwa ajili ya kupatiwa fedha za utekelezaji.

## Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai

61. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania ina utajiri wa viumbe hai wa aina tofauti. Ili kulinda na kutunza bioanuai hiyo, Tanzania inashiriki katika Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai. Katika mwaka wa fedha 2017/18, nimeteua wakaguzi sita wa kusimamia matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa. Aidha, Ofisi imeendelea kukusanya taarifa za utekelezaji wa Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai 2015 - 2020 (*National Biodiversity Strategy and Action Plan*). Taarifa hizi zitatumika katika maandalizi ya Mpango kazi wa Taifa wa Kuhifadhi Mazingira 2019 - 2023. Vilevile, katika kipindi hiki, Ofisi imetoa kibali cha kufanya utafiti wa mahindi yanayovumilia ukame na wadudu waharibifu aina ya Bungua katika Kituo cha Makutupora. Lengo la utafiti huo ni kupata matokeo yatakatayowezesha kutoa maamuzi sahihi kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa.

62. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha 2018/19, tutaendelea kukuza uelewa wa jamii pamoja na kujenga uwezo wa wataalam kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa nchini. Vilevile, Ofisi itaendelea kuratibu ukaguzi katika maduka ya vyakula na maeneo mengine ili kuhakikisha bidhaa zenye viambata vya mazao



yatokanayo na teknolojia ya uhandisi jeni (*Genetic Engineering*) zinadhhibitiwa nchini.

### **Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi**

63. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba na Itifaki zake. Katika mwaka 2017/18, Ofisi imeanza kukusanya maoni ya wadau kwa lengo la kufanya mapitio ya Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa Mwaka 2006 na Mkakati wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa wa mwaka 2008.

64. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaratibu maandalizi ya miradi ya utekelezaji wa Mpango wa Mkataba wa Nairobi wa Uhifadhi wa Mazingira ya Bahari ya Hindi Kutokana na Vyanzo na Shughuli Zinazofanyika Nchi Kavu (*The Strategic Action Programme for the Protection of the West Indian Ocean from land based sources and activities - WIOSAP*) inayolenga kupunguza uchafuzi wa bahari na ukanda wa pwani na Programu ya Kuwianisha Sera na Kuimarisha Taasisi Zinazosimamia Hifadhi ya Mazingira ya Bahari (*Strategic Action Programme Policy Harmonization and Institutional Reforms - SAPPHIRE*).

### **Mkataba wa Basel Kuhusu Udhhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka za Sumu Kati ya Nchi na Nchi**

65. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18, Ofisi imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mkataba huu. Kupitia mkataba huu, Ofisi imeweza kudhibiti uingizwaji wa taka zenye madhara hapa nchini na pia kusimamia usafirishwaji wa taka hizo kupitia nchini kwenda nchi nyingine bila kuleta madhara kwenye mazingira yetu. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaendelea kuratibu Mkataba huu na kushirikiana katika nyanja za teknolojia rafiki katika usimamizi wa taka hatarishi.

### **Mkataba wa Stockholm Kuhusu Udhhibiti wa Kemikali Zinazodumu Katika Mazingira kwa Muda Mrefu**

66. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm hapa nchini. Katika jitihada za kuzuia madhara ya kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu, Ofisi imeingia makubaliano na kituo cha *Africa Institute* kilichopo Afrika ya Kusini kwa kushirikiana na Shirika la Usambazaji Umeme Tanzania - TANESCO kwa ajili ya kuondoa kemikali aina ya *Polychlorinated Biphenyls – PCBs* zilizokuwa zikitumika kwenye transfoma. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaendelea kuratibu zoezi la kuondoa kemikali hizo.

### **Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

67. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi iliratibu ukusanyaji wa takwimu za uingizaji na matumizi ya kemikali mbadala wa zinazoharibu tabaka la Ozoni. Takwimu hizi zitasaidia kupanga mikakati ya kusitisha matumizi ya kemikali zinazoharibu tabaka la Ozoni. Aidha, tuliadhimisha Siku ya Tabaka la Ozoni tarehe 16 Septemba 2017 na kutoa mafunzo kwa mafundi mchundo na maafisa forodha 60. Katika kipindi cha mwaka 2018/19, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba huu ili kuzuia matumizi ya kemikali zinazoharibu tabaka la Ozoni na kuepusha madhara ya uharibifu wa tabaka hilo.

### **Mkataba wa Minamata Kuhusu Udhhibiti wa Matumizi ya Zebaki**

68. *Mheshimiwa Spika*, matumizi ya Zebaki katika shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini huhatarisha afya za binadamu na viumbe hai pale inapotumika kuzingatia taratibu. Katika kipindicha mwaka 2017/18, Ofisi imekamilisha ukusanyaji wa takwimu kwa ajili ya kuandaa Mpango-Kazi wa kitaifa wa kupunguza

matumizi ya Zebaki nchini. Katika mwaka 2018/19, Ofisi itakamilisha Mpango-Kazi wa kitaifa wa kupunguza matumizi ya Zebaki na kutoa elimu kwa wadau kuhusu utekelezaji wake. Aidha, Kanuni za Usimamizi wa Matumizi ya Zebaki na Viambata vyake zitaandaliwa.

### **Elimu kwa Umma Kuhusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira**

69. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya mazingira katika maadhimisho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Vilevile, elimu kwa umma imetolewa kupitia magazeti, televisheni, mitandao ya kijamii na ziara za viongozi na wataalamu kwa lengo la kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Aidha, Baraza limeanza kuchapisha Jarida la Mazingira *Environmental Newsletter* ambalo litakuwa linatoka kila robo mwaka.

70. *Mheshimiwa Spika*, katika kukuza uelewa kuhusu masuala ya hifadhi ya mazingira mada ziliwasilishwa kupitia vikao vya Kamati za ushauri za Mikoa na kwa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi itaandaa mkakati wa mawasiliano na elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira na kuendelea kutoa elimu na kujenga uelewa kuhusu hifadhi ya mazingira kwa makundi tofauti. Aidha, kwa Mujibu wa kifungu cha 174 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191, Ofisi itaanzisha mfumo Mkuu wa Taarifa kuhusu Mazingira (*Central Environmental Information System*) utakaoendana na mfumo wa teknolojia ya simu kuwawezesha watumiaji kupokea na kutoa taarifa zinazohusu masuala ya Mazingira.

### **III: BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

71. *Mheshimiwa Spika*, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ni msimamizi mkuu wa uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

## Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira

72. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18, Baraza limeendelea kusimamia na kutekeleza shughuli za uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake kwa kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi 627 katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Pwani, Morogoro, Kigoma, Tabora, Dar es Salaam, Tanga, Geita, Mwanza, Dodoma, Songwe, Iringa, Lindi, Kagera, Mbeya, Ruvuma, Singida, Mara, Shinyanga, Simiyu na Mtwara. Miradi 179 iliyokiuka Sheria ilichukuliwa hatua stahiki. Hatua hizo ni pamoja na kutoa maelekezo, maonyo, amri za katazo, amri za urejeshaji wa mazingira na baadhi walifikishwa mahakamani. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Baraza litaendelea kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi ya uwekezaji na kuchukua hatua stahiki kwa wataokiuka Sheria hiyo.

73. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18, Baraza limeshughulikia malalamiko 207 ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira kutoka kwa wananchi. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Baraza litaendelea kuwakumbusha na kuwaelimisha watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutatua changamoto na malalamiko ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira yanayotokea katika maeneo yao.

74. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18, Baraza kwa kushirikiana na Chuo cha Madini na Halmashauri za Wilaya husika katika mikoa ya Geita na Shinyanga limefanya tathmini kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu ili kuhakiki iwapo wanazingatia Sheria na Kanuni zake. Tathmini hii ilihusisha wachimbaji wadogo wanaotumia Zebaki na wachenjuaji wanaotumia Sayanaiidi (*Cyanide*). Katika mwaka wa fedha 2018/19, Baraza kwa kushirikiana na wadau husika litaendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kutatua changamoto zilizobainika katika tathmini hiyo.

75. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, sura 191 nimeteua wakaguzi 452 kutoka katika taasisi za Umma na Serikali za Mitaa. Hadi sasa jumla ya wakaguzi 512 wameteuliwa. Mwaka wa fedha 2017/18, Baraza limetoa mafunzo kwa wakaguzi wa mazingira 128 kati ya wakaguzi walioteuliwa. Wakaguzi hawa watasaidia kuongeza uwezo wa Serikali kusimamia hifadhi ya mazingira. Mafunzo kwa Wakaguzi waliobaki yatafanyika katika mwaka wa fedha 2018/19.

76. **Mheshimiwa Spika**, Baraza limesimamia uteketezaji wa taka hatarishi kutoka katika Vyuo Vikuu, Viwanda, Gereza, Mgodi, Uwanja wa Ndege na Maduka ya Madawa. Aidha, Baraza limesimamia uteketezaji wa madawa chakavu yenye uzito wa tani 244.617 na lita 97 kwenye mtambo wa Tindwa *Incinerator*, Mgodi wa Buzwagi, Hospitali ya Muhimbili (Kampasi ya Mloganzila) na *Safe Waste Incinerator* ya Mkuranga. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Baraza litaendelea kuboresha usimamizi wa utupaji taka hatarishi.

### **Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM)**

77. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Baraza limesajili jumla ya miradi 1,176 kwa ajili ya kufanyiwa mchakato wa kupata hati za TAM. Miradi 533 imepewa vyeti kati ya miradi iliyosajiliwa. Vilevile, hadi kufikia Desemba 2017, Baraza limesajili wataalamu elekezi wa TAM 757, Wakaguzi wa Mazingira (*Environmental Auditors*) 357, Kampuni za Ushauri wa TAM 152 na za Ukaguzi wa Mazingira 74. Aidha, Baraza limekamaliza maandalizi ya Mfumo wa kuchakata TAM kwa njia ya mtandao. Mfumo huo unatarajiwa kuanza kutumika baada ya mafunzo na majaribio kukamilika. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Baraza litaendelea kusajili miradi kwa ajili ya mchakato wa TAM, kusajili wataalam wa TAM na Wakaguzi wa Mazingira pamoja na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali kuhusu mchakato wa TAM.

78. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na malalamiko ya wawekezaji kucheleweshewa kupata cheti cha TAM, Baraza limechukua hatua zifuatazo ili kuharakisha utoaji wa vyeti: -

- i. Kutengeneza orodha ya mambo muhimu ya kuzingatia (*checklist*) ya miradi ya majengo chini ya ghorofa tatu, viwanda na umeme jua;
- iii. Kutoa vibali vya muda (*Provisional permit*) kwa miradi ya viwanda;
- iii. Kupunguza gharama za TAM; na
- iv. Kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya kanuni za TAM na ukaguzi za mwaka 2005.

79. **Mheshimiwa Spika**, Baraza limekuwa likishiriki katika hatua zote za utekelezaji wa miradi mikubwa ya kitaifa kama vile, mradi wa kufua umeme wa *Stiegler's Gorge* na mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi (*East African Crude Oil Pipeline*). Baraza litaendelea kushirikiana na wawekezaji katika sekta muhimu za kiuchumi ili kuhakikisha kuwa miradi yao inafuatiliwa kwa karibu na kupata hati kwa muda mfupi.

### **Mipango na Utafiti wa Mazingira**

80. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Baraza limeendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira (*National Environmental Research Agenda – NERA 2017 - 2022*) kwa kufanya tathmini ya hali ya mazingira kwenye maporomoko ya ardhi katika milima ya Mamba Miamba iliyopo Wilayani Same - Kilimanjaro kwa kushirikiana na wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kamisheni ya Matumizi ya Ardhi, Taasisi ya Huduma za Misitu na Halmashauri ya Wilaya ya Same. Utafiti huo umebaini chanzo cha maporomoko hayo ni aina ya udongo wa mfinyanzi uliopo katika eneo hilo pamoja na shughuli za kibinadamu zinazofanyika huko ikiwa ni pamoja na ukataji holela wa miti na uchomaji moto hovy katika maeneo hayo. Aidha, Baraza limepeleka mapendekezo ya kuzuia uharibifu wa mazingira katika eneo hili kwa wadau ili hatua thabiti za uhifadhi zichukuliwe, ikiwa ni pamoja na

kuangalia uwezekano wa kulitangaza eneo hilo kuwa ni eneo tete la mazingira (*Environmental Sensitive Area*) na kulitengenezea mpango wa kudhibiti uharibifu wa mazingira.

81. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Baraza limefanya utafiti wa uharibifu wa mazingira wa Bwawa la Mindu lililopo katika Manispaa ya Morogoro na mmonyonyoko wa ardhi katika fukwe za Ziwa Viktoria. Matokeo ya tafiti hizo yalibainisha vyanzo mbalimbali vya uharibifu na kupendekeza hatua za kuchukuliwa. Aidha, Baraza limefanya utafiti wa namna ya kuboresha mazingira ya mji wa Dodoma ili uwe 'mji wa kijani' kwa kutumia dhana za *green city, eco-buildings* na *sustainable construction*.

82. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Baraza limeendelea kuratibu shughuli za Hifadhi Hai (*Biosphere Reserves – BRs*). Aidha, Baraza limewasilisha taarifa za awali UNESCO kwa ajili ya kuingiza Hifadhi ya Gombe Ugalla -Masito kwenye mtandao wa Hifadhi Hai za Dunia. Vilevile, Baraza limeandaa Mpango wa Usimamizi wa Mazingira (*Environmental Management Plan - EMP*) kwa maeneo mawili ambayo ni Dakio la Bonde la Kihansi na eneo la Ziwa Chala – Jipe. Aidha, Baraza limekamilisha zoezi la uwekaji mipaka katika eneo la Kihansi ambalo linatarajiwa kutangazwa kuwa eneo lindwa la kimazingira (*Environmental Protected Areas –EPAs*).

83. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Baraza litaendelea kukusanya takwimu na na kuandaa taarifa za hali ya mazingira ya milima hapa nchini; Taarifa ya Mazingira ya Pwani (*State of the Coastal Environment Report – SOCR, 2018*); Utafiti wa mifumo ya ikolojia ya hali ya mabonde ya mito mikubwa, maeneo ya malisho ya mifugo na wanyamapori.

### Uratibu wa miradi ya Kuhifadhi Mazingira

84. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Baraza limeendelea kutekeleza na kuratibu miradi miwili kwa kupitia fedha za wafadhili. Miradi hiyo ni:

- i) Mradi wa Kuhifadhi Lindimaji la Bonde la Kihansi pamoja na dakio lake (*Kihansi Catchment Conservation Management Project - KCCMP*); na
- ii) Mradi wa kujenga uwezo wa sekta za mafuta na gesi (*Energy Sector Capacity Building Project - ESCABP*).

#### IV. MASUALA MTAMBUKA, (UTAWALA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU)

85. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi yetu imetekeleza maamuzi ya Serikali ya kuhamia Dodoma. Mnamo tarehe 15 Desemba, 2017 Mheshimiwa Makamu wa Rais alihamia rasmi Dodoma akiambatana na watumishi 127 wa Ofisi hii. Hivyo, shughuli zote zinazohusu Ofisi ya Makamu wa Rais zinafanyika Dodoma kwa sasa. Ofisi itakamilisha taratibu za kuhamisha watumishi wachache waliobaki Dar es Salaam ndani ya mwaka wa fedha 2017/18.

86. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utendaji kazi na kukabiliana na changamoto za uongozi katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi imeendelea na jitihada za kuimarisha uongozi wa Baraza ili kuboresha uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191.

87. **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2017/18, Ofisi pia imeendelea kuwawezesha watumishi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika kipindi hiki watumishi 97 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kuongeza ufanisi. Aidha, watumishi 23 wamepandishwa vyeo na watumishi wanane wamethibitishwa kazini.

88. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi imeajiri watumishi wapya wanne wa kada tofauti. Aidha, Mfumo wa Wazi wa Utendaji Kazi na Upimaji OPRAS umezingatiwa kwa watumishi wote kujaza fomu na kufanyiwa tathmini. Vilevile, Ofisi iliendelea



ushirikishwaji wa watumishi katika maamuzi na mipango ya Ofisi kupitia vikao vya menejimenti, Idara na Baraza la Wafanyakazi. Kupitia vikao hivyo, hoja mbalimbali za watumishi zilijadiliwa na kupatiwa ufumbuzi.

89. **Mheshimiwa Spika**, mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi itaendelea kutoa elimu ya UKIMWI kwa watumishi na kuwashawishi kupima afya zao kwa hiari na kuwapatia huduma zinazostahili kwa waliojitokeza na kuthibitika kuwa na VVU. Ofisi itaendelea kusimamia maadili ya Utumishi wa Umma na kuwashirikisha watumishi katika maamuzi na mipango ya Ofisi kupitia vikao na mabaraza ya wafanyakazi. Ofisi pia itawawezesha watumishi kuhudhuria mafunzo kulingana na taaluma na majukumu yao ya kazi. Ofisi itaajiri watumishi wapya wa kada tofauti ili kuongeza nguvu-kazi. Aidha, ofisi itawapandisha vyeo watumishi wanaostahili.

#### **Utawala na Maendeleo ya Rasilimaliwatu –NEMC**

90. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Baraza limewapatia watumishi wake vitendea kazi. Aidha, kupitia mradi wa ESCBP, Baraza limepata vifaa kwa ajili ya ukaguzi, ufuatiliaji na upimaji wa sampuli pamoja na vifaa vya maabara kwa ajili ya kufanyia uchunguzi.

91. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, wafanyakazi wamepata fursa ya kuhudhuria mafunzo mbalimbali. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, limetoa mafunzo kwa wafanyakazi 15 wa Baraza kwa ajili ya kuwajengea uwezo katika utumiaji wa mashine aina ya *Atomic Absorption na Gas Chromatography*.

92. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Baraza litaendelea kujenga uwezo wake kwa njia ya mafunzo, ajira mpya pamoja na kuboresha mazingira ya kazi na vitendea kazi.

## C: HITIMISHO NA SHUKRANI

93. *Mheshimiwa Spika*, kama tunavyoelewa nchi yetu ni ya Muungano. Muungano wetu una umuhimu wa pekee kwa Taifa letu na umekuwa ni utambulisho wa taifa letu na kielelezo cha umoja wetu katika kudumisha amani na usalama wa nchi yetu. Ninatoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kuuthamini, kuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano ili jitihada za kusukuma mbele maendeleo kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa faida ya pande zote mbili ziendelee kufanikiwa.

94. *Mheshimiwa Spika*, chini ya uongozi wa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Makamu wake, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Muungano wetu unaendelea kuimarika na kushamiri. Chini ya uongozi wao hakuna changamoto yoyote inayoweza kutufarakanisha, kututenganisha wala kuturudisha nyuma. Ofisi yetu inayo faraja kubwa kwamba, katika nchi yetu sasa, kwa watu wa itikadi zote na kutoka pande zote za Muungano, mjadala sio uhalali wa Muungano bali mbinu za kuuimarisha. Ofisi na Serikali kwa ujumla itaendelea kuyafanyia kazi maoni na mawazo ya watu wote wenye nia ya kuona Muungano wetu unashamiri.

95. *Mheshimiwa Spika*, mazingira pia ni muhimu na yana mchango mkubwa katika mustakabali wetu na maendeleo ya uchumi wa viwanda. Ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kuwa mazingira na maliasili za nchi yetu zinalindwa na kuhifadhiwa. Ofisi ina dhamira ya kuendelea na utaratibu wa kumshirikisha kila Mtanzania katika wajibu huu ili ulinzi na hifadhi ya mazingira lisiwe suala la shuruti bali la utamaduni. Ninapenda kutoa wito kwa wananchi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kuwa dhamira ya Serikali ya kulinda na kuhifadhi mazingira inazingatiwa

na kupewa kipaumbele kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

96. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Ofisi itaendelea kushika hatamu kwa uthabiti katika wajibu wake wa usimamizi na uratibu wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Tutaendelea kutoa miongozo ya hifadhi ya mazingira katika sekta na nyanja mbalimbali. Lengo ni kuongoza hifadhi ya mazingira kwa namna pana zaidi, kwa kuangalia mifumo ya ikolojia, mifumo ya uzalishaji mali, na mifumo ya uchumi wa matumizi ya rasilimali asili.

97. **Mheshimiwa Spika**, ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru walionisaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Shukrani zangu za dhati na za kipekee ni kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake na dira na mwelekeo aliotupatia kuhusu majukumu yetu. Vilevile, ninamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini uliotuwezesha kutekeleza majukumu yetu. Ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, (Mb.), Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano alionipa katika utekelezaji wa kazi za Ofisi. Aidha, ninapenda kuwashukuru Mhandisi Joseph K. Malongo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais; Bi Butamo K. Phillip, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais; Ndugu Ali Mufuruki, Mwenyekiti wa Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Mazingira na Wajumbe wa Bodi ya Mfuko huo; Dkt Vedasto Makota, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Wakuu wa Idara na Vitengo; na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza kwa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu. Pia ninawashukuru wale wote waliotwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita, na ambao wametwezesha kuandaa Mpango wa mwaka wa fedha 2018/19.

98. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imefanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo. Ninapenda kuwataja baadhi ya washirika wa maendeleo ambao Ofisi imefanya nao kazi kwa karibu kama ifuatavyo: Serikali ya Norway; Serikali ya Kanada; Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea; Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*); Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (*UNEP*); Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*Global Environment Facility - GEF*); Shirika la Umoja wa Mataifa la Huduma za Miradi (*United Nations Office for Project Services-UNOPS*); Benki ya Dunia (*WB*); Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*); Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*); Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la Denmark (*DANIDA*); *World Wide Fund for Nature - WWF*; Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo (*IFAD*); Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund - GCF*); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (*GIZ*); Kikundi cha Washirika wa Maendeleo kinachoshughulikia Mazingira (*DPGE*); Asasi Zisizo za Kiserikali (*AZISE*); na sekta binafsi zikiwemo Kampuni ya Tatu - Mzuka na Coca cola. Aidha, ninapenda nitumie fursa hii kuwaomba washirika wa maendeleo kuendelea kutoa ushirikiano katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi katika kulinda na kuimarisha Muungano wetu na kulinda na kuhifadhi mazingira, yetu.

#### **D: MAOMBI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19**

99. *Mheshimiwa Spika*, ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2018/19, kama ifuatavyo:

#### **Fungu 26: Makamu wa Rais**

100. *Mheshimiwa Spika*, ninaomba Bunge lako tukufu

liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya shilingi 6,308,631,000 fedha za Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2018/19. Kiasi hiki kinajumuisha fedha za Mishahara ya watumishi shilingi 1,053,666,000 na fedha za Matumizi Mengineyo shilingi 5,254,965,000.

### Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais

101. **Mheshimiwa Spika**, ninaomba Bunge lako tukufu, liidhinishe makadi makadirio ya matumizi ya shilingi 14,784,456,560 kwa Fungu hili. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi 9,721,116,560 fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi 5,063,340,000 fedha za Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha shilingi 5,942,065,000 fedha za mishahara na shilingi 3,779,051,560 fedha za Matumizi Mengineyo. Fedha za Mishahara zinajumuisha shilingi 3,017,072,000 za ruzuku ya Mishahara ya watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha Fedha za Ndani shilingi 3,000,000,000 na Fedha za Nje shilingi 2,063,340,000.

102. **Mheshimiwa Spika**, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, hoja imeungwa mkono. Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ili awasilishe taarifa, Mheshimiwa Amina Mollel kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria.

**MHE. AMINA S. MOLLEL K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kusimama mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 6(2)(c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 imeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Aidha, Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti ya Wizara inazosisimamia. Jukumu hili la uchambuzi wa bajeti linaenda sambamba na jukumu la ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) ina mafungu mawili ya bajeti ambayo ni:-

- (i) Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais; na
- (ii) Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais;

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne yafuatayo:-

- (i) Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(ii) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2018/2019; na

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018; Fungu namba 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais; kwa kuzingatia muundo na majukumu ya Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais (Muungano) hakukuwa na bajeti ya miradi ya maendeleo katika fungu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu namba 31, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano); katika kutekeleza Kanuni ya 98(1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Orodha ya Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mradi namba 6309 - ujenzi wa ofisi na nyumba ya makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar (*Construction of Vice President Office and Residence in Zanzibar*) ambao uliidhinishiwa shilingi milioni 400; na

(ii) Mradi namba 6389 - ujenzi na ukarabati wa ofisi na makazi ya Makamu wa Rais, Luthuli II (*Construction and Rehabilitation of Vice President Office Luthuli II and State Lodges*) ambao uliidhinishiwa shilingi milioni 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano ya tarehe 26 Machi, 2018 miradi hiyo miwili haikupokea kiasi chochote cha fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 26 Machi, 2018 Kamati ilipokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa

bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ulitazama mlinganisho kwa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili, 2017 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi, 2018 katika robo ya tatu ya mwaka huu wa fedha 2017/2018. Uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 na kiasi cha fedha kilichopokelewa katika miradi ya maendeleo hadi kufikia Machi, 2018. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu mwelekeo wa mpango wa bajeti ya mapato na matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kutoka Hazina ni kama ifuatavyo; katika mwaka wa fedha 2017/2018, Fungu namba 26 la Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais lilitengewa shilingi 4,914,608,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2018 Ofisi hiyo ilipokea shilingi 5,063,052,486.44 sawa na asilimia 1.03 ya bajeti ya matumizi ya kawaida ikiwa imeongezeka asilimia tatu zaidi ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kiasi hicho kilichoongezeka ni kutokana na gharama za kuhamisha watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka Dar es Salaam kuja Makao Makuu ya Serikali, Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Fungu namba 31 la Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ujumla lilitengewa shilingi 8,214,535,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2018, Ofisi hiyo ilipokea shilingi 10,552,751,913.27 sawa na asilimia 128.5 ya bajeti ya matumizi ya kawaida ikiwa imeongezeka asilimia 28.5 zaidi ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kiasi hicho kilichoongezeka ni



kutokana na gharama za kuhamisha watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka Dar es Salaam kuja Makao Makuu ya Serikali, Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huu unaonesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mafungu yote yaani Fungu namba 26 na Fungu namba 31. Maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa wakati na kwa ufanisi. Kwa hatua hii, Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa ujumla kwa kutoa fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Fungu namba 31. Kamati hii ina wajibu wa kusimamia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) na bajeti kubwa ya fedha za maendeleo ipo chini ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) ambayo haiko chini ya Kamati ya Katiba na Sheria. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Makamu wa Rais iliidhinishwa shilingi bilioni moja kwa ajili ya miradi miwili ya ujenzi wa Ofisi na makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar, mradi namba 6309 na mradi wa kujenga na kukarabati Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II, Dar es Salaam, mradi namba 6389.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Machi, 2018 hakuna fedha yoyote ya miradi hiyo miwili iliyopokelewa. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya tarehe 26 Machi, 2018 ni kwamba jengo la ofisi ya makazi ya Makamu wa Rais Tunguu-Unguja limekamilika na tayari limeanza kutumika na mapungufu yaliyobainika yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea na kuchambua mpango na bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2018/2019 tarehe 26 Machi

2018 ambayo imelenga kutekeleza masuala ya vipaumbele kama ifuataavyo:-

(i) Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vya Kushughulikia masuala ya Muungano pamoja na changamoto zinazojitokeza;

(ii) Kuratibu masuala ya kijamii na kiuchumi pamoja na kufuatilia utekelezaji wa program na miradi ya maendeleo kwa pande mbili za Muungano;

(iii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano kwa makundi mbalimbali ya kijamii; na

(iv) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zenye majukumu yanayoshabihiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vipaumbele hivyo, Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi mwenendo wa kuimarisha na kuulinda Muungano wetu kwa manufaa ya Watanzania wote na kudumisha udugu, umoja na mshikamano wa Watanzania kwa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, Fungu namba 26 inaomba jumla ya shilingi 6,308,631,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,053,666,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 5,254,965,000 ni fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba bajeti ya Fungu namba 26 imeongezeka kwa asilimia 28.4 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Ongezeko hili linatokana na Ofisi hiyo kuwa na ofisi za kudumu Mjini

Dodoma na hivyo kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu namba 31 inaomba jumla ya shilingi 9,721,116,560 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizo shilingi 5,942,065,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 3,779,051,560 ni fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Fungu namba 31 imeongezeka kwa asilimia 18.34 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge chini ya Fungu hili kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kama ilivyoelezwa hapo awali, ongezeko hili linatokana na ofisi hiyo kuwa na ofisi za kudumu Mjini Dodoma na hivyo kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), miradi miwili ya maendeleo inaendelea kuombewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Miradi hiyo ni mradi namba 6309 wa ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais, Zanzibar ambao unaombewa shilingi bilioni moja na mradi namba 6389 wa ujenzi na ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Luthuli II ambao unaombewa shilingi 538,800,000. Hivyo basi, kwa ujumla miradi hiyo miwili inaombewa shilingi 1,538,800,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uchambuzi wa Kamati umebaini miradi hiyo haikupokea kiasi chochote cha fedha iliyoidhinishwa na Bunge hadi Machi, 2018; Kamati inapendekeza fedha hizo zitolewe kabla ya kuisha kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018. Aidha, kiasi kinachoombwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kitolewe kwa wakati ili kurahisisha ukamilishaji wa miradi hiyo muhimu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali

yaliyojitokeza katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na taarifa za makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) katika mwaka wa fedha 2017/2018 ikiwa ni pamoja na kushughulikia mapungufu ya kitaalam katika jengo la Makamu wa Rais, Dar es Salaam na kuhamishia Ofisi ya Makamu wa Rais Mjini Dodoma. Aidha, Kamati inapongeza juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) za kuzikutanisha sekta za biashara za pande mbili za Muungano kwa ajili ya kujadili upatikanaji wa fursa za masoko kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo za kiutekelezaji zilizochukuliwa na ofisi hii, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kuhakikisha inaendelea na jitihada zake za kuzikutanisha Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kujadili na kutafuta ufumbuzi wa muda mfupi na wa muda mrefu kuhusu upatikanaji wa fursa za masoko kwa pande mbili za Muungano ndani ya Jamhuri ya Muungano na ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kushauri kwamba, katika kuboresha utendaji kazi wa Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint Finance Commission*) katika kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba, kutafutwe uwezekano wa Tume hiyo kusimamiwa moja kwa moja na Ofisi ya Rais au Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) na siyo Wizara ya Fedha na Mipango kama utaratibu ulivyo sasa.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuratibu utekelezaji wa Waraka wa Mgao wa Muda wa Ajira (*Quota*) ambapo Taasisi za Muungano zinatakiwa kuzingatia matakwa ya waraka huo pindi fursa za ajira zinapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kufanya ukarabati wa kutosha na wa kuridhisha kwa magari na mitambo yote inayotumiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa lengo la kuongeza na kuboresha vitendea kazi na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uchambuzi wa Kamati umebaini mradi namba 6309 na namba 6389 haikupatiwa kiasi chochote cha fedha iliyoidhinishwa na Bunge hadi Machi 2018, Kamati inashauri fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni moja kwa miradi yote miwili zitolewe kabla ya kuisha kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 na kiasi kinachoombwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa miradi hiyo inayotekelezwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kitolewe kwa wakati ili kurahisisha ukamilishaji wa miradi hiyo muhimu kwa mwaka wa fedha 2018/2019. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi alivyomwezesha Spika wetu kurudi salama akiwa na afya njema na tunaendelea kumuomba ili awe na afya njema na umri mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vyema na kwa weledi wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nikupongeze kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili katika kutekeleza kaulimbiu ya Hapa Kazi Tu na Tanzania ya viwanda kwa kuishauri vyema Serikali kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Naibu Spika wetu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa weledi na umahiri wake mkubwa katika kukusaidia kuliongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kushauri na kusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya njema na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mheshimiwa January Makamba; Naibu Waziri Mheshimiwa Alphaxad Kangi Lugola, Watendaji Wakuu wote na wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Naomba majina yao kama yalivyo katika taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Angelina Sanga; Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Stanslaus Kagisa, Ndugu Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndugu Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii.

Napenda pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) Ndugu Hanifa Masaninga na watendaji wote wa Idara hiyo kwa kuhakikisha kwamba taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri hivi punde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA  
SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA  
MAKAMU WA RAIS (MUUNGANI) KWA MWAKA WA FEDHA  
2017/2018; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA  
MWAKA WA FEDHA 2018/2019  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 6 (2) (c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, imeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rias - Muungano.

Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha

2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ina Mafungu 2 ya Bajeti ambayo ni:-

i) **Fungu 26** - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, na

ii) **Fungu 31** - Ofisi ya Makamu wa Rais,

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na;

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati

## **2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

### **2.1 Fungu 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais;**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Muundo na Majukumu ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Muungano), hakukuwa na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo katika Fungu hili.

### **2.2 Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano;**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano. Orodha ya Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-



i) **Mradi Na. 6309** – Ujenzi wa Ofisi na Nyumba ya Makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar (*Construction of Vice President Office and Residence in Zanzibar*), ambao uliidhinishiwa **Shilingi Milioni Mia Nne (400,000,000/=)**, na

ii) **Mradi Na. 6389** – Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais (Luthuli II) (*Construction and Rehabilitation of Vice President Office Luthuli II and State Lodges*), ambao uliidhinishiwa **Shilingi Milioni Mia Sita (600,000,000)**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano ya tarehe 26 Machi, 2018, miradi hiyo miwili haikupokea kiasi chochote cha Fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

### **3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MUUNGANO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mwaka wa fedha 2018/2019, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 tarehe 26 Machi, 2018. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

#### **3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2017 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2018 katika Robo ya Tatu ya Mwaka huu wa fedha 2017/2018. Uchambuzi huu pia

ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2018. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

### **3.2 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina**

#### **3.2.1 FUNGU 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 **Fungu 26** la Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais **lilitengewa Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tisa Kumi na Nne, Laki Sita na Nane Eflu (4, 914, 608, 000/)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari 2018, Ofisi hiyo ilipokea **Shilingi Bilioni Tano na Milioni Sitini na Tatu, Hamsini na Mbili Eflu, Mia Nne Themanini na Sita na Senti Arobaini na Nne (5, 063, 052, 486.44)** sawa na **asilimia 103%** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida, ikiwa imeongezeka **asilimia 3%** zaidi ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kiasi hicho kilicho ongezeka ni kutokana na gharama za kuhamisha Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka Dar Es Salaam kuja Makao Makuu ya Serikali Dodoma.

#### **3.2.2 FUNGU 31: Ofisi ya Makamu wa Rais**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 **Fungu 31** la Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ujumla lilitengewa **Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Mbili Kumi na Nne, Laki Tano Thelathini na Tano Eflu (8, 214,535,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2018 Ofisi hiyo ilipokea **Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Tano Hamsini na Mbili, Laki Saba Hamsini na Moja Eflu, Mia Tisa Kumi na Tatu na Senti Ishirini na Saba (10,552,751, 913.27)** sawa na **asilimia 128.5%**

ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida, ikiwa imeongezaka **asilimia 28.5%** zaidi ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kiasi hicho kilichoongezeka ni kutokana na gharama za kuhamisha Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka Dar Es Salaam kuja Makao Makuu ya Serikali Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na Mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mafungu yote (**Fungu 26 na Fungu 31**).

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa wakati na kwa ufanisi. Kwa hatua hii, Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa Ujumla kwa kutoa Fedha kwa wakati.

### **3.3 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - FUNGU 31**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hii ina wajibu wa Kusimamia Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano, na Bajeti kubwa ya Fedha za Maendeleo ipo chini ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ambayo haiko chini ya Kamati ya Katiba na Sheria. Hata hivyo, Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Ofisi ya Makamu wa Rais iliidhinishwa **Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000/=)** kwa ajili ya Miradi Miwili ya Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais (Zanzibar) (**Mradi Na.6309**) na Mradi wa Kujenga na kukarabati Ofisi ya Makamu wa Rais *Luthuli II* (Dar es Salaam) (**Mradi Na.6389**).

**Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2018 hakuna Fedha yoyote ya Miradi hiyo miwili iliyopokelewa. Hata hivyo, kwa Mujibu wa Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya tarehe 26 Machi, 2018, ni kwamba, Jengo la Ofisi ya Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu, Unguja limekamilika na tayari limeanza kutumika na mapungufu yaliyobainika yanaendelea kufanyiwa kazi.

#### 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 tarehe 26 Machi 2018 ambayo imelenga kutekeleza masuala ya vipaumbele vifuatavyo:-

i) Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vya Kushughulikia masuala ya Muungano pamoja na changamoto zinazojitokeza,

ii) Kuratibu masuala ya kijamii na kiuchumi pamoja na kufuatilia utekelezaji wa program na Miradi ya maendeleo kwa pande mbili za Muungano,

iii) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu Muungano kwa makundi mbalimbali ya kijamii, na

iv) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao vya ushirikiano kwa Wizara, idara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zenye majukumu yanayoshabihiana.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi mwendelezo wa kuimarisha na kuulinda Muungano wetu kwa manufaa ya Watanzania wote na kudumisha Udugu, Umoja na Mshikamano wa Watanzania wa pande zote mbili za Muungano.

#### 4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

##### 4.1.1 Fungu 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (**Fungu 26**) inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tatu na Nane, Laki Sita**

**The**lathini na Moja Eflu (6,308,631,000/=) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Moja na Milioni Hamsini na Tatu, Laki Sita Sitini na Sita Eflu (1,053,666,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Mbili Hamsini na Nne, Laki Tisa Sitini na Tano Eflu (5,254, 965,000/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, Bajeti ya **Fungu 26** imeongezeka kwa **asilimia 28.4%** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Ongezeko hili linatokana na Ofisi hiyo kuwa na Ofisi za kudumu Mjini Dodoma na hivyo kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa Ofisi hiyo.

#### 4.1.2 **Fungu 31; Ofisi ya Makamu wa Rais**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Makamu wa Rais (**Fungu 31**) inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Tisa , Milioni Mia Saba Ishirini na Moja, Laki Moja Kumi na Sita Eflu, Mia Tano Sitini (9,721,116, 560/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tisa Arobaini na Mbili na Sitini na Tano Eflu (5,942,065,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Saba Sabini na Tisa, Hamsini na Moja Eflu, Mia Tano Sitini (3,779,051,560/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa **Fungu 31** imeongezeka kwa **asilimia 18.34%** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge chini ya Fungu hili kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kama ilivyoelezwa hapo juu, Ongezeko hili linatokana na Ofisi hiyo kuwa na Ofisi za kudumu Mjini Dodoma na hivyo kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa Ofisi hiyo.

#### 4.3 Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 (FUNGU 31).

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano, Miradi miwili ya Maendeleo inaendelea kuombewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Miradi hiyo ni **Mradi Na. 6309** wa Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar ambao unaombewa **Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000/)** na **Mradi Na.6389** wa Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Luthuli II, ambao unaombewa **Shilingi Milioni Mia Tano Thelathini na Nane, Laki Nane (538,800,000/)**. Hivyo, kwa ujumla Miradi hiyo miwili inaombewa **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Thelathini na Nane, Laki Nane (1,538,800,000/=)**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa uchambuzi wa Kamati umebaini Miradi hiyo haikupokea kiasi chochote cha fedha iliyoidhinishwa na Bunge hadi Machi 2018, Kamati inapendekeza Fedha hizo zitolewe kabla ya kuisha kwa Mwaka huu wa Fedha 2017/2018 na kiasi kinachoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kitolewe kwa wakati ili kurahisisha ukamilishaji wa miradi hiyo muhimu kwa wakati.

#### 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kama ifuatavyo:-

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, ikiwa ni pamoja na kushughulikia mapungufu ya kitaalamu katika Jengo la Makamu wa Rais, Dar es Salaam, kuhamishia Ofisi ya Makamu wa Rais Dodoma.

Aidha, Kamati inapongeza juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) za kuzikutanisha Sekta za biashara za pande mbili za Muungano kwa ajili ya kujadili upatikanaji wa fursa za masoko kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua hizo za kiutekelezaji zilizochukuliwa na Ofisi hii, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kuhakikisha inaendelea na jitihada zake za kuzikutanisha Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanziba (SMZ) ili kujadili na kutafuta ufumbuzi wa muda mfupi na wa Muda mrefu kuhusu upatikanaji wa fursa za masoko kwa pande mbili za Muungano ndani ya Jamhuri ya Muungano na Ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kushauri kwamba, katika kuboresha utendaji kazi wa Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint Finance Commission*) katika kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba, kutafutwe uwezekano wa Tume hiyo kusimamiwa moja kwa moja na Ofisi ya Rais au Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na siyo Wizara ya Fedha na Mipango kama utaratibu ulivyo sasa.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuratibu utekelezaji wa Waraka wa Mgao wa Muda wa Ajira (*Quota*) ambapo Taasisi za Muungano zinatakiwa kuzingatia matakwa ya Waraka huo pindi fursa za Ajira zinapopatikana.

iv) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kufanya ukarabati wa kutosha na wa kuridhisha kwa magari na Mitambo yote inayotumiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa lengo la kuongeza na kuboresha vitendea kazi na kurahisisha utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa wakati.

v) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa uchambuzi wa Kamati umebaini **Mradi Na. 6309** na Na. **6389** haikupatiwa kiasi

chochote cha fedha iliyoidhinishwa na Bunge hadi Machi 2018, Kamati inashauri Fedha hizo kiasi cha **Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000/=)** kwa Miradi yote miwili zitolewe kabla ya kuisha kwa Mwaka huu wa Fedha 2017/2018 na kiasi kinachooombwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa miradi hiyo inayotekelezwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano, kitolewe kwa wakati ili kurahisisha ukamilishaji wa miradi hiyo muhimu kwa Mwaka wa fedha 2018/2019.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Tunamshukuru Mungu kwa jinsi alivyokuwezesha kurudi katika afya yako na tunaendelea kukuomba uendelee vizuri.

Aidha, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Napenda nikupongeze pia kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili katika kutekeleza Kauli Mbiu ya **HAPA KAZI TU na TANZANIA YA VIWANDA** kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaomba afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhe. Januari Makamba, (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Alphaxad Kangi Lugola, (Mb), Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano.



**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano. **NAOMBA MAJINA YAO KAMA YALIVYO KATIKA TAARIFA HII YAINGIE KATIKA TAARIFA RASMI YA BUNGE (HANSARD).**

- 1) Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb – **Mwenyekiti**
- 2) Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – **Makamu /Mwenyekiti**
- 3) Mhe. George Simbachawene, Mb - Mjumbe;
- 4) Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe;
- 5) Mhe. Makame Mashaka Foun, Mb - Mjumbe;
- 6) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
- 7) Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
- 8) Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
- 9) Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
- 10) Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
- 11) Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
- 12) Mhe. Susan Peter Maselle, Mb - Mjumbe;
- 13) Mhe. Alfredina Apolinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
- 14) Mhe. Latifah Hassan Chande, Mb - Mjumbe;
- 15) Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb - Mjumbe;
- 16) Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
- 17) Mhe. Jacqueline K. Ngonyani Msongozi, Mb - Mjumbe;
- 18) Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
- 19) Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
- 20) Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
- 21) Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
- 22) Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
- 23) Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb – Mjumbe
- 24) Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb – Mjumbe
- 25) Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbo, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Dunford Mpelumbe na Msaidizi

wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Ndg. Hanifa Masaniga na Watendaji wote wa Idara hiyo kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka wa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais -Muungano, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri hivi punde.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.

**MWENYEKITI,**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

17 APRILI, 2018

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Mollel kwa kuwasilisha taarifa kiufanisi kabisa kama mwandishi wa habari. (*Makofi*)

Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ili aweze kuwasilisha taarifa yake. Mheshimiwa Mussa Ntimizi kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na 117(11) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Fungu 31, Idara ya Mazingira kwa mwaka 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2018/2019 katika utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mujibu wa kifungu cha 6(1) kikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaoishia na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaoanza) ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ilipitiwa na kuchambuliwa na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na hatimaye kutoa maoni yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge katika kutekeleza majukumu yake ambapo ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira inayotekelezwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kuchambua mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchambua, kujadili na kushauriana na Wizara husika, Kamati sasa inawasilisha taarifa hii ili kuliomba Bunge lako Tukufu kukubali kuidhinisha maombi ya fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira.

Aidha, taarifa hii inalenga kutoa mapendekezo kwa Bunge kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi katika kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira katika kutekeleza kazi za uhifadhi na usimamizi wa mazingira ilitekeleza mambo mbalimbali. Kamati inaipongeza ofisi hii kwa kazi nzuri iliyofanya pamoja na kuwa na changamoto ya Bajeti ndogo. Miongoni mwa kazi ilizofanya ni kuokoa ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu ambapo Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania aliunda kikosi kazi cha kufanya kazi kwa ajili ya kutekeleza jukumu hilo na kuandaa taarifa ya tatu ya hali ya mazingira nchini. Ofisi imeendelea kukusanya taarifa mbalimbali kwa ajili ya kuandaa rasimu ya taarifa hii. Kamati inapongeza juhudi hizi za Ofisi katika kuandaa taarifa hii muhimu licha ya kuwepo na changamoto ya ukosefu wa fedha. Kamati inataka taarifa hii ikamilike na kuletwa kwenye Kamati kwa ajili ya kuiboresha na kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine iliyotekelezwa na Ofisi hii ni kufanya kampeni ya upandaji miti nchi nzima, ambapo kila Wilaya inatakiwa kupanda miti 1,500,000. Kamati inapongeza jitihada hizi lakini sambamba na hilo inaitaka Serikali kuwa na mkakati wa kufuatilia maendeleo ya miti hiyo kuhakikisha inakuwa na kuleta manufaa ya upandaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ilijikita katika kuchambua mwenendo wa upatikaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo pamoja na fedha zilizotengwa ili kutekeleza majukumu mengine ya ofisi. Katika kufanya uchambuzi Kamati ilitumia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, taarifa ya ziara kwenye miradi na mahojiano wakati wa vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) hufanya makusanyo kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Baraza lilipanga kukusanya kiasi cha shilingi 15,683,161,500 kutoka katika vyanzo vyake vya ndani.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia tarehe 8 Machi, 2018, Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) lilikuwa limekusanya jumla ya shilingi 6,700,911,516 tu sawa na asilimia 42.7 ya makadirio yote. Kwa matokeo haya, ni vigumu kufikiwa lengo la makusanyo ifikapo tarehe 30 Juni, 2018. Ni maoni ya Kamati kuwa lengo la maduhuli linapaswa kupangwa kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira iliidhinishwa jumla ya shilingi 9,634,020,437 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo shilingi 3,845,568,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 5,788,452,437 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya shilingi 3,845,568,000 ziliombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida shilingi 878,424,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 2,967,144,000 ni kwa ajili ya matumizi mengine . Kati ya fedha za matumizi mengine zilizoidhinishwa shilingi 2,215,044,000 ni ruzuku ya mishahara kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kiasi kinachosalia Sh.752,100,000 ni kwa ajili ya matumizi mengine katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge ni shilingi 5,788,452,437, kati ya hizo shilingi 2,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 3,788,452,437 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizopokelewa hadi 8 Machi, 2018; Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira iliidhinishwa jumla ya shilingi 9,634,020,437. Kati ya hizo ni shilingi 4,369,633,141 tu ndizo zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia 8 Machi, 2017. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 45.3 ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya shilingi 3,845,568,000 zilizoidhinishwa kwa ajili matumizi ya kawaida ni shilingi 1,875,032,651 tu ndizo zilizokuwa zimetolewa. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 48.4 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa fedha zilizotolewa ni shilingi 438,664,456 kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,436,368,194 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha za matumizi mengineyo zilizotolewa ni pamoja na shilingi 1,235,391,000 ruzuku ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Kwa uchambuzi huu fedha za Matumizi Mengineyo (OC) ambazo zimekwishatolewa kwa ajili ya Idara ya Mazingira ni shilingi 200,977,194 tu, kati ya shilingi 752,100,000 zilizoidhinishwa na Bunge, kiasi hiki ni sawa na asilimia 26.7 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya shilingi 5,788,452,437.00 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi 2,494,600,490 tu ndizo zilizopokelewa sawa na asilimia 43.1 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Kamati hairidhishwi na upatikanaji huu wa fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira. Utoaji huu wa fedha unakwamisha utendaji wa ofisi hii muhimu katika uratibu wa masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 8 Machi, 2018 hakuna fedha za ndani zilizoidhinishwa na Bunge lako kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilizokuwa zimetolewa. Hili inadhihirisha kuwa Serikali yetu halijaipa kipaumbele suala la uhifadhi wa mazingira na kuwa ikitokea wahisani wakaamua kusitisha ufadhili wao miradi ya uhifadhi wa mazingira haitatekelezwa. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ndiyo yenye dhamana ya kuratibu na kusimamia masuala yote yanayohusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

Katika kufuatilia utekelezaji wa jukumu hilo, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilipata fursa ya kutembelea maeneo mawili ambayo ni mgodi wa wachimbaji wadogo *Sekenke One* (Singida) na Bonde la Mto Ruaha Mkuu (Iringa). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa mazingira katika maeneo ya mgodi wa wachimbaji wadogo. Usimamizi wa mazingira katika maeneo ya migodi hapa nchini unatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na ukaguzi katika maeneo hayo unafanywa na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Kwa mujibu wa ukaguzi uliofanywa na Baraza hadi kufikia Disemba, 2017 kati ya migodi 128 ni migodi mitano tu sawa na asilimia nne ndiyo iliyoonekenka kuwa inazingatia Sheria za Mazingira na mingine ilikuwa na changamoto mbalimbali. Utekelezaji wa Sheria za Mazingira katika migodi mingi nchini bado siyo wa kuridhisha hivyo jitihada za dhati zinahitajika kuchukuliwa ili kuepusha madhara makubwa ya uharibifu wa mazingira unaoweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kutembelea eneo la Sekenke (Singida) ambapo kuna mgodi wa wachimbaji wadogo kwa lengo la kujionea hali ya mazingira katika eneo la mgodi.

Katika ziara hiyo, Kamati ilitaka pia kujiridhisha kuhusu mpango wa Serikali katika kutekeleza *Minamata Convention* wenye lengo la kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini ili kupunguza madhara ya kemikali hii kwa afya za binadamu na mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya mazingira katika eneo la mgodi si ya kuridhisha, inakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo ni:-

- Wachimbaji wadogo kutumia kemikali hatari ya zebaki katika kuchenjua dhahabu bila kuwa na vifaa vya kujikinga hali inayoathiri mazingira lakini pia afya za wachimbaji hao na jamii inayoishi eneo linalozunguka mgodi huo;
- Matumizi ya teknolojia duni ikiwemo matumizi ya magogo katika kuzuia kingo za mashimo/migodi na kusababisha ukataji wa miti katika maeneo mengi nchini;

- Uwezo mdogo wa kifedha kwa wachimbaji wadogo hivyo kushindwa kufanya upembuzi yakinifu na kuendelea na uchimbaji bila kujali athari zinazoweza kutokea;
- Uchimbaji unafanywa kwa kubahatisha bila kuwa na uhakika wa kiasi cha madini kilichopo ardhini. Uchimbaji wa aina hii unasababisha kuwepo kwa mashimo mengi ardhini kwa sababu ya kutokuwa na uhakika; na
- Kujaa maji katika mashimo hivyo kuwa kikwanzo kwa wachimbaji katika kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati huhusu ziara yake katika Mgodi wa Wachimbaji Wadogo Sekenke; ili kutatua changamoto ya mitaji midogo kwa wachimbaji wadogo, Kamati inashauri kwamba Serikali iwasiliane na taasisi za fedha ili kuona jinsi ambavyo wananchi wanaweza kukopeshwa kwa riba nafuu. Hatua hii itapunguza matumizi ya magogo na uchenjuaji wa kienyeji ambao unaathiri mazingira na afya za wachimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matumizi makubwa ya magogo katika kuzuia kingo za mashimo katika migodi hiyo na kusababisha ukataji hovyoy wa miti. Kamati inaishauri Serikali isaidie kupitia taasisi zake za ufundi hususani *SIDO* kubuni njia mbadala ambayo itakuwa rafiki kwa mazingira na afya kwa wachimbaji wadogo. Mfano ni mgodi unaomilikiwa kwa ubia kati ya Mtanzania na raia wa China ambao wametumia vyuma badala ya magogo katika kuzuia kingo zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya uduni wa teknolojia inayotumika katika uchimbaji na uchenjuaji, kiasi cha dhahabu wanachokipata ni asilimia 30 tu na asilimia 70 inabaki kwenye makinikia ambayo wanauziwa wenye mitambo ya kuchenjulia. Kamati ina maoni kwamba Serikali iangalie namna ya kuwasaidia ili kuongeza tija kwa wachimbaji wadogo na kuongeza mapato kwa Serikali.



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wengi wadogo nchini wanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mitaji na hivyo kulazimika kutumia zana duni na kusababisha athari kubwa za mazingira. Kamati inaishauri Serikali kuwasiliana na taasisi za fedha zinazoweza kuwakopesha fedha au vifaa kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea Bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa lengo la kujionea hali ya mazingira katika bonde hili. Kamati ilitaka pia kujua mkakati wa Serikali katika kukabiliana na athari za kimazingira katika eneo la bonde. Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) inatekeleza Mradi wa Usimamizi wa Ikolojia ya eneo la Bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa lengo la kurejesha mtiririko wa maji kwa kipindi cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde lote la Mto Ruaha Mkuu linajumuisha vyanzo vya mito mikuu tisa. Kwa ujumla hali ya bonde siyo ya kuridhisha na lipo katika hatari ya kukauka ndiyo maana Mheshimiwa Makamu wa Rais aliamua kuiagiza Ofisi yake Idara ya Mazingira kuunda kikosi kazi cha kuhakikisha Mto Ruaha unarudi katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Mto Ruaha Mkuu linakabiliwa na chanagamoto zifuatazo:-

(i) Kuendesha shughuli za kilimo katika maeneo ya bonde hivyo kusababisha uchepushaji mkubwa wa maji pasipo kuzingatia mahitaji ya watumiaji wengine hasa wakulima wa mpunga wa Mbarali;

(ii) Ongezeko kubwa la idadi ya mifugo inayochungwa katika eneo la hifadhi;

(iii) Kupanuka kwa shughuli za kilimo hasa kilimo cha mpunga katika mashamba ya Mbarali na kulima kandokando ya mikondo ya mito; na

(iv) Kukinzana kwa baadhi ya sheria katika kusimamia uhifadhi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusu ziara yake katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu ni kuwa Bonde la Mto Ruaha linatumiwa na wadau mbalimbali, mfano uhifadhi wa wanyama (*Ruaha National Park*), uvuvi, kilimo na ufugaji hali inayosababisha Bonde hili kuelemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati wakati wa ziara ilishuhudia madhara ya uchepushaji wa maji usiozingatia kanuni za mazingira pamoja na mahitaji ya watumiaji wengine. Tabia hii inasababisha upotevu wa maji mengi ambayo yangetumika kwa ajili ya shughuli nyingine za kiuchumi kama uzalishaji wa umeme. Kamati inaishauri Serikali iendelee kutoa elimu hasa kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mikubwa ya uzalishaji umeme ambayo inategemea maji kutoka katika bonde hili (Bwawa la Mtera, Kidatu na Mradi Mpya wa *Stieglers Gorge*). Kwa kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya miradi hii na uhifadhi wa mazingira itakuwa busara wakishirikishwa kwa kuchangia katika kuhifadhi wa mazingira haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jukumu la kusimamia shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira lipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira); na kwa kuwa, ofisi hii ipo kama wasimamizi wakuu shughuli hizo, hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha ofisi hii kifedha na kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kwa wakati ili kusaidia kuratibu masuala ya uhifadhi wa mazingira katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) inalo jukumu la kufanya ukaguzi katika maeneo yote ambayo yanaonekana kukua haraka kwa mfano, maeneo ya migodi, viwanda, hoteli za kwenye fukwe, kingo za bahari, machinjio na maeneo mengine hatarishi katika mazingira.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Kamati ilitoa ushauri na maagizo kwenye maeneo mbalimbali. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ilizingatia maoni na ushauri wa Kamati. Hata hivyo, kuna maagizo ambayo Serikali haikutekeleza ipasavyo. Maagizo ambayo hayakutekelezwa ipasavyo ni pamoja na:-

Moja, Serikali iangalie upya Sheria za Misituta, Mazingira na Mifugo ili kuondoa mgongano wa kisheria katika utekelezaji na uhamasishaji. Wizara zinazosimamia kazi hizi zifanye kazi kwa pamoja. Agizo hili halikutekelezwa kwani mpaka sasa tumeendelea kushuhudia migongano ya sheria katika kusimamia masuala mbalimbali ya mazingira. Kamati inaendelea kusisitiza utekelezwaji wa agizo hili na inazitaka Wizara kukaa pamoja na kuzileta sheria hizi Bungeni kwa ajili ya kuzifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira limepanga kukusanya shilingi bilioni 18 kutokana na vyanzo vyake vya ndani. Makisio ya mwaka wa fedha 2018/2019 ni zaidi kwa asilimia 20.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 15,600,000,000 ya mwaka 2017/2018 ambazo hazitafikiwa, hivyo kukosa uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ujumla wake na kubaini kuwa mahitaji ya bajeti ya usimamizi na hifadhi ya mazingira ni makubwa kuliko kiasi kilichotengwa. Kamati hairidhishwi na ukomo wa bajeti ya mazingira, hivyo, ni maoni ya Kamati kwa Serikali kwamba iangalie upya ukomo wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2018/2019 inaomba kuidhinishwa shilingi 8,118,494,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia 15 ikilinganishwa na shilingi 9,634,020,437 kwa bajeti

inayotekelezwa sasa. Kati ya fedha hizo shilingi 3,524,540,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo na shilingi 4,593,954,000.00 ni matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zinazombwa shilingi 3,017,072,000.00 ni ruzuku ya Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC), shilingi 898,782,000.00 ni mishahara ya watumishi wa Idara ya Mazingira na shilingi 678,100,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira inaomba kuidhinishwa fedha shilingi 3,524,540,000.00 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia 39.1 ikilinganishwa na shilingi 5,788,452,437.00 kwa bajeti inayotekelezwa sasa. Kati ya fedha hizo shilingi 1,238,800,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 2,063,340,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huu ni dhahiri kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Idara ya Mazingira kiasi kilichotengwa ni kidogo ikilinganishwa na changamoto za kimazingira zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ilikwishakamilisha mapendekezo ya vyanzo vya mapato na viwango vya uchangiaji kwa sekta nyingine katika Mfuko wa Mazingira na kuviwasilisha Serikalini. Kwa kuwa, hali ya utengaji fedha kwa ajili ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira si ya kuridhisha; hivyo basi, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha Mfuko wa Mazingira kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 unawezeshwa na kufanya kazi kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa hii yote iingie kwenye *Hansard*. Naomba nimalizie, katika kuelekea Tanzania ya viwanda, Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa jitihada wanazozichukua katika kukagua na kusimamia utunzaji wa mazingira viwandani. Aidha, Kamati inaitaka Ofisi hii pamoja na *NEMC* kuongeza kasi ya kuelimisha, kukagua na kuchukua hatua za kisheria kwa wanaokiuka sheria hii. Kukua kwa sekta ya viwanda nchini kuna uhusiano wa moja kwa moja na uhifadhi wa

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mazingira. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango mkakati kwa ajili ya viwanda vipya na vilivyopo ili kulipa kipaumbele suala la uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, machinjio mengi nchini hayazingatii Sheria ya Mazingira hivyo ni machafu sana na yanahatarisha afya za walaji. Machinjio haya ni ya zamani sana na yalijengwa katikati ya miji kutokana na hali halisi ya kipindi hicho. Kwa sasa miji imekuwa na machinjio haya yamekuwa karibu na makazi. Kamati inashauri kuwa machinjio haya yahamishiwe pembezoni mwa miji na ukaguzi wa mara kwa mara ufanyike ili kuhakikisha wanafuata Sheria ya Mazingira kwa ajili ya kulinda afya za walaji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ntimizi, naomba uhitimishe hoja yako.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; naomba nikushukuru sana wewe na Wenyeviti wote Bunge kwa kuratibu na kusimamia vyema shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa January Makamba; Naibu Waziri wake Mheshimiwa Kangi Lugola; Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa jinsi walivyoshiriki katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati

ya Bunge ya Viwanda, Biashara kama walivyoorodheshwa hapo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai, pamoja naye namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bwana Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Kamati za Fedha na Uchumi, Bwana Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Wilfred Magova, Bi. Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi. Pauline Mavunde kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi taarifa hii inakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Fungu namba 31 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni kiasi cha shilingi 8,118,494,000.00 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA  
NA MAZINGIRA MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA  
MAJUKUMU YA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA  
CHINI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA FUNGU 31  
KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 NA MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA 2018/2019 KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na 117 (11) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira **Fungu 31** Idara ya Mazingira kwa Mwaka **2017/2018** na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka **2018/2019** katika Utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Bajeti (Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaoanza) ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, ilipitiwa na kuchambuliwa na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na hatimaye kutoa maoni yake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia, ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1), ya Kanuni za kudumu za Bunge katika kutekeleza majukumu yake ambapo ilifanya Ziara katika baadhi ya Miradi ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira inayotekelezwa Ofisi ya Makamu wa Rasi-Mazingira kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za kudumu za Bunge Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kuchambua Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuchambua, kujadili na kushauriana na Wizara husika, Kamati sasa inawasilisha taarifa hii ili kuliomba Bunge lako tukufu kukubali kuidhinisha maombi ya Fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira. Aidha, Taarifa hii inalenga kutoa mapendekezo kwa Bunge kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi katika kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira nchini.

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2017/2018 NA MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 2.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018

#### 2.1.1 Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/18 Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira katika kutekeleza kazi za Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ilitekeleza mambo mbalimbali. Kamati inaipongeza Ofisi hii kwa kazi nzuri iliyofanya pamoja na kuwa na changamoto ya Bajeti ndogo. Miongoni mwa kazi ilizofanya ni;-

- Kuokoa ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu, ambapo Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania aliunda kikosi kazi cha kufanya kazi kwa ajili ya kutekeleza jukumu hilo;
- Kuandaa taarifa ya tatu ya Hali ya Mazingira nchini, Ofisi imeendelea kukusanya taarifa mbalimbali kwa ajili ya kuandaa rasimu ya taarifa hii. Kamati inapongeza juhudi hizi za Ofisi katika kuandaa taarifa hii muhimu licha ya kuwepo na changamoto ya ukosefu wa fedha. Kamati inataka taarifa hii ikamilike na kuletwa kwenye Kamati kwa ajili ya kuiboresha na kushauri.

**Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine iliyotekelezwa na Ofisi hii ni kufanya Kampeni ya Upandaji miti nchi nzima, ambapo kila wilaya inatakiwa kupanda miti milioni moja na laki tano (1,500,000). Kamati inapongeza jitihada hizi lakini sambamba na hilo inaitaka Serikali kuwa na Mkakati wa kufuatilia maendeleo ya miti hiyo kuhakikisha inakuwa na kuleta manufaa ya upandaji wake.



## 2.1.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, katika kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ilijikita katika kuchambua mwenendo wa upatikaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Miradi ya maendeleo pamoja na fedha zilizotengwa ili kutekeleza majukumu mengine ya Ofisi. Katika kufanya Uchambuzi Kamati ilitumia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, Taarifa ya ziara kwenye Miradi na mahojiano wakati wa vikao.

## 2.1.3 Makusanyo ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira hufanya Makusanyo kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Baraza lilipanga kukusanya kiasi cha Shilingi **15,683,161,500.00** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani. Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia tarehe 8 Machi, 2018 Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), lilikuwa limekusanya jumla ya Shilingi **6,700,911,516.00** tu sawa na asilimia **42.7** ya makadirio yake. Kwa matokeo haya ni vigumu kufikiwa lengo la makusanyo ifikapo tarehe 30 Juni, 2018. Ni maoni ya Kamati kuwa, lengo la maduhuli linapaswa kupangwa kwa umakini mkubwa.

## 2.1.4 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha **2017/2018** Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira iliidhinishwa jumla ya Shilingi **9,634,020,437.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,845,568,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **5,788,452,437.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya Shilingi **3,845,568,000.00** zinazoombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida Shilingi **878,424,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na Shilingi **2,967,144,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo

(OC). Kati ya fedha za matumizi mengineyo zilizoidhinishwa Shilingi **2,215,044,000.00** ni ruzuku ya mishahara kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na kiasi kinachosalia Shilingi **752,100,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo(OC) katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, jumla ya fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge ni Shilingi **5,788,452,437.00**, kati ya hizo Shilingi **2,000,000,000.00** ni fedha za ndani na Shilingi **3,788,452,437.00** ni fedha za nje.

#### 2.1.5 Fedha zilizopokelewa hadi 8 Machi, 2018

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira iliidhinishwa jumla ya Shilingi **9,634,020,437.00**. Kati ya hizo ni Shilingi **4,369,633,141.30** tu ndizo zilikuwa zimetolewa hadi kufikia 8 Machi, 2017. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **45.3** ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya Shilingi **3,845,568,000.00** zilizoidhinishwa kwa ajili matumizi ya kawaida ni Shilingi **1,875,032,651.30** tu ndizo zilizokuwa zimetolewa. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **48.4** ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha zilizotolewa ni Shilingi **438,664,456.92** kwa ajili ya Mishahara (PE) na Shilingi **1,436,368,194.40** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Fedha za Matumizi ya Mengineyo (OC) zilizotolewa ni pamoja na Shilingi **1,235,391,000.00** ruzuku ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Kwa uchambuzi huu fedha za Matumizi Mengineyo (OC) ambazo zimekwishatolewa kwa ajili ya Idara ya Mazingira ni Shilingi **200,977,194.40** tu, kati ya Shilingi **752,100,000.00** zilizoidhinishwa na Bunge, kiasi hiki ni sawa na asilimia **26.7** tu.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya Shilingi **5,788,452,437.00** zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ni Shilingi **2,494,600,490.00** tu ndizo zilizopokelewa sawa na asilimia **43.1**

ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

### 2.1.6 Maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/18

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi na upatikaji huu wa fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais –Mazingira, Idara ya Mazingira. Utoaji huu wa fedha unakwamisha utendaji wa Ofisi hii muhimu katika uratibu wa masuala ya Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia 8 Machi, 2018 hakuna fedha za ndani zilizoidhinishwa Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilizokuwa zimetolewa. Hili linadhihirisha kuwa Serikali yetu haijalipa kipaumbele suala la uhifadhi wa mazingira na kuwa ikitokea wahisani wakaamua kusitisha ufadhili wao miradi ya uhifadhi wa mazingira haitatekelezwa. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati.

## 3.0 MATOKEO YA ZIARA ZA UKAGUZI

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ndiyo yenye dhamana ya kuratibu na kusimamia masuala yote yanayohusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Katika kufuatilia utekelezaji wa jukumu hilo Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilipata fursa ya kutembelea maeneo mawili ambayo ni mgodi wa wachimbaji wadogo Sekenke One Singida na Bonde la Mto Ruaha Mkuu.

### 3.1 Usimamizi wa Mazingira katika Maeneo ya Mgodi wa Wachimbaji Wadogo

**Mheshimiwa Spika**, usimamizi wa mazingira katika maeneo ya migodi hapa nchini unatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, na ukaguzi katika maeneo hayo unafanywa na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Kwa mujibu wa ukaguzi uliofanywa na Baraza hadi kufikia Disemba, 2017 kati ya **migodi 128 ni migodi 5** tu sawa na **asilimia 4** ndiyo

iliyoonekana kuwa inazingatia Sheria za Mazingira na mingine ilikuwa na changamo mbalimbali. Utekelezaji wa Sheria za Mazingira katika migodi mingi nchini bado siyo wakuridhisha hivyo jitihada za dhati zinahitajika kuchukuliwa ili kuepusha madhara makubwa ya uhalibifu wa mazingira unaoweza kutokea.

➤ **Mgodi wa wachimbaji wadogo Sekenke One-Singida**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea eneo la Sekenke-Singida ambapo kuna mgodi wa wachimbaji wadogo kwa lengo la kujionea hali ya mazingira katika eneo la mgodi. Katika ziara hiyo Kamati ilitaka pia kujiridhisha kuhusu mpango wa Serikali katika kutekeleza Mkataba wa *Minamata Convention* wenye lengo la kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini ili kupunguza madhara ya kemikali hii kwa afya za binadamu na mazingira kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, hali ya mazingira katika eneo la mgodi si yakuridhisha inakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo ni;

- Wachimbaji wadogo kutumia kemikali hatari ya zebaki katika Kuchenjua dhahabu bila kuwa na vifaa vya kujikinga hali inayoathiri mazingira lakini pia afya za wachimbaji hao na jamii inayoishi eneo linalozunguka mgodi;
- Matumizi ya teknolojia duni ikiwemo matumizi ya magogo katika kuzuia kingo za mashimo/migodi na kusababisha ukataji wa miti katika maeneo mengi nchini;
- Uwezo mdogo wa kifedha kwa wachimbaji wadogo hivyo kushindwa kufanya upembuzi yakinifu na kuendelea na uchimbaji bila kujali athari zinazoweza kutokea;
- Uchimbaji inafanywa kwa kubahatisha bila kuwa na uhakika wa kiasi cha madini kilichopo ardhini. Uchimbaji wa aina hii unasababisha kuwepo na mashimo mengi ardhini kwasababu ya kutokuwa na uhakika;

- Kujaa maji katika mashimo hivyo kuwa kikwanzo kwa wachimbaji katika kuendesha shughuli zao;

### 3.1.1 Maoni ya Kamati huhusu Ziara yake katika Mgodu wa Wachimbaji wadogo Sekenke-Singida

**Mheshimiwa Spika**, ili kutatua changamoto ya mitaji midogo kwa wachimbaji wadogo, Kamati inashauri kwamba Serikali iwasiliane na taasisi za fedha ili kuona jinsi ambavyo wanaweza kukopeshwa kwa riba nafuu. Hatua hii itapunguza matumizi ya magogo na uchenjuaji wa kienyeji ambao unatathiri mazingira na afya za wachimbaji.

**Mheshimiwa Spika**, kuna matumizi makubwa ya Magogo katika kuzuia kingo za mashimo/migodi na kusababisha ukataji hovywa wa miti. Kamati inaishauri Serikali isaidie kupitia taasisi zake za ufundi hususani SIDO kubuni njia mbadala ambayo itakuwa rafiki kwa mazingira na afya kwa wachimbaji wadogo. Mfano ni mgodi unaomilikiwa na kwa ubia kati ya mtanzania na raia wa china ambao umetumia vyuma badala ya magogo katika kuzuia kingo zake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sababu ya uduni wa teknolojia inayotumika katika uchimbaji na uchenjuaji, kiasi cha Dhahabu wanachokipata ni asilimia **30** tu na na asilimia **70** inabaki kwenye makinikia ambayo wanauziwa wenye mitambo ya kuchenjulia. Kamati ina maoni kwamba Serikali iangalie namna ya kuwasaidia ili kuongeza tija kwa wachimbaji wadogo na kuongeza mapato kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, wachimbaji wengi wadogo nchini wanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mitaji na hivyo kulazimika kutumia zana duni na kusababisha athari kubwa za mazingira. Kamati inaishauri Serikali kuwasiliana na taasisi za fedha zinazoweza kuwakopesha fedha au vifaa kwa riba nafuu.

### 3.2 Ziara katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu

**Mheshimiwa Spika**, kamati pia ilipata fursa ya kutembelea Bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa lengo la kujionea hali ya mazingira katika Bonde hili. Kamati ilitaka pia kujua mkakati wa Serikali katika kukabiliana na athari za kimazingira katika eneo la Bonde. Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inatekeleza Mradi wa Usimamizi wa Ikolojia ya eneo la Bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa lengo la kurejesha mtiririko wa maji kwa kipindi cha mwaka mzima.

**Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika**, Bonde lote la Mto Ruaha Mkuu linajumuisha vyanzo vya mito mikuu tisa (9). Kwa ujumla hali ya Bonde siyo ya kuridhisha na lipo katika hatari ya kukauka ndiyo maana Mheshimiwa Makamu wa Rais, aliamua kuiagiza Ofisi yake Idara ya Mazingira kuunda kikosi kazi cha kuhakikisha mto Ruaha unarudi katika hali yake ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Bonde la Mto Ruaha Mkuu linakabiliwa na chanagamoto zifuatazo;-

- Kuendesha shughuli za kilimo katika maeneo ya Bonde hivyo kusababisha uchepushaji mkubwa wa maji pasipo kuzingatia mahitaji ya watumiaji wengine hasa wakulima wa Mpunga Mbarali;
- Ongezeko kubwa la idadi ya mifugo inayochungwa katika eneo la hifadhi;
- Kupanuka kwa shughuli za kilimo hasa kilimo cha mpunga katika mashamba ya Mbarali na kulima kando ya mikondo ya mito; na
- Kukinzana kwa baadhi ya Sheria katika kusimamia uhifadhi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu.

### 3.2.1 Maoni ya Kamati kuhusu Ziara yake katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu

**Mheshimiwa Spika**, Bonde la Mto Ruaha linatumiwa na wadau mbalimbali, mfano shughuli za Uhifadhi wa wanyama (Ruaha National Park), uvuvi, kilimo na ufugaji hali inayopelekea Bonde hili kuelemea.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati wakati wa Ziara ilishuhudia madhara ya uchepushaji wa maji usiozingtia kanuni za Mazingira pamoja na mahitaji ya watumiaji wengine. Tabia hii inasababisha upotevu wa maji mengi ambayo yangetumika kwa ajili ya shughuli nyingine za kiuchumi kama uzalishaji wa Umeme. Kamati inaishauri Serikali iendelee kutoa Elimu hasa kwa wakulima kuhusu kufanya matumizi sahihi ya maji.

**Meshimiwa Spika**, kuna miradi mikubwa ya uzalishaji umeme ambayo inategemea maji kutoka katika Bonde hili (Bwawa la Mtera, Kidatu na Mradi mpya wa *Stieglers Gorge*). Kwakuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya miradi hii na uhifadhi wa mazingira itakuwa busara wakishirikishwa kwa kuchangia katika kuhifadhi wa mazingira.

### 3.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa**, jukumu la kusimamia shughuli za uhifadhi na usimamizi wa Mazingira lipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais-mazingira, **na kwa kuwa** Ofisi hii ipo kama wasimamizi wakuu shughuli hizo, **hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Ofisi hii kifedha na kuhakikisha fedha hizo zinapatika kwa wakati ili kusaidia kuratibu masuala ya Uhifadhi wa Mazingira katika maeneo mengi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inalo jukukumu la kufanya ukaguzi katika maeneo yote ambayo yanaonekana kukua kwa haraka mfano, maeneo ya migodi, viwanda, hoteli za kwenye fukwe, kingo za bahari, machinjio na maeneo mengine hatarishi kwa mazingira.

#### 4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KUHUSU BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali na kutoa maagizo kumi (10). Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ilizingatia maoni na ushauri wa Kamati, hata hivyo kuna maagizo ambayo Serikali hayakutekelezwa ipasavyo. Maagizo ambayo hayakutekelezwa ipasavyo ni pamoja na;

i) *Serikali iangalie upya Sheria za Misitu, Mazingira na Mifugo ili kuondoa mgongano wa kisheria katika utekelezaji na uhamasishaji, Wizara zinazosimamia kazi hizi zifanye kazi pamoja.*

**Mheshimiwa Spika**, agizo hili halikutekelezwa kwani mpaka sasa tumeendelea kushuhudia migongano ya Sheria katika kusimamia masuala mbalimbali ya mazingira. Kamati inaendelea kusesitiza utekelezwaji wa agizo hili na inazitaka Wizara hizi kukaa pamoja na kuzileta Sheria hizi Bungeni kwa ajili ya kuzifanyia marekebisho.

ii) *Tozo zinazotokana na shughuli zinazochangia uharibifu wa Mazingira ni nyingi lakini zinakusanywa na Taasisi au Idara nyingine za Serikali. Kamati inashauri tozo hizo walau kwa asilimia 5 ziingie katika mfuko wa Mazingira. Mfano tozo ya magari chakavu, tozo ya mkaa, tozo ya mafuta na tozo ya magogo.*

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa agizo hili si wa kuridhisha, Kamati inaendeleza kusesitiza utekelezaji wa agizo hili kwa kuwa Ofisi ilikwisha kamilisha mapendekezo ya vyanzo vya mapato na viwango vya uchangiaji kwa sekta nyingine katika Mfuko wa Mazingira na kuviwasilisha Serikalini. Kwasababu ya umuhimu wa suala la Mazingira, Kamati inasisitiza mfuko huu uwezeshe kikamilifu.



## 5.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 5.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019

#### 5.1.1 Makisio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi Mazingira (*NEMC*) imepanga kukusanya shilingi **18,877,446,995.00** kutokana vyanzo vyake vya ndani. Makisio ya mwaka wa fedha **2018/2019** ni zaidi kwa asimia **20.4** ikilinganishwa na Shilingi **15,683,161,500.00** mwaka **2017/2018** ambazo hazitafikiwa, hivyo kukosa uhalisia.

#### 5.1.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Raisi kwa ujumla wake na kubaini kuwa mahitaji ya bajeti ya usimamizi na hifadhi ya mazingira ni makubwa kuliko kiasi kilichotengwa. Kamati hairidhishwi na ukomo wa Bajeti ya Mazingira hivyo ni maoni ya Kamati kwa Serikali kwamba iangalie upya ukomo wake.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, Idara ya Mazingira katika mwaka wa fedha **2018/2019** inaomba kuidhinishiwa Shilingi **8,118,494,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia **15.7** ikilinganishwa na Shilingi **9,634,020,437.00** kwa bajeti inayotekelezwa sasa. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,524,540,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo na Shilingi **4,593,954,000.00** ni matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa Shilingi **3,017,072,000.00** ni ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Shilingi **898,782,000.00** ni mishahara (PE) ya watumishi wa Idara ya Mazingira na Shilingi **678,100,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha **2018/2019** Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira, Idara ya Mazingira inaomba kuidhinishwa jumla ya Shilingi **3,524,540,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia **39.1** ikilinganishwa na Shilingi **5,788,452,437.00** kwa bajeti inayotekelezwa sasa. Kati ya fedha hizo Shilingi **1,238,800,000.00** ni Fedha za Ndani na Shilingi **2,063,340,000.00** ni Fedha za Nje.

**Mchanganuo wa Fedha zinazombwa ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018**

Maelezo	20017/2018	2018/2019	Tofauti	Asilimia
Mishahara (PE)	898,424,000.00	898,782,000.00	358,000.00	0.039
Matumizi Mengineyo (OC)	752,100,000.000	678,100,000.00	-74,000,000.00	9.8
NEMC	2,215,044,000.000	3,017,072,000.00	802,028,000.000	36.2
Matumizi ya Maendeleo	5,788,452,437.00	3,524,540,000.00	-2,263,912,437.00	39.11

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huu ni dhahiri kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Idara ya Mazingira kiasi kilichotengwa ni kidogo ikilinganishwa na changamoto za mazingira zinazo likabili Taifa letu. Ni maoni ya Kamati kuwa, kwa kuzingatia uchambuzi huu na ukubwa wa tatizo la mazingira katika nchi yetu, fedha zinazombwa kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, haziwezi kukidhi mahitaji halisi ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa** Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira ilikwisha kamilisha mapendekezo ya vyanzo vya mapato na viwango vya uchangiaji kwa sekta nyingine katika Mfuko wa Mazingira na kuviwasilisha Serikalini. **Na Kwa kuwa** hali ya utengaji fedha kwa ajili ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira si ya Kuridhisha. **Hivyo basi**, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha Mfuko wa Mazingira kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019, unawezeshwa na kufanya kazi kikamilifu.

## 6.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 6.1 HALI YA MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mwenendo wa uharibifu wa mazingira nchini zinahitajika jitihada za mahsusi za kuhifadhi mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, itakuwa ni ndoto kwa nchi yetu kufikiria maendeleo makubwa pasipo kulipa umuhimu suala la uhifadhi wa mazingira. Kuna uhusiana mkubwa sana kati ya uhifadhi wa mazingira na nyanja zote za maendeleo duniani, kwakuwa mazingira ni kila kitu. Ni kwa kuzingatia ukweli huu, Kamati inaishauri Serikali kulipa kipaumbele suala la mazingira kwa ajili ya kuwa na maendeleo endelevu.

### 6.2 MAONI NA USHAURI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishuhudia uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji katika nchi yetu ambao kwa kiasi kikubwa unachangiwa na shughuli za binadamu mfano; ufugaji usiozingatia kanuni na kulima kando ya vyanzo ya maji pasipo kuzingatia matumizi endelevu ya maji. Kamati inaishauri Serikali kusaidia na kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji lakini pia kuwasadia wananchi kwa kujenga malambo ya kunyweshea mifugo, hatua hii itapunguza shughuli za kijamii katika maeneo ya vyanzo vya maji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuwa Wizara zote mtambuka katika mazingira na ambazo sheria zake zinakinzana na Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, kukaa pamoja na kuleta mapendekezo ya marekebisho ya sheria hizo hapa Bungeni, hatua hii itasaidia katika kuongeza nguvu katika udhibiti wa uharibifu wa mazingira nchini.

**Mheshimiwa Spika**, wakati Serikali inaendelea na mchakato wa utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa *Stiegler's Gorge*, ambao kufanikiwa kwake kutategemea kwa kiasi kikubwa uhifadhi wa mazingira katika Bonde la Rufiji (Rufiji Basin), Kamati inaishauri Serikali kwamba ili mradi

huu uwe endelevu ni muhimu utekelezaji wake uwe sambamba na kuongeza juhudi katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira katika Bonde la Rufiji.

**Mheshimiwa Spika**, ufuaji wa umeme katika mabwawa ya Kidatu na Mtera kwa kiasi kikubwa unategemea Bonde la Mto Ruaha Mkuu, bila kuhifadhi mazingira ya Bonde hili na ikolojia yake uzalishaji huu utakwama. Kamati inashauri Serikali kuanzisha chombo maalumu ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais mazingira, kitakachosimamia na kuratibu shughuli zote katika Bonde hili.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na matumizi holela ya zebaki katika kuchenjua dhahabu kwa wachimbaji wa wadogo nchini tena bila vifaa vya kujikinga. Uchenjuaji huu wa kienyeji unasababisha kusambaa kwa zebaki katika maeneo ya makazi. Kwa kuwa zebaki ina athari kubwa kwa afya ya binadamu, Kamati inashauri Serikali kuangalia namna ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili wafanye uchenjuaji ambao ni rafiki kwa mazingira na kuepusha athari zinazoweza kutokea.

**Mheshimiwa Spika**, kuna upungufu mkubwa wa watumishi wa sekta ya mazingira nchini hivyo kuwepo ugumu katika usimamizi wa mazingira. Kamati inaishauri Serikali, kwa mara nyingine tena kuongeza watumishi katika Wizara, Mikoa na Hamashauri zote nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia nzuri ya Serikali kutaka kuwasaidia wachimbaji wadogo kumekuwepo na changamoto mbalimbali za hifadhi ya mazingira. Mfano kuhamahama kutoka eneo moja kwenda jingine bila ya kuzingatia kanuni za kimazingira zilizopo; wachimbaji kuanzisha makazi na shughuli nyingine za kijamii katika maeneo ya migodi bila kuzingatia kanuni za utunzaji wa mazingira. Kamati inashauri Serikali kwamba ili kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na na makazi holela yatengwe maeneo ya makazi katika kila mgodi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuelekea Tanzania ya viwanda, Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa jitihada wanazozichukua katika kukagua na kusimamia utunzaji wa mazingira viwandani. Aidha, Kamati inaitaka Ofisi hii pamoja na NEMC kuongeza kasi ya kuelimisha, kukagua na kuchukua hatua za kisheria kwa wanaokiuka sheria hii. Kukua kwa Sekta ya Viwanda nchini kuna husiana moja kwa moja na uhifadhi wa mazingira. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango mkakati kwa ajili ya viwanda vipya na vilivyopo ili kulipa kipaumbele suala la uhifadhi wa mazingira na uzingatiji wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, dhima ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ni kutoa miongozo itakayowezesha uratibu na usimamizi wa mazingira ili kuwa na maendeleo endelevu na ustawi wa watanzania. Ofisi hii ni msimamizi mkuu wa masuala yote ya mazingira, kiasi cha fedha kinachotengewa ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Ofisi hii, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Wizara zote, Mikoa na Halmashauri zote nchini kutenga kifungu katika bajeti zao na kukiwekea fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa nia yake njema ya kuwapatia maeneo wachimbaji wadogo, uamuzi huu umewakwamua kiuchumi. Changamoto ambayo bado inawakabili katika maeneo haya ni ukosefu wa fedha kwa ajili kufanya tathimini za kimazingira (EIA na EPP) hivyo huendelea na uchimbaji pasipo kufanyika tathimini kuhusu athari za mazingira. Kamati inaishauri Serikali kuwa ili kuepusha athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza ni vema Serikali yenyewe ikafanya tathimini hizi kabla ya kukabidhi maeneo haya kwa wachimbaji.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto za kimazingira Bonde lipo katika hatari ya kukauka. Kamati inashauri kwamba, Serikali iendelee kutoa elimu kwa wana jamii kuhusu athari za kuharibu vyanzo vya maji ya Bonde; kuandaa mipango endelevu ya matumizi ya ardhi ili kuepusha kufanyika kwa shughuli za kijamii katika eneo la Bonde;

kufanya jitihada za kuliingiza eneo la Bonde katika orodha ya maeneo lindwa; kuitumia kwa kamilifu Sheria ya mazingira ya waka 2004, kwa wote wanao kiuka.

**Mheshimiwa Spika**, hali ya utengaji fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira si ya kuridhisha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha Mfuko wa Mazingira kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019, unawezeshwa na unaanza kufanya kazi kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, machinjio mengi nchini hayazingatii Sheria za mazingira hivyo ni machafu sana na yanahatarisha afya za walaji. Aidha, machinjio haya ni ya zamani sana na yalijengwa katikati ya miji kutokana na hali halisi ya kipindi hicho, kwa sasa miji imekuwa na machinjio haya yamekuwa karibu na makazi. Kamati inashuri kuwa machinjio haya yahamishiwe pembezoni mwa miji na ukaguzi a mara kwa mara ufanyike ili kuhakikisha wanafuata sheria za mazingira kwa ajili ya kulinda afya za walaji. Baraza lifanye ukaguzi wa haraka katika machinjio yote hususani yaliyopo maeneo ya makazi ya binadamu na kuchukua hatua za haraka kwa maeneo yasiyozingatia Sheria za Mazingira nchini.

## 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe na Naibu Spika kwa uongozi wenu mahiri. Niwashukuru pia Wenyeviti wote Bunge kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira Mhe. January Makamba (Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Kangi Lugola (Mb) Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa jinsi walivyoshiriki katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha **2017/2018**, na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha **2018/2019**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Bajeti hii mbele ya Bunge lako tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa rukhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard).

i) Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb	Mwenyekiti
ii) Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb	M/Mwenyekiti
iii) Mhe. David Cecil Mwambe, Mb	Mjumbe
iv) Mhe. Balozi Dkt. Diodorus B. Kamala, Mb	Mjumbe
v) Mhe. Salim Hassan Turkey, Mb	Mjumbe
vi) Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb	Mjumbe
vii) Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb	Mjumbe
viii) Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb	Mjumbe
ix) Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb	Mjumbe
x) Mhe. Munde Tabwe Abdalah, Mb	Mjumbe
xi) Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
xii) Mhe. Munira Mustafa Khaibu, Mb	Mjumbe
xiii) Mhe. Mussa Rashid Ntimizi, Mb	Mjumbe
xiv) Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb	Mjumbe
xv) Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb	Mjumbe
xvi) Mhe. Kmamis Ali Vuai, Mb	Mjumbe
xvii) Mhe. Zainab Mdolwa Amiri, Mb	Mjumbe
xviii) Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb	Mjumbe
xix) Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb	Mjumbe
xx) Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb	Mjumbe
xxi) Mhe. Mansoor Hirani Sharif, Mb	Mjumbe
xxii) Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb	Mjumbe
xxiii) Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb	Mjumbe
xxiv) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb	Mjumbe
xxv) Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb	Mjumbe
xxvi) Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, pamoja na yeye namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Kamati za Fedha na Uchumi

Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bw. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu vema shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira Fungu 31 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni kiasi cha Shilingi **8,118,494,000.00** kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Suleiman Ahmed Saddiq, (Mb)  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA**  
**MAZINGIRA**

17 Aprili, 2018

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Musa Ntimizi kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa uwasilishaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza mjadala wetu wa jumla na tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Sware na baadae Mheshimiwa Mtolea ataendelea. *(Makofi)*

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ili nitoe maoni yangu katika Wizara hii husika na nitajikita katika eneo la mazingira. Katika eneo hili nitagusia maeneo matatu ambayo ni Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira; hali ya misitu nchini na athari za mazingira yaani *environmental impact assessment* ambayo inaratibiwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Miradi kupitia *NEMC*.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuzungumzia kuhusu Mfuko wa Mazingira na naomba ni-*quote* hotuba ya Waziri akisisitiza kwamba sekta zote za uzalishaji mali zinategemea mazingira na hivyo rasilimali zinazotokana na mazingira zina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi na hivyo shughuli zisizo endelevu za uzalishaji mali zimechangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira.

Nilikuwa nataka tujikumbushie pia siyo tu kwenye mali au kwenye uchumi lakini sekta zote za kimazingira ndiyo uhai wetu, ndiyo tunachokitegemea. Ni hewa tunayoivuta, maji tunayoyanywa, ni vyakula tunavyovipata kutoka kwenye ardhi au wanyama au mimea yoyote. Cha kushangaza hiki tunachokitegemea ili tuwe hai, wenye afya na wenye uchumi mzuri wa binafsi na wa nchi hatuupi kipaumbele na kipaumbele hiki jinsi kilivyo chini kimekuwa *reflected* kwenye bajeti inayotengewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu wa mazingira ambao unasimamia dhamana ya uhifadhi wa mazingira nchini mwaka unaoenda kuisha 2017/2018 ilikuwa umetengewa shilingi milioni 300 tu na hawakupata hata senti. Mwaka huu wa fedha unaokuja 2018/2019 imetengewa shilingi milioni 500 tu. Sasa sijui kati ya hizo shilingi milioni 500 zinaenda kufanya nini na *probability* ya kuzipata haipo wakati hili ni eneo nyeti ambalo ndiyo linalotuweka hapa duniani na linatufanya tuishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, ukurasa wa 16 walionesha chanzo ambacho tunaweza tukapata fedha kidogo kwa ajili ya Mfuko huu wa Hifadhi wa Mazingira nchini. Pale kwenye *bullet* ya pili wamesema kwamba tozo zinazotokana na shughuli zinazochangia uharibifu wa mazingira ni nyingi lakini zinakusanywa na taasisi au idara nyingine za Serikali. Kamati inashauri tozo hizo walau kwa asilimia tano ziingie katika Mfuko wa Mazingira mfano tozo za magari chakavu, mkaa, mafuta na magogo.

Mimi nilikuwa na-*propose* siyo asilimia tano tu bali twende hata asilimia 90 kingine kidogo ndiyo kibaki kwenye sekta nyingine ili ku-*make sense*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la pili nililokuwa nataka niliongelee ni tathmini athari za mazingira ambapo wanasimamiwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*). Hii ni nyenzo ya pili ya kusimamia hali ya mazingira yetu nchini, lakini hawa *NEMC* ambao ndiyo kitendea kazi chetu na wasimamizi nao wamekatwa mikono. Bajeti hii iliyopita wamepata tu asilimia 36 ya kile walichokiomba ili wafanye kidogo wanachoweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi hela zinazotengwa na nyingine za maendeleo hawapati kabisa, tunafanya hivi makusudi kujiharibia wenyewe au hatuna wataalam wa kusitiza umuhimu wa mazingira nchini na katika uchumi na hali ya wananchi wetu. Tatizo ni nini? Ni Serikali haina macho na masikio, hatujifahamu au tunajifahamu lakini tunafanya makusudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mifano michache, sasa hivi ni nyakati za mvua za masika, Dar es Salaam tunalia mafuriko, Arusha tunalia mafuriko na Morogoro tunalia mafuriko. Ukiangalia kwa upana wake mafuriko ya Dar es Salaam *literally* hayakutakiwa kuwepo. Mafuriko ya Dar es Salaam yamechangiwa na mito mikuu miwili mmojawapo ni Mto Msimbazi. Kwa mfano tu kwenye Bonde la Mto Msimbazi eneo la Jangwani kuna mradi pale wa Serikali (*UDART*), sasa unajuliza *NEMC* walikuwa wapi, *environmental impact assessment* (tathmini ya uharibifu wa mazingira) iko wapi kwa sababu hii mito ina *overflow* kwa sababu mto una njia yake ya asili. Sasa tunapoanza kuingilia njia za asili za mito aidha kwa ujenzi au kutupa taka mle ndani tunaifanya iteme (*overflow*) kwa sababu tumeingilia lile bonde. Sasa unajuliza, mkono wa *NEMC* ulikuwa wapi kwenye mradi wa *UDART* kwa sababu tayari wananchi wa kawaida waliondolewa. Sasa tunalalamika mafuriko na kuwaletea wananchi hasara na vifo juu yake kwa sababu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nijulize nikawa nasema *okay*, NEMC hawana hela, lakini nawafahamu NEMC wana wataalam, ni *colleagues* wangu, kwa hiyo shida siyo utalam. Hapa sasa kuna la ziada zaidi ya hela. Tukumbuke kwamba NEMC ni mkono wa Serikali, NEMC huyu ndiye mtathmini wa shughuli za Serikali kwenye masuala ya mazingira, NEMC ana-*evaluate* vipi mradi wa Serikali ambapo naye ni mpango wa Serikali? Kwa hiyo, *decisions* tunazifanya *politically* badala ya kufanya kitaaluma. Kwa hiyo, nafikiri hii NEMC iangaliwe kwa jicho la ziada iwe *an independent entity* ya kusimamia madhara haya tunayoona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie haraka haraka, kuna *proposal* naona inaanza kuzaa matunda ya uzalishaji wa umeme *Stieglers Gorge*. Mradi huu *proposal* ya kwanza ilianza 1960 lakini umeenda ukisusua siyo kwa bahati mbaya lakini ni kwa sababu ya athari za mazingira. *Stieglers Gorge* iko ndani ya *Selous Game Reserve, the largest game reserve*, si ndiyo? Ina wanyama na ikolojia ambazo ni *unique*, ni *world heritage site*. Mradi huu ambao unaenda kuanzishwa unaenda ku-*affect* Mto Rufiji na vyote vinavyohusiana na Mto Rufiji. Kwenye mdomo wa Mto Rufiji kuna *mangroves*/mikoko, ni msitu mkubwa kuliko yote kwa *East Africa*. Mto Rufiji ndiyo unaoifanya Mafia yako iwepo Mheshimiwa Dau, naomba uniunge mkono kwenye hili. Mradi huu unaenda ku-*affect Ramsar Site* ya Mafia, Kilwa na Rufiji. Sasa tunaenda kuangalia siyo uhai tu shughuli za uvuvi bali na wananchi wote wanaotegemea pale, maeneo yote ya Kilwa, Rufiji, Mtwara wote mnaenda kupata changamoto za kimazingira na za kusihi. Sasa tunavyoongelea haya mambo ya *environmental impact assessment* ndugu zangu tusiende *politically* (kisiasa).

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mtolea na Mheshimiwa Zitto Kabwe ajiandae.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukupa uwezo wa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti inayohusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nianze kwanza kwa kutoa pole kwa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam hasa wapiga kura wangu wa Temeke kwa mvua kubwa ambazo zinakwamisha shughuli zao za kila siku kwa namna moja au nyingine. Niiombe pia Serikali baadhi ya maeneo madhara yamekuwa makubwa kwa sababu ya wao kutotimiza wajibu wao vizuri. Kama pale kwenye barabara ya Mandela kwenye mataa ya Serengeti ambapo kuna shule ya sekondari ya Kibasila mifereji ya barabara imeshindwa kubeba maji yale ya mvua matokeo yake maji yote yanakwenda kwenye shule ile. Sasa hivi naambiwa madarasani maji ni ya kiuno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna barabara ya Jet Lumo - Davis Corner na yenyewe pia Serikali hajaitengea fedha ya kumaliza toka mwaka wa fedha uliopita na mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, mitaro iliyochimbwa mkandarasi hajamalizia, maji yanakwenda kwenye makazi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirudi kwenye hoja mimi nina machache tu na haya machache nayazungumza kwa sababu mara zote yanazunguka kichwani kwangu siyapatii majibu.

Moja, mara kadhaa nimekuwa nikiona vitabu vikiandika kwamba pande mbili za Muungano zilika kujadili Muungano. Huwa nafahamu sana upande wa Zanzibar wana Baraza la Wawakilishi, kwa hiyo, huwa linakaa linakusanya kero na linawapa Wajumbe wake kwamba hizi mwende mkazisimamie kwa maslahi ya Zanzibar. Sijui wanaotoka upande wa Tanganyika huwa wanakaa wapi, wanaambiwa na nani kwamba hizi ndiyo hoja za Tanganyika mwende mkazipiganie. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili huwa sielewi kwa nini tunavunja Katiba hasa tunapokwenda kwenye sherehe za Mapinduzi. Kwenye sherehe za Mapinduzi mtakumbuka ukiacha ile ya mwaka 2016 ambayo Mheshimiwa Rais hakwenda alienda Shinyanga, mara zote Mheshimiwa Rais akihudhuria pale tunamvua madaraka yake tunamvalisha Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye anapanda *motorcade*, anapigiwa mizinga 21 lakini Rais wa Jamhuri ya Muungano mwenye hadhi hiyo amekaa pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo mambo mawili ndiyo nilikuwa hasa nataka kuyazungumzia. Sasa nianze na la kwanza. Kwanza nawapongeza sana wenzetu Wazanzibari kwa namna ambavyo wamekuwa wamoja wakiipigania Zanzibar yao. Mara kadhaa tumeona hata wakiwa hapa ndani linapokuwa jambo ni la Zanzibar wanalipigania bila kujali wanatokea upande upi wa kisiasa na ndiyo maana wenzetu wanafanikiwa. Wametujengea picha kwamba sasa hata Serikali inafikiri kushughulikia kero za Muungano ni kwenda kujibu hoja za kutoka upande mmoja tu wa Zanzibar, wanahisi kwamba Tanganyika hakuna kero. Tanganyika kuna kero nyingi, lakini hatuna pa kusemea kwa sababu hakuna chombo ndani ya Tanganyika ambacho Watanganyika watakaa, watasema kwamba kero zetu au tungependa Muungano wetu uwe hivi. Sasa tumekataa kwenda kwenye Katiba Mpya, lakini kwa nini tusitafute mazingira ambapo Watanzania na wenyewe watapata kusema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namnukuu Msomi Profesa Palamagamba Kabudi ambaye kwenye hii Serikali ya Dodoma yeye ni Waziri wa Katiba na Sheria, siku moja aliwahi kusema siku moja kwamba kwenye kero za Muungano yeye haofii kero za kutoka Zanzibar kwa sababu nyingi ziko mezani na zinajadiliwa, anapata wasiwasi sana na Watanganyika ambao muda mrefu wamekaa kimya na kimsingi hatujakaa kimya, lakini tunasemea wapi? Hakuna kikao chochote mahali popote Watanganyika wanaweza wakakaa wakasema tunataka haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Muungano huu uwe na tija, bora na imara ni lazima tupunguze manung'uniko kutoka kwenye pande mbili za Muungano. Muungano wenye manung'uniko hauwezi kuwa na afya. Japo kuna taswira zile kwamba watu ambao wanataka kuufanyia marekebisho Muungano ndiyo wanaonekana kama hawapendi Muungano lakini kiukweli hata nyumba yako kama unaipenda sana utakuwa unaifanyia ukarabati ili iendelee kuwa nzuri wakati wote. Kwa hiyo, msiotaka tujadili Muungano na kujiaminisha kwamba Tanganyika haipo na wala haikuwepo, ninyi ndiyo hamuutaki Muungano kwa sababu bado hitaji la Watanganyika kukaa na kusema linaendelea kuwa la msingi. Sasa ni vizuri hili kama ni jipu Serikali mlililiki jipu hili ili mpange hata tarehe ya kulipasua, mkiacha wananchi walililiki watakuja kulipasua siku ambayo ninyi hamjajiandaa kushika usaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwafurahisha Watanganyika siyo kuwabana Wazanzibari, ni kuwaacha Watanganyika nao waseme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea, naomba hilo neno Tanganyika utumie Tanzania Bara, ndio ilivyo rasmi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuufurahisha upande huu huku, siyo lazima kuwaminyia Wazanzibari kwamba labda wakitaka kujiunga na FIFA tuwakatalie, wakitaka kujiunga na IOC tuwakatalie, hapana. Tuwaunge mkono ikiwezekana wapate hata mamlaka kamili lakini na upande huu pia tupate pa kuzisemea kero zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa upande huu ambao hutaki niwaite Watanganyika, wa upande huu, kuna mambo ambayo kwa kweli... *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea ni Watanzania Bara siyo wa upande huu. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Ni Tanganyika.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama muda wangu unanitunzia maana unani-*interrupt* sana wakati si lazima niseme Tanzania Bara, nikisema upande huu, huku ni Bara. (*Kicheko*)

## T A A R I F A

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa mara moja.

**MHE. AIDA J. KHENAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie mzungumzaji kwamba nchi zilizoungana ni Tanganyika na Zanzibar na siyo Bara na Zanzibar. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea endelea, lakini tusifanye ubishani, Katiba inatambua Tanzania Bara, tuendeleo. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo naliacha kama halikufurahishi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha mwisho nachotaka kusema kwa nini tunayapora mamlaka ya Rais tunapomtaka ahudhuri Sherehe za Mapinduzi? Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 33(1) na (2) inamtaja Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ndiye Kiongozi Mkuu wa nchi hii, ndiye Kiongozi Mkuu wa Serikali na ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yote, lakini anapokwenda kwenye Sherehe za Mapinduzi yeye anaingia wa pili na Mheshimiwa Dkt. Ali Shein anaingia mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Wakati Mheshimiwa Dkt. Ali Shein anaingia, Rais wa Jamhuri ya Muungano ambaye ndiye mwenye hadhi ya kuwa wa mwisho

inabidi asimame kumkaribisha anayeingia, hakuna itifaki ya namna hii duniani hapa. Ingekuwa ni busara kwenye sherehe zile Mheshimiwa Rais asiende, anaweza kwenda Naibu Waziri wa Mazingira akawakilisha Serikali ili Mheshimiwa Dkt. Shein anapointia awe mkubwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtolea. Tunaendelea na Mheshimkiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru. Nina mambo mawili tu ambayo napenda kuchangia. Kwanza, nimpongeze sana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, dakika tano.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Ndiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Makamba kwa kazi kubwa anayoifanya, tumemuona maeneo mbalimbali hasa maeneo ya mazingira na kule Zanzibar kutatua matatizo mbalimbali. Hata hivyo, kuna mambo ambayo nadhani juhudi zinazofanyika haziendani na matokeo yatakavyokuja kuwa. Na mimi nina mambo mawili tu ambayo nataka kuchangia kwa dakika hizi tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni la Zanzibar, bidhaa kutoka Zanzibar kuingia katika soko la Tanzania Bara (soko la Tanganyika). Nimeona kwenye taarifa ambayo Waziri amezungumza, amesema kwamba miongoni mwa majukumu anayoyafanya ni kuondoa vikwazo vya biashara kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Kamati imempongeza Waziri na Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kuzikutanisha sekta za biashara za pande mbili za Muungano kwa ajili ya kujadili upatikanaji wa fursa za masoko kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.



Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba katika *stages* za *integration* sisi tuko *stage* ya juu kabisa ya *political federation*. Kwa maana ya kwamba tumeshapita kwenye *free trade area, customs union, common market, monetary union* na sasa tuko kwenye *political federation*. Iweje leo tuanze kuzungumza kuondoa vikwazo vya biashara wakati katika hali ya kawaida ilitakiwa bidhaa zote zinazozalishwa Zanzibar ziingie kwenye soko la Bara bila vikwazo vya aina yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo mengi ya Muungano yanasababishwa na Tanzania Bara kuzuia fursa za kiuchumi za Zanzibar. Leo hii Serikali inasema kwamba, inazuia kwa mfano, sukari kutoka Zanzibar kwa sababu ya kuzuia magendo, lakini hii Tanzania Bara ambayo inazalisha sukari Kagera na bado ina-*import* sukari kutoka nje, inaruhusu Kagera kuuza sukari Uganda. Kuna sukari kutoka *Mumias Sugar* inayoingia huku Tanzania Bara kwa sababu tupo kwenye *East African Common Market*, bidhaa zinatembea bila vikwazo vya aina yoyote, iweje Zanzibar izuiwe kuleta bidhaa zake huku? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni suala la udhibiti wa bidhaa ambazo zinatoka nje wanasema kwamba sijui kuna sukari kutoka Brazil na kadhalika kwenye *customs union* kuna kitu kinaitwa *rules of origin*. Kwa hiyo, wataalam na maafisa wa Wizara ya Viwanda na Biashara wangukuwa kule Zanzibar wakatazama kinachozalishwa, wakatoa *rules of origin* bidhaa hii ikaingia huku kuuzwa.

Kwa hiyo, inavyoonesha hapa ni dhahiri kwamba uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano sasa hivi hauna nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba Zanzibar inajitegemea kiuchumi ili Tanzania Bara iendelee kuitawala Zanzibar kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba jambo hili liweze kupatiwa ufumbuzi kwa sababu hakuna sababu yoyote ile ya kuzuia bidhaa yoyote kutoka Zanzibar kuingia Tanzania Bara kwa sababu sisi...

## T A A R I F A

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 64.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1), taarifa zinazozungumzwa si za kweli kwa misingi ifuatayo; yeye Mheshimiwa Zitto anafahamu fika namna gani Muungano wetu wa Zanzibar na Tanzania Bara ulivyo na kwa mujibu wa Katiba na sheria tunashirikiana. Kwa hiyo, asilazimishie kupata umaarufu usio wa kweli...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Kwa kujaribu kupotosha kwa kuleta mambo ambayo yanasababisha kutokuwa na upendo, usifanye hivyo mwanangu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Zitto muda wako umemalizika.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**MWENYEKITI:** Dakika moja tu.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mazingira. Nafahamu kwamba sasa hivi tunashughulika na *Stiglers' Gorge* na kadhalika, lakini tunafahamu kwamba kuna madhara makubwa sana ya mradi huu. Kwa sababu Waziri amesema wamefanya tathmini wanayo ofisini, tunaomba Bunge lipate tathmini ambayo Wizara imefanya kuhusiana na mradi wa *Stiglers' Gorge*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu zaidi ni kwamba, kuna miradi mingi sana iliyoainishwa kwenye *Power System Master Plan* ambayo ingeweza kuzalisha umeme sawasawa na huo umeme ambao tunaenda kuuzalisha *Stiglers' Gorge*. Serikali haitekelezi miradi hiyo, inaamua kuingiza fedha za umma, tena tunajitamba kwamba tutatengeneza kwa fedha zetu za ndani, tunaenda kupoteza fedha nyingine kwenye mradi ambao utakuwa *white elephant*. Kwa sababu *Stiglers' Gorge* iko *down stream*, kuna miradi ambayo ilipangwa ipo *up stream* ambayo ingeweza kuzalisha umeme huohuo ambao tunataka kuuzalisha kwenye *Stiglers' Gorge*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tiswekwa dakika tano na tutamalizia na Mheshimiwa Jamal dakika tano.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii.

Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kazi nzuri wanazozifanya lakini pongezi za pekee zimuendee Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama yetu Mheshimiwa Samia kwa juhudi kubwa sana anazozifanya katika kuifanya Tanzania kuwa ya kijani. Kwa hiyo, tuendeleo kumuunga mkono, tunamuona katika upandaji wa miti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi hizi za mama yetu naona kama vile zinakinzana, yeye anasema tupande miti na miti inapandwa, lakini kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira, wengine wanaendelea kukata miti. Nitolee mfano kwenye Mkoa wangu wa Morogoro katika Halmashauri ya Morogoro, ile Milima ya Uluguru ndiyo chanzo kikubwa sana cha maji, lakini ukiangalia kwenye ile milima ambapo kulikuwa hakuna shughuli ya kibinadamu inafanyika lakini sasa hivi kuna ujenzi holela. Ukiangalia milima ile ya Bigwa, Kigurunyembe kuelekea Pangawe, ujenzi unaendelea tena wa nyumba za nguvu, nani anatoa vibali na hawa watu wanachukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro leo tunakunywa maji ya chumvi? Kwa kweli, haikubaliki. Kwa hiyo, tunaomba juhudi hizi za Serikali ziungwe mkono mpaka huku kwenye halmashauri zetu maana ndiyo kwenye watu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kingine niseme uharibifu wa mazingira unasababishwa pia na shughuli za kiuchumi na maendeleo ya binadamu. Hatuwezi tukazuia maendeleo, lakini tunatakiwa tuwe na *sustainable development*. Kwa hiyo, kila aina ya maendeleo inayofanywa basi lazima tuhakikishe maendeleo haya yanakuwa rafiki kwa mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza kuhusu suala la *Stiglers' Gorge*, hii haikwepeki, tunajua matatizo ya umeme ambayo tunapata katika nchi yetu na tunasema Tanzania ya viwanda lazima tuwe na umeme ambao ni *sustainable*. Ombi langu ni kwamba ile tathmini iliyofanywa (*environmental impact assessment*) vile vitu vizingatiwe ili isije ikaleta madhara, lakini mradi una umuhimu wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nizungumzie uchafuzi wa mazingira ambao umekithiri na sasa hivi unatuletea madhara makubwa sana nchini. Tumeona mafuriko Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza, Arusha, kila sehemu, lakini tatizo kubwa hapa ninaloliona mojawapo ni taka ngumu hizi ambazo ni *product* za *plastic bags* pamoja na chupa. Kama Serikali tulifanya mkakati wa makusudi kuweza ku-*ban* viroba ambavyo pia vilichangia kuharibu mazingira lakini hata afya za watu, kwa nini tusifanye mkakati huo huo katika ku-*ban* uzalishaji wa *plastic* na matumizi haya ya *plastic* kwa sababu inaleta madhara makubwa sana kwa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapata hasara, hivi ukiangalia kodi inayopata kwa vile viwanda na gharama inazopata ambapo wananchi wanapata hasara ya mali zao, magonjwa, miundombinu, hivi tukifanya *cost benefit analysis*, kweli hii *plastic* ina tija katika nchi yetu? (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Haina.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie kizazi cha leo na cha kesho kwa sababu inatengeneza *pollution*. Sasa hivi mito mingi Dar es Salaam huwezi ukanywa maji, inakuwa *depleted*. Maji hayatumiki, ardhi itafika mahali haitumiki, hewa yetu itakuwa haitumiki, sasa kitu kisipotumika maana yake kinakuwa *depleted*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mazingira Mheshimiwa Waziri, pamoja na mikakati hii utekelezaji sasa ndiyo unaotakiwa kwa sababu, madhara, vyanzo, tumeshavijua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kingine niseme kuhusu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jasmine, ahsante.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jamal.

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi, acha nijielekeze moja kwa moja kwenye kuchangia hotuba na mimi nitajiekeza kwenye suala la mikopo ya nje. Suala la mikopo ya nje linasimamiwa na Serikali ya Muungano, ni suala la Muungano. Kumekuwa na ucheleweshaji wa muda mrefu sana kupatia *approval* miradi ya kimkakati ambayo inafanyika kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi, jengo la *Terminal II* katika Uwanja wa *Amani Abeid Karume International Airport* limesimama toka mwaka 2014. SMZ

imeomba *extension* ya mkopo kwa ajili ya kukamilisha mradi ule lakini mpaka leo hii bado. Sote tunajua uchumi wa Zanzibar unategemea utalii na bila kuwa na *airport* kubwa yenye uwezo hatuwezi kufikia lengo lile ambalo tumejiwekea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Zanzibar kwa takribani 40% unachangiwa na sekta ya utalii. Matarajio ya Zanzibar ni kupokea mwakani wageni wapatao 500,000. Kwa *infrastructure* iliyokuwepo pale haitoshi. Tunaomba kabisa suala la *approval* ya mikopo hii lifanywe kwa wakati na kwa haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, tuna mradi mwingine wa Bandari ya Mpigaduri. Kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 tumeahidi katika kipindi cha miaka mitano hii tutajenga Bandari ya Mpigaduri kwa ajili ya mizigo, lakini mpaka leo bado *approval* za mikopo hii haijatokea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu miradi hii mikubwa miwili ni toshelezi kabisa kwa kusaidia uchumi wa Zanzibar. Kukamilika kwa miradi hii kutaufanya uchumi wa Zanzibar kuimarika, lakini si kuimarika kwa uchumi wa Zanzibar tu, pia kuimarika kwa uchumi wa Tanzania kwa ujumla wake. Uchumi wa pande zote hizi zina-*compliment each other*, tunajua mizigo itakayoshushwa Bandari ya Mpigaduri mingine itaenda Rwanda, Burundi, Zaire, Congo lakini itaenda kupitia wapi, itapitia Bandari ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri aje atuelezee nini hasa tatizo katika *approval* ya mikopo hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine ni suala la biashara ya pamoja. Mimi naamini kabisa moja ya sababu kubwa na faida za Muungano wetu ni fursa za biashara kwa upande wa Zanzibar kuja Bara na upande wa Bara kwenda Zanzibar. Ukifanya *trade analysis*, hizi changamoto za leo miaka ya 1990 hazikuwepo. Ukichukua *analysis* za miaka ya 1990 Zanzibar ilikuwa inauza zaidi Bara kuliko Bara inavyouza Zanzibar. Nimeona jitihada ambazo Waziri anasema kuna

ZBS na ZFDA, lakini kwa nini haya mambo yako upande mmoja tu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vikija Bara ndiyo kunakuwa kuna TBS na TFDA lakini vitu vya Bara vinakuja Zanzibar bila ya haya matatizo. Hizi changamoto zimechukua muda mrefu kutatuliwa. Kwa hiyo, mimi pia nimuombe Mheshimiwa Waziri, hili suala alitizame kwa upana na uzito wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza ni suala la kodi ya forodha. Kodi ya Forodha iko kwa mujibu wa utaratibu. Leo hii ukienda kukaa Bandari ya Dar es Salaam pale, watu wanaotoka Zanzibar, mtu akinunua kitu chake kidogo tu akifika pale anatozwa kodi. Unajuliza hizi base za kodi wanazotozwa ni zipi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano hai, juzi kuna mwananchi wa Jimboni kwangu amesafiri na cherehani moja tu, amefika Bandari ya Dar es Salaam ametakiwa alipe shilingi 100,000. Cherehani ya shilingi 200,000 Dar es Salaam, alivyofika bandarini ametozwa shilingi 100,000. Kwa hiyo, haya tunayoyazungumza ni muhimu sana yatizamwe na haya mazungumzo yanazungumzwa nenda, rudi...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jamal muda wako umemalizika. Ahsante sana kwa mchango wako. Naamini Mheshimiwa Waziri atayachukua kwa uzito wake.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge, naomba niwataje tu wachangiaji ambao wataanza kuchangia jioni ya leo. Tutaanza na Mheshimiwa Ali King, Mheshimiwa Ussi Pondeza, Mheshimiwa Tauhida Galos na Mheshimiwa Machano Othman. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 07.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tunaanza na Mheshimiwa Ussi Pondeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi hii. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunjalia afya njema, lakini la pili nataka nizungumzie zaidi hii Wizara yetu ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya mambo ambayo humu kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri ameeleza kuwa kuna Kamati ile ya SMT inayashughulikia, lakini muda mrefu umepita na kila siku tunapata majibu ya kuwa kero hizi zinashughulikiwa. Nataka nijielekeze sehemu moja tu katika huduma ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemwa Zanzibar tunadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 131, lakini ukweli uliokuwepo hazifiki hata shilingi bilioni 40. Kila mwezi tumekuwa tukilipa *current bill still* wenzetu upande wa pili ambao ni *TANESCO* wamekuwa wakituwekea *bill* ile ile ya kutuambia tunadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 130. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, hivi juzi juzi tu tulipokuwa katika Kamati ya Nishati na Madini tuliweza kui-*raise* hoja hiyo, Mheshimiwa Waziri upande wa huku akawaita na watu wa Zanzibar, lakini wamekaa bila kupata muafaka wa kusema juhudi hizi zinaendelea kuchukuliwa. Ukweli uliokuwepo na ushahidi upo sisi hatudaiwi zaidi ya shilingi bilioni 133. Cha kushangaza kila mwaka imekuwa kelele Zanzibar inadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 130, Zanzibar hatulipi umeme, lakini ushahidi upo ambapo tunalipa lakini hii kero imekuwa kubwa. (*Makofi*)



## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kulisema hili kwa sababu hii ni kero ambayo inawakera sana Wazanzibar kwa maana kuna baadhi ya watu hufikia *stage* ya kusimama humu ndani ya Bunge na kuanza kusema Wazanzibar tunawabeba tu, umeme wanatumia hawalipi, kuna baadhi ya mambo hivi na hivi wao kazi yao ni kupewa tu. Ukweli uliokuwepo hizi kero zingekuwa zinashughulikiwa kwa muda kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Waziri basi haya yote yasingekuwa yanajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili imekuwa ni kawaida kuambiwa kila siku vinakaa vikao baina ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar, lakini hakuna hata mara moja ambapo unakuja mrejesho kwamba watu wamekaa na wameamua hivi na kero hii imeisha na imebaki kero hii. Sisi tunaelewa kero ni sehemu ya maisha na changamoto ni sehemu ya maisha, lakini tupewe zile kero ambazo kweli zinatuhusu sisi Wazanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofika mahali jambo tunalifanya kwa kutimiza wajibu wetu, lakini leo hii wenzetu upande wa pili wanafika mahali wakaona kama labda sisi tunasaidiwasaidiwa tu bila kuwa na nguvu yetu wenyewe kusema kweli hatuwezi kujisikia vizuri upande wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu mambo ya biashara. Kwenye ufanyaji wa biashara kuna utozaji wa kodi mara mbili. Zanzibar ukinunua mzigo Dar es Salaam *let say Tanzania Cable* unapeleka Zanzibar huku unalipa VAT na ukifika Zanzibar pia ulipe VAT. Hili suala linawaumiza wananchi wetu wa chini kwa sababu tunalipa VAT mara mbili maana yake tunalipa VAT asilimia 36. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili mwaka 1995 mpaka 2000 halikuwepo, kulikuwa na utaratibu baina ya Serikali ya Tanzania Bara na Serikali ya Zanzibar kubadilishana zile *tax invoice* kwa ajili ya kudai upande wa pili lakini unalipia VAT sehemu moja *last destination*. Leo hii ukitoa mzigo Zanzibar

ambapo umelipia kila kitu ukifika Dar es Salaam lazima pia ulipe. Sasa hili linaonesha jinsi gani sisi upande wa pili tunapata uonevu au tusiseme uonevu tuseme labda kuna jambo ambalo halijakaa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri katika kikao cha tarehe 28 basi hili ni jambo moja la msingi lichukuliwe kwa umuhimu wake na kwa ufasaha kabisa tupate majibu ya haraka. Kwa sababu wananchi wetu wanafika mahali wanaudharau Muungano wanasema una faida gani maana mtu akinunua tv Dar es Salaam akienda nayo Arusha halipi kodi lakini ukichukua tv Dar es Salaam ukienda nacho Zanzibar inabidi ulilipie tena kodi. Hivi ni vitu ambavyo vinaturudisha nyuma sisi kama Wazanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba kuna mambo ambayo yana faida ya Muungano lakini hayaelezwi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya Muungano ambayo na sisi tunakiri inatusaidia kama *MIVARP*, tumepata masoko, barabara zimejengwa zote zile ni faida ya Muungano, lakini wananchi wa chini hawana habari kama hivi vitu vinatoka kwenye Serikali ya Muungano. Wanafika mahali wanakwambia kwa *style* hii sisi Muungano hatuoni faida yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mzanzibari namba moja nakubali Muungano huu ni mzuri isipokuwa unahitaji kurekebishwa na kero hizi ndogo ndogo ndizo ambazo zinazaa haya mengine yote ya kusema tuna kero na kuona Muungano hauna faida lakini kiukweli una faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri January Makamba kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Kuna baadhi ya mambo mengi ambayo ameyatatua yeye kwa kipindi chake ambayo yalikuwa ni kero kubwa ambazo sisi tunazifahamu.

Tunampongeza sana na tunataka tu kumwambia kwamba, aendeleze juhudi zake kutoka hapa alipofika na haya mengine *inshallah* Mwenyezi Mungu atamjalia ayamalize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niliseme ni kuhusu kodi ya magari. Ukitoa gari Zanzibar lina namba ya *ZNZ* ukifika nalo Dar es Salaam unazuiwa lakini ukitoa gari Tanzania Bara ina namba za *STK, TZD* zote zinaenda Zanzibar na zinatumika. Magari yetu Zanzibar yakija Tanzania Bara wanaya-*treat* kama magari ya nje kitu ambacho siyo cha maana kweli kweli na hii yote ni nchi moja. Unapokuja hapa ukisema nchi yetu ni ya Muungano lakini magari ya Tanzania Bara yakija Zanzibar ...

## T A A R I F A

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa tu mzungumzaji kwamba magari kutoka nchi jirani za Afrika yakiingia Tanzania wanapewa kibali maalum cha kutumia kwa ajili ya matumizi yao, lakini hilo kwa Zanzibar halipo. Nampa taarifa hiyo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ussi Pondeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naipokea taarifa hiyo kwa sababu ndiyo kitu nilichokuwa nakisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la ushuru hizi ni zile kero ndogo ndogo ninazomwambia Mheshimiwa Waziri January Makamba azitazame. Zile kero ambazo zinatukabili ambazo zinatakiwa kuuweka sawa huu Muungano wetu basi ni kama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sioni sababu kwa nini gari ikitoka Zanzibar inakuwa *treated* kama gari ya kutoka nje, lakini gari ya Kenya au Uganda ikifika hapa inapewa kibali na mtu anatumia mpaka anamaliza shida zake. Kwa nini sisi Zanzibar na sisi tusiwe hivyo na hii ni nchi moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafika mahali tunajuliza aah au sisi huku tumeegemeaegemea tu, tunabebwabebwa, lakini sisi tuna haki zetu na tumesimama kwa miguu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo Mheshimiwa Waziri nakuomba unapokuja kuhitimisha basi moja ya mambo ambayo tunataka utupe ufafanuzi Wazanzibar ni kuhusu magari na mizigo yao inavyokuja na kwenda jinsi gani VAT inachukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ussi. Tunaendelea na Mheshimiwa Othman Machano.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machano, baadae ajiandae Mheshimiwa Tauhida.

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachangia hotuba hii lakini wiki moja ijayo tutakuwa tunaadhimisha miaka 54 ya Muungano wetu. Kwa hiyo, jambo hili ni jema sana kwa leo kulizungumza katika Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia mambo matatu. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wa Nchi kwa kitabu chake hiki kizuri, nikienda katika ukurasa wa sita amezungumzia jinsi ambavyo wamefanya vikao vya kuzungumzia kero za Muungano. Kwa bahati nzuri vikao hivi vimeanza muda mrefu sana na kwa bahati mbaya hapo hapo matokeo ya vikao hivi utekelezaji wake unakuwa mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pande mbili za Muungano yaani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar walifikia makubaliano kuhusu ajira za taasisi za Muungano kwamba katika taasisi za Muungano asilimia 21 za ajira zote zitengwe kwa ajili ya Zanzibar kwa watu ambao wana elimu na weledi wa kazi ambazo zitatangazwa kwa upande wa Bara. Ukiacha taasisi za ulinzi kama Jeshi la wananchi wa Tanzania, Polisi na Uhamiaji, taasisi zote zilizobakia hazijatekeleza suala hili.

Naomba Mheshimiwa Waziri akija kufanya majumuisho atuambie ni sababu gani za msingi zaidi ya miaka mitano sasa suala hili halijatekelezwa. Suala hili linaleta kero, manung'uniko kwa watu ambao wana sifa, baadhi ya Wizara wanazona za Muungano lakini Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi mpaka watumishi wote hamna. Siyo jambo jema na linaleta ukakasi sana katika shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika makubaliano ambayo yamefanywa pia pande mbili zilikubaliana kwamba Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu ifanyiwe marekebisho katika Bunge hili ili iweze kuridhiwa na Zanzibar kwa kupitia Baraza la Wawakilishi. Hadi leo sheria hii haijafanyiwa marekebisho na bado suala la uvuvi wa bahari kuu linaleta tabu na haliwezi kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hili ambalo Mheshimiwa Pondeza alilizungumzia la vyombo vya usafiri au vyombo vya moto. Ni kweli kwamba vyombo kutoka Zanzibar vikija Bara vinatozwa fedha na havipati *permit* vizuri. Hata hivyo, nalo hili wamekubaliana Serikali mbili kwamba

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wafanye marekebisho kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kifungu kimoja tu cha sheria ili sheria hii iwe vizuri, lakini mpaka leo bado haijafanyiwa marekebisho. Hili nalo nataka ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri wakati akija kuhitimisha hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika kitabu hiki imeelezwa kwamba pamoja na kuimarisha Muungano ofisi hii imejenga makazi na Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar, lakini hadi leo wajenzi wa Ofisi zile hawajamaliziwa malipo yao karibu mwaka wa nne au wa tano sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamuomba Mheshimiwa Waziri nalo hili alione kwamba ni kero pia kwa wale ambao wamejenga ofisi hizi. Ni vizuri kwa Makamu wa Rais kuwa na Ofisi nzuri Zanzibar lakini pia kuwa na *staff* wazuri Zanzibar ili kuweza kushughulikia masuala haya ambayo ni sehemu ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala ya Muungano ambayo yamekubaliwa nje ya Muungano ni kutoa fursa kwa upande wa Zanzibar kupata soko kwa Tanzania Bara. Jambo hili utekelezaji wake umekuwa mgumu sana hata bidhaa ndogo ndogo ambazo zinazalishwa Zanzibar kuingia Bara ni jambo gumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linaambatana na sheria ya kwamba ukianzisha kiwanda Zanzibar lazima upate leseni kutoka Bara yaani *BRELA*. Kwa hiyo, tunafikiria kwamba ni vyema kwa upande wa Jamhuri wangepikiria kuanzisha wakala ama Ofisi ya *BRELA* Zanzibar ili Wazanzibar waweze kuanzisha viwanda kukidhi mahitaji ya Zanzibar na kukidhi soko la Tanzania Bara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ahadi za viongozi. Viongozi wetu wa Kitaifa wanatembelea Zanzibar na Bara na kote huko wanatoa ahadi, lakini utekelezaji wa ahadi kwa upande wa Zanzibar unakuwa mgumu na wa muda mrefu. Zipo ahadi tangu Awamu ya Nne ambazo

zimetolewa Zanzibar ikiwemo ahadi ya barabara ya Fuoni mpaka leo bado haijajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili kwamba ni changamoto katika Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nisilalamike tu pia niwapongeze sana kwa kupitia mradi wa *TASAF*. Serikali ya Jamhuri ya Muungano imefanya vizuri sana katika mradi huu na kwa upande wa Zanzibar mradi huu unafanya vizuri. Tunaipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano na tunasema kwamba ni vyema miradi kama hii iwe inapelekwa Zanzibar kwa kiwango kizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa kwa upande wangu mimi ni kuhusu fursa za kibiashara kama nilivyozungumza mwanzo, lakini pia Zanzibar ni sehemu ya kisiwa kwa hivyo shughuli nyingi za kibiashara zinakuwa katika huduma. Huduma za kibiashara ndiyo ambazo zinaingiza fedha nyingi Zanzibar kama mitandao ya kijamii, simu na kadhalika.

Kwa hiyo, fursa hizi zifunguke zaidi ili Zanzibar waweze kufaidika. Wenzangu asubuhi walizungumzia utalii na majengo ya kisasa ya *airport* na bandari haya ni msingi mkubwa katika uchumi wa Zanzibar. Tunaomba sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano iwaunge mkono Serikali ya Zanzibar katika utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii na sina mengi zaidi ya hayo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Machano. Tunaendelea na Mheshimiwa Tauhida na Mheshimiwa Ally Keissy ajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya

kuchangia. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Rais wangu wa Zanzibar kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue fursa hii nimpongeze Makamu wa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya hususani wakati huu amejikita kwenye suala la mazingira pamoja na Wizara yake, kazi inafanyika vizuri. Matumaini yangu kwamba baada ya hapo mtaendelea kuondosha kero ndogo ndogo za Muungano zilizobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa jinsi ya pekee nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi na vitendo vikubwa na mambo mengi anayowafanyia Watanzania yenye tija, yenye muonekano na yenye faida kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kumshukuru Waziri na Naibu wake kwa kitabu chao kizuri, chenye mwelekeo na mwonekano wa kutatua kero za Muungano hususani pale kaka yangu Mheshimiwa January alipomalizia kusema yupo tayari kupokea kasoro ndogo ndogo na kero ndogo ndogo za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi hiyo basi nafarijika kumwambia kwamba kero ndogo ndogo za Muungano zipo na kweli zinahitaji utatuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwenda moja kwa moja kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa tisa ambapo amezungumzia suala la elimu juu ya la Muungano.

Mheshimiwa Waziri na Naibu wako suala la elimu kwa Muungano linahitajika na siyo kuhitajika nje tu kwa wananchi hata Bungeni kwa Wabunge sisi tuliokuwepo humu tunahitaji kujua faida za Muungano, tunahitaji kujua uwepo wa Muungano na tunahitaji kujua nini maana ya Muungano. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, namwambia kaka yangu Waziri inawezekana ukachukua muda mkubwa kuwaelimisha wananchi lakini wenyewe Wabunge hatukuelimika juu ya suala la muungano. Maana leo ukisimama Mbunge unazungumza suala la Muungano kana kwamba sio Mbunge inakuwa haina afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili kwangu ni ombi kwa Waziri naomba suala la elimu ya Muungano tupewe na sisi Wabunge, inawezekana Tauhida ninavyouangalia sivyo anavyouangalia mwingine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri niombe elimu hii atakapopata fursa atulettee Bungeni ili tunapotoa michango kama Wabunge tujue nini tunazungumza juu ya suala la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kati ya hivyo vitu vidogo vilivyopo. Kaka yangu Mheshimiwa January anakuja kila siku Zanzibar na tunamwona, sasa hivi hata mtoto wa miaka mitatu anamjua. Tunachokiomba kwake sasa atumie boti aache kutumia ndege, atumie boti kwenda Zanzibar ili apate kuona kero za wananchi wanyonge, mnyonge hapandi ndege, mnyonge siku zote anapanda boti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwambia kaka yangu Mheshimiwa January kwa sababu akipanda boti atajua nini kinachowakabili wananchi wa Tanzania katika suala zima la Muungano. Leo kaka Mheshimiwa January kijana kuliko yeye, umri chini yake, anatoka Zanzibar kwenye sherehe za pasaka Mtanzania bara anabeba TV ya inchi 14 kafurahia pasaka anasema nakuja huku nipate hii TV ya inchi 14, anatozwa ushuru ambao hatuufahamu mpaka leo. TV kainunua 125,000 anaambiwa TV ile ilipiwe 100,000, kijana kwa jicho langu namwona anaipiga chini TV bandarini vitu ambavyo ni vya masikitiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wakati anazindua mradi wa reli...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MJUMBE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji pale kwamba sio kijana tu, mwenyewe nimepita bandarini nimetozwa shilingi laki moja kwa ka-TV ka inchi sijua saba, sijui inchi ngapi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tauhida taarifa.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa kaka yangu January zinapoongelewa kero achukulie mfano wa ndoa ya mtu mwingine yoyote, maana hata kero kwenye ndoa zetu huwa haziishi. Kwa hiyo, Mheshimiwa January hizi ni changamoto aziandike aone jinsi gani ataweza kuwasaidia Watanzania. Leo kijana anakwenda pale anaipiga TV, amini Mungu kuna baba amebeba viporo vitupu zaidi ya ishirini anaenda kutia dagaa anatoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar vitupu, anachajiwa kiporo kimoja kanunua shilingi 100 anaambiwa alipe elfu 50, gharama ya vipolo vile 20,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama nimwambie Mheshimiwa kaka yangu January, Rais alizungumza wakati anazindua mradi wa reli, alisema kuna watu wana hujumu Taifa hili kwa kusingizia Muungano, kwa kutupia tope Muungano na wanatumwa na baadhi ya viongozi wenzetu. Mheshimiwa January kaka yangu, naomba kama kuna watu tusimsubiri kila kitu afanye Rais, aende, apite bandarini, tukisema hili Mheshimiwa kaka yangu atoke Makamu wa Rais aende litatia aibu, atoke, aende, akaangalie nini kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unawatoza wananchi kodi? Hiki kinafanywa kaka yangu sio lengo la Serikali, baadhi

yao hawajaagizwa na Serikali, wanafanya kusudi kuupaka tope Muungano wetu. Kaka amepewa dhamana kubwa, dhamana aliyopewa Rais alijua ataitendea haki nchi hii, atawasaidiaje Watanzania, atumike kwenye nafasi yake, atoke, aende kama kuna viongozi au watendaji anahisi ni wabovu awatoe, afute. Rais amewazungumza sio mara moja, mara mbili wala mara tatu, Rais kila siku anawakemea lakini hivi vilivyobaki vifaurongo ahakikishe anaviondoshaye, hatuhitaji Rais aende akamalize kazi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwambia Mheshimiwa kaka yangu January leo kero iliyopo pale kwenye Muungano ndio tutazimaliza hapa, kuna kero kubwa. Unakuta mtoto anatoka shule hii Tanzania ni yetu, anatoka shule Tanzania Bara labda anasoma Morogoro, anakwenda zake Zanzibar, tumezoea tiketi ni Sh.25,000/= anafika pale mwanafunzi wa shule anaambiwa akate tiketi ya Sh.50,000/= au Sh.60,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai kuna biashara za watu binafsi tunajua hakuna uhuru usiokuwa na mipaka, uhuru wowote una mipaka. Ikiwa nchi watu wanataka kufanya kazi bila kuwa na mipaka hatutokwenda, lazima kama kuna wafanyabishara binafsi washughulike nao, wazungumze nao. Huwezi kumchukua mtoto wa miaka 15,12 au 13 kavaa sare zake za shule na begi yake anatoka shule likizo, simu haruhusiwi kwenda nayo shule, mzee wake kamtumia pesa kupanda boti ya Sh.20,000/=... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tauhida, muda wako umemalizika ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Ally Keissy dakika tano...

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Waheshimiwa, Mheshimiwa Amina Mollel dakika tano.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika Wizara hii. Naomba niende moja kwa moja katika mazingira, niwapongeze pia Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo katika msimu wa mvua na katika msimu huu wa mvua tumeshuhudia ni kwa jinsi gani baadhi ya wenzetu walivyoathirika, tunawapa pole. Hata hivyo, haya yote ni kutokana na baadhi ya wenzetu ambao utendaji wao wa kazi uliwezesha kutoa vibali ambavyo havikustahili kutolewa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tukienda katika Bonde la Msimbazi kuna baadhi ya wananchi ambao leo hii ukienda wana vibali vinavyowaruhusu kuwepo maeneo hayo. Kama hawa watu wasingetoa vibali hivyo ni dhahiri kabisa mafuriko haya yasingewakumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mazingira yetu tunaharibu sisi wananchi wenyewe. Twende katika mito yetu ambayo kwa namna moja au nyingine tumekuwa tukimwaga taka ngumu lakini sio hiyo tu hata katika mitaro tumeona kuziba kwake ni kutokana na uharibifu wa mazingira unaofanywa na baadhi ya wananchi wenzetu wenyewe. Kwa hapa niwaombe wenzangu wananchi wa kawaida tujue umuhimu wa kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaona mafuriko na kama tunavyofahamu katika mafuriko maji mingine yanatoka katika vyoo na takataka mbalimbali zimechanganyika. Baada ya mafuriko kunakuwepo na tahadhari ya ugonjwa wa kipindupindu. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa jukumu hili sio la Serikali peke yake, hata sisi wananchi tunapaswa kuhakikisha kwamba tunashuhudia na kuyalinda mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania sera iliyopo sasa ni kuhakikisha kwamba ujenjaji wa viwanda, nakubaliana kabisa na naunga mkono, lakini katika viwanda hivyo tuangalie kwamba ni kwa jinsi gani tunahitaji viwanda lakini viwanda ambavyo vitalinda mazingira yetu. Tunafahamu Mataifa makubwa kama Marekani na China ambayo yalikataa kusaini Mkataba wa Kyoto kutokana na uhitaji wa viwanda vikubwa vilivyopo kwao, lakini pia ndio chanzo cha uharibifu wa mazingira. Kwa hiyo na sisi wakati huu tunapoanzisha ujenzi wa viwanda, tuhakikishe kwamba viwanda sio chanzo cha uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa *air pollution* ni tatizo kubwa na sio Tanzania tu, maeneo mengi. Kwa hiyo, katika viwanda naiomba Wizara inayohusika kuhakikisha kwamba viwanda hivi vinakuwa sio chanzo cha uharibifu wa mazingira bali vinakuwa ni chanzo cha utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona tatizo kubwa la ukataji wa miti ni kutokana na uhitaji mkubwa wa mkaa. Hivi sasa Tanzania Mwenyezi Mungu ametujalia tuna gesi, basi tuone ule uharaka wa kuhakikisha kwamba hii gesi inakuwa ni chanzo cha utunzaji wa miti yetu, miti yetu isikatwe na kusiwepo na uharibifu wa mazingira kwa sababu wananchi wengi watakwenda katika utumiaji wa gesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili waende katika utumiaji wa gesi tunahitaji gesi kwa gharama nafuu, kwa maana hiyo tutaweza kulinda mazingira yetu, watu na hasa kwa sababu mkaa usipohitajika kwa kiasi kikubwa mjini, ni dhahiri kabisa wale waliopo kule Vijijini hawatoharibu miti yetu, hawatokata miti kwa ajili ya uchomaji wa mkaa. Kwa hiyo, ni uharaka unahitajika kwa hivi sasa kuhakikisha kwamba mazingira, gesi inakuwa ni chanzo cha kuhifadhi misitu, ni chanzo cha utunzaji wa misitu ili wananchi wasiweze kuharibu kwa kiasi kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi pia ya maeneo yamekuwa na uharibifu mkubwa na hasa tunavyofahamu

wananchi wenyewe ndio chanzo kikubwa. Itumike elimu na kuhakikisha kwamba kwa mfano wanaochimba mchanga maeneo mengi wanakuwa ni chanzo cha uharibifu. Yale maeneo kama tulivyoona Makamu wa Rais alichokianzisha hapa Dodoma, basi elimu hiyo ya upandaji wa miti iendelee katika maeneo mengi kwenye mikoa mingine ili kulinda mazingira yetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Juma Kombo dakika tano.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia hizi dakika tano niseme machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu tulikuwa tunazungumzia juu ya suala la Muungano na hizi zinazoitwa kero za Muungano, lakini sasa ni dhahiri kwamba imenoga. Imenoga kwa sababu pande zote hususan za Wabunge kutoka Zanzibar sasa wameungana na wamekutana kwenye *angle* moja ya kusemea namna kero hizi za Muungano zinavyoathiri maendeleo na uchumi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Zanzibar ni uchumi wa visiwa, uchumi wa visiwa siku zote unategemea zaidi biashara, biashara za fedha, benki na biashara nyingine. Leo biashara hizi zote kwa kutumia kivuli cha Muungano zimekufa na uchumi wa Zanzibar tayari ni kusema kwamba tayari ni sawa na kusema umekufa kwa sababu umesimama na biashara Zanzibar haziendi kwa sababu ya mfumo mbovu wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisikitike sana, leo wafanyabiashara kutoka Tanzania Bara wameona bora kwenda kuchukua bidhaa Mombasa, Uganda na Kongo kuliko kusafiri kwenda Zanzibar kuchukua bidhaa kama ilivyokuwa zamani kwa sababu tu ya mifumo mibovu ya kodi, kuna nini hapa? Ni kutokana na ukiritimba na mfumo mbovu wa kodi na mfumo mzima wa mzunguko wa biashara hasa katika Tanzania yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala la pili, Zanzibar ilikuwa na *system* ya kusajili meli, miezi miwili mitatu nyuma mfumo huu wa usajili meli umezuiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nikwambie Zanzibar kwa mwezi ilikuwa inakusanya jumla ya dola 79, jumla ya shilingi milioni 333 kwa mwezi. Nikwambie sasa ninavyozungumza Zanzibar mpaka inazuiwa ilikuwa imesajili meli 457. Leo kwa sababu Zanzibar imezuiwa na vikwazo vile vimewekwa leo zimebakia meli 350 tu, watu mmoja mmoja waliosajili meli zao wanaondoka kwa sababu ya vikwazo ambavyo vimewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme usajili wa meli, Zanzibar toka miaka kumi iliyopita, Zanzibar zimekamatwa meli mbili kwa hizo sababu zilizotajwa kwamba ni sababu ya unga, lakini kuna nchi mwezi mmoja zinakamatwa meli zisizopungua 27, Zanzibar miaka 10 zimekamatwa meli mbili? hivi kuna sababu ipi kwamba Zanzibar zimekamatwa meli ipi na iwekewe vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizopo sasa ni wazi na ni dhahiri kwamba Zanzibar inanyang'anywa usajili wa meli na usajili wa meli sasa unawekwa kwa jina la Tanzania. Huu ni uonevu na ni uonevu ambao haukubaliki, Muungano huu ambao tunauhufiri kila dakika na kila wakati kwa kweli umekuwa ni tatizo kwa uchumi wa Zanzibar na kwa kweli umekuwa ni kilio kikubwa kwa uchumi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukisikitikia mifumo hii ya kodi ambayo tumekuwa tukizungumza, kila Mzanzibar anaenyanyuka analilia mfumo wa kodi. Mimi

binafsi nimewahi kumfuata Waziri wa Fedha tukazungumza kirafiki kabisa, nimemfuata Naibu Waziri wa Fedha nikamfuata nikazungumza naye, lakini kwa masikitiko majibu ninayoyapata ni ya aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafika Waziri wa Fedha au Naibu wake anakujibu na anakwambia hasa kwamba wewe nia yako Bandari ya Tanzania Bara ife, sasa ndio maana nikamuuliza tu ina maana wewe umeridhika baada ya kuua Bandari ya Zanzibar, kwa sababu Bandari ya Zanzibar ni kama vile imekufa, biashara hakuna lakini yeye ameridhika kwamba Bandari ya Zanzibar ife, lakini amefurahi kuinyanyua Bandari ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii haikubaliki, lazima tuwe na mkakati na msimamo imara wa kuhakikisha kwamba bandari zote mbili zinatumiwa na tunaziimarisha kwa maslahi ya uchumi wa pande zote mbili, Tanzania Bara na Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na Waziri wa Fedha au Waziri wa aina yoyote ambaye ana-*favor* upande mmoja na kuukandamiza upande mwingine, hii haikubaliki na haitokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi kama kuna watu ambao watawunja Muungano ni watu wanaowadanganya wananchi kwamba tunatatua kero za Muungano, lakini tukitizama kero za Muungano kila uchwao zinazidi, uchumi wa upande mmoja kila uchwao unanyanyuka na uchumi wa upande mwingine kila uchwao unakufa. Sababu hii kizazi kinachokuja hakitokubali na nina kuhakikishia Muungano huu utaenda kuvunjika bila ridhaa na mitazamo ya watu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Hamad tunaendelea na Mheshimiwa Ali King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Kwanza nashukuru...



**MWENYEKITI:** Sahamani Mheshimiwa King, kabla hujaendelea naomba tafadhali. Naomba niwataarifu kwamba kuna wageni wa Mheshimiwa Spika katika *gallery* ya Spika ambao ni Balozi wa Mauritius nchini Tanzania, Mheshimiwa Jean Jhumun mwenye makazi yake Maputo Msumbiji akiambatana na Mbunge Mstaafu Kapt. John Chiligati, karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ali King tuendelee.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, kwanza nashukuru Mungu kwa kutujalia uhai na pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii lakini niwashukuru na kuwapongeza Wizara ya Makamu wa Rais inayoshughulikia mambo ya Muungano kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nathamini juhudi zao kubwa ambazo wanazozifanya katika kuzitatua changamoto, siwezi kusema kero ni changamoto na kitu chochote kinachohitajika kuendelea ni lazima kitakuwa kina changamoto zake, sasa nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri January Makamba kwa hotuba yake nzuri na kwa ziara ambayo aliifanya kule Zanzibar. Sasa Mheshimiwa katika ziara yake alipokwenda kule Zanzibar alilalamikiwa na wafanyabiashara. Namshukuru kwa kukutana na wafanyabishara wale ambao walilalamikia *double VAT* ambayo wanapata, ile *VAT* wakati wananunua bidhaa zao Tanzania Bara na pia wanapofika Zanzibar wanapata tatizo lile lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo hilo lilizungumzwa mbele ya Rais wetu Mtukufu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wafanyabiashara kutoka Zanzibar walimlalamikia lakini tukisema kodi tunazungumza kodi gani? Kodi hii iko sehemu gani? Kwa hiyo, kodi hiyo, naitaja, *Finance Act* ya mwaka 2016 kifungu cha 94 ya mwaka 2016 iliweka kifungu kipya katika *VAT* cha 55A ambacho kinasema:

*“A supply of locally manufactured goods by a local manufacturer shall be zero rated if the goods are supplied to a taxable person registered under the Value Added Tax Law administered in Zanzibar and such goods are removed from Mainland Tanzania without being affectively used or enjoyed in Mmainland Tanzania”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndipo pallipoleta tatizo la hiyo kodi ambayo ilikuwa ikizungumzwa na nashukuru Mheshimiwa Waziri kifungu hiki alipoenda kuwauliza mwenyewe wafanyabiashara na kwa bahati aliweka vikao tofauti jinsi ya kuvishughulikia. Sasa tamaa au matumaini yetu kwamba Serikali itakapokuja kwenye *Finance Act* ina maana kwamba jambo hili ni lazima lishughulikiwe, vinginevyo sisi ni watunga sheria, kama hatujalisema wazi hapa tutaliacha na litakuwa linaendelea kututafuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kitu ambacho kinapatikana kutokana na kifungu hiki, kwamba mtu akinunua bidhaa zake kutoka Tanzania Bara akipeleka Visiwani ikiwa yule mtu hajawa-*registered by ZRB* ina maana kwamba atachajiwa hapa asilimia 18, akifika Zanzibar atachajiwa na *ZRB* asilimia 18, kwa maana hiyo atalipa asilimia 36. Kwa hiyo, kwa mfanyabiashara mwenye mfuko mdogo hapa msingi wake unakufa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasara nyingine tunayopata ni kwamba watu wako tayari kwenda kununua bidhaa zile Kenya na wakati sisi tumo ndani ya Tanzania hii moja, mtu mmoja analipa asilimia 36 mwingine analipa asilimia 18 ya *VAT* kutokana na kifungu hiki. Sababu ya kifungu hiki kwamba ametajwa mtu lazima awe ame-*register* na *ZRB* kama ni *taxable person*. Sasa kwa *taxable person* wengine sio *taxable person*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano zipo *NGO* au mashirika mengine ya kijamii, yanahitaji kujenga shule, kununua saruji, mabati na vitu vingine. Wakija kununua hapa wanaanza kuchajiwa huku mwanzo asilimia 18 na akifika Zanzibar anachajiwa tena asilimia 18. Nashukuru Mheshimiwa

Waziri kwa taarifa ambazo zipo kwamba kikao kimefanyika, lakini tunataka utekelezaji wake na utekelezaji wake tunaomba Mheshimiwa Waziri alete hapa sheria tuje tubadilisha ili hii kero/changamoto iondoke. Bila kuondoka changamoto hii ina maana kwamba hatutoweza kufikia mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Serikali mwanzo ilipoona kuna hili tatizo wakasema wabadilisha sheria. Walibadilisha sheria hii naamini kwa nia nzuri tu, lakini utekelezaji wake baada ya kuingizwa haya mambo mawili kwamba lazima iwe *manufacturer* na lazima awe *taxable person* ndipo penye tatizo. Kwa hiyo, hili tatizo litakapoondoshwa, *whether* tukarudi kulekule mwanzo tukatumia *origin principal* kwa sababu hapa imepelekwa katika *destination principal* na ukipeleka kwenye *destination principal* bila ya kuwa na *refund scheme* ina maana hicho kitu si rahisi kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nakuomba ulete sheria hiyo hapa tuje tufanye marekebisho katika *Finance Act*. Bila ya hivyo utekelezaji wa hili tunalosema humu tutakuwa tunapiga kelele na sheria yenyewe ni hiki kifungu 55A kilichoongezwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, napenda kuzungumzia biashara, tumesema Tanzania ya viwanda, hatujasema Zanzibar ya viwanda wala hatukusema Tanzania Bara ya viwanda, tulisema Tanzania ya viwanda. Sasa ninachokiomba katika hili, ikiwa tunasema Tanzania ya viwanda ina maana kwamba hii *movement of goods* kama mtu akiweka kiwanda chake Zanzibar ina maana kwamba hatopata soko la Bara na ikiwa hatopata soko la Bara ina maana *investment* itakuwa haiwezi kufanyika Zanzibar kwa sababu bidhaa zake mtu hawezi kuingia kwenye soko la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachoomba, kwa kuwa soko ni kubwa na mtu anapofanya biashara anatazama *location* yake kwa mujibu wa soko lilivyo

anapima Tanzania, Zanzibar ikiwa *location* kuna tatizo gani huyu mtu kumpatia ufumbuzi, kuna matatizo gani kuweka soko hili *free*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nijulikane wazi sipiganii suala la askari, katika suala la askari niko pamoja na msimamo wa Serikali, lakini bidhaa nyingine, tukisema kwamba kila kinachozalishwa Zanzibar hakiingii Tanzania Bara ina maana kwamba tuna-*discourage investment* Zanzibar. Hakuna *investor* atakayekubali kwenda kuwekeza kule ikiwa msimamo kila kinachotoka kule kitakuwa hakifai kuingia huku, mtu anatazama soko kubwa na sisi tuko katika Afrika Mashariki, tunapima soko la *SADC*, tunatazama na soko la Tanzania. Sasa tukianza kujikataa wenyewe nani atatukubali? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kingine, endapo nitazungumza nje ya miko ya taasisi inayoniongoza kisiasa nitaitwa Msungu na kama atatokezea mtu kwamba hana miko katika kuzungumza na taasisi inayomwongoza jambo la ndani akalitoa nje au jambo la kusema ndani yeye akalifanya nje, mtu yule kisiasa anaitwa msungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili jambo la usungo linafanyika humu. Inakuwaje mtu jambo kama hili inakuwa mtu unalifanya, kitu ambacho kwamba kinajulikana faida za Muungano au chama fulani ndiyo kina msimamo wa Muungano huu, lakini anatokezea mtu pengine umri mkubwa tu akaja akafanya mambo akacheza shere Muungano. Kwa maana hiyo huyo mtu yeye sasa ndio anabakia anakuwa ndio kero ya Muungano, Muungano hauna kero kama alivyo kero huyo mtu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, nina wasiwasi huenda ikawa kuna minazi ya mpakani humu *la sharikia wala gharibia*, maana huo mnazi hauko mashariki, hauko magharibi, hatuujui mnazi wa wapi. Kwa hiyo aseme mtu waziwazi, lakini asifanye usungo wa kisiasa katika Bunge lako hili tukufu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa King, tunamalizia na msemaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Jaku Hashim.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru, ntakuwa mchoyo wa fadhila kama sikukushukuru kwa kupata nafasi hii. Niyakumbuke maneno ya Mheshimiwa Rais Mstaafu, Mheshimiwa Salmin Amour Juma, almaarufu Komando, alikuwa na maneno mawili akisema urafiki na nchi, kwanza nchi urafiki baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijamtendea haki Mheshimiwa January Makamba, Waziri wa Wizara hii jinsi anavyojituma bila kujali mvua, jua, usiku au mchana, anapoitwa Zanzibar wakati wote anatii amri; nimpongeze sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu cha kupendeza sana Wizara hii, hasa Naibu, angetoka angalau Zanzibar, ingeleta sura nzuri sana ya Muungano, ndiyo Wizara ya Muungano, ingeleta sura ya Muungano. Hata hivyo, siwezi kuingilia mamlaka ya Mheshimiwa Rais, nataka kujua nini Muungano, nini *definition* ya Muungano; *what is union?* Umuhimu wa kuungana watu, kuwa pamoja, kushirikiana katika nyanja mbalimbali kiuchumi, ulinzi, ajira, huu ndiyo Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini Muungano, *definition* yake ni hii; umuhimu wa kuungana watu kushirikiana, kuwa pamoja kiuchumi, nchi, ulinzi, ajira. Hata Tume ya Mheshimiwa Jaji Warioba ilisisitiza sana umuhimu wa Muungano huu kuwepo, katika watu 1,000 labda watu wawili watakataa Muungano huu kuwepo. Lakini kuna mambo muhimu au fomula gani ya kuendesha Muungano wetu huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mheshimiwa Jaji Warioba haikukataa Muungano huu kuwepo, katika watu

1,000 labda watu wawili watakataa Muungano huu. Kwa hiyo Muungano huu tunauhitaji na ukizingatia keshokutwa, Mheshimiwa Machano amezungumza, tunatimiza miaka 54 ya Muungano wetu huu. Hata hivyo, kuna baadhi ya watu mnawalea vibaya, wanachafua Muungano huu bila kuwaonya. Tatizo tutafute *formula* ya kuendesha Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda, nije kwenye changamoto za Muungano, akiwemo Mheshimiwa Keissy. Ya nini kusema... (*Kicheko*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Moja moja, mbili mbili, tatu tatu...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpe taarifa yake, wacha niipokee.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, ngoja nimpe taarifa yule.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, naomba ukae kidogo.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Asiniletee ujinga mimi hapa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Keissy, pilipili usiyoila inakuwashia nini wewe? Usirukie gari ambalo hujui mwendo wake Mheshimiwa Keissy, itakutoa meno. Umekuwa ukidhalilisha watu, wewe mambo ya Muungano hayakuhusu Mheshimiwa Keissy, tetea mambo

ya Nkasi. Kama maji hayatoki, ndiyo utetee humu Bungeni...  
(*Makofi*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Umetaja jina langu, kwa nini utaje jina langu wewe?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Ndio unayechafua humu ndani, kwani wewe nani, wewe si Mbunge? Wazanzibari ni wasikivu. Kitu cha mwanzo wazee wangu walinifundisha malezi, adabu, kumheshimu mkubwa na mdogo, mimi namheshimu sana huyu, sana, lakini pia kafuturu adah, kavuka mipaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtu mmoja yeye yote, huu Muungano tunauhitaji. Mimi ni jamaa yangu, ni mwenzangu, ndugu yangu, jirani yangu, lakini hakuna kitu kizuri kama kuwa na malezi, asiyefunzwa na mzazi wake hufunzwa na ulimwengu. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Anataka *ambulance* huyo.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumestahimili, tumevumilia vya kutosha. Mambo ya Muungano yanamhusu nini?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Kwa nini anitukane?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa; kwa nini Mheshimiwa anitukane?

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku, kaa chini. Mheshimiwa Keissy, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini.

## T A A R I F A

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelelewa kuliko yeye alivyolelewa, mimi nina adabu kuliko alivyokuwa na adabu yeye, lakini mambo ya Muungano yana sheria zake, hatuwezi Serikali mlete vitu bila ushuru mtunyonye sisi tubaki kama makapi, hiyo haiwezekani.

**WABUNGE FULANI:** Buuuu!

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Keissy. Mheshimiwa Jaku, malizia.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, narudia yaleyale, ni mzee wangu, adabu kitu cha bure, nitaendelea kumheshimu hata tukatoka nje. Mimi ni jirani yangu, nikianguka leo ataniokota yeye na akianguka leo nitamuokota mimi, sisi sote Waislamu, sisi ndugu moja lakini ukweli utabaki ukweli; moja moja mbili mbili, kavu kavu mbichi mbichi, mimi naendelea kukuheshimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye changamoto mwaka jana Mheshimiwa January alizungumza zimebaki changamoto tatu, nimpongeze. Hata hivyo, changamoto hizo mpaka leo nafikiri zipo *ICU*, hazijapata ufumbuzi, wanakaa vikao lakini zinafika mahali zinapata kigugumizi. Angalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ukurasa wa sita Sura ya Saba, vifungu 133 na 134, huu ndiyo mzizi wa fitna yetu ya Muungano, ni *Joint Finance Commission*, ukamaliza huu Muungano umekwisha, Mungu atuweke hai. *Joint Finance Commission*, Jamhuri ya Muungano Katiba 1977, nafikiri ukurasa wa sita, kifungu 133 na 134, huu ndiyo mzizi wa fitna uliobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamezungumza humu katika mahali palipokuwa nidhamu yake siwezi kusema nzuri bandarini. Watu wamekuwa wanapata mpaka maradhi. Waziri wa Fedha hayupo hapa, Naibu Waziri ampelekee salamu Mheshimiwa Waziri. Huu Muungano tumeungana kwa nia njema, isiwe kama Lugha ya Kiarabu



ukiandika unavutia kwako tu, maandishi ya Kiarabu ukiandika unavutia kwako tu. Naibu Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha hayupo hapa, lakini mahali wanapoteseka watu, Mheshimiwa Tauhida kazungumza, mtu kavunja TV kwa uchungu, ule ni uchungu, tunaumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara Rais wetu tumemuona shahidi anawatetea wanyonge, anasimamisha misafara njiani kuwasikiliza wananchi, Wamachinga kaachia huru wafanye biashara. Leo mtu katoka Zanzibar, Zanzibar uchumi wake ukiacha karafuu ni biashara, tuwe wakweli. Imefika mahali kero hizi hazijafika mahali, *double standard*, VAT imekuwa kupita kiasi, tutaendelea kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuna msemu usemao asemaye hachoki...

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa

## T A A R I F A

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nimpe taarifa mzungumzaji ambaye anazungumza hapa kwa sasa, sifa ya Muungano wa Baba wa Taifa pamoja na Mzee Abeid Aman Karume. Jambo la kwanza walilokuwa wakilionia ni suala la kufanya biashara, wananchi wa Zanzibar waweze kupata soko Tanzania Bara, ni jambo la umuhimu sana hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri na mzungumzaji ambaye anazungumza alione hili, katika mambo yote katika hili suala la kufanya biashara Wazanzibari wanahitaji lazima wapate soko Tanzania Bara. Vinginevyo hatuwezi kufanya biashara ndani ya Zanzibar tu bila kufanya biashara *Mainland*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku, taarifa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa aliyonipa nimeipokea kwa mikono miwili. Taarifa nzuri, taarifa ambayo inaleta sura ya Muungano wetu; nimshukuru sana Mheshimiwa Mattar kwa umakini wa hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukizingatia kuna mambo matatu ya uchumi haya yako Tanzania Bara, sera za kodi ziko Tanzania Bara, sera ya sarafu iko Tanzania Bara. Hebu tufike mahali haya madogomadogo wenzetu mtuachie au tubadilishane, miaka mitano mchukue ninyi, miaka miwili tupeni sisi. Sera hizi muhimu, nyenzo hizi muhimu mnazo ninyi, Sarafu ya Tanzania, Benki Kuu, kodi hizi, mna mbuga nyingi za kuendesha, mna madini mengi. Zanzibar uchumi wake ni biashara, mambo madogo madogo haya ifike mahali... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, michango yetu kwa upande wa Wabunge imemalizika, sasa tunaingia kwa Waheshimiwa Mawaziri; tunaanza na Mheshimiwa Subira Mgalu, dakika tano na baadaye Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ajiandae dakika tano.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nianze kusema naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge wakati wanachangia hoja hii, lilijitokeza suala la utekelezaji wa Mradi wa *Rufiji Hydro Power* maarufu kama *Stiegler's Gorge*. Michango ile ilielezea wasiwasi wao kuhusu utekelezaji wa mradi huu na masuala ya mazingira. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kuwa utekelezaji ni kweli Serikali ya Awamu ya Tano itatekeleza Mradi huu wa *Rufiji Hydro Power* ambao utazalisha Megawati 2,100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hata historia mbalimbali za mradi huu tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza mpaka ya Nne na mpaka hii ya Tano, tathmini mbalimbali juu ya mazingira zilifanyika. Katika taarifa zile za tathmini hakuna mahali popote ambapo ilionekana mradi huu usitekelezwe kwa sababu ya mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nilithibitishie Bunge lako tukufu kuwa mradi huu Serikali zote zilizopita zimefanya tathmini lakini Serikali hii ya Awamu ya Tano imeamua kuutekeleza kupitia mapato ya ndani kutokana na uhitaji mkubwa wa nishati ili kutekeleza uchumi wa viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, Serikali imejielekeza kuzalisha Megawati 5,000 ifikapo mwaka 2020. Ni kweli mpango huu kabambe wa *Power System Masterplan* umeelekeza miradi midogomidogo ya kuzalisha umeme kwa kutumia maji, lakini mradi huu na ukilinganisha na gharama ya kuzalisha umeme kwa *unit* moja kwa kilowati kwa kutumia maji ni Sh.36/=, kwa kutumia gesi ni Sh.147/=, kwa kutumia mafuta ni Sh.346/=, ni wazi utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia maji ni nafuu. Vile vile kwa kuwa lengo la Serikali ni kupata nishati ya umeme yenye unafuu na Watanzania waweze kuitumia majumbani, viwandani, kwa hiyo, lazima tutekeleze huu mradi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ambayo imetajwa kwa huu mradi kabambe wa kuzalisha umeme

kwa mfano Rumakali, Luhuji, Mpanga, Songwe, Rusumo, Malagarasi, Kakono, ni kweli ipo, lakini hii itatekelezwa baina ya ubia binafsi na wadau mbalimbali. Kwa hiyo, nataka nilitaarifu Bunge lako kwamba kwa kweli naomba watuunge mkono, mahitaji ya umeme ni mengi na Serikali imethubutu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa uthubutu wake na mradi huu unatekelezeka bila tatizo lolote. Hata sasa wataalam wa chuo kikuu wameshamaliza *Environmental na Social Impact Assessment* na wataiwasilisha Wizarani na *NEMC* baada ya wiki moja. Kwa hiyo, naomba tu Bunge lako Tukufu lituunge mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, lilijitokeza suala la upatikanaji wa nishati au deni la umeme kwa Shirika la *ZECO* Zanzibar. Naomba niwaarifu wenzetu upande wa Zanzibar kwamba Serikali inaendelea na mazungumzo na tumeipa kazi *EWURA* ifanye *study* ya gharama mbalimbali za kuzalisha umeme ili tufikie muafaka. Naamini Kamati yetu ya Nishati na Madini ilitu-*task* hiyo kazi na tunaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu Zanzibar kupitia *ZECO* wanalipa lile deni kiwango ambacho tunakubaliana, lakini lile deni ambalo hatujafikia muafaka mazungumzo yanaendelea na baada ya miezi miwili utafikiwa muafaka na hili deni litakaa vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wazara hii kwa kazi nzuri. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Subira. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na baadaye Mheshimiwa Kangi Lugola ajiandae.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nami naomba nichangie kwenye jambo hilo hilo la kuzalisha umeme kwenye Mto Rufiji na nitachangia zaidi katika muktadha wa uhifadhi na ikizingatiwa kwamba mradi huu unatekelezwa kwenye eneo la Hifadhi ya Pori la Akiba la Selous ambalo lipo chini ya Usimamizi wa Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu na uthamani wa kipekee ambao unawekwa kwenye Pori la Akiba la Selous, lakini naomba Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kwa ujumla watambue kwamba Selous ni rasilimali ya Taifa na rasilimali zina sifa moja ili ziwe rasilimali; zinapaswa kuleta manufaa kwa wananchi, zinapaswa kuleta manufaa kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba tutambue kwamba rasilimali ambazo tumejaliwa kama urithi katika nchi yetu haziwezi kututenganisha na mahitaji ambayo sisi tunahitaji kuyapata kutokana na rasilimali ambazo tumepewa kama zawadi. Kwa hiyo, ni lazima tuwianishe uwepo wa rasilimali na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *schools of thought* mbalimbali, kuna watu wanaoamini kwamba rasilimali zihifadhiwe kama zilivyo mpaka mwisho wa dunia, lakini wanasahau kwamba na sisi binadamu ni sehemu ya dunia, ni sehemu ya ikolojia na tuna mahitaji yetu na kwa maana hiyo ni lazima na sisi tutumie rasilimali hizi. Kitu cha msingi cha kuzingatia ni kuhakikisha kwamba tunatumia rasilimali kwa uendeleu wake bila kuziharibu, bila kuathiri bionuwai nyingine iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihakikishie Bunge lako Tukufu hapa kwamba Serikali kupitia Wizara yetu imezingatia matakwa ya uhifadhi endelevu wa rasilimali iliyopo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Pori la Akiba la Selous. Tumefanya hivyo kwanza kwa kuhakikisha mradi unatekelezwa kwa kufuata misingi ya utekelezaji wa miradi. Ndiyo hiyo *Environmental and Social Impact Assessment* anayoizungumzia Mheshimiwa

Naibu Waziri wa Nishati. Hilo ni hitaji la kwanza la lazima na tumesema itafanyika kwa haraka na ikamilike kabla utekelezaji wa mradi haujaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, Waziri wa Maliasili na Utalii nimeunda kikosi kazi cha Wataalam kutoka Taasisi za *TAFIRI TAWIRI*, *TITISA* na Taasisi nyingine zinazohusika na maliasili ili wafanye utafiti wa kina wa kuangalia bionuwai iliyopo katika eneo husika. Utafiti huu utatuwezesha kujua kuna *species* gani zipo katika eneo la utekelezaji wa mradi na tufanye nini tuweze kuzihifadhi zisipotee na nini kitatokea kama tutafanya mradi huu kwa zile *species* zilizopo pale. Je, *species* zilizoko pale ni *endemic* kwa maana pale ni makazi yao ya kudumu ama ni *species* hizi ambazo *exotic* ambazo zimekuja kuhamia kwa kufuata mahitaji mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuzitambua hizo *species* na mahitaji yake na kujua kama *endemic* ama ni *exotic* tutaweza kujua tufanye nini ili kuokoa zisipotee na ndiyo kazi ambayo sisi Wizara yetu tunafanya kuhifadhi bionuwai mbalimbali za wanyama pamoja na mimea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo kuna timu ya Wataalam iko *site*, inakusanya mbegu za wanyama, samaki na mimea na kila aina ya bioanuwai iliyoko pale na kuzitunza kwa ajili ya matumizi ya baadaye. Pia tumehakikisha kwenye *design* ya mradi kutabaki na *Oxbow Lakes*, maziwa ya asili yaliyoko pale, lakini pia tunaongeza maziwa mengine ambayo yatasaidia kuweka uhai wa viumbe hai ambavyo viko katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali iko macho na sisi wahifadhi tuko macho hatutokubali Pori la Akiba la Selou lishuke hadhi yake kwa sababu ya utekelezaji wa mradi huu. Madhara yanaweza yakajitokeza, lakini mpaka sasa hakuna anayejua ni nini kitatoke kwa sababu hakijatokea. Kwa hivyo, nyingi zinazozungumzwa hapa kwa mfano

mchango wa Dkt. Sware ni nadharia tu, ni *theory's* tu ni *rhetoric* hakuna ushahidi wa nini kitatokea kwa hakijatokea na uharibifu haujafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tunachokifanya kwa sasa ni kujipanga kupunguza madhara yanayoweza kutokea endapo mradi utatekelezwa ndicho tunachojipanga. Kuna nadharia kwamba joto litaongezeka kwa sababu ya utekelezaji wa mradi, kuna nadharia kwamba *flow* ya mto itabadilika kutokana na utekelezaji wa mradi. Zote ni nadharia, huwezi kuwa na uhakika kwamba zitaathiri mto pamoja na wanyamapori kwa namna gani, sambamba na hilo. (*Makofi*)

## T A A R I F A

**MHE. DKT. IMMACULATA S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuwa *quoted* vibaya...

**MWENYEKITI:** taarifa.

**MHE. DKT. IMMACULATA S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mhehsimiwa mzungumzaji anachokisema kwamba ni nadharia, siyo nadharia ni vitendo. Nimetoa mifano kwamba binadamu mfano tu mdogo binadamu unahitaji hewa *oxygen* ukiikosa *oxygen* unakufa. Sasa nikisema binadamu unahitaji *oxygen*, ukikosa unakufa hiyo siyo ni nadharia, *you don't need* kusema nina *suffocate myself to prove* kwamba nitakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna mimea ambayo inahitaji maji ya Mto Rufiji nimekutolea mfano wa mikoko, sasa ukipunguza yale maji ile mikoko inaenda kufa. Unaenda ku-*block* unatengeneza *dam* una- *reduce segments* ambazo zinaenda kwenye eneo la Pwani na *nutrients* ambazo mazingira yale yanahitaji. Sasa unahitaji...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Sware. Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake siipokei na sipokei kwa sababu za kisayansi kama yeye ni Dkt na mimi ni Dkt. vilevile na mimi ni mwanasayansi, nampa sababu ya kisayansi kama yeye ni daktari anaamini kwenye sayansi,, tusikilizane kama yeye ni daktari na anaamini kwenye sayansi nampa sababu ya kisayansi, hakuna haja ya kubishana kwa kelele, tulieni msikie sayansi. Anachokisema kinaweza kikatoka ndiyo ninachosema kwamba ni nadharia, ni *theory* hakijatokea bado kwa sababu mradi haujatekelezwa, ninchokisema...

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako umemalizika.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kuna kitu kitakachojitokeza ni kwamba wanyama, mimea wana kitu kinaitwa *adaptation*, kwenye mabadiliko yanayojitokeza.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Kwa hivyo mazingira yatakapobadilika wale wanyama wanabadilisha tabia zao wanaweza waka-*adapt* kwenye mazingira mapya yaliyojitokeza. Kwa hiyo,hiyo ni sababu ya kisayansi na nina uhakika anaifahamu. Kwa hivyo hatuna haja ya kubishana sana kwa sababu hii ni sayansi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Kangi Lugola, dakika 20.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,



nakushukuru kunipa nafasi niweze kuchangia na kutoa baadhi ya ufafanuzi kwenye hoja ambazo Kamati zote mbili pamoja na Wabunge wameweza kuziwasilisha. Kwanza kabisa nianze kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Kigwangalla Dkt. na Mheshimiwa Sware Dkt. wanatunishiana misuli ya kiudokta kwenye suala la *Stiegler's Gorge*, sasa nikasema mimi ambaye ni Naibu Waziri wa mambo haya ya mazingira nikiingia hapo nafikiri tutaelewana vizuri. Hata hivyo, namshukuru Dkt. Kigwangalla amemaliza masuala yote ya *Stiegler's Gorge*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu mtoto wa baba January namshukuru kwa sababu tangu alivyonipokea kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais amekuwa msaada mkubwa sana na hivyo kunifanya niweze kukimbia haraka katika kumsaidia masuala haya ya mazingira katika nchi yetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa mtoto wa Mzee Makamba, nakushukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Katibu Mkuu wa Wizara yetu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Jemedali *Engineer* Joseph Malongo na Naibu Waziri Mwanasheria Butamo wamenisaidia sana katika kuhakikisha kwamba nafanya shughuli hizi za mazingira kwa raha mustarehe kwa sababu kila nilichokuwa nikiwaelekeza wamekuwa wakitekeleza ninachokihitaji wamekuwa wakifanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru wafanyakazi wote, Ofisi ya Makamu wa Rais namna ambavyo wamekuwa nami muda wote katika kunipa msaada na kuweza kupata uzoefu kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais. Vile vile nimshukuru sana Dkt. Makotha ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *NEMC* pamoja na timu yake wamekuwa wakifanya kazi nzuri kazi ambayo imetukuka, wamekuwa watu wa msaada sana katika kunifanya mimi

niweze kutekeleza majukumu yangu pasipo wasiwasi wala vikwazo vyovyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambazo zimeibuliwa na Kamati zipo nyingi, lakini wamejikita katika kutushauri. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu kuwaondolea wasiwasi Wajumbe wote chini ya Mwenyekiti Saddiq na Makamu wake Bashungwa kwamba yale yote ambayo wametushauri juu ya mazingira tutayafanyia kazi na nitagusia machache juu ya mazingira na nitagusia machache ambayo wameyasisitiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wako Wabunge wengi ambao wamechangia kwa maandishi kwenye masuala ya mazingira na pia wamechangia kwa kusema hapa Bungeni kwa sababu ya muda nitakwenda kugusia masuala machache ambayo yamewasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kufafanua hizi hoja, kwa nafasi ya pekee nimshukuru Mheshimiwa Rais ambaye aliniteuwa na hii ni bajeti yangu ya kwanza na Mheshimiwa Rais ameendelea kuniamini nami namuahidi kwamba sitamwangusha, nitaendelea kuifanya kazi hii katika kasi yake ya hapa kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia niendeleo kumtia moyo Mheshimiwa Rais kwamba baadhi ya Watanzania wenzetu na baadhi ya Wabunge wenzetu humu ndani wamekuwa wakimkebehi na kumkejeli kwamba Rais huyu amekuja na mambo ambayo sasa Taifa hili linaenda kuangamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya ni ya upotoshaji na siyo ya kweli. Kati ya Rais ambaye katika bara la Afrika na duniani kote ambaye amejibainisha kwamba sasa atakwenda kulinda kwa nguvu zote rasilimali za Watanzania ni Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Rais Dkt. John Pombe Magufuli ni miongoni mwa Marais ambao hawazaliwi mara kwa mara na hawapatikani kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anapokuwa anawaambia Watanzania kwamba katika shughuli zetu hizi tumtangulize Mungu mbele, wananchi wengi wanashindwa kuelewa maana yake ni nini. Maana yake ni kwamba Rais Dkt. Magufuli ni chaguo la Mungu na ndiyo maana anapotamka maneno hayo Mungu anamwambia kwamba hapo hapo uliposhikilia hapo usibadilishe gia endelea kulitetea Taifa la Watanzania na ndiyo maana.

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Taarifa

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kanuni zetu hazitutaki kujadili mambo ambayo hayako mbele yetu. Hapa hatumjadili Rais, Naibu Waziri arudi ajibu maswali ambayo Wabunge tumehoji maswali ya Muungano na Mazingira; kama anataka mjadala wa Rais uwekwe hapa mbele tumjadili Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Kangi Lugola.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gekul namheshimu sana, lakini napenda nimkumbushe kwamba hii kazi niyayofanya hapa nimeteuliwa na Rais na nafanya kazi ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama yeye hataki kusikia maneno ambayo nayasema juu ya aliyeniteua, basi avute subira pale ambapo vizazi vinavyokuja inawezekana na wenyewe wakawa Rais ambao watampatia majukumu ili aweze kuwazungumzia. Hata hivyo, nimhakikishie kwamba yeye na chama chake kuingia madarakani ni vigumu sana...*(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba utulivu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Na ni rahisi sana ngamia kupenya kwenye tundu la sitando. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa kujibu hoja za Wabunge najua wana kiu ya kusikiliza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi kwa kusema hapa na kuchangia kwa maandishi wamezungumzia kwa uchungu sana juu ya uchafuzi na uharibu mkubwa unaofanyika kwenye vyanzo vya maji. Vyanzo vya maji katika nchi yetu vina uhusiano mkubwa sana na maisha yetu na uhai wetu. Pia vyanzo hivi vya maji vina uhusiano mkubwa sana ndoto ya Mheshimiwa Rais ya Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuwa na viwanda lazima tuwe na umeme wa uhakika; ili tuwe na umeme wa uhakika lazima tulinde vyanzo vya maji kwa gharama zote na kwa nguvu zote. Ndiyo maana katika nchi yetu vyanzo vya maji ambavyo vinazalisha umeme kwa kutumia maji tuna Kihansi, Kidatu, Mtera, Maporomoko ya Pangani, Hale, Nyumba ya Mungu, Uwemba, Tulila, Mwenga, Darakuta pamoja na Iyovi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote hii wanazalisha kwa ujumla *megawatt* 560.6, kwa kuwa sasa tunakwenda kuwa na mradi mkubwa huu wa *Stiegler's Gorge* ambao utazalisha *megawatt* 2100. Maana yake ni nini kwenye vyanzo vya maji maana yake ni kwamba sisi Ofisi ya Makamu wa Rais tusiposaidiana na Watanzania katika kuhakikisha kwamba tunalinda vyanzo vya maji katika nchi nzima, uzalishaji wa umeme ambao unatumia maji hautaweza kufanikiwa kwa kiwango ambacho tunakihitaji. Ndiyo maana Ofisi ya Makamu wa Rais tunayo mikakati kuhakikisha kwamba tunalinda vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi walikuwa wanaulizia tuna mikakati gani? Tuna mikakati wa mwaka 2006 ambao unahusu uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji na ndiyo maana katika mikakati huu Ofisi ya Makamu

wa Rais iliwaandikia barua Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini kuhakikisha wanabaini vyanzo vyote vya maji pamoja na changamoto zake ili wawasilishe Ofisi ya Makamu wa Rais ili vyanzo vingine viwe *protected* viweze kuwekewa utaratibu wa kuvitangaza kwenye gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia Bunge lako Tukufu muda tuliowaongeza wa hadi tarehe 20 mwezi huu unakaribia kwisha na kama nilivyosema juzi kwenye Bunge hili. Wakurugenzi ambao watakaidi na kutotekeleza agizo hili hakika Ofisi ya Makamu wa Rais itaorodhesha majina yao na kumpelekea Mheshimiwa Rais ambaye ndiye amewateuwa ili aweze kutafakari na kuona vitumbua vyao ama vitiwe mchanga ama laa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna mkakati mwingine wa mwaka 2008, mkakati huu ni wa kuhifadhi mazingira katika hatua za haraka kwenye bahari na kwenye ukanda wa Pwani pamoja na mito, maziwa na mabwawa makubwa. Tuna mkakati mwingine wa 2012, huu ni wa kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, mikakati yote hii pamoja na wananchi kuwataka watekeleze sheria ya mazingira tuna uhakikika tunakwenda kulinda vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tuliweza kufanya mazoezi makubwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kunusuru bonde la Mto Ruaha Mkuu, *Task Force* ambayo Mheshimiwa Makamu wa Rais aliunda. Ndiyo maana maeneo yote ambayo yana mabonde, maeneo yote ambayo yana shughuli za binadamu lazima tutoe miongozo namna ya kufanya *agriculture* ambayo ni ya kihifadhi yaani *conservation agriculture*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumziwa sana ni jambo hili la upandaji wa miti na hasa Kamati pamoja na Wabunge kwamba tumekuwa na kawaida ya kupanda miti ikiwa ni pamoja na uzinduzi wenye sherehe, lakini siku ya siku miti hiyo tukiilhesabu haifiki idadi ile

ambayo inakuwa inapandwa; Kamati ilitaka kujua tuna mpango gani Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwenye ilani ya CCM ukurasa wa 212 hadi 213 halmashauri zote nchini wanatakiwa kupanda miti isiyopungua milioni moja na laki tano, lakini ni pamoja na kuweka sheria ndogo zitakazosimamia masuala hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kuanzia mwakani Ofisi ya Makamu wa Rais inaandaa utaratibu wa kufanya sensa kubwa itakayokwenda kujua miti ambayo imepandwa imekuwa mingapi na mingapi imekufa. Ili tuweze kutoa miongozo ambayo itatusaidia kuwa na Tanzania ya kijani na hiyo imeenda sambamba, Mheshimiwa Makamu wa Rais alipohamia Dodoma alianza na mradi mkubwa wa kujianikisha Dodoma na kwa utaratibu huo tunaendelea kujanikisha maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati mingine ni pamoja na siku ya mazingira duniani, tumekuwa tukihamasisha wananchi wapande miti ikiwa ni pamoja na kuomba shule, Taasisi za Dini pamoja Taasisi Zisizo za Kiserikali katika upandaji wa miti. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niwatoe wasiwasi kwamba nchi yetu itakwenda kuwa na mkakati huo kuhakikisha kwamba miti tunayoipanda tunaitunza na kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hili la UDART kwamba *NEMC* ilikuwa wapi; nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, mwaka 2009 *UDART* waliweza kupata cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira na walipewa masharti ambayo watakuwa wanayazingatia katika kuhakikisha kwamba wana-*mitigate* na kuepuka athari ambazo zingeweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo mara kwa mara tunawaambia mojawapo ya madhara ni mafuriko makubwa ndiyo maana katika eneo hilo mafuriko ambayo

hayakutarajiwa yamechangia kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kwamba UDART inakuwa kwenye mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shughuli za binadamu ambazo zinafanyika kando kando ya Mto Msimbazi na zenyewe zimechangia kwa kiasi kikubwa na ndiyo maana tuna mpango wa kupitia mito yote na miji yote kuhakikisha kwamba hawa ambao wako ndani ya mita 60 na wengine wamejenga mpaka kwenye kingo tuweze kuotoa mwongozo wa namna gani wanaweza wakaepusha mambo haya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine tutawapa kwa maandishi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa January Makamba aje ahitimishe hoja yake kwa muda wa dakika 30.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa uliyonipa ya kuhitimisha hoja hii. Nianze kwa shukrani kwa Kamati zote kwa maoni, ushauri, mapendekezo waliyoyatoa. Pia nawashukuru Waheshimia Wabunge wote waliochangia idadi yao ni 45; Wabunge 30 walichangia kwa maandishi na Wabunge 15 walichangia kwa mdomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi na niseme tu kama alivyosema Naibu Waziri kwamba kama hatutayafikia yote, basi kwa ujumla kabla ya mwisho wa Bunge hili la bajeti, tutawawekea kwenye *pigeon holes* zenu majibu ya maswali yote mliyouliza. Hata hivyo, nizungumze mambo ya jumla ambayo yamezungumzwa na kubwa ni lile la kwanza la masuala ya biashara, vikwazo vya biashara na kwamba imetolewa kauli hapa na baadhi ya Wabunge ambayo kwa kweli sisi kama Serikali ni lazima tuelezee vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli yenyewe ni kwamba, baadhi ya wachache ni kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano haina dhamira ya kuisaidia Zanzibar kiuchumi na kwamba inabana fursa za biashara na ukuaji wa uchumi wa Zanzibar sasa kauli kama hiyo haiwezi kubaki bila kutolewa maelezo na sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kwamba, kihistoria hata kabla ya mapinduzi, hata kabla ya uhuru, miaka mingi iliyopita, mahusiano kati ya bara na Zanzibar msingi wake mkubwa ulikuwa ni biashara na hata kabla Serikali hizi mbili hazijaundwa na kwa kweli Muungano umekuja kurasimisha tu mambo yaliyokuwepo tayari. Uhusiano mkubwa kabisa na mzuri kabisa wa kibiashara watu wengi wa bara ambao wamekuwepo Zanzibar miaka mingi kwa sehemu kubwa walienda kule kwa sababu ya biashara na watu wa Zanzibar wengi waliokuwa wamekaa bara kwa vizazi na vizazi sababu kubwa iliyowaleta ilikuwa ni biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fursa za biashara tunazoziongea sasa hivi ziko kwa namna mbili; kwanza, ni uwezo na urahisi wa kusafirisha bidhaa kati ya pande zote mbili, hiyo ni namna moja na ndiyo ambayo imechukua sehemu kubwa ya mjadala. Namna ya pili, ni uwezo na urahisi wa mtu yeyote kutoka upande wowote kwenda kuishi upande wowote kwa urahisi zaidi na kuanzisha biashara hiyo ni namna ya pili ambayo haikuzungumzwa sana lakini ni kubwa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunafahamu kwamba hii ya pili, uwezo wa mtu yeyote kwenda upande wowote wa Muungano kutengeneza makazi, kutengeneza maisha na kufanya biashara huu pia umekuwa msingi mkubwa wa uimara wa Muungano wetu na maingiliano yetu. Sidhani ndiyo maana haikuzungumzwa, kwa sehemu kubwa kabisa, tunapotafakari kuhusu mchango na hatua za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwezesha ukuaji wa uchumi na ustawi wa watu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili pia ni muhimu kulitazama; je, ni rahisi zaidi kwa mtu kutoka Zanzibar kuja bara kupata mahali kuanzisha biashara na kushamiri na kusaidia nyumbani Zanzibar? Jibu ni ndiyo, ni rahisi na kwa nini ni hivyo? Ni kwa sababu ya Muungano. Kwa hiyo, huwezi kuuondoa Muungano katika ustawi wa watu wa Zanzibar unaotokana na urahisi wa watu wa Zanzibar kuja Bara na kufanya biashara na kushamiri. Kwa hiyo, hiyo ni manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili la pili na hili ni jambo jema kabisa na tunataka iendelee kuwa hivyo. Tunafurahi kuona Wazanzibar wengi zaidi wanakuja kuishi bara na kustawi na kusaidia Zanzibar na Wazanzibari walioko bara sasa hivi ni wengi zaidi kuliko Wazanzibari wote waliko Kisiwa cha Pemba. Miaka 20 au 30 ijayo, Wazanzibari kwa mwenendo tunaokwenda, Wazanzibari wanaoishi Bara wanaweza kuwa wengi kuliko Wazanzibari wote walioko Zanzibar na hilo ni jambo jema, ndiyo Muungano na tunaoutaka na ndiyo fursa na muingiliano sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani kwamba katika mazungumzo tunayozungumza hapa kuhusu ustawi wa Muungano wetu tusisahau uzuri na ukubwa wa fursa inayotokana na urahisi wa Wazanzibari kuja kufanya biashara bara. Wote tunajua kwamba katika maeneo yetu hasa ya Pwani, sisi tunaotoka Tanga, tunaotoka Dar es Salaam na kwingineko na hata katikati ya nchi yetu huwezi kwenda maduka mawili, matatu bila kukuta duka la Mzanzibari

ambaye anafanya kazi na ananufaika na anasaidia Zanzibar hivyo hivyo. Kwa hiyo, kikubwa tu tunaomba kwamba wakija huku pia tujue wote ni raia wa nchi moja na pia wasaidie kwenda kujenga nyumbani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili la kwanza la urahisi wa kufanya biashara, urahisi wa kupeleka bidhaa; hakuna anayebisha kwamba kuna changamoto kabisa siwezi kusimama hapa kama Waziri mwenye dhamana ya Muungano nikasema hakuna shida yoyote kuhusu bidhaa zinazokwenda kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafahamu kwamba kihistoria, biashara kati ya pande zote mbili haikuwa rasmi sana na baada ya sisi kuunda Serikali, kufanya Muungano na katika historia ya maendeleo ya uchumi wa nchi yetu na biashara, kumetokea hatua mbalimbali za kurasimisha uchumi na biashara na zile hatua zililazimika kuunda Taasisi mbalimbali na baadhi ya Taasisi hizo ni Taasisi za udhibiti zikiwemo *TFDA, ZFDA, TBS, ZBS*, sasa *TRA* ambayo haikuwepo mpaka mwaka 1996 ndiyo ilianzishwa *TRA*.

Sasa katika utendaji kazi katika hizi mamlaka na mamlaka ikishaitwa ya udhibiti wakati mwingine lile neno udhibiti linapitiliza mipaka. Inadhibiti siyo kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri bali inadhibiti hata kuhakikisha mambo yenyewe yanafanyika. Kwa hiyo, sisi tunafahamu kwamba sasa hivi tunapitia kipindi cha tunaweza kusema *readjustment* ya hizi mamlaka kufahamu wajibu wake na kufahamu kwamba zina wajibu wa kusaidia masuala ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa imezungumzwa hapa kwamba nilifanya ziara mahususi kule Zanzibar mwezi wa Oktoba na hili suala la biashara na vikwazo vya biashara, sisi Serikali tulianza kulifanyia kazi kabla halijazungumziwa Bungeni hapa. Nimeenda Zanzibar, mkutano wangu wa kwanza mkubwa kabisa tulikuwa na Zanzibar *Chamber of Commerce* ambao kulikuwa na mamlaka nyingine

na Taasisi zingine pale za wafanyabiashara kama vile Zanzibar *Freight Bureau*, Zanzibar *Exporters Association* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikutana na wafanyabiashara wanaohangaika kufanya biashara kila siku kati ya Bara na Zanzibar na wakanieleza kwa kina na kwa umahiri mkubwa jinsi biashara kati ya Bara na Zanzibar inavyofanyika na changamotozo zilizopo katika biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukazungumza *structure* ya uchumi wa Zanzibar kwamba kwa sehemu kubwa ni *service oriented*, utalii na biashara na *structure* ya uchumi wa Bara ambao kwa sehemu kubwa ni *diverse*; kuna madini, kuna kilimo, kuna ufugaji, kuna uvuvi na kadhalika na kwamba *currency* ya nchi yetu ambayo pia inasaidia wafanyabiashara wa Zanzibar kuagiza bidhaa kutoka nje, *stability* yake inategemea na *mix* kati ya hizi chumi mbili ambazo lazima ziwe *interdependent*, lazima ziwe zinategemeana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata ustawi wa uchumi wa Zanzibar vilevile kwa kiasi kikubwa unategemea *diversity* ya uchumi wa Bara kwamba sisi na hata *control* ya *inflation* ya Zanzibar inategemea *stability* ya *currency* inayotokana na *diversity* ya uchumi wa Bara. Kwa hiyo, haya mambo lazima yatazamwe katika upana wake na tukazungumza na wafanyabiashara kuhusu hayo mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikafanya ziara bandari ya majahazi na mahali kwingineko, tukazungumza kuhusu ughali wa kuleta mizigo Zanzibar kutoka siyo tu Bara bali kutoka kote duniani na ni kwa namna gani tutarahisisha uagizaji wa Zanzibar wa bidhaa usiwe ni *through transshipment* kwa Bara kwamba mzigo unashushwa mahali kwingine ndiyo unachukuliwa na majahazi au meli ndogo kuja Zanzibar. Ni kwa kiasi gani Zanzibar inaweza kuagiza mzigo *directly* yenyewe moja kwa moja kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikafanya ziara *TRA* kwa upande wa Zanzibar, *ZRB*, Mamlaka ya Bahari Kuu, nikakutana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na vijana na tukakusanya mambo yote ambayo yanawakwaza Wazanzibari kuhusu biashara na tarehe 23 Oktoba, nikakutana na Waziri wa biashara wa Zanzibar, Mheshimiwa Amina Salum Ally na jopo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nilimwomba Waziri Ummu anipe mtu wa *TFDA* na Waziri Mwijage anipe mtu wa *TBS* ili wawepo kwenye ule mkutano, tukapitia hoja moja mpaka nyingine inayosababisha watu wa Zanzibar iwe vigumu wao kufanya biashara na tukazichukua zile hoja, tukazitengenezea *matrix*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 27 Oktoba, tukamuomba Mheshimiwa Makamu wa Rais atuite wote, Wizara ya Fedha Zanzibar, Wizara ya Fedha ya Muungano, Wizara ya Biashara ya Zanzibar na mamlaka zote za uhibititi mpaka *TRA* tukapitia hoja moja bada ya nyingine ya vikwazo vya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Biashara akaelekezwa kwamba aende na wataalam wake Zanzibar akakutane na Waziri mwenzake wapitie hoja moja baada ya nyingine na kikao hicho kikafanyika tarehe 22 Machi na *matrix* hapa ninayo na mambo yote yaliyoorodheshwa ikiwemo ya *VAT*, ikiwemo hizi Mamlaka mengine yalitatuliwa katika mchakato huu na mengine yataendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikutana na Waziri wa Fedha wa Zanzibar ambaye alieleza masuala ya biashara kwa upande wa fedha. Kwa hiyo, baada ya kueleza hizi jitihada ambazo tumefanya sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kukutana na wafanyabiashara kwa makundi na mmoja mmoja, kukutanisha sekta, mimi kukutana kama Waziri wa Muungano na Waziri wa Biashara inaniuma sana akisimama Mbunge akisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano haina dhamira ya kutatua changamoto za biashara kwa

upande wa Zanzibar, kwa sababu najua kabisa kazi ambayo tumeifanya na siyo sahihi kabisa kusema hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na inawezekana hatuna uhodari sana wa kuyatangaza haya mambo ambayo tunayafanya, lakini kwa kweli tunayafanya. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge tusaidiane mawazo hapa, nini zaidi yatulichofanya kinafaa kufanywa zaidi na sisi tuko tayari. Nimesikitika kwamba wakati baadhi ya Wabunge wanaeleza shida zilizopo na hizo shida zinathibitishwa na Wabunge wengine kunakuwa na makofi ya kufurahia kwamba shida zile zimekuwa *confirmed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani siyo sawa, tusifurahie kunapokuwa kwamba tume-*confirm*, nadhani kuzomea na kuzodoa ni rahisi zaidi kuliko kushauri, lakini kazi yetu ni kushauri na sisi tuko tayari kupokea ushauri wowote ambao utasaidia tuondoe haya mambo kwa haraka zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muamini kabisa kwamba suala la biashara kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalijua, imelishughulikia na inaendelea kulishughulikia. Nimetengeneza marafiki wengi sana wafanyabiashara wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara yangu na nimekutana nao akina Mohamed Masoud Rashid, Omar Hussein Mussa, Abdallah Abbas Omar, Wakili Awadh Ally alikuwepo kwenye mkutano na kuna baadhi ya mambo tuliyashughulikia pale pale, wale waliniambia kwamba Benki Kuu imetoa waraka kwamba *minimum* ya kiwango cha *bureau de change* ni milioni 300 na kwamba *bureau de change* za Zanzibar ni ndogo ndogo wanaomba tusaidie kwa upande wa Zanzibar kufanyike *exception* na tulifanya. Tulimpiga simu *Governor* Ndullu akasema ataenda. Kwa hiyo wakati mwingine haya mambo tunayafanyia kazi wakati huo huo tukiwa kwenye ziara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo alizungumza Ndugu Jamal na ningependa kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *terminal two*, ni kweli kumekuwepo na changamoto pale ya *extension* kuongeza mkopo mwingine kwa ajili ya kumaliza lile jengo na limekuwa ni jambo kubwa la lawama wakati anazungumza watu wakapiga makofi kwamba ni kweli kabisa mkopo umenyimwa. Hata hivyo, nataka kusema kwamba mchakato wa kutoa mikopo kwenye Serikali una hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya hatua za mwisho mwisho kabisa, ni mkopo ule kupitishwa na Kamati ya madeni ya Taifa. Kwa hiyo, nataka niwambie Mheshimiwa Jamal na Wazanzibari, rafiki zangu, ndugu zangu wapendwa kwamba mapema mwezi huu Kamati ya madeni ya Taifa ilipitisha na kukubali Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikope dola milioni 58 zaidi kwa ajili ya kumaliza jengo lile le *terminal two* pale uwanja wa Ndege wa Zanzibar. Kwa hiyo, jambo hilo litakwisha, litakuwa siyo hoja tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa Bandari ya Mpigeduri. Taarifa tulizonazo sisi kutoka kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha na Zanzibar na hapa barani kwamba bado kuna maelezo ya ziada ya kitaalam na kibiashara na kuchumi yanahitajika ili kuweza kujenga hoja nzuri zaidi hata kule tunakokopa pesa, lakini Serikali ya Jamhuri haina dhamira ya kunyima uwezo Zanzibar kujitengenezea Bandari yake ambayo ni mhimili wa uchumi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hapo hapo kuna mradi wa *e-government*, kuna mkopo, nadhani masuala haya ni muhimu yazungumzwe vizuri kwa sababu mikopo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayokwenda kufanya miradi Zanzibar bado marejesho ya fedha zile yanalipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ndiyo maana kuna ushirikishwaji mkubwa na ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna miradi mingine ya maendeleo Zanzibar, hospitali ya Mnazi mmoja,

SUZA, Barabara ya Chake-Wete hadi Gando kupitia mifuko mbalimbali kama vile *Saudi Fund, Kuwait Fund* na *BADEA*, yote hiyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasaidia na inashiriki kuwezesha fedha zitoke ili kazi hiyo ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi na usumbufu, tumesikia na ni kweli ni changamoto. Dada yangu Tauhida nimekusikia, nakubali na nimekuelewa, nitapanda Boti ya Azam lakini nadhani *MV*. Mapinduzi basi siku moja nitapanda tujionee nini kinaendelea. Hata hivyo, tumeelezewa changamoto nyingi zilizopo pale na kuna mambo mawili pale yanayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni kweli kwamba nchi yetu sisi vituo vya forodha vipo popote ambapo unaweza kuingia kutoka nje ya nchi ikiwemo Zanzibar na tunapaswa kuwa na mfumo wa pamoja wa forodha kwamba ukiingiza bidhaa kwenye kituo cha forodha cha Zanzibar labda umechukua gari kutoka Dubai iwe sawa na umeingiza Tanga kutokea Dubai. Yote hiyo inategemea mfumo wa pamoja wa uthamini wa kodi. Sasa tumesimika mfumo wa pamoja wa kuthamini kodi lakini hatujaanza kuutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfumo mpya unaitwa *TANSIS* ambao ndiyo una *database* ya thamani ya bidhaa zote duniani ili kodi iweze kuthaminishwa kwa pamoja ili usilazimike kuonekana kama umelipa mara mbili, ukija Bara kumbe umelipa tofauti. Sasa ukadiriaji unaotegemea macho ya mtu, akili ya mtu moyo wake ndio unasababisha tuwe na changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo tunalijua na bahati nzuri kuna kikao tarehe 28 mwezi huu hapa na limezungumzwa sana na kuna baadhi ya mambo madogo tu ya kitaalam yamebakia ili tuwe na mfumo wa pamoja wa kuthaminisha bidhaa. Huo mfumo ukiwekwa, basi hizi shida zote zilizozungumzwa hapa zote zitakwisha, kikubwa ni hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi, kwa hiyo, nipande upande mmoja wa mfumo. Upande wa pili ni watu kwamba wakati mwingine kwenye vituo hivi vya forodha kuna watu wakorofi tu ambao kazi yao ni ku-*harass* watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona kabisa kwamba huyu mama ametoka Zanzibar, amefungasha khanga na kuna watu wa kutoka kule Makunduchi anakotoka Mheshimiwa Wanu, wakienda kuoja, basi wanabeba masanduku na masanduku ya khanga, kuna jina lao wanatumia, nimelisahau. Wakifika pale, unaona kabisa akinamama wa watu wamepaka hina, unaona wanaenda harusini, unaona wako kundi na wanakuelezea, lakini mtu hataki kukubali. Sasa inawezekana mtu akili hana, lakini hata macho ya kuona hana, kuona kwamba hapa hili jambo ni la wazi kabisa kwamba hawa watu ni mizigo binafsi na wala wazi biashara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili tumezungumza na wenzetu wa mamlaka ili tuwe tunaambiana. Kama kuna wafanyakazi wakorofi ambao wanawasumbua watu, basi watupe majina ili waweze kubadilishwa kwenye vituo hivyo. Mchango wa watu binafsi kwenye kuharibu mambo upo na ni mkubwa. Kwa hiyo, tunaweza tukaja hapa tukalalamika sana kumbe ni mtu tu utashi wake kwenye kusumbua watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine ni mambo makubwa sana yanatokea. Nitatoa mfano wa jambo moja ambalo tumelishughulikia ambao ulikuwa ni uamuzi wa mtu mmoja tu. Zanzibar inapata watalii wengi kutoka Italia, nadhani nusu ya watalii wa Zanzibar wanatoka *Italy*. Siku moja Afisa mmoja wa Ubalozi wetu kule Roma akaamua kuandika kwa *Travel Agency* wote *Italy* kwamba kuanzia mwezi wa Kwanza tarehe moja ukitaka kwenda Zanzibar *visa* huipati kule, lazima uje Ubalozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu *Italy* wanatoka miji mbalimbali; wengine wanatoka *Nepals*, wengine



*Frolence*, wengine wapi; kwa hiyo, ukiwaambia kwamba walazimike kwenda Roma, maana yake utafanya usumbufu na kupunguza watalii Zanzibar. Sasa ilipokuja ile habari, wote sisi, Waziri wa Muungano ndio unaaambiwa, namtafuta Waziri wa Mambo ya Ndani ambaye anahusika na masuala ya Uhamiaji, kumwuliza, hana habari. Waziri wa Mambo ya Nje mwenye Ubalazi, hana habari, kwamba jambo kubwa kama hili limeamuliwa lakini hana habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe ulikuwa ni uamuzi wa mtu mmoja. Sasa wenzetu Wazanzibari, baadhi walivyolipata wakajua tayari ni siasa hapa, tunaminywa, wanataka kutuuu, wanataka kutumaliza, utalii ndiyo uchumi wetu, hawatupendi. Ikawa jambo kubwa! Kumbe kuuliza, hamna mtu yeyote mkubwa wa Serikali anayelijua. Ni Afisa mmoja tu. Kwa hiyo, tukalazimika kubadilisha ule uamuzi ili utaratibu ule wa zamani wa kupata *visa on arrival* uendelee pale pale; na unaendelea mpaka sasa hivi. Hatukutangaza kujitutumua kwamba tumesaidia, kwa sababu ni mambo ya kila siku ya kawaida ya utendaji wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kuna kikao kikubwa kinakuja cha tarehe 28 mwezi wa Nne, baadhi ya mambo ambayo Waheshimiwa Mbunge wameyazungumza; mambo ya VAT na mifumo ya kodi yatazungumzwa na kumalizwa na Mawaziri wa Fedha pamoja na wataalam wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kombo amezungumza kwamba uchumi wa Zanzibar unakufa, uchumi unasimama, mfumo mbovu. Sasa nadhani tueleze, maana nimemsikiliza kwa makini sana na nilichokisikia ni lawama, nikawa na kalamu yangu nangoja aniambie nini sasa tufanye ili tuweze kufanikiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usajili wa meli, ni jambo ambalo wote tunalijua na kuna hoja hapa kwamba Zanzibar sasa inanyang'anywa usajili wa meli. Bahati nzuri nimeshughulika nalo hili mwenyewe binafsi. Ambacho kinataka kufanywa ni kwamba zoezi la usajili wa meli liwe

shirikishi. Tufahamu kwamba hizi meli zinabeba bendera ya Tanzania ya nchi yetu. Wote tunajua meli kadhaa zimekamatwa na mihadarati, nyingine zinabeba silaha, nyingine zinatia nanga katika bandari zilizoziwa, nyingine zinakiuka vikwazo vya Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeitwa na kuaibishwa mara nyingi kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, tumetishiwa kuwekewa vikwazo vya kiuchumi kama nchi. Wasiwasi wetu mkubwa ni kwamba hizi meli zimekutwa na silaha na mihadarati, Mungu epusha siku ingekutwa na watu (*human trafficking*) ndiyo ingekuwa shida kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wote tunajua kwamba Mamlaka ya Kusajili Meli za Nje ni mamlaka ya nchi, lakini huko nyuma kulikuwa na makubaliano kwamba Zanzibar itafanya kwa niaba ya Tanzania na itabaki na hayo mapato, kabisa. Hili ni jambo ambalo wengi hawajui. Iliamuliwa kwamba Zanzibar ifanye kwa niaba yetu wote na ibaki na mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatokea utaratibu pale kwamba wamemtafuta *Agent* Dubai, ndio ana muhuri wa Tanzania. Fikiria nchi kubwa ya Tanzania, mtu pale Dubai ana kaofisi, ndio anawakabidhi watu bendera ya Tanzania. Hatumjui ni nani? Sasa kilichofanyika na bahati nzuri mimi nilishiriki, tumesema, sawa, sahihi iendelee kuwa ya Waziri wa Zanzibar, lakini vyombo vya usalama vishiriki, meli zinazoomba bendera ya Tanzania tuzijue zinatoka nchi gani? Zinataka kufanya shughuli gani ili tulinde sifa na heshima ya nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu yangu akija kusema hapa kwamba tumewanyang'anya na nini, nadhani hatutendei haki na anatulaumu bila haki kabisa kwa kweli. Tunachotaka kufanya ni jambo zuri kabisa ambalo siyo litaisaidia tu Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hata Zanzibar yenyewe itaisaidia. Kwa sababu tungenyang'anywa huu usajili kama nchi kutokana na makosa ya hizo meli, hata

Zanzibar haya mapato yasingekuwepo. Kwa hiyo, hili linafanyika kwa nia njema na kwa ajili ya manufaa ya watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Pondeza namshukuru kwa pongezi. Ni kweli kuna changamoto kwenye kiwango cha deni la umeme na wote tunajua masuala ya *VAT*, tunajua *calculations* zinazotokana na uwekezaji wa miundombinu na jambo hili bahati nzuri Wizara zinakaa na zinaendelea kulfanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usajili wa vyombo vya moto, bahati nzuri *AG* yupo hapa. Suala lile limeshughulikiwa muda mrefu. Sisi tunataka gari yoyote ikisajiliwa Zanzibar iwe sawa na imesajiliwa Bara na ikisajiliwa Bara iwe sawa na imesajiliwa Zanzibar. Nasi Ofisi ya Makamu wa Rais, jambo hili tulilisukuma sana na mimi binafsi kwa nguvu zangu zote na Mawaziri wahusika wanajua; na viongozi wetu Wakuu, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu wametuunga mkono. Tulifikisha jambo hilo mpaka kwenye vikao muhimu vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri jambo hili lina *dimensions* za masuala ya kodi na hicho kipengele kimeenda kutazamwa. Imani yetu ni kwamba katika mabadiliko ya sheria mchanganyiko, *miscellaneous amendment* ni kwamba jambo hili litaingizwa ili tuweze kubadilisha hizi sheria ili magari yaruhusiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nami nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, ni aibu kwa gari ya Zambia kutembea kwa urahisi Tanzania kuliko gari ya Zanzibar. Hilo jambo hamna anayeona aibu kulisema, hata sisi tunaona ni aibu vilevile. Tutalirekebisha, kwa sababu Serikali imeonesha utayari na lilishaingia hadi kwenye vikao vikubwa vya Serikali na lilipitishwa huko nyuma muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vikao, tangu kwenye mchango wa hotuba ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanazungumza kwamba mnakaa

vikao, kero haziishi. Labda Waheshimiwa Wajumbe watupe njia mbadala ya kuzungumza zaidi ya vikao, kwa sababu vikao ndiyo mahali pakubwa ambapo tunaweza kuzungumza na kufanya maamuzi na yakafuatiliwa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizungumza katika kuhitimisha hotuba yake kwamba kikao kikubwa ni kile cha Kamati ya pamoja chini ya Mheshimiwa Makamu wa Rais na maamuzi ya kila kikao ni maamuzi ya kiserikali yenye nguvu ya kiserikali na sisi kazi yetu ni kuyafuatilia na kuhakikisha kwamba yanatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata mchango wa Mheshimiwa Machano na tunapokea mapendekezo na ushauri aliotupa kuhusu fursa za utalii na kwenye simu na kuhusu vyombo vya moto, nimelizungumzia. Malipo ya ujenzi wa Ofisi, hili limewekwa kwenye bajeti kwa sababu ni deni na litaendelea kulipwa. Ahadi za viongozi, tutazifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema pale awali, kwamba yale ambayo hatujayazungumza, tutayajibu kwa maandishi; yapo mambo ya mifuko ya *plastick* kwenye masuala ya mazingira. Dhamira yetu ya kuzuia kabisa mifuko ya *plastick* ipo pale pale na tutalitekeleza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwisho kabisa kwa kusema kwamba mwaka 1965, mwaka mmoja baada ya kuwa na Muungano wetu, kulikuwa na Mkutano wa Pamoja wa *TANU* na *ASP* wa kupendekeza Mgombea Urais wa Muungano. Kwenye ule Mkutano Mheshimiwa Karume alimpendekeza Mwalimu Nyerere kuwa Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ule Mkutano, Mwalimu Nyerere aliuhadithia ule mkutano na hadithi hiyo alirudia mara nyingi jinsi Muungano huu ulivyokuja. Aliwaambia Wajumbe na Mzee Karume akiwepo kwamba Shehe Karume, ninyi Wazanzibari mkiwa tayari kuungana, Wabara nasi tutakuwa tayari. Marehemu Mzee Karume

akajibu, wewe unazungumzia utayari wa nini? Hii habari ya kuwa tayari ya nini? Sisi tuko tayari. Ita Waandishi wa Habari sasa hivi, tutangaze sisi ni nchi moja, wewe Rais. Mwalimu akasema, hapana, mambo haya yanahitaji sheria, na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nazungumza hili tujue kwamba urithi wa Muungano wetu chanzo chake ni nini? Dhamira ya Muungano wetu ilitokana na nini? Ilitokana na nyoyo, dira na maono ya viongozi wetu Wakuu, Waasisi wa Taifa hili kwamba tumetawaliwa na tukaleta mapinduzi na tukaleta Uhuru. Tunao uwezo kabisa wa kutengeneza mipaka mipya ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi Watanzania hatujui thamani tuliyonayo duniani kwamba ni nchi pekee iliyotengeneza mipaka mipya kama nchi, tunachukulia hili jambo la mzaha tu. Tumetengeneza mipaka mipya na Taifa jipya kwa utashi wetu. Sasa hii habari ya kwamba mkopo umechelewa, hiki kimechelewa, naomba sana tusiweke doa kwenye jambo hili kubwa katika changamoto ambazo kabisa tuna uwezo wa kuzimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba mtu unaoitwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na unapata manufaa kutokana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, halafu unakuja unaupaka masizi Muungano ambao wote sisi ni warithi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, imani yangu kwamba tutapitisha bajeti hii ili baada ya hapa tuendeleo kufanya kazi kwa pamoja kuimarisha Muungano wetu, nchi yetu hii iendeleo kupata sifa kubwa iliyonayo duniani. Kama nilivyosema asubuhi kwenye hotuba yetu ni kwamba sisi sote tutaondoka hapa duniani, lakini *legacy* yetu kubwa ni kuondoka Muungano huu ukiwa imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wote, wana CCM wenzangu ambao sote tunasema kwamba tunataka

kumsaidia Mheshimiwa Rais, namna kubwa ya kumsaidia Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kwamba anamaliza wakati wake Muungano huu ukiwepo na ukiwa imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naafiki.

*(Hoja litolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, (Muungano na Mazingira), hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 26 - Makamu wa Rais**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Mgt.....* Sh. 6,308,631,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tayari tuna majina hapa ya ambao watasimama kwenye shilingi. Tunaanza na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, Mheshimiwa Cosato Chumi na Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware na Mheshimiwa Khatib Said Haji.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nataka nijue kauli ya Serikali. Serikali ina mpango gani kuhusiana na mabonde au mafuriko ambayo yametokea Dar es Salaam na sana yamesababishwa na bonde la Msimbazi ambapo hilo bonde pia limepita kwenye Jimbo la Segerea. Mwaka 2012 tullipata mafuriko kama hayo, wananchi wakapata shida, lakini pia tukapata maafa. Pamoja na hayo pia, tukapoteza nyumba nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa imekuwa kama ni utamaduni kwamba kila mvua inaponyesha kubwa mafuriko yanatokea, maji yanapeleka nyumba lakini pia kuna hasara kubwa ambazo zinatokea ikiwemo shughuli za wananchi kusimama. Dar es Salaam sasa hivi kuna kama siku tatu wanafunzi pia hawajaenda shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua Serikali au Wizara imejipangaje ikiwa haya mafuriko yataendelea kutokea kila mwaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja majibu. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Dar es Salaam ni moja ya majiji yanayokua kwa haraka duniani na kwa kipindi kirefu limekuwa linakabiliwa na changamoto za mipango miji, makazi holela na masuala mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Serikali kupitia TAMISEMI, kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, tumekuwa tunafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kwamba tunadhibiti; tunakuwa na miradi, kwanza tuna masuala ya kisera, lakini pia kuhakikisha kwamba usimamizi wa Sheria za Mipango Miji, Sheria za Mazingira na Sheria nyinginezo zinazodhibiti masuala ya ujenzi holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hilo ni kwa upande mmoja, usimamizi wa sheria. Bahati mbaya sana kwenye hili, moja ya changamoto Mheshimiwa Mbunge atafahamu ni siasa, kwamba wakati mwingine pale ambapo mnataka kuchukua hatua ngumu za kuhakikisha kwamba mambo yanakaa vizuri, basi kunajitokeza masuala ambayo yanaleta ugumu. Bahati nzuri tunakaa kama viongozi tunafanya pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili, ni miradi mbalimbali mikubwa ambayo Serikali inatarajia kuifanya. Naomba nitaje miradi miwili ambayo itanufaisha pia kwenye Jimbo la Mheshimiwa Bonnah Kaluwa. Mradi wa kwanza unaitwa *Tanzania Urban Resilient Program* ambao utajenga mifereji na miundombinu mbalimbali ya kuelekeza maji yaende kule kunakostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine mkubwa kabisa ni wa Dar es Salaam *Metropolitan Project* ambao uko chini ya TAMISEMI. Miradi yote hii thamani yake ni karibu shilingi bilioni 600. Ni hela nyingi zinawekezwa kwenye Mji wa Dar es Salaam kuhakikisha kwamba miundombinu inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais, inao mradi ambao pia unanufaisha Jimbo la Mheshimiwa na asubuhi niliutaja, mradi wa mifereji mikubwa kabisa kule Bungoni na mwingine kule Temeke. Kwa hiyo, Serikali inafanya mambo mawili; kwanza, kusimamia sheria, lakini pili, kuja na miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kwanza utaanza mwezi Juni, mwaka 2018 na mradi wa pili utaanza mwezi Aprili mwakani 2019. Miradi hii itakapokwisha, basi mafuriko Dar es Salaam tutakuwa tumeyapunguza kwa kiasi kikubwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri nimeshafanya naye ziara kwenye Jimbo langu siyo chini ya mara tano. Ameona vile ambavyo Bonde la Msimbazi ambavyo limekula nyumba; kwa sababu kuna mambo ambayo yangeshughulikiwa kitaalam, pengine mafuriko yasingekuwepo. Kwa sababu maji yamezuiwa, kwa hiyo, yametafuta sehemu na yamekwenda kwenye nyumba za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tulishafanya ziara wote Vingunguti, akaona kuna nyumba



zaidi ya 12 pamoja na makaburi, akashuhudia kwamba pia na miili imeondoka na maji. Sasa kwa mafuriko ya juzi na jana, tukisema kwamba tusingiri mpaka mwezi wa Sita ili sasa hiyo *project* iweze kuanza au utengenezaji wa hiyo mitaro, kwa kweli tutakuwa tumepata tatizo kubwa hasa kwa wakazi wa Vingunguti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wa Vingunguti pamoja na Dar es Salaam nzima, wanahitaji wajue Serikali ina mpango gani wa haraka na huo mpango ambao utasubiri mwezi wa Sita ambapo hiyo *project* itaanza, ni jinsi gani mnaweza kuwasaidia? Kwa sababu Wizara wanajua matatizo hayo muda mrefu, wameshakuja kwenye Jimbo la Segerea siyo chini ya mara tano kwa ajili ya kuangalia Mto Msimbazi wanaweza wakausaidia vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri nafikiri tulivyotembelea mara ya mwisho, alisema kwamba Wizara inaweza ikasaidia; pamoja na kwamba wale watu wamekaa kwenye lile bonde, lakini kwa kutumia utaalam wanaweza wakatengeneza ile mifereji, wenyewe wakaendelea kukaa hapo hapo, lakini pia wasipate mafuriko. Sasa kutokana na majibu yake Mheshimiwa Waziri, naona kwa mwezi wa Sita itakuwa mbali sana kwa sababu hatujui kwamba mvua itakwisha lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue ni mpango gani wa haraka ambao Wizara imejiandaa kuwasaidia hao wananchi kwa kipindi hiki kwa hizi siku? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo naomba kushika shilingi na naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono. Naomba kutoa hoja.

*(Hoja haikuungwa mkono na Wabunge)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimemsikia Mheshimiwa Mbunge na kwa kweli nataka nimpongeze sana kwa sababu ni kweli tumefanya ziara nyingi na kwa sababu amekuwa anasisitiza sana kwamba twende tukaone hali ya makazi kwa watu wa Jimbo lake; na mara nyingi nimeenda na wataalam wa ofisi yetu, lakini na wataalam wengine wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa yaliyotokea juzi baada ya mafuriko, kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais nikisema kwamba tuna mpango wa haraka wa kutengeneza na kurekebisha yale yaliyotokea juzi wakati tayari tumetumia muda mrefu sana kufanya *design* na *studies* ili kutatua tatizo kwa ujumla na kwa muda mrefu, nitakuwa namdanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho naweza kusema ni kwamba kwa sababu lina *element* ya maafa, kwamba kilichotokea juzi ni mafuriko, yameondoa nyumba za watu, wengine wamekosa makazi; na mara nyingi upande wa maafa huwa kuna hatua za haraka pale watu wanapopata maafa; kwa hiyo, yuko Waziri anayehusika na maafa, kwa hiyo, yeye anaweza kuzungumza. Kwa sababu hilo kama ni la maafa ndilo linaloweza kuwa na hatua za haraka za kimaafa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, tunaendelea na Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nina jambo moja na ikiwa Mheshimiwa Waziri majibu yake hayatanitosheleza, nitashika shilingi yake. Nataka nifahamu kama nchi na kama Taifa tumejipangaje kuhakikisha kwamba tunanufaika na fedha ambazo zinatengwa na Mifuko mbalimbali duniani kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifuko imetengwa, mingine iko chini ya *African Development Bank*, mingine iko chini ya *UN*, lakini kama Taifa ukilinganisha na majirani zetu, bado hatujaweza kuanza kunufaika kupata hizo fedha sababu hatujaweza kutengeneza mipango mikakati. Je, Serikali ina mpango gani? Maelezo ya Mheshimiwa Waziri yasiponitosheleza, nitashika shilingi ili kusudi tuweze kuona tutanufaika vipi na fedha hizo? Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu asubuhi, Mheshimiwa Mbunge yuko sahihi kabisa kwamba duniani huko na kwenye nyanja za Kimataifa kuna fursa mbalimbali za kupata fedha kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za mazingira na ziko namna mbili za kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya kwanza ni kushiriki katika mikataba mbalimbali ya Kimataifa ambapo ile mikataba inakuja na fursa. Kwenye hotuba yetu tumezungumza kuhusu mikataba. Niseme tu kwamba, ukisoma hotuba yetu pale kwenye kipengele cha uanachama wetu kwenye mkataba wa mabadiiko ya tabianchi utaona kwamba nchi yetu imenufaika zaidi kwa takriban shilingi bilioni 600 kwa kuwa tu wanachama wa ule mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ya shilingi bilioni 600 tumeeleza imeenda wapi, lakini mradi mmojawapo ni mradi mkubwa wa maji wa karibu shilingi bilioni 250 kwenye eneo lililopata ukame mkubwa Mkoani Simiyu, maji kutoka Ziwa Victoria kupitia *Green Climate Fund*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunashiriki kama *National Entity* kwa ajili ya fedha za Mfuko wa Mazingira (*Global Environment Fund*) na *Adaptation Fund* na mengineyo. Kwa hiyo, namna mojawapo ni ya uanachama kwenye mikataba

na tumeiorodhesha; Mkataba wa Stockholm, Mkataba wa Bazel, Mkataba wa Montreal na yote hiyo inatupa pesa za kufanya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Bunge hili limeridhia majuzi tuwe wanachama rasmi sasa wa Mkataba wa Paris, jambo ambalo pia linafungua fursa zaidi. Kwa hiyo, kwa Serikai kuleta hapa Bungeni kibali cha kuomba ridhaa ilikuwa ni katika hatua hizo za kupata rasilimali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya pili ya kupata fedha ni kuandika maandiko kwenye mifuko mbalimbali (*proposals*) na hapo ndiyo kulikuwa na changamoto kwa sababu ya uwezo wa watu wetu wa kuandika *proposals*. Sasa tumejenga uwezo, nami pale ofisini niliwaambia wataalam kwamba wanipe *proposal* kumi baada ya kipindi fulani hivi, halafu tuchambue zipi tunaweza tukazipeleka mbele. Baadhi zimeanza kutoa matunda; kwenye hotuba yetu tumeiorodhesha miradi mbalimbali ambayo tumeipata kupitia *proposals* tulizoandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya tatu ni ya kupata ithibati kwa Taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi kwenye nchi yetu. Tumeeleza asubuhi kwamba tumeiwezesha *NEMC* iwe *National Implementing Entity Adaptation Fund*, tutaiwezesha TAMISEMI ipate *accreditation* ya *Green Climate Fund*, Wizara ya Fedha. Hapa Tanzania Benki ya *CRDB* ndiyo itakuwa benki ya kwanza nchini kupata ithibati ya kuweza kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilialika mabenki yote hapa nchini kuwa na kikao na mimi ili kuwawezesha tuwasaidie wapate ithibati ili waweze kupata fedha. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Chumi, jitihada zipo na tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *resource mobilization* kwa ajili ya hifadhi ya mazingira kwangu ni muhimu sana na ofisini wanajua hilo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kiasi fulani na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, lakini pamoja na kuwa fedha tunapata kwa kuwa wanachama, hizo ni sehemu tu ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fedha nyingi ambazo tunaweza kupata ikiwa ni pamoja na masuala kama aliyosema kujenga na kutengeneza *proposal*, lakini kuwa na *accredited entity* katika nchi; sisi kama Taifa mpaka sasa hivi hatuna taasisi hata moja ambayo iko *accredited* Mheshimiwa Waziri akiwa mkweli. Nchi kama Kenya wana taasisi zaidi ya 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuliona hilo, *African Development Bank* kupitia mfuko unaitwa *Africa Climate Change Fund* iliona kwamba nchi za kiafrika kwa sababu zina kitu kinaitwa *Limited Institution of Capacity to Access and Manage Finance and Develop Bankable Climate Project*, wakaanzisha *fund* ambayo mwaka 2017 baadhi ya nchi zimeomba jumla ya fedha dola bilioni 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri maelezo yake nayaona kwamba hayajitoshelezi na ndiyo maana kuna madhara ambayo yanatokana na mabadiliko ya tabianchi (*climate change*) tungeweza kukabiliana ukiacha hiyo miradi ya maji. Matatizo kama hayo yanayotokea Dar es Salaam, kwa sababu fedha hizo zinahusisha *training, capacity building* na ku-*fund* mambo kadha wa kadha; kwa hiyo, naliomba Bunge lako Tukufu waniunge mkono tujadili jambo hili kwa sababu sisi tunalala nyuma wakati hizo fedha zipo na nchi kubwa zinasababisha hayo matatizo na tunaoumia ni sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na hiyo mikataba, kuna *a lot of funds* ambazo tungeweza ku-*exhaust* kama Taifa, lakini bado tumekaa tu. Kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu liniunge mkono ili tuweze kujadili hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Mapema mchana wa leo wakati nachangia, niligusia umuhimu wa kufanya Tathmini ya Madhara katika Mazingira kwa miradi mbalimbali nchini (*Environmental Impact Assesment*) na mkono wa NEMC unawezaje kufanya kazi. *Decisions* nyingine zinaonesha kwamba *Environmental Impact Assesment* ya nchi hii kwenye miradi mikubwa hasa inayohusiana na miradi ya Kiserikali inakuwa na changamoto na nikatoa mfano wa UDART na mafuriko tunayoona sasa hivi katika Bonde la Mto Msimbazi. Mfano wa pili nilioutoa ni wa *Stieglers gorge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mawaziri wanasema kwamba *Environment Impact Assesment* itafanyika ili kuangalia madhara ya mradi huu na jinsi ya *ku-manage adaptation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kitabu cha maendeleo, Wizara ya Nishati ukurasa wa 140, *item 3172*, tayari zimeshatengwa shillingi bilioni 700 kwa ajili ya huu mradi. Sasa tunaendaje kutekeleza mradi huu wakati nilichokuwa nakiongelea, ile *Environmental Impact Assesment* haijafanyika *according to* Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, wakati huku tayari mmesea *go ahead*, tunaanza huu mradi, wakati huu mradi una *consequences* kubwa sana kimaslahi katika ikolojia na wananchi kwa ujumla katika Taifa hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina lengo la kumnyima Waziri shilingi yake au fedha zake, lakini ningependa ufafanuzi wake wa kina na kama sitaridhika, basi nitaomba kushika shilingi yake ili tuweze kuangalia tunatokaje hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mtoa Hoja. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba rafiki yangu Mheshimiwa Sware akumbuke kwamba tathmini ya athari kwa mazingira, kuna wakati wawekezaji walilalamika sana kwamba *NEMC*, Ofisi ya Makamu wa Rais tuna urasimu sana katika utoaji wa vyeti hivi vya tathmini ya athari kwa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ndoto ya Mheshimiwa Rais ni viwanda na tunahitaji umeme, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo ya namna ya kuboresha utoaji wa vyeti hivi na kutowakwaza wawekezaji. Ndiyo maana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, alichukua maamuzi ya kupunguza muda wa utoaji wa vyeti kukawa na *provisional permit*, kwamba katika kipindi cha siku tatu, wale wawekezaji wakishatoa *documents* zile muhimu, kwa sababu inahusisha wakati mwingine na mikopo na ku-*mobilize resources*, wawe wanaendelea na tathmini ya mazingira kwa muda wa miezi sita; na baadaye watakapokuwa wameleta *documents* zote na hizi fedha anazosema kwamba *TANESCO* wametenga hizi shilingi bilioni ni katika ku-*mobilize* hizi *resources*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo kwamba ni *go ahead* kwamba hata pasipo tathmini ya athari kwa mazingira, basi wanaruhusiwa. Siyo kwamba wanaruhusiwa, ni pale ambapo katika mlolongo ule ambao nimeusema ndipo pale ambapo ule mradi unaweza ukaanza baada ya kuonesha zile changamoto na namna ambavyo watazi-*manage* au wataziepuka. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Naomba mjadala wenzangu wanisaidie kwenye hili. Tuko hapa kwenye kujenga, hatuko hapa kwenye kukomeshana. Naomba nianzie hapo. Ni bahati mbaya kwamba upande huu ukiongea, maana naona Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla unajiandaa na... (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko hapa kwenye kujenga. *Cost benefit analysis* imegoma kwenye huu mradi. Ilianza tangu mwanzo kwamba huu mradi tangu miaka ya 1960; miaka ya *late 1980's* nao ukawa umetaka kufufuliwa lakini tena ukawa *shelved*, ilikuwa ni kwa sababu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu ametujaalia *resources* nyingi sana ambazo ni vyanzo vya nishati nchini. Sasa hivi tuna *oil and gas*, tuna *gas* imekuwa, yaani haija-*materialize*, tunakimbia kwenye *project* ambayo ina *big consequences* kwenye Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niwaoneshe picha nyingine tena. Unapoleta madhara haya, siyo tu kwa wanyamapori, bali na kwa binadamu, kwa watu. Tunaongelea ile *oxygen* ya binadamu ambayo ni muhimu. Sasa hii ni *oxygen* ya rasilimali zilizopo katika bonde hili la mto Rufiji tukianza na Selous. Tunasema kwamba bahari ni uhai. Bahari hii inaishi *through* huu Mto Rufiji unavyoingia Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, usijiangalie kwamba kwa kuwa wewe unakaa bara, hawa watakaopata madhara ni watu fulani *few* wa Kusini; siyo kweli. Bahari hii ndiyo inayokuletea wewe *oxygen* Mheshimiwa; bahari hii ndiyo inayokuletea wewe maji yanayozunguka yanakuwa mvua inanyesha huko uliko bara ambapo unafikiria mimi havinihusu, lakini huu mradi unakuhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla Selous *Game Reserve is the largest*, ina kilometa za mraba 1,300 zitakuwa chini ya maji. Wengine wote watakosa. Kwa hiyo, takwimu ni muhimu kwa sababu takwimu ndiyo inakufanya uitengeneze *decision*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. KABWE Z. R. ZITO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.



**MWENYEKITI:** Majina, matatu huku na huku. Huku wawili, huku watatu. Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ngoja tuandike majina. Mheshimiwa Ruth; katika nyie mmoja, Mheshimiwa Nassari na huku Mheshimiwa Waziri wa Ardhi. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Mheshimiwa Subira. Tunaanza na Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MBUNGE FULANI:** Inatosha.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kuunga mkono hoja aliyozungumzia Mheshimiwa Dkt. Sware kuhusu huu mradi mkubwa wa *Stieglers Gorge*. Kama alivyoainisha, hata mimi nasema kwamba hatuna dhamira ya kuzuia huu mradi, lakini nakubaliana naye kwamba huu mradi unatakiwa ufanyiwe tathmini kamili ya athari kwa mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *report* zilishatolewa nyingi tu kabla hata ya sasa hivi. Kwa kawaida, ni lazima tena turudi tuangalie zile *report* ambazo zilishatolewa na tuangalie *environment* ya sasa hivi ilivyo na kuja na *proposal* za kuweza ku-*mitigate* masuala ambayo yanaweza kuathiri mazingira kwa baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwa kweli, Serikali irudi ikaangalie zile *reports* ambazo zilishatolewa mara mbili, mara tatu, halafu tuangalie hali ya sasa hivi ilivyo na viumbe hai na kuja na *proposal*, tathmini ya athari kwa mazingira, mpya, ambayo ndiyo itakuwa inatoa *information* ya kuona huu mradi tuweze kuutekeleza kwa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo ushauri wangu kwa Serikali. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lukuvi. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani nilikuwa naongea kidogo na Mheshimiwa Zitto, anasema tunafanya siasa hapa, lakini ukweli wanaujua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kama Watanzania lazima tuangalie maslahi mapana ya mradi huu. Mimi siamini kabisa kwamba haya tunayozungumza hatujui sababu za kufanya mradi huu pale *Stieglers Gorge*. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa hoja ya Serikali ya kuendelea na mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya anayoyasema Mheshimiwa ambaye sasa hivi amechangia, ndiyo ambayo alisema hata Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla. Serikali itachukua hatua zote kuhakikisha mradi huu unafanyika na unafanyika kwa mujibu wa utaratibu. Hakuna maji yatakayopotea; *actually*, tunayaweka vizuri ili yaende kwa utaratibu mzuri zaidi. Yataenda kiasi kile kile na yataendelea kuingia baharini. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, *Selous ni Game Reserve*. *Reserve* ya nani? Tumepanga sisi iwe *reserve*. *Reserve* ya nini? *Reserve* ya nchi. Leo mbona wao kila mara wanamwambia Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla hapa apunguze misitu, apunguze miti, apunguze hifadhi, wananchi wachunge, wafanye shughuli za maendeleo? Kwa nini *Selous* tusiipunguze tukafanya shughuli ya maendeleo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku hapa wanalalamika na kwenye hoja hapa wanasema; leo tuna tatizo, mwingiliano wa shughuli za kibinadamu ambazo ni za msingi. Tumejenga shule kwenye *game reserves*, tumeweka mifugo kwenye *game reserves*, tumejenga miundombinu kwenye *game reserves*. Serikali wanaishauri ipunguze zile *game reserves* kwa sababu ni *reserve* ya nchi, tumepanga, tumeamua, tutatengeneza umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko sababu ambazo zilitufanya tusifanye mradi huu wakati ule, lakini sababu hizo

hazipo hivi sasa. Tunazo fedha sisi wenyewe. Kama wafadhili hawana fedha ya kutukopesha, tutajenga na tumedhamiria kujenga kwa fedha zetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mikopo ni migumu na kwa sababu wanajua tunataka kujitegemea, ni ngumu sana kutupa fedha za mikopo. Hiyo, ndiyo sababu imetumika kutukwamisha. Safari hii hawawezi, tuna fedha zetu, tutajenga wenyewe, mradi huu mpaka utakamilika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna upotoshaji mkubwa sana ambao unafanyika kwenye mijadala. Maana Mheshimiwa Waziri Lukuvi anasema kwamba wana pesa. Pesa hawana. Tumepitisha bajeti hapa mwaka 2016/2017, bajeti yao ya kwanza, wamekwenda kukopa *10% more of what* Bunge liliidhinisha. Pesa wanatoa wapi? *CAG* ameonesha *1.5 trillion* hazionekani zimetumika kufanya nini. Pesa wanatoa wapi? Hawana pesa, hawana pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho wakati tathmini inafanyika ya mradi wa *Stieglers Gorge, 1979* mpaka sasa uwezo wa Ruaha Mkuu kuzalisha maji kupeleka kule kwenye eneo la *Stieglers Gorge* umepungua kwa 47%. Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wana taarifa, Wizara ya Nishati ina taarifa, Wizara ya Maliasili ina taarifa na Wizara ya Ardhi ina taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *SAGCOT; 4.4 million people* wanategemea *SAGCOT*. Tumechukua fedha, tumekopa, tumechukua *private sector* tumewaingiza. *Stieglers Gorge* inakwenda kunyonya maji yote, 36% ya maji ya *SAGCOT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokitaka hapa, hatuzuii mradi, hatuwezi kuzuia maendeleo ya nchi yetu. Tunachokisema ni kwamba mna bomba. Bomba mnatumia 6% sasa hivi; bomba likifika tu 25% linazalisha umeme wote

ambao wanaenda kuuzalisha *Stieglers*. Kwa nini wakafanye *replacement* ya watu kule ambao wanatumia maji ya Ruaha na maji ya Rufiji? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mwisho.

**MBUNGE FULANI:** Muda.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo namaliza, mbona Mheshimiwa Lukuvi ameongea sana hamkusema? Tulieni tuwapige nondo.

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yetu na hoja ya Mheshimiwa hapa ambayo tunaiunga mkono ni kwamba *Detailed Environmental Impact Assessment* ifanyike, iletwe ndani ya Bunge, tujiridhishe kwamba wananchi wetu hawataathirika, hawatakuwa *replaced*. Then mradi uendelee. Ninyi hamjafanya *Environmental Impact Assessment*, halafu mnatenga fedha *seven hundred billion*. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Nassari na Mheshimiwa Olenasha.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Sitagusa habari ya hela kwa sababu Mheshimiwa Zitto amegusa vizuri sana, lakini wakati mwingine huwa tunapenda kushauri kama Taifa. Kuna wakati mwingine natamani sana tuwe tunazungumza tukiwa peke yetu, bila kujua CHADEMA ni wapi na CCM ni wapi, ili kushauri vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UNESCO* wamepiga chini hiki kitu na wamezungumza, dunia nzima inajua. *IUCN*, (*International Union for Conservation of Nature*), hakuna sehemu watapata pesa kama mashirika yote haya yamekataa; *WWF* wamekataa, pesa za ndani ziko wapi? Hazipo, huu ni mradi mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kingine amezungumzia kidogo habari ya gesi hapa nami nikumbushie. Leo hii tunalipa pesa kwa sababu ya bomba la gesi ambalo tumejenga, *we are paying*, halafu hatutumii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kingine imezungumzwa habari ya *SAGCOT* hapa; kuna wakulima, *4.4 million people*, Mheshimiwa Zitto amesema. Kuna wavuvi, ni wa kwetu hawa. Vile vile kila Waziri wa Maliasili na Utalii hapa anazungumzia habari ya *Southern Circuit* kwenye utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia *Southern Circuit*, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii leo anakubali vipi *Selousiondoke*? Anakubali vipi? Aah, zote ni Kusini, Ruaha maji hayo hayo. Sasa hapa ameongea Mheshimiwa Dkt. Sware kuhusu *mangrove trees* na mikoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema vizuri kabisa kwamba ameunda kikosi kinafanya *study ya flora and fauna*. *At the same time* wanasema kwamba kuna kikosi kinafanya habari ya *Environmental Impact Assessment (EIA)*, *at the same time* wanakuja na *seven hundred billion shillings* za Watanzania kwenye bajeti. Kwa nini tusipeleke watu wanywe maji wakati tunasubiri *report*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tusionekane tunapinga mradi, wote tunataka umeme. Kila mtu anataka hizo *megawatt* 2,500 ziingizwe. Mimi natamani sana, lakini kabla hatujaenda huko, basi hii *report* iletwe iangaliwe.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni *report* ije, tuangalie, tui-*study*, tuone kikosi kazi cha Mheshimiwa Makamu wa Rais, halafu tufanye maamuzi kwa ajili ya Taifa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na...

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. taarifa.

### TAARIFA

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtaarifu mzungumzaji anayezungumza. Pengine inatokana na watu kufikiria wakiwa wanatawaliwa na Wakoloni.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anapewa nani taarifa sasa kwa sababu, hakuna mzungumzaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamaliza kutoa taarifa kwa mzungumzaji.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Unampa nani taarifa? Unampa nani taarifa sasa? Hamna mzungumzaji.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tufikirie kwa sayansi ya kawaida, yaani tusitumie akili nyingi tu. Hivi maji yakiwa yana-*flow* halafu yakapita yakazalisha umeme, yanapungua? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Simbachawene, umeeleweka.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maji hayapungui. Mto Kongo ule wanazalisha umeme, maji yanaendelea.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mfano ni Dodoma. Angalia Mtera hapa jirani kwako. Angalia Mtera. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olenasha, halafu Mheshimiwa January.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi. Namwomba sana rafiki yangu, Mheshimiwa Dkt. Semesi aachie shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu, nina hakika hili suala amelileta tu kwa ajili ya mjadala, yeye mwenyewe anajua majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya mazingira ni kitu cha kawaida kabisa kwenye miradi. Hakuna mradi wowote ambao unaweza ukatekelezwa ambao hauna athari za mazingira. Mradi wowote una *social* na *environmental impact*. Kinachofanyika kwa kawaida, unafanya tathmini ili uangalie namna ya ku-*mitigate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ni lazima tufahamu na yeye najua anafahamu, ni mara nyingi sana *Environmental Impact Assessment* imetumika kuzuia miradi ya maendeleo kwenye nchi zinazoendelea. Aje, anieleze leo hii mradi wowote ambao umeshaitishwa Marekani au Ulaya au nchi yoyote iliyoendelea kwa sababu kuna athari za kimazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ni kwamba tuwe wazalendo. Hatuwezi tukaacha kutekeleza mradi ambao una maslahi kwa Taifa kwa sababu tu kuna watu wana wasiwasi kwamba una athari wakati sisi tunajua hauna athari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Selous* wanayosema kwamba itaathiriwa, *Selous* ina ukubwa wa kilometa za mraba 50,000. Zote zitaathirika vipi, *as if* mto ule unapita

kwenye *Selous* yote. *How?* Hiyo ni *reasoning* ya aina gani? Yeye ni mwanasayansi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu rafiki yangu Mheshimiwa Zitto *of all people, honestly*, hakuna *requirement* yoyote kwenye sheria yetu ya mazingira ya mwaka 2004 ya kutaka *Environmental Impact Assessment* ya mradi kuletwa Bungeni kwa ajili ya kupitishwa. Unaitoa wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba tu; rafiki yangu najua ataachia shilingi. Yeye ni msomi, ni mtafiti, aachie kwa sababu mradi huu tunauhitaji kwa ajili ya maslahi ya Taifa. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu alivyoiumba dunia na akamuumba mwanadamu, alimpa mwanadamu kuwa khalifa wa dunia. Kuwa khalifa, maana yake ni kuwa kiongozi. Mwanadamu alivyopewa nafasi hiyo kubwa na Mwenyezi Mungu ya kuwa kiongozi, hakupewa kitu kingine chochote kile, ndiyo maana kuna viumbe vingine ni vikubwa zaidi, vingine ni vigumu zaidi kuliko mwanadamu. Mwanadamu alipewa na Mwenyezi Mungu akili ili imsaidie kuitawala dunia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanadamu alipewa rasilimali ili azitumie. Nasi wanadamu leo hii tunazitumia rasilimali tulizopewa. Tanzania ina haki ya kutumia rasilimali ilizopewa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tulipewa akili na Mwenyezi Mungu, tunajipanga kutumia rasilimali ya *Stieglers Gorge* kwa kutumia akili, kwamba tutatumia rasilimali yetu kwa faida yetu, tutapata umeme, lakini tutapunguza sana athari za kimazingira kwa kutumia mbinu za kisayansi. Ndiyo akili tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, ndiyo uongozi tuliyopewa kwamba tuitawale dunia kwa kutumia akili. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi wanadamu wa Tanzania tumedhamiria kuwekeza kwenye mradi huu na tutawekeza. Hatutaacha, tutawekeza na tumejipanga, wawe *IUCN*, wawe *WWF*, wawe *UNESCO*, hatutawasikiliza. Tutawekeza, tutapata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa rasilimali hii ni yetu na tunaithamini, tumeweka mikakati ya kuitunza isiharibike. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Subira Mgalu na baadaye Mheshimiwa Kakunda amalizie.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Kwanza napenda nijielekeze kwenye mchango wa Mheshimiwa Zitto aliposema tuna vyanzo, kwa mfano gesi na kwamba tutakapofikia 25% ya matumizi ya bomba la gesi, basi nchi itakuwa imejitosheleza kinishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Zitto, ni kweli tunazalisha umeme kwa kutumia gesi, lakini kama Serikali tumetathmini gharama ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi na gharama ya kuzalisha umeme kwa kutumia maji. Takwimu zinaonesha gharama ya kuzalisha umeme kwa kutumia maji ni 36/= kwa Kilowati, lakini gharama ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ni 147/= ni zaidi ya mara nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa vyovyote vile hata kama tukifikia 25% ya matumizi ya bomba hilo, lakini gharama ya kuzalisha umeme huo utakuwa ni ghali zaidi na utakuwa ni umeme ambao ni wa gharama kwa mwananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Zitto alieleza suala la Ruaha Mkuu kwamba mto umekauka. Nataka nitoe taarifa kwamba Bonde la Mto Rufiji linapokea maji kutoka chanzo cha Mto Ruaha Mkuu, ambacho

kinachangia 15% tu zaidi ya lita za ujazo bilioni tatu. Chanzo cha Mto Kilombero kinachangia 65% za zaidi ya lita za ujazo bilioni 13. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na *study* ambayo imefanyika ya *Tanzania Hydropower Sustainability* mwaka 2015. Katika hiyo *study*, imeonesha pale kidakia maji cha Kidatu kiwango hakijabadilika. Uwepo wa maji yaliyokuwepo pale, unatosheleza kwa matumizi ya sasa na ya baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa, tafiti hii ni kuongezeka kwa shughuli za binadamu ambapo Serikali hii itasimamia hizo shughuli za kibinadamu. Kwa kuwa, mradi huu unapita katika Mikoa 10, Wilaya 30, Majimbo 54 na Kata 259, naamini kwa pamoja tukiwa wadau wa mradi huu tuna uwezo wa kupambana na shughuli za binadamu ili kufanya maji yatiririke katika Mto Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono na tumetenga kweli shilingi bilioni 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira. Mheshimiwa Kakunda. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kabla sijawa Mbunge nilikuwa Mkurugenzi wa Programu ya Maji Tanzania. Nafahamu kwamba Mto Rufiji ni mto muhimu zaidi katika nchi yetu ya Tanzania. Mnamo mwezi Machi mto huu una maji jumla ya mita za ujazo bilioni 20.5 ambayo yanapita kwenda baharini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipofika Mhandisi Stiegler kwenye maporomoko hayo mwaka 1905, alishangaa kuhusu uwezo wa maporomoko hayo kusaidia uchumi wa nchi hii. Mara moja akaanza kuchora michoro ya kujenga bwawa na daraja katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana mwaka 1907 alifariki kwa kuuliwa na tembo katika eneo hilo hilo na mwili wake ukaangukia kwenye maporomoko hayo na ndiyo sababu mpaka leo yanaitwa *Stieglers Gorge*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka niwaelimishe, kama Wazungu waliona kwamba eneo hilo ni muhimu sana kusaidia uchumi wa nchi hii, nashangaa leo Mtanzania anasimama ndani ya Bunge anawawakilisha Watanzania anasema mradi huu haufai. Kwa miaka 111 kumekuwa na majadiliano, kulikuwa na *studies* nyingi sana. *Studies* za mazingira zimefanyika zaidi ya 1,000 kwa ajili ya maporomoko hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida kubwa iliyopo zaidi ya kuzalisha *Megawatt* 2,100 pale ni *flood plain* kule chini ambako unaweza ukalima hekta 150,000 za kilimo ambazo zitazalisha tani zaidi ya 500,000 za chakula. Kwa hiyo, mradi huo ni muhimu sana utekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda wako umemalizika.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijampa Mtoa Hoja, naongeza nusu saa ili Kamati ya Matumizi imalize kazi yake.

Mheshimiwa Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Sware kwa sababu nafahamu kwamba ni Mwanamazingira hasa, kabisa, wala hakuna shaka kwenye hilo. Ni jambo liko moyoni mwake na amelisomea na wote lazima tukubali. Hilo la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Dkt. Sware ambacho anaomba ni kwamba kufanyiike

*Comprehensive Environmental and Social Impact Assessment*, ndiyo ombi lake. Hakuna haja ya kuwa na mjadala, Serikali tunalikubali. Siyo tu kwamba tunalikubali, tumeshaanza kulifanya na kazi hiyo wamepewa taasisi pale inaitwa *Institute for Resource Assessment (IRA)*; anaifahamu Mheshimiwa Dkt. Sware. Kwa hiyo, mjadala huu hauna haja ya kuwa mrefu. Mheshimiwa Dkt. Sware anaomba kufanyike *Comprehensive Environmental and Social Impact Assessment*, sisi Serikali tunasema sawa, ndiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja ya ndugu yangu Mheshimiwa Zitto kwamba, iletwe Bungeni, hiyo siyo sawa kwa sababu hakuna *requirement* hiyo na hakuna kipengele hicho kwenye sheria. Kuhusu kufanyika, yes, kabisa. Kwa hiyo, naomba arudishe shilingi ili tuendelee mbele.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Dkt. Sware umeridhika na hayo maelezo au tulihoji Bunge?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nafurahi kwamba Mheshimiwa Waziri husika amenielewa ninachokitaka. Sikuwa na lengo la kuleta huu mjadala leo hapa Bungeni, lakini niliposoma Kitabu cha Maendeleo, Wizara ya Nishati, nilipoona shilingi bilioni 700 zimetengwa kwa ajili ya huu mradi, ikawa ni *red flag*. Nikasema tunarudi kama kwenye mradi mdogo tu wa *UDART* ambao umetushinda, unatuumbua kila mwaka tunapata mafuriko: Je, mradi wa *magnitude* kubwa kiasi hiki na *impact* viashiria vinatisha, tutafika wapi kama Taifa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Nafikiri Serikali husika itafanyia kazi na kwa wale tuliotoa mijadala humu ndani, nafikiri *Hansard* ime-capture vizuri, ikiwa ndivyo sivyo, basi tusije tukanyoosheana vidole. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Sware. Tunaendelea na Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nadhani kwa uungwana alionao Mheshimiwa Waziri huyu msikivu, hata mimi hatutabishana sana, huenda nami akanikubalia mapema ninayoyataka ili twende mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwetu hususan Wazanzibari tumezungumzia sana suala la vikwazo vya kibiashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ameonesha wazi kukubaliana na mengi kiasi ambacho kimetupunguza nguvu kuona haja ya kuendelea na misimamo mikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi, hata mimi nilitaka ku-*withdrawal* nisiongee tena, lakini nimerudi kwenye kumbukumbu, haya aliyoyaahidi leo, kwa mfano kikwazo cha Wazanzibari au Watanzania wanaotoka Visiwani kuingia na usafiri wao au vyombo vyao huku Bara kimekuwa ni tatizo kubwa na la muda mrefu sana. Leo hii yalaiti ingekuwa ni siku ya mwanzo tunalijadili hili moja kwa moja ningesema nimeridhika na yale majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi Bunge la Kumi nilizungumza mara tatu jambo hili na hili Bunge la Kumi na Moja tayari nilishazungumza hapo nyuma na leo tayari tumezungumza tena. Kwa hiyo, dhamira iliyomo kwenye moyo na maneno yanayotoka mdomoni haviendani katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo inakuja tafsiri kwamba Muungano huu ni tunu kwetu. Siyo tafsiri tu, lakini inajengeka kwamba labda wanaoleta hoja za kutaka kuweka mambo sawa ni Wapinzani wa Muungano. Hilo tuondoe, hakuna mpinzani wa Muungano. Mimi binafsi Muungano naupenda ndani ya roho yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama unampenda kuku, humchukui kibandani tu ukamweka kwenye sufuria

ukamla, haiwezekani, utakula uchafu, lazima umchinje, umtoe visivyostahiki ili upate upate kuku safi, ndiyo unakunywa supu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na Muungano huu siyo kwamba tuseme tu tunaupenda lakini tunaacha uchafu mwingi. Mambo haya, kero hizi ndogo ndogo, yalaiti toka siku ambayo wameanza kujibu kwamba wanashughulikia, wangukuwa wanayashughulikia, haya yasingekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kero hii moja ya magari na usajili wa vyombo vya moto kutumika hapa yeye mwenyewe imemsuta nafsi na kusema ni aibu kama mtu wa kutoka Zambia anaweza kuingia na chombo chake aka-*enjoy* Tanzania lakini Mzanzibari kwake yeye inakuwa ni kosa. Hilo ni aibu, tena ni aibu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka atupe ahadi, ni muda gani jambo hili litashughulikiwa ili tuondokane na kero hii moja? Kwa leo nataka hili tu anipe *commitment* kwamba ndani ya muda gani jambo hili litakuwa limefikia mwisho?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khatib. Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri wa Nchi ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Ni kweli jambo hili wamelifanyia kazi kwa kiwango kikubwa sana. Kwa sababu ni taratibu za kisheria ndiyo maana unaweza ukasema kwamba kuna kipindi kimepita likiwa bado halijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea, tayari makubaliano yale yaliyofikiwa katika vikao ambavyo vimekuwa *chaired* na Makamu wa Rais, vikiratibiwa na Waziri

husika, imeshapelekwa kwa Mwandishi wa Sheria kwa ajili ya kufanya *amendment* maeneo yale ambayo yalikuwa yanaleta ule utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *amendments* zile kufanyika, pia tayari waraka mpana ambao utashughulikia masuala ya usafiri ni pamoja na usafiri wa barabarani, umeshaandaliwa na wenyewe unaelekea kwenye ngazi ya Baraza. Lile la eneo ambalo analisemea Mheshimiwa Khatib, lenyewe limeshapelekwa kama sehemu ya *amendment* ambazo zitafanyika ili kuweza kulimaliza tatizo hilo kwa jinsi ambavyo amekuwa amelielezea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo majibu anayoniambia Mheshimiwa Waziri, naheshimu sana na nakubaliana nayo sana, lakini yalishatoka miaka nenda miaka rudi. Siyo leo, si mapya, hayajaanza leo. Sasa nilichoomba ni kitu kidogo na wala sikuwa na nia; na bado naeleza kwamba sina nia ya kuzuia shilingi ya Mheshimiwa Waziri juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu dhamira ya dhati wameshaionesha na hatua mbalimbali ambazo Mheshimiwa Waziri amezieleza hapa kwamba wameanza kuzichukua, tunaomba ahadi ya sasa mpya kwamba *at least* jambo hili litachukua muda gani? Mwaka au miaka miwili? Maana yake tunasubiri sana na ngoja ngoja inaumiza matumbo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kile anachokinukuu zamani, tulikuwa tunaongelea kwamba vikao vitafanyika. Tulikuwa tunanukuu kwamba kuna Kamati itakaa, lakini sasa hivi tunachoripoti, Kamati zote zimeshaka na haya majibu hayawezi yakawa ya siku zile zile, kwa sababu hivi vikao vimeratibiwa Mheshimiwa Mama Samia akiwa Makamu na ndugu yangu

Mheshimiwa January akiwa Ofisi ya Makamu wa Rais. Ndiyo vimeratibiwa vikatoka kwenye vikao. Sasa tunavyoongea, imeshapelekwa kwenye kuandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, hili jambo la lini? Ni itakavyopangiwa tu kwa sababu taratibu nyingine zinakuwa za Kibunge. Itakavyoletwa *miscellaneous amendment*, ni taratibu za Kibunge tu, iko hatua za mwisho na hili jambo linaenda kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaweza tukasema itakapokuwepo fursa ambazo ni taratibu za kibunge za kupitisha yale masuala ya *miscellaneous amendment* kwa sababu limeshapelekwa kwa Mwandishi wa Sheria, *definitely* na lenyewe litakuwepo. Kwa maana hiyo, kwa sababu taratibu za kiratiba hizi hazipangwi na Waziri, ni taratibu za Kibunge, sisi tunaweza kusema kama Serikali yale yaliyokuwa yanahusu michakato, yalishakwisha, ishapelekwa kwenye kuandikwa. Basi *miscellaneous* zile zitakapofanyika, matumaini yetu ni kwamba na lenyewe litakuwemo, kwa sababu lilishamaliza *procedures* hizi nyingine.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **FUNGU 31 - OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

Kif. 1001 – <i>Administration and Human Resources Division</i> .....	Sh.3,009,806,560/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i> .....	Sh.250,089,000/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning Division</i> .....	Sh.576,232,000/=
Kif. 1004 – <i>Government Comm. Unit</i> .....	Sh.170,446,000/=
Kif. 1005 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.166,770,000/=
Kif. 1006 – <i>Procurement Manag’nt Unit</i> .....	Sh.117,344,000/=



Kif. 1007 – *Information and Commun. Technology Unity*.....Sh.153,934,000/=

Kif. 1008 – *Legal Services Unit*.....Sh.183,354,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisimama)

**MWENYEKITI:** Tumshaafiki tayari, tuendeleo na kifungu kingine.

Kif. 2001 – *Union Secretariat*.....Sh. 499,187,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo katika *program 20 - Union coordination, subvote 2001*. Naenda kwenye *item 22007 - Rental Expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki, ukiona katika mwaka uliopita kulikuwa na Sh.64,500,000/=, mara hii kuna shilingi milioni 51 na kwa mujibu wa randama, kina fedha hizi ni kulipia gharama za Vikao vya Kamati ya pamoja ya Serikali ya SMT na SMZ na usafiri wa Ndege na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema wana nia njema, jambo hili litakwenda kwa vikao, lakini fedha zenyewe za vikao vya kutatua kero za Muungano wamezipunguza. Sasa hawaeleweki, hawasomeki kwamba wana nia njema ya kukaa vikao vingi, wanasema watakaa katika vikao na vikao ndivyo ambavyo vitaleta utaratibu, watapanga mipango mizuri ili kuona kwamba wanapunguza kero za Muungano, lakini fedha za vikao vyenyewe wameziona, wakazipunguza. Hebu watuambie lipi kwa lipi? Mbona hawasomeki? Kwa nini fedha hizi zimepungua? Watueleze kwa makini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za vikao zimepungua kwa sababu tumefanikiwa sana kupunguza kero za Muungano, hatuhitaji kukaa na hela nyingi kama ilivyokuwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 – *Environment*.....Sh. 4,593,954,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuendeleo wameshaafiki Waheshimiwa Wabunge.

## MIPANGO YA MAENDELEO

### FUNGU 31 – OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Kif. 1001 – *Administration and HR Div*.....Sh. 1,538,800,000/=

Kif. 1003 – *Policy and Planning Division*.....Sh. 0/=

Kif. 5001 – *Environment*.....Sh. 3,524,540,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Subvote* 5905 kuhusiana na *The National Environment Fund* kimepangiwa Sh. 300,000,000. Natambua kwamba mwaka 2017 pia zilipangwa fedha hizi lakini hazikwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, ni kwa nini fedha hizi haziendi na tunajua kabisa kwamba hizi ndiyo zinasaidia pia *NEMC*? Kwa hiyo, naomba kujua ni kwa sababu gani fedha za mwaka 2017 hazikwenda? Je, hizi shilingi milioni 300 ndiyo ambazo zitafanya kazi ya mazingira

kwa mwaka huu mzima wakati tunajua kuna matatizo makubwa sana ya kimazingira?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, mtoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoeleza kwenye hotuba yetu ya Bunge kwamba mfuko huu uliundwa kwa Sheria ya Mazingira iliyopitishwa mwaka 2004, bahati mbaya sana tangu wakati huo Mfuko huu haujawahi kuundwa wala kuwa *operational*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulipokuja tukawa wa kwanza kusema ufanye kazi. Kwa hiyo, tukapendekeza kwa Mheshimiwa Rais, akamteua Ndugu Ali Mafuruki kuwa Mwenyekiti na tukateua Bodi ya watu wazito sana. Walivyoanza kazi sasa kukaa na kupanga mambo, wakagundua kwamba kuna udhaifu mkubwa sana kwenye sheria ilivyoandikwa na *in fact* Msajili wa Hazina alielekeza kwamba hatuwezi kuusajili Mfuko ule uanze kazi kwa sababu ya upungufu huo wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa tumepeleka mapendekezo ya mabadiliko ya sheria madogo tu ya kuiweka vizuri ili mfuko huu uweze kuanza kazi. Kwa hiyo, ndiyo maana utaona mwaka 2017 hata hizo pesa zilizopangwa zilishindwa kupatikana kwa sababu, kwa namna ile ambayo tulitarajia Mfuko huu ufanye kazi usingeweza ku-*operate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuanzishwa kwa Mfuko kumetusaidia kuona kwamba hauwezi kufanya kazi ilivyotarajiwa. Kwa hiyo, hayo ndiyo majibu yetu Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mheshimiwa Waziri, Mtoa hoja.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kanuni ya 104 (3)(a) na (b) kwamba Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba kutoa hoja kwamba Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Mazingira na Muungano) ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Bajeti ya Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Mazingira na Muungano) imepitishwa na Bunge hili kwa ajili ya mwaka 2018/2019. Natumia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa January Makamba na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Kangi Lugola pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya.

Naamini kwamba changamoto zilizopo sasa hivi baadaye hazitaonekana, kama zitakuja nyingine kwa mujibu wa wakati nazo naamini mtazifanyia kazi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Nawatakia kila la heri katika kutekeleza bajeti hii ambayo tumeipitisha leo na ninaamini Mwenyezi Mungu atakuwa pamoja nasi.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.56 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 18 Aprili, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*